22 MEI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 22 Mei, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Tatu, Kikao cha Thelathini na Tano, leo tarehe 22 Mei, 2026.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. GHATI Z. CHOMETE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 410

Kupunguza Tatizo la Ajira kwa Vijana Wanaomaliza Masomo

MHE. AMINA ALI MZEE aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua zipi kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wanaomaliza masomo?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO (MHE. DKT. EVALINE W. MUNISI) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuwawezesha vijana, hususan wahitimu wa vyuo vikuu, ili kupunguza tatizo la ajira. Miongoni mwa hatua hizo ni kuandaa Mwongozo wa Taifa wa Mafunzo ya Uzoefu Kazini wa Mwaka 2017 unaoratibu utoaji wa mafunzo kwa kushirikisha sekta ya umma na binafsi, pamoja na kuwezesha mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mafunzo hayo, jumla ya wahitimu 32,194 wamenufaika kwa kupata ujuzi, maadili ya kazi na uzoefu unaowawezesha kuajiriwa au kujiajiri popote walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeanzisha programu maalum za kuwawezesha vijana katika sekta zenye ajira nyingi kama kilimo *(BBT),* madini *(MBT)* na uvuvi *(BBT-LIFE),* sambamba na kuunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi katika fani mbalimbali kupitia mikataba na Qatar, Saudi Arabia, Falme za Kiarabu na Iran ambapo vijana 7,593 wamenufaika katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

MHE. AMINA ALI MZEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali:-

(a) Je, mpaka sasa Serikali inatumiaje kuhakikisha vijana wanapata ajira kupitia mawakala?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani katika kuhakikisha mawakala wanaoajiri nje ya nchi vijana wetu hawanyimwi haki? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Amina Ali Mzee, kwa maswali mafupi ya kibunge. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO (MHE. DKT. EVALINE W. MUNISI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na nimpongeze Mheshimiwa Amina Ali Mzee kwa namna anavyowapambania vijana na suala zima la ajira. Pia tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa usikivu uliotukuka, utatuzi na utekelezaji wa changamoto hii ya ajira kwa programu maalumu ya kuwezesha vijana katika sekta zenye ajira nyingi na ajira za nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ambao unafanywa na Wizara katika kupata mawakala, Wizara inasajili mawakala na kuwapa vibali maalum vya kuwaunganisha vijana hawa kwa kupata kazi za nje ya nchi. Utaratibu huo unafanyika chini ya mwongozo maalum ambapo Wizara inasimamia utoaji wa mafunzo kwa vijana hawa ambapo wanafundishwa mila na tamaduni za nchi ambazo wanakwenda kufanya kazi. Pia wanafundishwa maadili na utu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mawakala hao wanapewa utaratibu wa kuhakikisha kuwa kazi za staha zinapatikana zinazolinda utu na kutetea haki za vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la pili, la nyongeza la Mheshimiwa Amina Ali Mzee kwamba hatua tunazochukua kama Wizara, kama Serikali kwa mawakala wanaodhulumu na kutishia usalama wa vijana wetu wanaokwenda kufanya kazi za nje, ni kuwanyang'anya vibali vya uwakala. Mpaka dakika hii, mawakala watatu tayari wameshanyang'anywa vibali, kuonesha kwamba tunatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea kidogo, vijana ambao wamepita kwa utaratibu huu ambao Serikali imeelekeza hatujawahi kupata malalamiko yoyote zaidi ya wale ambao wamekwenda nje ya nchi kwa njia zao wenyewe binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba nitoe rai kama Wizara, kama Serikali, kwa ambao wamekwenda kwa utaratibu usio rasmi, wajitahidi kuwasiliana na balozi zetu zilizoko nchi hizo, wataunganishwa na mawakala na kupata kusajiliwa rasmi

kwenye utaratibu mzuri, ambapo watapata kazi za staha zenye kulinda haki na masilahi yao binafsi kama Watanzania. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mbunge wa Msalala aulize swali lake.

Na. 411

Kuongeza Shule za Sekondari Msasala

MHE. MABULA J. MAGANGILA aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuongeza Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Msalala?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mbunge wa Jimbo Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Msalala ina kata 18 na shule za sekondari 26 ambapo kata zote zina shule za sekondari. Hata hivyo, shule zilizopo Kata za Bulyanhulu na Segese zina wanafunzi wengi, huku kata za Mwalugulu, Mwanase, Busangi, Ntobo, Shilela wanafunzi wanatembea umbali mrefu kwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 603.89 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kata ya Bulyanhulu ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule za kata hiyo.

Vilevile, mwaka wa fedha 2026/2027 Halmashauri kupitia mapato ya ndani imetenga shilingi milioni 336 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule mbili za sekondari katika kata za Jana na Lunguya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa shule mpya katika kata zenye mahitaji ya shule, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabula Magangila.

MHE. MABULA J. MAGANGILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Sasa kwa kuwa tayari ya Halmashauri yetu ya Msalala tumeshatenga fedha kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa shule za sekondari kwa ajili ya kupunguza umbali wa watoto wetu wanaosafiri kilometa 15 kwenda sekondari, je, Serikali ina mpango upi wa kuongeza madarasa katika shule zetu za msingi zote zilizopo katika halmashauri yetu, kwa sababu tayari shule zetu zina maeneo ya kuweza kujenga sekondari ili tuweze kuepuka hili tatizo la watoto wetu kusafiri kilometa 15 kuifuata sekondari?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mabula Magangila, Mbunge wa Jimbo la Msalala kwani amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ujenzi wa madarasa na shule mpya katika Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na shule karibu na wananchi ili watoto wetu wasitembee umbali mrefu. Ndiyo maana katika bajeti hii ya 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 603.89, na fedha hiyo itapelekwa kwa ajili ya kujenga shule ya sekondari ya kata, katika Kata ya Bulyan'hulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo halmashauri imetenga shilingi milioni 336 na Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za wananchi na halmashauri katika kujenga madarasa na

kujenga shule ili kusogeza huduma ya elimu karibu zaidi na wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali fupi la nyongeza.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, ninaipongeza Serikali kwa kasi kubwa ya ujenzi wa shule za sekondari katika halmashauri zetu na katika kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata ya Mngazi katika Jimbo la Morogoro Kusini ina wanafunzi wengi sana ambao shule ya sekondari iliyopo haiwezi kuwa-*accommodate* wote, na tayari tumeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari nyingine kwa ajili ya kupunguza idadi ya wanafunzi, na pia kupunguza umbali wa wanafunzi kusafiri kwenda shule. Je, Wizara ina mpango gani katika kutusaidia kuhakikisha tunapata sekondari nyingine katika Kata ya Mngazi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali imeweka utaratibu lakini pia imetoa miongozo katika mamlaka za Serikali za mitaa kote nchini. Kwanza, kupitia Maafisa Elimu Msingi na Sekondari kufanya tathmini na kuona shule ambazo zina wanafunzi wengi zaidi ya vigezo na sera yetu watambue maeneo kwa ajili ya kujenga shule nyingine za sekondari ama za msingi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanyia kazi suala la kata hiyo ili tuweze kuona kama inakidhi vigezo, kwa maana ya idadi ya wanafunzi katika eneo hilo ili tuweke mpango wa kujenga shule ya sekondari na kupunguza msongamano katika shule nyingine.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninasisitiza maswali mafupi ya nyongeza ili wengi mpate kuuliza. Mheshimiwa Clayton Chipando.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilikiri kwenye Bunge hili kwamba itapeleka fedha kwa ajili ya kumrudisha mkadarasi pale kwenye Bwawa la Katubuka, bwawa ambalo linaleta mafuriko kwa wananchi wa Kata ya Katubuka na mpaka leo hakuna kinachoendelea pale, je, Serikali ina majibu gani kuhusiana na kumrudisha mkandarasi aende akayaondoe yale maji kwenye Bwawa la Katubuka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Clayton Chipando, swali itabidi liende kama ni swali la msingi kwa sababu sasa hivi yanaulizwa masuala ya shule na wewe unazungumzia suala la bwawa. Kwa hiyo, utapeleka swali lako kama swali la msingi. Mheshimiwa Exaud Kigahe, Mheshimiwa Nape Nnauye, ajiandae.

MHE. EXAUD S. KIGAHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mapanda katika Jimbo la Mufindi Kaskazini ni kata ambayo ina vijiji vilivyo mbali sana na sekondari ambayo ni moja tu pale Kihanzi. Wanafunzi kutoka Ihimbo, Uhafiwa, Ukami ambao ni zaidi ya kilometa 20 wanasafiri kwenda kwenye sekondari hiyo. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa sekondari katika Kijiji cha Uhafiwa ili kupunguza mwendo mrefu wa wanafunzi hawa kwenda kusoma shule ya sekondari Kihanzi pale Mapanda? Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, na kwa mpango wa kuanza kidato cha kwanza Januari, 2028 kwa wanafunzi wa darasa la sita na la saba, Serikali imeweka mpango madhubuti, kwanza wa kuainisha maeneo yote ambayo shule za sekondari ziko mbali ama shule za sekondari zina wanafunzi wengi; na tutakwenda kutekeleza mpango wa ujenzi wa shule katika maeneo hayo zikiwemo kata ambazo hazina shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Kigahe kwamba, katika Jimbo la Mufindi Kaskazini

tutahakikisha kuwa tunatoa kipaumbele kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari katika kata hiyo ili tuweze kusogeza huduma hiyo karibu zaidi na wanafunzi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nape Nnauye.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Jimbo la Mtama, Halmashauri ya Mtama tuna kata tatu ambazo hazina sekondari kabisa; Kata ya Mtama yenyewe Mtumbya pamoja Longa. Je, Serikali lini itatusaidia kujenga sekondari kwenye kata hizi kwa sababu uhitaji umeongezeka na wanafunzi wamekuwa wengi, hawawezi kuendelea kwenda kwenye sekondari mama?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli katika Jimbo la Mtama, na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo, kaka yangu Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, ameshawasilisha mara kadhaa. Pia, Mkurugenzi na Afisa Elimu wamewasilisha uhitaji wa ujenzi wa shule za sekondari katika kata hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba Serikali tuko kwenye hatua za kibajeti kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari katika kata hizo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Kilolo.

Na. 412

Ujenzi wa Barabara ya Ilula – Image - Ibumu

MHE. DKT. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Je, lini Barabara ya kutoka Ilula – Image – Ibumu itajengwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Ilula – Image - Ibumu katika Wilaya ya Kilolo ipo katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kupitia mradi wa Uboreshaji wa Barabara Vijijini na Ufunguaji wa Fursa za Kiuchumi na Kijamii *(RISE)* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mtaalamu mshauri ameshapatikana na Serikali ipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba kwa ajili ya kufanya usanifu wa barabara hii. Kazi ya usanifu inatarajiwa kufanyika kwa muda wa miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarabitu za kibajeti kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Ilula – Image - Ibumu kwa kiwango cha lami utaanza baada ya usanifu wa barabara kukamilika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini hii ni barabara ambayo inaenda kuunganisha Kilolo na Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapoongea sasa hivi, wananchi wanaopitia hii barabara ya Ibumu - Image, hakuna basi la abiria linaenda kule na wanatoka umbali mrefu sana kufuata matibabu kwenda Ilula. Malori pia yamekwama. Ninaomba sasa Serikali iniambie, wakati tunasubiri usanifu wa barabara hii, maana yake imesema ni miezi sita, hatujui unaanza lini. Je, wanawasaidiaje wananchi wa Ibumu - Image ili waweze kusafiri kwa mabasi na vile waweze kwenda kwenye Kituo cha

Afya cha Ilula, maana yake wanasafiri kwa umbali mrefu sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna barabara nyingine ya Lulindi - Ipalamwa - Ukwega mpaka Kimara, Kata ya Ukwega, na barabara ya Otarisoli - Udepwa mpaka Mabondwa, kilometa 38. Barabara hizi hazipitiki kabisa. Ninaomba Serikali isaidie wananchi wa Kilolo, barabara zote hazipitiki. Tunafanyaje ili wananchi wa Kilolo waweze kutengenezewa barabara zao Maana yake mazao hayapiti na ni barabara za kiuchumi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba, Serikali inatambua kwamba barabara hii ya Ilula – Image - Ibumu ni barabara muhimu sana na ni kweli kufuatia mvua nyingi zilizonyesha mwaka huu, barabara zile zimeathirika kwa kiasi kikubwa. Ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali ipo hatua za mwisho za zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninavyoongea, Mkoa wa Iringa uko hatua za ukamilishaji wa kuwapata makandarasi ili kutumia zile fedha 60% kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya barabara zetu zilizoathirika na mvua. Barabara hii imewekwa kwenye mpango huo na gharama yake ni takribani shilingi bilioni 2.983.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha barabara hii inajengwa mapema, ili wananchi waendelee na shughuli zao za usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, barabara hizo nyingine ambazo amezitaja ni miongoni mwa barabara ambazo pia zimepewa kipaumbele kuhakikisha kwamba zinatengewa fedha na kufanyiwa matengenezo, ili shughuli za usafirishaji zirejee katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kilolo kwamba, Serikali iko kazini na tutahakikisha kwamba barabara zinafanyiwa matengenezo mapema iwezekanavyo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, ajiandae Mheshimiwa Issa Mchungahela.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali. Mheshimiwa Waziri, kuna barabara ya Kilimanjaro - Inyala ambayo ipo katika Jimbo la Katoro. Mheshimiwa Waziri, hii barabara imekatika sehemu kubwa na inahitaji marekebisho madogo sana ili wananchi waweze kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inatumika kusafirisha chakula kutoka Bukondo, Butundwe kuja Katoro, leo haifanyi kazi. Tukimpigia Meneja anatueleza kwamba, fedha za dharura tunafuatilia. Je, Lini sasa hizi fedha za dharura zitapatikana, ili wananchi hao waweze kuunganishiwa kutoka Kilimanjaro kwenda Inyala ili watu hao wa Jimbo la Katoro wapite?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba barabara zetu zilizoathirika na mvua zinatengenezwa, Serikali tayari imeshatoa maelekezo kwa Mameneja wa *TARURA* mikoa na wilaya, kutumia 60% ya bajeti iliyoko mwaka huu wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya kufanya marekebisho ya dharura kwenye barabara zote ambazo zimekatika na hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumsisitiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Geita na Wilaya ya Geita, kufika kwenye barabara hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, kufanya tathmini ya kipande kilichoharibika na kufanya matengenezo kwa haraka iwezekanavyo, ili shughuli za usafirishaji

ziendelee wakati tunasubiri ule mpango wa kukarabati barabara hizi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Issa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika Jimbo la Lulindi, barabara zake zote zimeharibika, na hivi sasa, huwezi kutoka katika kata moja kuelekea kata nyingine. Ni kama jimbo limejifunga hivi. Je, Serikali ina kauli gani kutokana na hii hali katika Jimbo la Lulindi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lulindi ni moja ya majimbo ambayo barabara zake zimeathirika na mvua na ni kweli kipindi hiki mvua zilikuwa bado zinaendelea kunyesha. Kwa taratibu za kitaalamu ilikuwa ni vizuri kusubiri kwanza mvua zikatike, na baada ya hapo tuendelee na taratibu za matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kufuatia maelekezo ya Serikali ya kutumia 60% ya bajeti zetu kwa ajili ya marekebisho ya dharura, tutasimamia kuhakikisha kwamba barabara za Jimbo la Lulindi zinafanyiwa matengenezo na Meneja wa *TARURA* wa Masasi na Mkoa wa Mtwara wazingatie maelekezo ya Serikali. Wakamilishe taratibu za manunuzi na kuhakikisha kwamba barabara hizo zinatengenezwa ili ziweze kurejesha shughuli za usafiri kama kawaida.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, jana tulishapitisha Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Ninaamini kabisa maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanatosheleza kwa matengenezo ya barabara zilizoharibika.

Tunaendelea na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Chemba.

Na. 413

Hitaji la Madawati – Chemba

MHE. KUNTI Y. MAJALA aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kutatua changamoto ya uhaba wa madawati katika Wilaya ya Chemba kwa Shule za Msingi na Sekondari?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya madawati kwa shule za msingi katika Halmashauri ya Chemba ni madawati 21,887, yaliyopo ni madawati 12,473, na upungufu ni madawati 9,414, na mahitaji ya seti za viti na meza kwa shule za sekondari ni 14,483, yaliyopo ni 11,812 na upungufu ni 2,671.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Halmashauri ya Chemba kupitia mapato ya ndani, ilitenga shilingi milioni 129.53 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 1,759 na seti za viti na meza 80 ambapo hadi Aprili, 2026, shilingi milioni 127.93 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa madawati 1,759 na seti za viti na meza 60. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 halmashauri imetenga shilingi milioni 44.1 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 640.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na kuhakikisha kuwa ujenzi wa madarasa mapya unaambatana na ununuzi wa madawati 15 au seti 40 za viti na meza kwa kila darasa linalojengwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kunti Majala.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia muda niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Halmashauri ya Chemba kuna uchakavu na upungufu mkubwa wa madawati kwa shule zetu, lakini ni kweli kwamba halmashauri haitaweza kumaliza tatizo hili la upungufu wa madawati ndani ya wilaya yetu. Je, Serikali iko tayari kubeba mzigo huu kutuchangia angalau shilingi 500,000,000 ili twende tukapunguze adha kubwa ya watoto wetu wanaokaa chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Serikali (TAMISEMI) iko tayari kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii *(TFS)* kuhakikisha kwamba wanakwenda kukamilisha uwepo wa madawati kwa shule zetu zote za msingi 121 pamoja na shule 31 za sekondari ndani ya Wilaya ya Chemba?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kama Mbunge wa Chemba, Mheshimiwa Kunti Majala alivyosema kwamba tuna upungufu wa madawati katika Halmashauri ya Chemba, lakini katika kipindi chote cha miaka mitano Serikali imeendelea kupeleka fedha na kuhakikisha kwamba madawati, viti na meza kwa ajili ya shule za sekondari vinatengenezwa na kuendelea kupunguza lile pengo la upungufu wa madawati, viti na meza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo mtiririko wa upelekaji wa fedha unaonekana, Serikali imedhamiria kuhakikisha tunaondoa kabisa changamoto ya upungufu wa madawati, viti na meza katika shule zetu na ndiyo maana katika mpango wa ujenzi wa madarasa na shule mpya, bajeti ya ujenzi wa darasa inakwenda moja kwa moja na bajeti ya ununuzi wa madawati na viti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *gap* lililopo sasa ni ile ya madarasa ya zamani ambayo tayari tumeshatenga fedha kupitia mapato ya ndani. Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha ya Serikali Kuu kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za halmashauri ili kupunguza pengo hili la madawati katika shule zetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kujenga madarasa mapya pamoja na shule mpya za sekondari na msingi katika Jimbo la Hanang. Kabla ya ujenzi wa shule hizi mpya pamoja na madarasa, tulikuwa na upungufu wa madawati. Baada pia ya kujengewa shule hizi pamoja na madarasa, tumekuwa na upungufu zaidi wa madawati. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya kununua madawati?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa madarasa mapya na shule mpya tunaweka bajeti pia ya kununua madawati, viti na meza. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Asia Halamga kwamba tutahakikisha katika mipango yetu ya ujenzi wa shule mpya na madarasa mapya, bajeti ya ununuzi wa madawati, viti na meza itazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa zile shule ambazo tayari zipo na zina upungufu wa madawati, nikuhakikishie kwamba tumekubaliana na tumeelekeza, kwanza, halmashauri watenge fedha kupitia mapato ya ndani. Serikali Kuu kupitia bajeti zake tutaendelea kupeleka fedha, kuhakikisha kwamba madawati yananunuliwa na wanafunzi wetu wanapata mazingira bora ya kusoma. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Hanang kwamba Serikali iko kazini na tutahakikisha tunaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli ya madawati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali za kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia nchini, Halmashauri ya Mji wa Tarime bado ina upungufu mkubwa wa madawati kwa maana ya shule ya msingi, viti na meza sekondari, pamoja na samani za walimu katika ofisi zao. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha kwamba inapeleka fedha ili kuboresha, kuondoa huu upungufu wa madawati, viti na meza pamoja na samani za walimu, ili iweze kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuweza kupelekea wanafunzi kufaulu vizuri? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa kuboresha elimu ya msingi na sekondari, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya madarasa na miundombinu mingine, moja ya kipaumbele ambacho Serikali imeweka ni kuhakikisha kwamba tunaboresha upatikanaji wa madawati, viti na meza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Mjini, katika Halmashauri ya Tarime Mjini pia tumepeleka fedha kwa ajili ya madawati na viti, lakini tunaendelea kuhakikisha kwamba tunapeleka ikiwa ni pamoja na samani za ofisi za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya hivyo. Nitumie nafasi hii kuwasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini kwamba kipaumbele cha madawati, viti na meza kwa shule za sekondari ni kipaumbele cha juu katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu watekeleze wajibu wao wa kutenga fedha za mapato ya ndani za kutosha kwa ajili ya kuondoa pengo la madawati, viti na meza katika shule zetu za sekondari wakati Serikali inaendelea kuunga mkono juhudi hizo za halmashauri.

MWENYEKITI: Tunamalizia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini aulize swali lake.

Na. 414

Ujenzi wa Stendi ya Kisasa – Muleba

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga stendi ya kisasa katika Wilaya ya Muleba?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na stendi ya kisasa katika Wilaya ya Muleba. Aidha, ili kuhakikisha huduma ya stendi inapatikana. Kwa sasa Serikali inafanya uboreshaji wa stendi ndogo iliyopo Muleba Mjini, ili kuwezesha utoaji wa huduma ya usafiri na usafirishaji wa abiria katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga shilingi 200,000,000 ili kuweka lami nyepesi na mageti imara kwenye lango la kuingia na kutoka katika stendi hiyo. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, kwa sasa inatafuta eneo kubwa zaidi litakalofaa kwa ujenzi wa stendi ya mabasi ya kisasa. Mara Halmashauri itakapopata eneo la ujenzi, utaratibu wa kuanza maandiko na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi utaanza mara moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na nina swali moja tu la nyongeza. Je, katika ukarabati huu unaoendelea ambao utakuwa kwenye bajeti ya 2026/2027, unajumuisha na uwekaji wa taa za kumulika usiku? Kwa sababu stendi imezungukwa na maduka, lakini kuna giza kubwa pale.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya 2026/2027 kiasi cha shilingi 200,000,000 kimewekwa kwa ajili ya kufanya tathmini, lakini pia kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya matengenezo madogo ya lami nyepesi na mageti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, suala la taa ni muhimu. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muleba kuona uwezekano wa kupata bajeti ya nyongeza au ndani ya bajeti hii, ili waweze kuweka taa wakati stendi inatumika wakati tunasubiri ujenzi wa stendi ile nyingine katika eneo lingine. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Stendi ya Segerea Mwisho ni stendi kubwa sana yenye *route* ya magari zaidi ya 10 na kwa siku takribani magari 450 yanaingia na kutoka ndani ya stendi hii, lakini stendi hii imechakaa sana kiasi kwamba haiingiliki kabisa, pamoja na kwamba inaipatia kipato Serikali. Ningependa kufahamu, nini mpango mkakati wa Serikali kwa ajili ya kuifanyia marekebisho ili iendane na hadhi yake ilivyo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mpango wa Serikali katika stendi za mabasi ni kuhakikisha kwamba tunaziboresha barabara za kuingia na

kutoka, na pia kuweka *paving* au zege katika maeneo ya stendi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba stendi ya mabasi ya Segerea mwisho ni stendi muhimu kwa wananchi wa Jimbo la Segerea, pamoja na wananchi wa Dar es Salaam na Watanzania kwa ujumla. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Serikali Kuu, tutashirikiana kuhakikisha tunatafuta fedha na kufanya marekebisho ya stendi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii nimsisitize Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kulifanyia kazi suala hili kama kipaumbele kwa mazingira ya dharura, ili stendi iwe katika mazingira bora wakati tunaendelea na mipango ya muda mrefu ya kuiboresha kwa kiwango cha kudumu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Yannick Ndoinyo ajiandae.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Karatu ni mji wa kitalii na kuna uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanyika wa wadau katika sekta hiyo ya utalii, lakini hatuna stendi nzuri ambayo inakidhi mahitaji ya wadau na wananchi kwa ujumla. Je, ni lini Serikali itatujengea stendi ya kisasa katika Mji wa Karatu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Karatu ni mji wa kitalii lakini pia ni mji ambao una shughuli nyingi za kiuchumi kama ambavyo amesema Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mipango ya Serikali, ili kuboresha shughuli za usafiri na usafirishaji, moja ya kipaumbele ambacho tumetoa maelekezo kwa Wakurugenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu,

TAMISEMI tunasimamia kwa karibu, ni kuendelea kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa stendi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa zile stendi ambazo zinahitajika katika maeneo ya kimkakati, tunaandaa miradi ya kimkakati na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Karatu kwamba kupitia mapato ya ndani, waanze ukarabati na ujenzi wa stendi hiyo, lakini pia waandike kuleta Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI mapendekezo ya mradi wa kimkakati ili tuweze kuona namna nzuri ya kuboresha stendi katika Mji wa Karatu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yannick Ndoinyo.

MHE. YANNICK I. NDOINYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mji wa Wasso ni mji unaokua kwa kasi, uko ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na hauna stendi ya kisasa, hauna stendi kabisa na hauna soko. Ni nini mpango wa Serikali wa kujenga stendi ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia wasafiri na usafirishaji katika Mji wa Wasso?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro Mheshimiwa Yannick ameshawasilisha hoja hiyo mara kadhaa Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na tulishawasiliana na Halmashauri ya Ngorongoro kwamba, kupitia Baraza la Madiwani, pia kupitia halmashauri hiyo, waone uwezekano wa kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kwa awamu ili kuanza ujenzi na maboresho ya stendi katika Mji wa Wasso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Yannick kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaendelea kufuatilia kuona utekelezaji wa maelekezo ya Serikali, ili tuweze kuboresha huduma za usafiri katika Mji wa Wasso.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zacharia Paulo, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Motto maswali mafupi ya nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa *TACTIC* katika Mji wa Mbulu kwa ajili ya ujenzi wa stendi, soko na barabara?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mbulu uko kwenye mradi wa *TACTIC* wa uboreshaji wa miji awamu ya tatu na tayari tuko hatua ya mwisho ya usanifu, na Serikali yetu na Benki ya Dunia tuko kwenye mazungumzo ya kupata fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Zacharia Issaay wa Jimbo la Mbulu Mjini kwamba Serikali iko hatua nzuri sana kuhakikisha kwamba tunaanza utekelezaji wa mradi wa *TACTIC* kwa ajili ya ujenzi wa stendi, soko, na barabara katika Mji wa Mbulu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Mtwara una Manispaa ya Mtwara, Mikindani. Manispaa ya Mtwara, Mikindani ndiyo iliyobeba taswira ya mkoa, lakini Manispaa ile haina stendi ya kisasa mpaka leo. Ni lini Serikali itajenga stendi ya kisasa Mkoa wa Mtwara, Manispaa ya Mtwara Mikindani? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa stendi katika makao makuu ya mkoa ni kipaumbele cha Serikali. Ninafahamu katika Mji wa Mtwara

Mikindani hatuna stendi kubwa ya kisasa kwa maana ya stendi ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeweka mpango kwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, lakini pia Serikali Kuu, kuhakikisha kwamba tunaendelea kutenga fedha kwa awamu. Kwa ajili ya kwanza, kuboresha stendi zilizopo ili ziweze kuboresha huduma za usafiri. Pili, kuendelea kutafuta maeneo kwa ajili ya ujenzi wa stendi kubwa za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali italitekeleza suala hilo kwa sababu ni moja ya vipaumbele vya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani, atamalizia Mheshimiwa Mecktridis Mdaku.

MHE. ENG. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mgwashi, Kata ya Mgwashi, Bumbuli ni miongoni mwa miji ya kiuchumi inayokua kwa haraka sana, lakini hatuna stendi kabisa na magari yaliyopo yanapaki barabarani. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu kupata stendi katika mji huu ili kuweza kuinua uchumi zaidi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, kwamba kwa kuwa ujenzi wa stendi ni kipaumbele cha Serikali, lakini ni mahitaji ya wananchi. Nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bumbuli kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuboresha na kujenga stendi. Wakati huo huo wawasilishe maombi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili tuweze kuona namna nzuri ya kushirikiana nao katika ujenzi wa stendi katika Halmashauri ya Bumbuli, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mecktridis Mdaku.

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Jimbo la Malinyi lina fursa nyingi za kiuchumi, lakini hadi sasa ujenzi wa stendi ya wilaya umekuwa ukisuasua. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha inakamilisha ujenzi huu ili stendi ianze kufanya kazi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Malinyi na Jimbo la Malinyi ni moja ya halmashauri mpya, na ina uhitaji mkubwa sana wa miundombinu ikiwemo ujenzi wa stendi ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Malinyi kwamba, katika mipango yetu ya Serikali kupitia fedha za Serikali Kuu na fedha za mapato ya ndani ya halmashauri, tutahakikisha tunaweka kipaumbele kuanza maboresho na ujenzi wa stendi katika Halmashauri ya Malinyi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Sasa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, Mbunge wa Kalambo aulize swali lake.

Na. 415

Kukamilisha Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Kalambo

MHE. EDIFONSI J. KANONI aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilayani Kalambo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali Na. 415 la Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kalambo ni miongoni mwa mpango wa Serikali wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi 65 katika Wilaya 64 na Mkoa mmoja wa Songwe. Utekelezaji wa mpango huu unafanyika katika Wilaya na Mkoa ambao hauna Chuo cha *VETA* ili kuhakikisha fursa za mafunzo ya ufundi stadi zinasogezwa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kalambo ambacho kinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026. Hadi sasa, Serikali imeshatumia jumla ya shilingi bilioni 1.1 kati ya shilingi bilioni 1.6 zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi huu. Ujenzi umefikia 73% ya utekelezaji wake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edifonsi Kanoni.

MHE. EDIFONSI J. KANONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri kwa niaba ya Serikali. Hata hivyo, niseme, Jimbo la Kalambo, hicho Chuo cha *VETA* tunakisubiri sana kwa hamu, hasa vijana ambao ni zaidi ya 30,000 ambao wapo katika Jimbo la Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utekelezaji wa Chuo cha *VETA* umefikia 73%, Serikali inatuahakikishiaje kwamba ikifika mwezi wa Nane, au mwezi wa Tisa, hicho Chuo cha *VETA* kitakuwa kimekamilika na vijana waanze kujiandaa kujiunga na hicho Chuo cha *VETA* Wilaya ya Kalambo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze

Mheshimiwa Joackim kwa ufuatiliaji wake. Amefika mara kadhaa ofisini kuulizia kuhusu chuo hiki cha Kalambo. Nimhakikishie, kwamba 27% iliyobaki tunaenda kumalizia mwezi Septemba, 2026 kama tulivyoji-*commit* kwenye bajeti yetu ya Wizara ya Elimu, na tulisema kwamba fedha zimeshaingia. Mipango ya kugawanya fedha hii inaendelea. Kwa hiyo, vyuo hivi vinaenda kumalizika katika mwaka huu 2026, mwezi Septemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla Wabunge wengine hawajasimama kuulizia vyuo hivi. Vyuo hivi vinajengwa kwa pamoja, yaani *at per*. Vyote ujenzi wake unaenda sambamba. Kwa hiyo, fedha zinavyoingia, zinagawanywa kwa vyuo vyote ambavyo vinajengwa. Kwa hiyo, kabla Wabunge wengine hawajasimama, niwahakikishie kwamba *by September, 2026* vyuo hivi vinaenda kukamilika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Maelezo ya Serikali kwenye suala la *VETA* yamejitosheleza. Kwa hiyo, ninaamini kilichozungumzwa na Serikali ndiyo kitakachofanyika na wameshasema maeneo ya wilaya ambayo hakuna, na mikoa yote itajengwa *VETA* kwa ajili ya watoto wetu. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, aulize swali lake. Mheshimiwa Cecilia.

MBUNGE FULANI: Kwa niaba yake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia, nilishakutaja.

Na. 416

Kukamilika kwa Kivuko cha *MV* Kome

MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. ERIC J. SHIGONGO aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kivuko cha *MV. Kome* cha kutoka Nyakaliro hadi Kome?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* katika mwaka wa fedha 2025/2026 unaendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vivuko mbalimbali nchini. Mojawapo ya miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa kivuko kipya cha Nyakaliro kwenda Kome ambacho ni *MV. KOME III*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu kwa sasa umefikia 90% na unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2026 kwa mujibu wa mkataba. Aidha, kazi zilizobakia ambazo mkandarasi anaendelea na utekelezaji wake ili kukamilisha mradi huu ni usimikaji wa mifumo ya umeme, vifaa vya usalama na mawasiliano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imeeleza kwamba kazi hii itakamilika tarehe 30 Juni 2026, na kwa kuwa katika majibu mmekiri kwamba bado kuna usimikaji wa mifumo unaendelea kufanyika au bado haujaanza kufanyika, je, usimikaji wa mifumo hii na hiyo kazi iliyobaki yote itakamilika tarehe 30 Juni, 2026? Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Cecilia Paresso, kwamba tunategemea tutakamilisha kama tulivyoahidi mwezi Juni; na kwa kuwa vifaa vipo, tunaamini kazi hii itakamilika katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati kivuko hiki kinatengenezwa kikamilike, hili eneo lilikuwa na kivuko kidogo. Ile *MV Mwanza* sasa hivi iliyokuwa ina-*operate*, iliyokuwa inafanya kazi pale Kigongo-Busisi, sasa hivi imeenda kule kufanya kazi. Kwa hiyo, tunaamini tuna vivuko kama vitatu katika Ziwa Victoria ambavyo vilikuwa vinafanya kazi. Kwa hiyo, tutarahisisha sana, pamoja na kivuko hicho kitakuwepo pale, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Arif Premji, swali la nyongeza.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kivuko cha *MV* Kilambo kilichopo Kata ya Tangazo, Kijiji cha Kilambo ndiyo kinafanya huduma ya kutoa usafirishaji baina ya Tanzania na Msumbiji, na sasa hivi kipo kwenye ukarabati. Je, lini ukarabati huo utaisha ili huduma hiyo irejee? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vitu vikubwa ambavyo Serikali hii ya Awamu ya Sita imefanya chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni vivuko. Ninadhani amevunja rekodi kutengeneza vivuko sita vipya kwa wakati mmoja, lakini pia vivuko vyote ambavyo vilikuwa na changamoto viko kwenye ukarabati mkubwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kivuko hicho ukarabati wake utakamilishwa ili kiweze kutoa huduma katika kile kivuko cha Mto Ruvuma.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chacha Wambura.

MHE. CHACHA M. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Mji wetu wa Geita unategemea sana mazao yanayotokea kule Nzera, na barabara imeanza kujengwa kutoka Nzera kuja Geita, lakini ukiangalia bajeti iliyopangwa imeishia hapo katikati. Sasa ninapenda kujua, Serikali ina mpango gani ili kuiunganisha ile barabara kutoka Geita mpaka Nzera iwe lami, na watu wa Geita waweze kupata mazao kirahisi kutokea kule Nzera?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Mbunge aweze kuuliza swali tena ili niweze kumwelewa vizuri. Ni kama ameongelea mambo ya barabara, sijamsikia vizuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chacha, ninaomba uulize kwa ufupi na *straight forward*.

MHE. CHACHA M. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza, Geita tunategemea sana mazao pale mji wetu kutoka kule Nzera na Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kule Nzera kuna bajeti walipanga ya kuanza ujenzi wa kipande cha barabara kutoka kule kuja Geita, lakini bajeti ambayo ilipangwa imeishia hapo katikati, kuna kipande ambacho hakijaguswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kufahamu, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba mnaunga hiki kipande cha kutoka Geita na kile cha Nzera, ili basi lami iweze kutoka Geita mpaka Nzera na watu wa Geita waweze kusafiri kwa urahisi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chacha, unazungumzia barabara ama kivuko? Kwa maana hapa tuna swali la kivuko. Kwa hiyo, kama ni swali la barabara itabidi upeleke kama swali la msingi.

Mheshimiwa Waziri, ninafikiri ni swali la barabara, kwa hiyo, ninakushukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 417

Ujenzi wa Barabara ya Holili – Tarakea

MHE. ZUENA A. BUSHIRI aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa barabara ya Holili – Tarakea?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajenga barabara ya Holili – Tarakea (km 52.8) kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa, ujenzi kwa kiwango cha lami wa kipande chenye urefu wa mita 680 katika barabara hii umekamilika. Aidha, kwa kipande cha Ikuini – Kirongo Chini (km 10) Mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, swali la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mkandarasi ameshasaini hizo kilometa 10, je, ni lini Serikali italipa fedha hizo ili mkandarasi aanze kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Barabara hii ya Rombo ni barabara ya uchumi, inapitisha malori mengi sana yanayobeba makaa ya mawe kwenda nchi jirani ya Kenya na malori mengi sana ya biashara. Pia barabara hii ni barabara ya usalama, na iko katika mpaka wa Kenya na Tanzania. Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya haraka kulipa fedha ili barabara hii ikamilike kwa umuhimu wa mahitaji hayo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumeshasaini mkataba, na mkandarasi. Mkandarasi huyu ni mkandarasi mzawa, ambaye amefanya vizuri sana katika kazi zake ambazo Serikali imekuwa inampa. Kwa hiyo, tuna uhakika, kazi hii pia ataifanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kusaini, tayari tunafanya maandalizi ya kumlipa fedha ya awali ili aweze kuanza kutekeleza huu mradi, hizo kilometa 10 ambazo tutaanza nazo kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, na nimhakikishie kwamba swali lake hili siyo mara ya kwanza kuliuliza, amekuwa analiuliza mara kwa mara kuhakikisha kwamba hii barabara inajengwa. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, wao wanaita *Lower Road*, tunaamini kwamba magari mengi ya makaa ya mawe, pia magari makubwa yatapita huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na barabara ambayo inatumika ya sasa, yenye miinuko na kona, lakini pia ni nyembamba, hii ni barabara ambayo inaambaamba na mpaka wa Kenya, na ndiyo maana Serikali imeamua, kwa sababu ni moja ya kipaumbele kujenga barabara za ulinzi kwa kiwango hicho, tutahakikisha kwamba tunaijenga na kuikamilisha yote, na hii tu ni awamu ya kwanza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante sana, ninakushukuru kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Ujenzi. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 418

Kulinda Watoto katika Mazingira Hatarishi

MHE. MARYAM AZAN MWINYI aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kulinda Watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwemo Watoto yatima na wenye Ulemavu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninapenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya Pili (MTAKUWWA II – 2024/2025 - 2028/2029) ambapo katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026: -

(i) Wizara imesajili jumla ya Makao ya Watoto 29 na kuhuisha leseni za Makao 39 yenye jumla ya watoto 855 (ME 441 na KE 414) hivyo kufanya jumla ya Makao 433 yenye watoto 16,130 (ME 8,138 na KE 7,992);

(ii) Jumla ya vituo 809 vya kulelea watoto wadogo mchana vimesajiliwa na vinahudumia watoto 27,270;

(iii) Kampeni ya kuokoa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani imefanyika na jumla ya watoto 5,353 walitambuliwa na kati yao 5,007 wameunganishwa na familia zao, 256 wanapatiwa hifadhi na matunzo katika makao ya watoto, 65 wako kwa walezi wa kuaminika, 25 wameunganishwa na Vyuo vya Ufundi Stadi na 17 wamehitimu programu mbalimbali na kuwezeshwa kujitegemea;

(iv) Jumla ya wahudumiwa 1,300 walipatiwa huduma katika Nyumba Salama 18 zinazohifadhi manusura wa vitendo vya ukatili na wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu; na

(v) Jumla ya Madawati 14 ya Huduma za Ustawi wa Jamii yameanzishwa katika vituo vya usafirishaji ili kushughulikia changamoto za watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi.

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya

nyongeza. Pamoja na hatua nzuri zinazochukuliwa na Serikali, bado kuna wimbi kubwa la watoto wa mitaani. Je, Serikali inashirikiana vipi na sekta binafsi katika kutatua suala hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Baadhi ya watoto mitaani, wana walezi na wazazi. Je, Serikali inawawajibisha vipi wazazi au walezi kuhakikisha kwamba hawakwepi majukumu yao hasa kwa watoto wenye ulemavu? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo mawili ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Maryam Mwinyi kwa swali lake zuri. Hakika ni mama anayejali watoto na amewakilisha wanawake wote wa Tanzania vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inashirikiana kwa karibu sana na sekta binafsi na kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, tayari tuna mahusiano na makao ya watu binafsi zaidi ya 433. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Gwajima ameweza kukutana na kushirikiana na kuweka rasmi Umoja wa Makao ya Watoto Tanzania (UMAWATA) na Mwenyekiti wake ni Ndugu Evans Tegete, kaka ambaye amekuwa kwa miaka mingi anashiriki kuona kwamba, anatunza watoto wa mitaani, watoto walio katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Gwajima yeye kwa binafsi yake ameweza kufanya kwa jitihada kubwa sana, lakini na sisi sote kama Wizara na idara maalumu inayoshughulika na watoto, tunaendelea kuwa karibu kabisa na makao ya watu binafsi. Kwa sababu, sisi kama Serikali tunayo tu makao mawili hapa Dodoma pale Kikombo na Dar es Salaam (Kurasini), lakini wenzetu watu binafsi wana makao 424. Kwa hiyo, ushirikiano ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wazazi ambao hawatimizi wajibu wao, hawa tunaendelea kushughulika nao kwa namna mbalimbali. Kuna wazazi ambao kupitia ugomvi wao wanapelekea madhara kwa watoto. Wamekuwa wakiitwa mara

kadhaa na Maafisa Ustawi wetu, wanashauriwa namna njema ya kuhakikisha kwamba kila mzazi kwa pande zote mbili anatimiza wajibu wake, hivyo kuhakikisha watoto wanapata matunzo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa wale wazazi ambao wanakuwa wagumu, basi sheria inafuata mkondo wake na wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria na ikibidi hata Mahakamani ili huyu mzazi aweze kutimiza majukumu yake kwa nguvu ya sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maryam Yahya, Mheshimiwa Lucy Kombani ajiandae.

MHE. MARYAM U. YAHYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa, kuna mikoa mingine hatuoni kabisa tatizo la watoto wa mitaani, lakini bado Mkoa wa Dar es Salaam unasumbuliwa na tatizo hili, bado kuna watoto mitaani, je, Serikali imejipangaje kuondoa kabisa tatizo la watoto wa mitaani katika Mkoa wa Dar es Salaam? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri. Kwanza Mkoa wa Dar es Salaam ni mkoa ambao unapokea magari kutoka mikoa mingi, na hawa watoto wengine wanaingia kutoka nchi mbalimbali kwa kufuata *green pasture* ambayo Tanzania ipo. Mazingira rafiki ambayo nchi yetu inayo, watoto wanatoka nchi jirani pia. Hivyo, tumeweka madawati ambayo Maafisa Ustawi wako pale kwenye vituo vyetu vya mabasi vikubwa vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna ushirikiano na wale wa wasifirishaji hata wale wapiga debe wa mle ndani ya stendi wanatupa ushirikiano sana. Kwa hiyo, tunawachukua, tunaongea nao na Maafisa Ustawi wakishirikiana na wenzetu wa Uhamiaji, tunawarejesha kwenye nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliotoka mikoani pia tunawahoji na wanatoa ushirikiano, wanatupa namba za wazazi,

wanatoa ramani ya nyumbani Maafisa Ustawi wetu wanawarejesha kule walipotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndugu zangu niseme tu, kwa umoja wetu tutaendelea kufanikisha ili kuhakikisha kwamba, hawa watoto wote wanaozurura mitaani wanaweza kurejea kwenye makazi ya familia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Kombani.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na changamoto ya mabinti walemavu wa viungo au wenye changamoto ya akili kupatiwa ujauzito na watu wasiojulikana. Je, ni upi mwongozo wa Serikali kuhusu changamoto hii? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri umemwelewa? Watoto ambao wana mahitaji maalumu kwa maana ni wenye ulemavu, ambao wanapata ujauzito na watu wasiojulikana.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wenye ulemavu ambao wako kwenye makao maalumu, Maafisa Ustawi wa Jamii wamepewa mafunzo maalumu ya namna ya kuwahudumia wenzetu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mlemavu, halafu yuko mtaani, Wizara ya Waziri Mkuu ambayo inashughulikia walemavu, kwa baba yangu Mheshimiwa Prof. Kabudi, na Naibu Waziri, Mheshimiwa Nderiananga; mmewahi kumwona Mheshimiwa Nderiananga akifuatilia kwa karibu, kuhakikisha anawanusuru hawa wenzetu wenye ulemavu. Alifika hatua hata ya kuwachapa viboko wale ambao wanawatumia vibaya wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya ni kuona kwamba tunawarejesha na tunahakikisha kwamba tunawatendea haki na wao wanapata huduma bora. Majibu ni hayo kama nimeelewa vizuri swali lake.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge suala hili siyo la Serikali peke yake ni suala la Kitaifa. Wazazi tunawajibika; akina baba, akina mama, jamii nzima na hata sisi Wabunge tunawajibika katika maeneo yetu kuhakikisha kwamba masuala haya ya watoto kuwa wanaishi mitaani, siyo ya Serikali peke yake. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, aulize swali lake.

Na. 419

Kuanza kwa Skimu ya Umwagiliaji Likokona na Nangomba

MHE. YAHYA A. MHATA aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Likokona na Nangomba utaanza ikizingatiwa kuwa Mkataba ulishasainiwa?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Likokona na Nangomba na zilizoko Wilaya ya Nanyumbu kwa ujumla hakuna skimu ya umwagiliaji iliyosainiwa mkataba wa ujenzi. Katika kata hizo, kuna mradi wa uchimbaji wa visima pekee. Kata hizo ni miongoni mwa maeneo ambayo Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imewekeza kwa kuchimba visima viwili virefu vya umwagiliaji kwa ajili ya kuhudumia wakulima wadogo wanaolima mazao ya mbogamboga na nafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Nangomba, kisima kimechimbwa, na hatua inayofuata ni uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Kisima hicho kina uwezo wa kutoa maji kiasi cha

lita 3,000 kwa saa na kitanufaisha wakulima wasiopungua 80 katika Kijiji cha Nangomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Nanyumbu, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu ya Lukula kupitia Mradi wa Bonde la Mto Ruvuma *(Ruvuma Basin)* umekamilika na sasa Serikali inatafuta fedha ili kukamilisha ujenzi wake. Ujenzi wa Skimu ya Lukula ukikamilika utaweza kumwagilia eneo la hekta 2,186 na kuwanufaisha wakulima wa Vijiji vya Lukula, Masuguru na vijiji jirani. Pia, kuna mradi wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bwawa katika skimu ya Masuguru kupitia Mradi wa Mabwawa Matano. Mradi huu unaendelea na sasa umefikia 60%.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Mradi huu wa uchimbaji wa visima virefu kwa ajili ya umwagiliaji ulianza mwaka 2024/2025 na visima vile vimekamilika. 2025/2026, Bunge lako hili Tukufu lilipitisha bajeti kwa ajili ya Wizara hii ya Kilimo. Je, ni sababu zipi za msingi ambazo zimekwamisha uwekaji wa miundombinu katika maeneo haya ili wananchi waweze kufaidika na mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Skimu ya Umwagiliaji ya Lukula, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika. Hatua inayofuata ni utafutaji wa fedha. Moja za hatua ni utafutaji wa fedha; ni kupitia Bunge hili Tukufu na Bunge hili limepitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana maneno gani ya faraja kwa wananchi wa Jimbo langu baada ya kupitisha bajeti yake? Lini watanufaika kwa kupata fedha na kuweza kutekeleza mradi huu?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Ally Yahya Mhata Mbunge wa Nanyumbu kwa maswali yake ya msingi kabisa kwa wananchi wake. Nina majibu ya uhakika kabisa. Moja, sababu zilizocheleweshwa kumalizia ufungaji wa pampu pamoja na

kumalizia ile miundobinu kwa ajili ya wananchi kunufaika ni kwamba, tulichelewa katika *procurement* ya vile vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumefanya hiyo *procurement* ya vifaa vyote kwa ujumla kwa ajili ya visima vyote ambavyo tume itaendelea kuvichimba, zikiwemo zile pampu kubwa ambazo tunaagiza kutoka India na ziko njiani. Ninaamini kwamba, zitafika ndani ya muda muda mfupi. Kwa hiyo, vikishafika tu, cha kwanza ni kwenda kupeleka katika maeneo ambayo tulishachimba, pamoja na yale ambayo tunaendelea kuchimba. Kwa hiyo, wawe na uhakika kabla ya mwisho wa mwaka huu 2026, tutakuwa tayari tumeshaweka miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Skimu ya Lukula, ni kweli tumemaliza hatua zote. Hatua inayofuata ni kutangaza ili tupate mkandarasi. Sasa hivi tuna *assurance* ya Wizara ya Fedha kuihakikishia tume kwamba, kila mwezi itakuwa inatoa shilingi bilioni 25 kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa, kwa *trend* hiyo ambayo Wizara ya Fedha wameweka hiyo *commitment* kwetu, maana yake tutakuwa na uhakika, moja, kumalizia miradi ambayo ilikuwa imeanza. Pili, kulipa wakandarasi ambao tumeshasaini nao mikataba ili wafanye. Tatu, kuanzisha miradi mipya ambayo tayari tumeshaiahidi, na Serikali inatarajia kuikamilisha kwa wakati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Subira Mgalu. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe jiandae.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo letu la Bagamoyo lina skimu moja tu ya umwagiliaji ambayo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo changamoto ya uchakavu wa mashine ya kupeleka maji mashambani, na Meneja wa Umwagiliaji wa Mkoa alitutembelea na kutuahidi kwamba, Serikali

italeta mitambo mingine, je, Serikali inatupa ahadi gani wasaidie wakulima katika skimu hii ya umwagiliaji wa Bagamoyo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mbunge ni kweli na Serikali iliahidi kwamba, katika Skimu ya Bagamoyo tutapeleka mashine, na taratibu za Serikali Mheshimiwa Mbunge anazifahamu, ikiwemo kufanya *procurement* kwa ajili ya kununua. Kwa hiyo, tupo katika hizo hatua, na tukishamaliza, wananchi wa Bagamoyo chini ya Mbunge wetu, dada yangu Mheshimiwa Subira Mgalu, tutapeleka mashine hiyo na itafanya kazi kama ambavyo imekusudiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilituahidi kutujengea Skimu ya Mbatakero na Mkalama, na pale Mkalama tayari wananchi wameunda umoja wao na wametenga ekari 80 kuwa na shamba la mfano kama *BBT*. Je, lini sasa Serikali italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa skimu hii? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru kaka yangu Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, na ninafahamu jambo hili tumeshalizungumza mara kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa, tulikuwa na *challenge* kidogo ya kifedha, lakini baada ya kupata hii *commitment,* maana yake sasa tutakuwa na nafasi ya kupeleka fedha katika maeneo yote ambayo tulishaahidi na ambayo tayari yalishafanyiwa *feasibility study,* na yale ambayo tayari wakandarasi wako *site,* lakini bado wamekuwa wakisuasua. Kwa hiyo, uko katika mpango wa Serikali.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Kilimo.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia sasana Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Mvomero aulize swali lake.

Na. 420

Kuanguka kwa Nguzo za Umeme Mgeta

MHE. LUCY D. S. KOMBANI K.n.y. MHE. SARA M. ALLY aliuliza:-

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya kuanguka kwa nguzo za umeme katika Tarafa ya Mgeta?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa changamoto ya kuanguka kwa nguzo za umeme katika baadhi ya maeneo ya Tarafa ya Mgeta kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo maeneo hayo kukumbwa na mvua nyingi, uwepo wa udongo usiohimili pamoja na uchakavu wa baadhi ya nguzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kubadili nguzo chakavu kwa kuweka nguzo imara zaidi, zikiwemo nguzo za zege na chuma, pamoja na kuimarisha misingi ya nguzo katika maeneo yenye udongo laini. Aidha, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya umeme ili kubaini na kushughulikia changamoto hizo mapema pindi zinapojitokeza. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lucy Kombani.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Wizara, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la kubadilisha zile nguzo za kawaida na kuweka nguzo za zege ambazo ni imara zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kuanguka kwa nguzo hizi kunachangiwa sana na shughuli za kibinadamu hasa kilimo, je, Wizara ina mkakati gani kuhakikisha wananchi wanapewa elimu ya kutosha jinsi ya kutunza miundombinu hii ya umeme? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa mwenyekiti, kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Lucy kwa kumwakilisha Mheshimiwa Sara Msafiri, Mbunge wa Mvomero, lakini pia kwa kuendelea kufuatilia kuhakikisha Jimbo hili linakuwa na nguzo imara ambazo zitasaidia kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kujibu swali lake la kwanza kuhusu lini Serikali itakamilisha ujenzi wa nguzo za zege ili kuweza kuongeza uimara katika *supply* ya umeme kwenye Jimbo hili. Serikali kupitia Wizara ya Nishati imetenga bajeti maalumu kuhakikisha kwamba, tunabadilisha nguzo zote za miti hasa katika maeneo ambayo yana unyevunyevu au yana shughuli mbalimbali za kibinadamu, na hilo tunaendelea kulitekeleza kwa kadiri ambavyo bajeti inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kuhusiana na shughuli za kibinadamu, Mheshimiwa Mbunge, bahati nzuri ni mwakilishi wa wananchi na tunajua amekuwa pamoja na sisi kuhakikisha tunawahimiza wananchi waachane na matumizi mabaya ya ardhi, kama kuchoma moto mashamba, jambo ambalo linaathiri sana nguzo zetu za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kutoa elimu, lakini niendelee kuwasisitiza Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kutoa elimu kwa sababu nguzo hizi zina gharama kubwa na

zinapoungua zinaleta changamoto kubwa sana ya usambazaji wa umeme, na kusababisha umeme kukatika, lakini pia wananchi kupata hasara kubwa katika maeneo yao. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pius Yanda.

MHE. PIUS Z. YANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Ni lini, Serikali itajenga kituo cha kupoozea umeme katika Wilaya ya Buhigwe ili wananchi waweze kupata umeme wa uhakika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ni swali la kupoozea umeme. Kama unalo jibu sawa; kama huna, basi Mheshimiwa atalileta kama ni swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, na uzuri hapa ninayo orodha ya vituo vya kupooza umeme vinavyojengwa katika nchi yetu kwa awamu ya pili na awamu ya tatu. Nimtoe wasiwasi kwamba katika jimbo lake pia ni moja kati ya sehemu ambazo ni za kipaumbele kujenga *substation* au kituo cha kupooza umeme ili kuweza kusaidia kupata umeme wa uhakika katika eneo hilo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Simon Lusengekile.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wawekezaji ambao wanawekeza katika viwanda na wamekuwa wakipata shida sana kupelekewa nguzo za umeme pamoja na transfoma. Hawa wawekezaji kama wana uwezo wa kupeleka nguzo na transfoma katika maeneo ya viwanda, je, Serikali inaweza kuingia nao mkataba ili sasa wanapokuwa wamemaliza kazi hiyo waweze kukatana kwenye malipo ya luku?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, umemwelewa? Majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wapo wawekezaji ambao wamewekeza fedha nyingi katika miradi mbalimbali na wanapata changamoto ya umeme, kwa

sababu wakati mwingine kunakuwa kuna changamoto za kibajeti kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumweleza Mheshimiwa Songe kwamba, sisi Serikali tunao utaratibu kwa mwekezaji ambaye yuko tayari kuvuta umeme kwenye eneo lake na tunaweza kufanya mikataba maalumu ya kuhakikisha kwamba gharama alizotumia kuweka umeme kwenye eneo lake au kupeleka transfoma zinakatwa taratibu katika malipo yake ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie jukwaa hili kutoa maelekezo kwa mameneja wote wa *TANESCO* wa mikoa, kuangalia maeneo ambayo kuna wawekezaji wakubwa na kuhakikisha kwamba, wawekezaji hao wanapata tija ya miradi yao kwa kupata umeme kwa wakati. Hivyo, waende wakazungumze nao na watengeneze mazingira mazuri ya kuhakikisha hakuna mwekezaji ambaye ameweka fedha zake katika mradi halafu anashindwa kufanya uzalishaji, kwa sababu ya kukosa umeme. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwita Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Tarime pale mjini ndiyo Makao makuu ya Wilaya, kwa hiyo, shughuli zote za Kiserikali, za kibiashara, wageni kutoka Kenya, na watalii wanakuja kupumzika pale, lakini kwa muda ambao Mheshimiwa Naibu Waziri amepata hapo kujibu maswali, umeme unakatika zaidi ya mara tano, kwa muda huo tu. Lini hii shida itaisha pale Tarime Vijijini? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze pia Mheshimiwa kwa kufuatilia hali ya umeme katika Jimbo lake la Tarime Vijijini. Ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge, sijajua pale kuna changamoto ya nini? Mara baada ya kuahirisha Bunge hili, nitafanya ziara katika Jimbo la Tarime Vijijini ili kujua changamoto ni nini, na mimi nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba changamoto hiyo

tunaitatua na Wanatarime wanafanya kazi kwa utu wenye tabasamu.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, aulize swali lake.

Na. 421

Kupeleka Umeme Vitongoji 169 Bunda

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Vitongoji 169 vya Kata ya Ketare, Mihingo, Nyamang'uta, Mugeta, Salama, Hunyari, Mnyago na Nyamuswa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa, Jimbo la Bunda lina vijiji vyenye vitongoji vingi na jiografia ngumu sana. Pamoja na hayo, Serikali imefikisha huduma ya umeme kwa 86.4% katika vitongoji vya Jimbo la Bunda. Aidha, vitongoji vilivyosalia vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili (B) yaani *(Hamlet Eletrification Project Phase IIB – HEP IIB)* ambao utekelezaji wake umeanza mwezi Januari, 2026 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2029.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali kupitia *REA,* imekamilisha upimaji, yaani *survey* na usanifu wa kina na kuanza ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme katika vitongoji hivyo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara, wamejitahidi sana, lakini ninawashukuru watu wa *REA,* ninamshukuru Meneja wangu wa Bunda, wanafanya vizuri, wamejitahidi kupeleka baadhi ya vitongoji. Sasa hivyo 169 kuna vitongoji 45 ambavyo vimeandikwa tayari, Mheshimiwa Waziri anavyo, wewe unavyo, kila mtu anavyo, pale kwenye *REA*. Ni lini sasa Wizara itapeleka umeme kwenye vitongoji 45?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali la pili. Swali la msingi amejibu vizuri. Vitongoji vya Bunda vipo *scattered* sana na Bunda ni eneo ambalo kijiji kimoja kina vitongoji 11, Tanzania nzima haipo hivyo. Sasa, ni lini atakuja Bunda tumtembeze kwenye maeneo hayo naye ajionee hiyo hali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Getere kwa swali lake zuri, lakini pia, kwa kufuatilia miundombinu ya umeme katika eneo lake. Kama nilivyotoka kusema katika majibu yangu ya awali, sisi Wizara ya Nishati, tunatambua kwamba Jimbo la Mheshimiwa Getere lina jiografia ngumu. Ni jimbo ambalo unakuta kijiji kimoja kina vitongoji vingi zaidi ya 10, jambo ambalo *of course* inaonekana kwamba kasi ya upelekaji wa umeme sio kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, lengo la Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha mpaka inapofika mwaka 2030 vitongoji vyote viwe vimepata umeme na sisi wasaidizi wake hatupo nyuma. Ndiyo maana mwezi Februari, 2026 tumeanza na vijiji 9,000 na kuhakikisha kwamba, tunafikia azma hiyo kwa ari hiyo hiyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, vitongoji vyake vyote vitapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, kazi yangu kubwa ni kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Nishati kutatua changamoto za wananchi kupitia wawakilishi wao ambao ni Waheshimiwa Wabunge. Niko tayari kwenda kwenye Jimbo la Bunda kuangalia changamoto iliyoko pale na nitashirikiana na

Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba tunafikisha umeme. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ado Shaibu.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakiri kwamba, Serikali imemlipa mkandarasi wa kituo cha kupozea umeme pale Tunduru, hatua ambayo inapaswa kupongezwa sana, lakini ninataka kupata *assurance* ya Serikali, ni lini sasa mradi ule wa Kituo cha Kupooza Umeme Tunduru utakamilika na kuleta faraja, siyo kwa Wanatunduru tu, bali kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tunatoka Kanda ya Ziwa tunaelekea Tunduru, kama una jibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Ado Shaibu, kwanza kwa kuishukuru Serikali. Anasema usiposhukuru kwa kidogo hata kwa kikubwa pia, huwezi kushukuru. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa kwa kutushukuru, kwa kumlipa mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli, ule mradi ulikuwa unasuasua kwa sababu tulikuwa hatujapeleka fedha bado. Nimtoe wasiwasi, Mheshimiwa Mbunge, lengo la Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha Mikoa ya Kusini, Mtwara na Lindi, inaingia kwenye Gridi ya Taifa na lengo hilo tunalitimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi, Wizara ya Nishati, tunatamani unapofika mwezi wa Sita mwishoni, wawe wameingia kwenye Gridi ya Taifa. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi kabisa kwamba, kituo kile kitakamilika, tunakwenda vizuri na tutakuja kusherehekea pamoja kuwasha na kuwaangazia Wanatunduru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Josephine Kapoma.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa Morogoro wanashukuru sana kwa jitihada zinazofanywa na Wizara yako. Sasa tuna kata moja ambayo ipo Morogoro Manispaa, Kata ya Mlimani, tumeomba umeme kwa

muda mrefu katika mitaa iliyobakia mitano, tumefanikiwa mtaa mmoja, lakini bado mitaa minne; Mtaa wa Kisosa, Tulo, Choma na Chagule. Sasa tunataka kujua, ni lini wakazi hawa wa Manispaa nao watapata huduma hii ya umeme? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, tunaelekea Morogoro.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Josephine, Kapteni wangu, kwa kufuatilia kuhusiana na suala la umeme katika mitaa aliyoitaja. Ninamtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya kumaliza kujibu maswali hapa, Meneja wa *TANESCO* atakwenda kufanya *survey* na tutakapohitimisha bajeti hii, tutapeleka umeme katika mitaa hiyo. Mheshimiwa Mbunge ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Tunamalizia na Mheshimiwa *Eng*. Kija Ntemi na Mheshimiwa Sigrada Mligo.

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza ninawapongeza, wanafanya kazi nzuri katika Wizara yenu ya Nishati. Naibu Waziri pamoja na Waziri wake, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, waliagizwa kupeleka umeme katika migodi, na hii ni pamoja na Jimbo la Katoro, kwani kuna migodi mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli umeme umepelekwa, lakini changamoto ni *transformer* zile walizozipeleka, ni ndogo. Je, ni lini watabadilisha zile *transformer* ndogo, ili kuwasaidia wachimbaji wetu kufanya kazi kwa wakati kwa muda mrefu, wapate *transformer* kubwa? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru kaka yangu Mheshimiwa Kija Ntemi, kwanza kwa kunipa pongezi. Ninamshukuru sana. Pia, nami ninakupongeza, naye amekuwa mjumbe mzuri wa Kamati. Wanakamati wametushauri vizuri kwamba tutenge fedha kwa ajili ya kupelekwa kwenye migodi midogo midogo kwa sababu, umeme

siyo kwa ajili ya kuwasha taa peke yake, lakini pia, unatakiwa kuwa kichocheo cha uchumi na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, katika migodi ambayo ina *transformer* ndogo, ambayo inashindwa kusukuma umeme wa kutosha kuendesha mitambo, tutabadilisha *transformer* zile na kuhakikisha tunaweka zinazoweza kuhimili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamweleza Mheshimiwa Mbunge, kwa uhakika, kwenye bajeti hii mmetupitishia zaidi ya shilingi bilioni 20, kwa ajili ya kupeleka umeme kwa wachimbaji wadogo wadogo. Tuko tayari kutekeleza. Wale Waheshimiwa Wabunge ambao wana mahitaji katika maeneo ya migodi midogo ambao wanadhani kwamba tija haipatikani kwa sababu ya *transformer* kuwa ndogo, niko tayari kupokea maoni yao na kufanya marekebisho. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Njombe, *especially* Jimbo la Njombe Mjini kuna maeneo yamerukwa, kwa maana ya kwamba, meneja amesema kuna *phase* inakuja. Ninataka kujua, yale maeneo ambayo yamerukwa na mfumo wa umeme, lini hiyo *phase* ambayo meneja amesema, watakuja na *phase* nyingine itaanza? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Njombe.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *to be precise,* nitaongea na Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuniambia maeneo hayo yaliyorukwa, lakini ninamhakikishia, hakuna atakayepitwa na fursa ya kupata umeme kwenye nyumba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutazungumza baadaye, ili tuweze kujua maeneo hayo ni yapi na nitamwelekeza Meneja wa *TANESCO* kwenda kufanya *survey* na kuweza kupeleka mradi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Hongera sana kwa kuweza kuelewa maeneo mbalimbali ya nchi yetu yanayohitaji umeme na matatizo yake.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umeishia hapo na sasa tuna matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Spika; tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Spika wetu ambaye ni Mheshimiwa Mbunge pia. Hawa ni wafanyabiashara wa Kariakoo kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na viongozi wao, Ndugu Severine Mushi ambaye ni Mwenyekiti; Ndugu Mfaume Mfaume - Makamu Mwenyekiti na Ndugu Donald Kibwana - Kaimu Katibu Mkuu. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Spika kutoka Kariakoo. Hawa ni wapiga kura wa Mheshimiwa Spika wetu. Karibuni sana. Ninaamini mnaendelea kututunzia Mheshimiwa Spika wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ni wageni 94 ambao ni wanachama wa *Tanzania Patriotic Organization (TPO)* kutoka mikoa mbalimbali nchini Tanzania. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Spika katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia, tuna wageni ambao wamekaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Wageni wa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge na Waziri wa Viwanda na Biashara, wa kwanza ni Balozi Waziri Rajabu, Katibu Mkuu; karibu sana Katibu Mkuu wetu, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mwingine ni Ndugu Aristides Robert Mbwasi, Naibu Katibu Mkuu; karibu sana Naibu Katibu Mkuu Wetu. *(Makofi)*

Tunaye Brigedia General Ahmed Ahmed, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma; karibu sana Mkuu wa Mkoa wetu. *(Makofi)*

Yupo Profesa Ulingeta Mbamba, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania; Prof. Othman Othman, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la

Viwango Tanzania *(TBS)*. Profesa Neema Mori, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELLA);* karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Prof. Valerian Silayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini; Profesa Zakaria Mganilwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)*. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Wilhus Karumuna, Mwenyekiti wa Bodi ya *TEMDO*; Ndugu Farid Nahdi - Mwenyekiti wa *Simba Group;* Ndugu Shufaa Albert - Kamishna wa Tume ya Ushindani *(FCC);* na Dkt. Adelhem Meru - Katibu Mkuu Mstaafu na Mshauri wa Kiwanda cha *Dangote Cements*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Godfrey Kilenga, Mkurugenzi wa *Agriculture Growth Corridors of Tanzania;* Ndugu David Nelwa, Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya *Mati Super Brand Limited;* Ndugu Frank Mnyabundege, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB);* na Ndugu Kuhani Musa Richard, Kiongozi wa Dini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Kapinga. Hawa ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. Yupo Ndugu Paul Kaunda, mume wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana shemeji yetu katika Bunge letu. Pia yupo Ndugu Antonia Alanus, ni dada wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Mhandisi Leonard Tenga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania *(CTI),* karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Kapinga ni Mheshimiwa Kisare Makori, Mkuu wa Wilaya ya Mbinga; karibu sana Mkuu wetu wa Wilaya. Mheshimiwa Shaka Hamdu Shaka, Mkurugenzi Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, karibu sana, Muenezi Mstaafu Taifa CCM. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, makofi hayo kwa wingi yanaashiria kumbukumbu yake akiwa Mwenezi wetu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Janus Mfaume, katibu wa CCM Wilaya ya Kilosa; karibu sana katibu wetu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Desdarius Haule, Mwenyekiti wa Halmashauri, Wilaya ya Mbinga; Ndugu Pendo Daniel, Katibu Tawala Wilaya ya Mbinga; Ndugu Joseph Kashushura, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga; Ndugu Mwenuka, Mkurugenzi wa Halmashauri Wilaya ya Kilosa; na Ndugu Ratis Kamania, Mkurugenzi Mtendaji wa *Mtison Group,* karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wengine ambao ni Ndugu Edeyemi Fayobi Fajobi, Mkurugenzi Mtendaji *Dangote Cement*; Mhandisi Benedict Lema, Mshauri wa Kiwanda cha *Tanga Cement;* na Ndugu Ahmed Mhada, Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha *Mbeya cement*; karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Ndugu Jenipher Bashungwa, Mkurugenzi wa Alaska Tanzania; Ndugu Samir Santosh, Mkurugenzi Mtendaji wa *Kamal Group*; Ndugu Rashid Soud, Kaimu Mkurugenzi Mkuu Kiwanda cha *Farm Base;* na Ndugu Eliya Jeset, Mhasibu Mkuu *GSM group,* karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Fatma Mnaro, Mkurugenzi Mtendaji *CFA Group* na Ndugu Alfred Mapunda, Meneja Mkuu wa Kampuni Tanzu ya Uswiss inayotoa teknolojia ya udhibitishaji na ufuatiliaji.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ambao ni wa Waheshimiwa Wabunge. Nitaanza na wageni wanne wa Mheshimiwa Ngwasi Damas Kamani, Mbunge na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Hawa ni wafanyabiashara kutoka Kampuni ya *Dubai to Dar es Salaam*, wauzaji na wasafirishaji wa vifaa vya umeme. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Ng'wasi, Naibu Waziri wetu; na pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, ambaye ni rafiki yake, anaitwa Ndugu Paskazia Murugi kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Zainab Athman Katimba kutoka Taasisi ya *Bridge for Change;* karibuni sana.

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Khamis Kassim Ali, ni wapiga kura wake kutoka Zanzibar, hawa ni wapiga kura wake. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watano wa Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge, ambao ni Wafanyabiashara wa *Serengeti Queens* kutoka Serengeti, Mkoani Mara. Karibuni sana wageni wetu kutoka Serengeti. *(Makofi)*

Wapo wageni 74 wa Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. Mheshimiwa Ditopile una marafiki wengi kwa kweli. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo. Nitaanza na wafanyakazi sita wa Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi *(OSHA)* kutoka Kanda ya Kati; karibuni sana wageni wetu kutoka *OSHA*. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 10 na walimu watano kutoka *Tanzania Institute of Project Management* ya Jijini Dar es Salaam; karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wafanyabiashara 30 wa Soko la Kariakoo, ambao ni washindi na wadau wa mafanikio katika Tuzo za *Kariakoo Business Awards (KBA) 2026* kutoka Jijini Dar es Salaam; karibuni sana katika Bunge letu wafanyabiashara wetu kutoka Soko la Kariakoo. *(Makofi)*

Wengine ni wakurugenzi na wafanyabiashara vijana 10 wa Taasisi ya *Young CEO Round Table Africa* kutoka mikoa mbalimbali Tanzania. Karibuni sana vijana wetu ambao ni wakurugenzi wa biashara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo ya Wageni wetu kwa siku ya leo.

Katibu, tuendelee.

22 MEI, 2026

NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamkaribisha Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Judith Kapinga, ili kutoa Taarifa ya Wizara kwa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Karibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 24 na 26 Machi, 2026, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaliomba Bunge lako likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa afya njema na kuwepo hapa siku hii muhimu ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyeyekevu na moyo wa shukurani, nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Kupitia Bunge hili Tukufu nimwahidi Mheshimiwa Rais kushirikiana na watendaji wenzangu akiwemo Naibu Waziri wa Wizara na taasisi pamoja na wadau wote wa Wizara katika kutekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia ili tuweze kufikia malengo mahususi ya kuendeleza sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie tena fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu ya sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi hawa wamekuwa wakitoa miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika kutekeleza majukumu ya sekta ya viwanda na biashara. Ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini na umahiri katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Halikadhalika, ninawapongeza watoa hoja wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ya bajeti aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 01 Aprili, 2026. Hotuba hiyo ilitoa hali ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka 2025/2026, pamoja na kuonyesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa mwaka 2026/2027 katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Bunge lako Tukufu liliondokewa na wapendwa wetu, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na Mbunge wa Jimbo la Isimani, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho, na Mheshimiwa Halima Iddi

Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti maalum. Tunaendelea kutoa pole wa Waheshimiwa Wabunge, familia, ndugu na jamaa na wananchi na tunaomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa pumziko na milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, ninaomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Kondoa Mjini. Kamati hii imekuwa na mchango madhubuti kwa Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kupitia maelekezo, maoni na ushauri katika masuala mbalimbali, hususan maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa shukrani, ninamshukuru Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri na Mbunge wa Mikumi kwa umadhubuti wake, na kwa mchango mkubwa anaoutoa katika Wizara yetu. Naibu Waziri ni kiongozi mchapakazi anayejituma na anayeipenda kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninamshukuru Balozi, Waziri Rajab Salum, Katibu Mkuu kwa utendaji wake mahiri, Bwana Aristides Robert Mbwasi, Naibu Katibu Mkuu viongozi wa bodi, watendaji na watumishi wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na wasaidizi wa ofisi yangu, Katibu wangu Bi. Loyce Lubonera, dereva wangu Bwana Paul Mtulo na Mwandishi Mwendesha Ofisi yangu Bi. Pheby Bundala. Ninawashukuru kwa utumishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha salamu za awali na za shukrani, ninaomba niishukuru familia yangu, mume wangu kwa namna anavyonipa utulivu unaonisaidia katika kutimiza majukumu yangu. Ninamshukuru sana yeye, watoto wetu na wazazi wangu kwa namna wanavyoniwezesha kufanya majukumu yangu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa hatua hii, ninawashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Mbinga

Vijijini kwa kunipa kura za heshima za kuwa Mbunge wa kwanza mwanamke wa Jimbo letu. Ninawaahidi kuwatumikia kwa upendo na moyo thabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi ninaomba hotuba yangu yenye kurasa 110 iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ninayowasilisha imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni taarifa ya hali na mwenendo wa sekta ya viwanda na biashara nchini, utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2025/2026, vipaumbele vya Wizara kwa bajeti ya mwaka 2025/2026 na shughuli zitakazotekelezwa na Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na hali na mwenendo wa sekta ya viwanda na biashara nchini, na nianze na hali na mwenendo wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara ili kuchochea mageuzi ya uchumi funganishi, jumuishi na shindani unaojengwa katika misingi wa kuongeza thamani ya rasilimali zinazozalishwa nchini na kuimarisha viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa wingi kwa kutumia malighafi za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizo ni utekelezaji wa malengo ya Dira 2025 ambayo yamejielekeza katika kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa muhimu, kuzalisha bidhaa bora, kutoa ajira kwa wingi, na kuongeza mauzo nje ya nchi. Kupitia mwelekeo huo viwanda vipya vimejengwa na vingine vimefanyiwa upanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi hizo, katika kipindi cha mwaka 2025/2026 jumla ya viwanda vipya vikubwa na vya kati 25 katika sekta mbalimbali vimejengwa na kuanza uzalishaji. Viwanda hivyo vimetoa jumla ya ajira 39,250 ambapo kwa ajira za moja kwa moja 7,635 na zisizo za moja kwa moja ni 31,615.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uzalishaji viwandani imeendelea kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika uchumi. Ninaomba uniruhusu nielezee kuhusu baadhi ya viwanda vinavyozalisha bidhaa muhimu zinazotumika kwa wingi nchini na vyenye uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni viwanda vya mabati. Tanzania ina viwanda vikubwa vitano vya mabati ambavyo ni Lodhia, *MMI Still*, *ALAF Limited*, *Kinglion* na *GSM Roofing Sheet,* vikiwa vina uwezo uliosimikwa kwa kuzalisha mabati tani 410,000 ya rangi na tani 700,000 meupe kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026 viwanda hivyo vimezalisha jumla ya tani 350,000 za mabati ya rangi na tani 500,000 ya mabati meupe sawa na 70% ya uzalishaji wa mabati nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mahitaji ya mabati ya rangi ni takribani 250,000 na mabati meupe ni 380,000. Mabati ya ziada huuzwa katika nchi jirani. Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 2,300 na sisizo za moja kwa moja 11,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya viwanda hivyo vikubwa, kiwanda cha *GSM Roofing Sheet* kilichomo Dar es Salaam ni kipya na kinazalisha mabati ya rangi chenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mabati tani 150,000 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 800 na zisizo za moja kwa moja 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda kimezalisha mabati tani 45,000. Pamoja na kukidhi uzalishaji kwa ajili ya matumizi ya ndani ya mabati, Wizara kupitia *NDC*, inatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mabati na kupunguza uagizaji wa malighafi kutoka nje ya nchi kwa kusaini mkataba wa Mradi wa Maganga Matitu. Mradi huu unakadiriwa kuwa na hifadhi ya chuma tani milioni 101. Hatua iliyofikiwa ni uingizaji wa mitambo ya uchimbaji na uchakataji wa madini ya chuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pindi mradi huo utakapoanza katika mwaka ujao wa fedha tutaweza kufanya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za chuma, na vilevile utawezesha uanzishwaji wa viwanda vingine vitakavyoongeza mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda vya saruji, Tanzania ina jumla ya viwanda 15 vya kuzalisha saruji vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 13,600,000 za saruji kwa mwaka. Kati ya hivyo, viwanda saba vinazalisha *clinker* na saruji na viwanda nane vinazalisha saruji pekee. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda vimezalisha jumla ya tani 10,300,000 za saruji, ambapo mahitaji ya sasa ni takribani tani 8,500,000 kwa mwaka. Saruji ya ziada huuzwa katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 6,020 na zisizo za moja kwa moja 20,280. Katika kuongeza uzalishaji wa saruji nchini, katika mwaka 2025/2026 kiwanda cha *WIH Holdings Limited* kilichopo Mkoa wa Kigoma ambacho kina uwezo uliosimikwa kwa kuzalisha tani 1,900,000 za saruji kwa mwaka, na kutoa ajira za moja kwa moja 800 na zisizo za moja kwa moja 3,050 kimejengwa. Hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda hicho kimezalisha saruji tani 1,500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya sukari. Tanzania ina jumla ya viwanda saba vya kuzalisha sukari ambavyo ni *Kilombero Sugar, Tanganyika Planting*, *Kagera Sugar*, *Mtibwa Sugar*, Mkulazi, Manyara na Bagamoyo. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalishwa sukari tani 800,000 kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026 viwanda vimezalisha jumla ya tani 400,000 za sukari ambapo mahitaji ya sukari ni takribani tani 550,000. Aidha, viwanda vimetoa ajira za moja kwa moja 28,500 na zisizo za moja kwa moja 95,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa nchi inapunguza uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi, viwanda viwili vya sukari vya Mkulazi na Kilombero vimefanya upanuzi ili kuongeza uzalishajiwa sukari nchini. Kufuatia upanuzi huo, kiwanda cha Kilombero kitakuwa na uwezo wa kuzalisha sukari tani 226,000 kutoka tani 123,000 kwa mwaka, ambapo majaribio ya uzalishaji yamekamilika na uzalishaji utaanza mwezi Juni, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kiwanda cha Mkulazi kimeongeza mtambo utakaowezesha kuzalisha sukari ya kiwandani *(industry sugar)*. Majaribio ya mitambo yamefanyika na tayari kiwanda kimezalisha tani za mwanzo za sukari. Kukamilika

kwa upanuzi huo kunawezesha viwanda vyote viwili kuzalisha ajira za moja kwa moja 8,500 na zisizo za moja kwa moja 25,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda vya mbolea, Tanzania ina jumla ya viwanda 49 ambapo viwanda vikubwa ni viwili tu, viwanda vya kati ni 10 na vingine vyote vilivyobaki 37 ni viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vikubwa hivyo, pamoja na viwanda vya kati na vidogo vina uwezo wa kuzalisha kwa uwezo uliosimikwa tani 1,700,000 za mbolea kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili 26 viwanda vimezalisha jumla ya tani 123,000 za mbolea na kutoa ajira za moja kwa moja 2,687 na zisizo za moja kwa moja 9,200. Katika kupunguza uagizaji wa mbolea kutoka nje hususan mbolea ya chumvi chumvi ambayo hutumika kama malighafi muhimu katika uzalishaji wa mbolea nyingine hapa nchini, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaendelea na jitihada za uwekezaji ili kuzalisha mbolea nyingi zaidi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya dawa za binadamu na vifaatiba. Tanzania ina jumla ya viwanda 14 vya kuzalisha dawa za binadamu na vifaa tiba. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha 20% ya dawa na vifaa tiba vinavyohitajika hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na uagizaji wa dawa kutoka nje ya nchi, Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza mikakati mahsusi ili kuhakikisha kuwa sekta hii inaongeza uwekezaji wa viwanda vya dawa na vifaatiba angalau kufikia mahitaji ya dawa na vifaatiba ifikapo 2035.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda vya mafuta ya kula, tunavyo viwanda vya mafuta ya kula ambapo viwanda vidogo vidogo sana ni 1,038; viwanda 543 ni viwanda vidogo, viwanda tisa ni vya kati na viwanda 14 ni vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivyo jumla vipo 1,604 ambapo vingi ni vile viwanda vidogo vidogo sana. Viwanda hivi vina uwezo uliosindikwa wa kuzalisha mafuta ya kula tani 2,527,739 kwa mwaka na vinatoa ajira za moja kwa moja 10,755 na zisizo za moja kwa moja 36,416. Aidha, viwanda hivyo

vinazalisha tani 302,000 za mafuta ambapo mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takribani tani 700,000 kwa mwaka. Hivyo, tani 430,000 huagizwa ili kutosheleza mahitaji ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tukiratibiwa na Wizara ya Kilimo tunaendelea na juhudi mbalimbali za nchi kujitosheleza na mahitaji ya mafuta ya kula. Juhudi hizo zinahusisha kuzalisha mbegu bora na kuzigawa kwa wakulima, kutoa ruzuku ya mbolea kuendelea kuhamasisha wawekezaji wakubwa kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula na kuendelea kuboresha teknolojia za wasindikaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi za Serikali kuna viwanda vingine vipya vimejengwa katika mwaka 2025 na 2026 kama ambavyo vinasomeka katika bajeti yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nieleze kuhusiana na hali ya biashara yetu duniani. Biashara ya Tanzania nje ya nchi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Mathalan, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 10,080.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,702 mwaka 2024, sawa na ongezeko la 16%. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa mikakati ya kuboresha mazingira ya biashara nchini, utafutaji wa masoko, kuzalisha bidhaa zinazokidhi ushindani nje ya nchi, na kupunguza milolongo ya hatua za kusafirisha bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na mazao ghafi ya kilimo kama ufuta, tumbaku, mbaazi, ngano, mchele, maharage, mahindi, kahawa, pamba na parachichi. Mazao ghafi ya mifugo ni pamoja na samaki na bidhaa za viwandani ikiwa ni pamoja na dhahabu, kakao, makaa ya mawe, vigao, na mabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025 bidhaa zilizoingizwa nchini zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 16,033.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 15,684.5 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia mbili nukta mbili. Ongezeko hilo linatokana na kuagiza kwa wingi bidhaa ambazo hazizalishwi hapa nchini na zinazotumia teknolojia ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na bidhaa za mitaji *(capital goods)*, magari, bidhaa za kutengeneza lami, bidhaa za chuma, mashine mbalimbali za hospitalini, madawa baridi, mafuta ya petroli na gesi, na sukari ya viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Umoja wa Ulaya. Mwaka 2025 thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda nchi za Umoja wa Ulaya yameongezeka kufikia dola za Marekani kufikia milioni 943.5 kutoka dola za Marekani milioni 686.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la 37.5%. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa ushiriki wa wafanyabiashara wa Tanzania katika soko hilo. Juhudi za Serikali na sekta binafsi katika kuboresha ubora wa bidhaa ili kukidhi viwango vya Soko la Umoja wa Ulaya, na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za kakao. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni kama ambavyo inasomeka katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwaka 2025 Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1,264.6 katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,163.8 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia nane nukta saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hilo limechangiwa na juhudi za Serikali za kuboresha mazingira ya biashara nchini na kuimarika kwa uzalishaji wa bidhaa ambazo zina soko kubwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa zilizouzwa ni kama inavyosomeka kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika mwaka 2025 thamani ya bidhaa zilizouzwa katika Soko la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ilikuwa dola za Marekani milioni 3,545 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,968 mwaka 2024, sawa na ongezeko la 19.4%. Ongezeko hilo limechangiwa na mauzo ya bidhaa kama vile madini, samaki, nyanya, vitunguu, maharage, viazi vitamu, ndizi, parachichi, pamoja na bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Bara *Asia*. Mwaka 2025 thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda baadhi ya nchi za Bara la *Asia* tunazofanya biashara kwa wingi hususan China, India na Japan ilikuwa Dola za Marekani milioni 3,213.2 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 2,840 mpaka 24 sawa na ongezeko la 13.1%. Ongezeko hilo lilichangiwa na uhitaji mkubwa wa bidhaa kama vile ufuta, kakao na parachichi. Ufafanuzi zaidi kuhusu hali na mwenendo wa sekta ya viwanda na biashara unapatikana katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa nne hadi ukurasa wa 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na fedha zilizoidhinishwa na kupokelewa. Utekelezaji wa bajeti kulingana na fedha zilizopokelewa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44, iliidhinishiwa jumla ya shilingi 135,783,232,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 93,897,697,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 41,887,535,000 ni za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea shilingi 95,630,301,245.82, sawa na 70.43% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 74,603,022,813.73 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 21,27,800,432.09 ni ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya viwanda; kuendeleza miradi ya kimkakati na kielelezo. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imekamilisha majadiliano na mwekezaji wa kampuni ya *Shudao Investment Group Company Limited* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa chuma cha Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji huyu mpya ni kampuni inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambayo imenunua kampuni ya awali ya *Sichuan Hongda Group Company Limited* kwa lengo la kutekeleza mradi unganishi wa Mchuchuma na Liganga kwa kushirikiana na Shirika letu la Taifa la Maendeleo *(NDC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia majadiliano hayo, pande zote mbili zimefikia makubaliano ya msingi na sahihi, ya mgawanyo wa hisa na muundo wa uwekezaji, kiwango cha mtaji wa mwekezaji unaohitajika, muundo shirikishi wa usimamizi wa uendeshaji wa mradi, muda wa mkataba wa uwekezaji, uhuishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi, uandaaji wa modeli ya kifedha ya pamoja, vivutio vya uwekezaji vinavyoendana na sheria ya Tanzania na uongezaji wa thamani kwa madini yote yakiwemo chuma, *vanadium* na *titanium* hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, uandaaji wa rasimu za mikataba ya ubia na mikataba ya wanahisa kwa miradi ya uchimbaji na kiwanda cha kutengeneza bidhaa za chuma umekamilika. Kwa ujumla, majadiliano ya mradi ambao umekaa kwa muda mrefu wa Liganga na Mchuchuma yamekamilika kwa mafanikio makubwa na kwa sasa pande zote zinawasiliana na mamlaka zao kwa ajili ya hatua za idhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mabunge kadhaa, hoja yao kubwa ilikuwa ni Liganga na Mchuchuma, lakini leo tunafurahi kusema kwamba majadiliano yamekamilika. Hii ni hatua ya kihistoria kwa mradi huu wa kielelezo kwa Taifa letu ambao utakuwa na manufaa makubwa. Aidha, mikataba ya ubia na wanahisa inatarajiwa kusainiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2026/2027 ambapo ujenzi wa miradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekelezwa kwa mradi huo kutawezesha nchi kuokoa matumizi ya Dola za Marekani bilioni 1.22 sawa na shilingi trilioni 3.2 ambazo zimekuwa zikitumiwa kununua bidhaa za chuma kutoka nje ya nchi ikiwa ni bidhaa ya pili kwa matumizi makubwa ya fedha za kigeni baada ya bidhaa za mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, utekelezaji wa mradi utaongeza mnyororo wa thamani kwa bidhaa mbalimbali zitakazozalishwa kupitia viwanda vingine vitakavyoanzishwa na utaondoa au kupunguza uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na mahitaji ya chuma chakavu katika uzalishaji wa bidhaa za chuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa za awali za moduli, *(Joint Financial Model)* iliyoandaliwa kwa pamoja na wataalamu wa Serikali na mwekezaji, makadirio ya mapato ya Serikali kutoka kwa kodi mbalimbali pamoja na malipo ya mrabaha kwa kipindi cha miaka 25 ni jumla ya Dola za Marekani shilingi trilioni 1.99. Aidha, mapato ya mradi yatakayotokana na mauzo ya umeme, makaa ya mawe, bidhaa za chuma, *titanium, vanadium* na *aluminium sulphate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, utekelezaji wa mradi huu utawezesha kupatikana kwa ajira za moja kwa moja 6,500 na zisizo za moja kwa moja takribani 26,000 lakini kwa sababu tuna-*confirm feasibility study*, tutaendelea ku-*update data* hii kulingana na takwimu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Magadi Soda Engaruka; Wizara kupitia *NDC* inaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa kimkakati na kielelezo wa Magadi Soda uliopo katika Bonde la Engaruka Wilaya ya Monduli kwa kulipa leseni ya uchimbaji, kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi na kutafuta mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2026 jumla ya shilingi bilioni 5.82 sawa na 98% ya fedha ya fidia, ililipwa kwa wafidiwa 513 kati ya wafidiwa 594. Zoezi la kukamilisha ulipaji wa fidia linaendelea kwa wafidiwa 81 waliobaki ambao wanakamilisha nyaraka zao zikiwemo nyaraka za mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanikiwa kupata mwekezaji, timu ya majadiliano inaendelea na majadiliano ya mkataba. Kutekelezwa kwa mradi huu kutaokoa fedha za kigeni zaidi ya Dola milioni 121 zitakazotumika kwa mwaka kuagiza malighafi ya magadi soda pamoja na bidhaa zinazotokana na magadi soda kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni muhimu sana na kwa sasa tunafanya tathmini iwapo majadiliano yanaweza kuleta matokeo. Vilevile, tukijiridhisha kama majadiliano haya hayana matokeo, hatutasita kusitisha majadiliano na kutafuta mwekezaji mwingine ambaye anaendana na kasi ambayo Serikali tunaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *NDC* imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Maganga Matitu unaotekelezwa kwa ubia kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Kampuni ya *Fusion Industry* Tanzania *Company Limited*. Hadi Aprili, 2026 malipo ya fidia yamefanyika ambapo wananchi 380 kati ya 385 sawa na 98.7% ya wananchi waliopisha mradi wamelipwa fidia kiasi cha shilingi bilioni 4.196. Shughuli za kutekeleza mradi zinaendelea ambapo mitambo ya kiwanda imeanza kuingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza kiwanda cha Tanzania *Biotech Product Limited (TBPL)*. *TBPL* ni kiwanda cha kuzalisha bidhaa za kibaiolojia kilichopo Kibaha Mkoani Pwani kinachotumia teknolojia kutoka nchini Cuba kuzalisha bidhaa mbalimbali za kibaiolojia zinazotumika kwenye sekta ya afya, kilimo na mazingira. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa 100% na kina uwezo wa kuzalisha hadi tani milioni sita kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia Aprili, 2026 jumla ya lita 491,361 za viuadudu zimezalishwa ambapo kati ya lita hizo, lita 124,121 zimechukuliwa na Halmashauri 80 nchini. Aidha, uzalishaji na usambazaji wa viuadudu katika Halmashauri zilizosalia unaendelea. Pamoja na uzalishaji na usambazaji, kiwanda kimeweza kuuza dawa za viuadudu nchi za jirani zenye thamani ya shilingi milioni 344. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa imani ya watumiaji na kupanuka kwa soko la dawa hii nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza kiwanda cha *KMTC, (Kilimanjaro Machine Tools)*. Wizara kupitia *NDC* imeendelea na juhudi za kukiendeleza na kukisimamia kiwanda chetu cha *KMTC Manufacturing Limited* kilichopo Kilimanjaro na hadi Aprili, 2026 kiwanda kimefanikiwa kuzalisha jumla ya mashine 14 na vipuri 159.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji. Wizara kupitia *TIRDO* imeendelea kutekeleza zoezi la tathmini ya viwanda na uainishaji wa fursa za uwekezaji katika viwanda nchini. Tathmini hiyo inaainisha idadi ya viwanda, ajira, uwezo wa uzalishaji, teknolojia zinazotumika nchini na maeneo yenye fursa za uwekezaji ili kuchochea maendeleo ya viwanda na kuziongezea thamani rasilimali za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 zoezi hili limefanyika katika mikoa miwili na hivyo kuwa na jumla ya mikoa tisa. Hadi kufikia Aprili, 2026 kanzidata hiyo ina jumla ya viwanda 25,650 ambapo 482 ni viwanda vikubwa, 625 vya kati, 8,980 vidogo na 15,000 ni viwanda vidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvumbuzi, utafiti na uendelezaji teknolojia. Katika mwaka 2025/2026 kupitia *SIDO* tumefanikiwa kuhawilisha teknolojia nane za kuchakata mazao mbalimbali. Teknolojia hizo ni utengenezaji wa kinu cha kuchoma masalia ya kilimo, mashine ya kutengeneza mkaa mbadala, mashine ndogo ya kusafisha mafuta ya alizeti, mashine za kuzalisha chakula cha samaki, mashine za kusaga mawe yenye madini, mashine za kukamua na kuchuja mafuta ya nazi, mashine za kubangua korosho na utengenezaji wa *cage* za ufugaji wa samaki kwenye maziwa, mito na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TEMDO,* inaendelea kusanifu na kuunda vifaatiba kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya hospitali. Hadi kufikia Aprili, 2026 *TEMDO* imefanikiwa kusanifu na kutengeneza vifaatiba vya aina 15 vilivyopo daraja la kwanza, (A) ambavyo vimepata ithibati na mamlaka za uthibiti wa madawa na vifaatiba *TMDA*. Aidha, kufuatia usanifu huo vifaatiba mbalimbali vimetengenezwa vikiwemo vitanda vya kujifungulia, mitambo ya kuchomea taka ngumu za hospitali na hifadhi kuta *(hospital screens)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *CAMARTEC* imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za uendelezaji wa teknolojia za kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uchumi wa *blue* pamoja na nishati safi ya kupikia. Hadi Aprili, 2026 *CAMARTEC* imekamilisha ujenzi wa mitambo miwili ya *biogas* ya ngazi ya taasisi katika kambi za JKT Oljoro na JKT Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *CAMARTEC* imeanza kutekeleza miradi ya ujenzi wa mitambo ya *biogas* katika magereza nane kama awamu ya kwanza kati ya magereza 14 yaliyopangwa kutekelezwa. Lengo la miradi hii ni kutoa nishati safi na endelevu ya kupikia, kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa,

kulinda mazingira pamoja na kuboresha usafi na usimamizi wa taka katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa ujasiriamali mdogo na wa kati. Katika kuhamasisha na kuendeleza uanzishwaji wa kongani nchini, hadi kufikia Aprili, 2026 wajasiriamali wamepata mafunzo kuhusu usimamizi wa biashara, uzingatiaji viwango katika uzalishaji na utafutaji wa fursa za masoko ya bidhaa. Aidha, Wizara kupitia *SIDO* imeendelea kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo, ushauri wa kitaalamu, mikopo na mbinu za utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali katika kongani 20 kwenye mikoa ya Geita, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Shinyanga, Mtwara na Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara kupitia *SIDO* imewezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo vipya 296 katika mikoa yote Tanzania na kuchangia jumla ya ajira 1,409.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa huduma za kifedha kwa wajasiriamali. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (*NEDF)* unaosimamiwa na *SIDO* imetoa jumla ya mikopo 829 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.95. Mikopo hiyo imezalisha ajira 1,859 ambapo wanawake ni 955 sawa na 51% na wanaume ni 902 sawa na 49%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tangu Mfuko ulipoanza kutoa huduma za mikopo mwaka 1994 hali ya marejesho ya mikopo imekuwa ni ya kuridhisha ambapo wastani wa marejesho ni 91.1%. Kupitia programu ya uwezeshaji wa viwanda vidogo, Wizara imewezesha jumla ya wajasiriamali 11 kuunganishwa na Benki ya Azania na kupata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtangamano wa biashara. Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na Kimataifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye nchi na nchi, tumeweza kufanya utekelezaji wa mkataba wa mfumo uliorahisishwa wa ufanyaji biashara kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wadogo

na wa kati katika kufanya biashara za mipakani kati ya Tanzania, Zambia na Malawi, *(Simplified Trade Regime - STR)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kukuza na kuimarisha biashara ya uwili, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara imeratibu majadiliano na hafla ya utiaji saini wa mkataba wa mfumo uliorahisishwa kwa wafanyabiashara wadogo *(Simplified Trade Regime)* kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Malawi iliyofanyika mwezi Februari, 2026 Jijini Lilongwe, Malawi. Mfumo huo unajumuisha utaratibu maalum wa biashara unaolengwa kurahisisha taratibu za forodha na kupunguza vikwazo visivyo vya kikodi kwa bidhaa 61.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huo umewezesha wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao kwa urahisi na kupeleka biashara baina ya Tanzania na Malawi kuimarika. Ili kuwa na ufanisi wa utekelezaji wa mkataba huo, Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Taifa ya wafanyabiashara imeendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wa mipakani. Aidha, mwongozo uitwao *Kasumulu Business Model* umeandaliwa ili kutoa utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa mazao ya soya, ufuta na mbaazi baina ya Malawi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada zetu za kikanda, utekelezaji wa mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika umeendelea ambapo Wizara inashiriki katika majadiliano ya biashara kupitia mpango wa majaribio ya biashara *(Guided Trade Initiative)* ambapo kampuni za Tanzania zimefanikiwa kufikia masoko mapya na kupata uzoefu wa moja kwa moja katika taratibu za forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili, 2026 jumla ya kampuni 40 za Tanzania zimefanya biashara kwa kutumia vyeti vya uasili wa bidhaa ambapo jumla ya vyeti 500 vimetolewa. Kupitia soko hili, mauzo ya Tanzania kwenda nchi ya Ghana yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 62.9, Nigeria dola za Marekani milioni nane, Algeria dola za Marekani milioni 3.7, na mauzo kwenda Misri yalikuwa dola za Marekani milioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni nyuzi za katani ambazo zilikuwa na thamani za dola za Marekani milioni 56, ikifuatiwa na kahawa na viungo ambavyo vilikuwa na jumla ya Dola za Marekani milioni tatu, na vioo ambavyo vilikuwa na jumla ya dola za Marekani milioni 2.4. Katika jitihada zetu za mtangamano wa biashara Kimataifa, kuna utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara kwa Shirika la Biashara Duniani *(Trade Facilitation Agreement - WTO)* na Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji wa Biashara *(National Committee on Trade Facilitation)* inaendelea na utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara kwa Shirika la Biashara Duniani. Kamati hiyo imeendelea kutatua changamoto za wafanyabiashara kupitia kliniki ya wafanyabiashara hasa katika mpaka wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kliniki hiyo, wafanyabiashara wamepatiwa uelewa kuhusu taratibu za kuvuka mipakani, kutumia mfumo uliorahisishwa kwa wafanyabiashara wadogo, uondoaji na upitishaji wa mizigo mipakani na usafirishaji, na taratibu na fursa za biashara ya kikanda. Kupitia mpango huu, jumla ya wafanyabiashara 72 wamenufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na jukumu la kuboresha mazingira ya ujenzi wa viwanda na ufanyaji biashara nchini ambapo katika mwaka 2025/2026, Wizara imefanikiwa kudhibiti biashara ambazo inabidi zifanywe na wazawa ambazo zinastahili kufanywa na Watanzania kupitia Tangazo la Serikali Namba 487A la Tarehe 28 Julai, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangazo hilo linatoa katazo kwa raia wa kigeni kujihusisha na biashara 15 zinazostahili kufanywa na Watanzania. Biashara hizo ni pamoja na uuzaji wa bidhaa kwa jumla na rejareja, huduma za watalii wa ndani, huduma za fedha kwa njia ya simu, mawakala, saluni, usafirishaji wa mizigo, uuzaji wa vinyago, uchimbaji mdogo wa madini, uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya redio na runinga, uendeshaji wa viwanda vidogo, kampuni za huduma ya usafi na uuzaji wa nyumba na viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sheria ya Katazo hilo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali imechukua hatua madhubuti za kisera, kisheria na kiutendaji ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* imezuia uhuishaji wa leseni za biashara 901. Kati ya hizo, leseni 737 ni za biashara za uingizaji na uuzaji wa bidhaa, leseni tano katika huduma za posta na utoaji wa vifurushi ndani ya mipaka ya Kitaifa, leseni 119 za uwakala au udalali katika biashara na sekta ya mali isiyohamishika na leseni 86 za huduma ya utoaji na usafirishaji wa shehena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii imerejesha imani ya wazawa kwa Serikali kwa namna inavyosaidia kutatua changamoto za biashara, imeboresha mazingira ya biashara kwa wazawa, na hivyo kuongeza uwekezaji kwenye biashara, na imeongeza uwezo wa ushindaji kwa wazawa kwenye biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya maombi 373 ya vibali vya kazi kwa raia wa kigeni wanaokuja kufanya kazi nchini katika tasnia ya biashara hayakuidhinishwa kutokana na kutokukidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria na katazo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na Mbeya zimezuia uhuishaji wa leseni za biashara 191 kwa biashara za uuzaji wa bidhaa kwa jumla, uuzaji wa bidhaa kwa rejareja, uchimbaji mdogo wa madini na biashara ya maghala/stoo ambazo zinamilikiwa na wafanyabiashara au kampuni wasio raia wa Tanzania kwa kuzingatia amri iliyotolewa. Biashara 13 kati ya 191 zilizozuiwa kuhuishwa au kupewa leseni zilikuwa katika eneo la Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wa shughuli za biashara nchini; Masuala ya ubora wa bidhaa. Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania imekamilisha viwango muhimu pamoja na viwango mbalimbali katika sekta ya kilimo, chakula na uhandisi. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya viwango 230 vimetayarishwa. Aidha, jumla ya viwango 499 vipo kwenye hatua za mwisho za maandalizi ambapo vitakamilika ndani ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya leseni 856 za nembo ya ubora ya *TBS* zilitolewa sawa na 85.6% ya lengo la kutoa leseni 1,000 kwa mwaka. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 349 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa mbalimbali. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia *TBS* imesajili bidhaa za chakula na vipodozi 2,070 ambavyo ni sawa na 86.3% ya lengo la kusajili na kutoa vibali 2,400 kwa mwaka. Kati ya bidhaa hizo, bidhaa 1,406 ni za chakula na bidhaa 664 ni za vipodozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha bidhaa za chakula na vipodozi zina ubora unaotakiwa, Wizara kupitia *TBS* imesogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kuanzisha ofisi katika kanda tisa, ujenzi wa maabara katika Kanda ya Kati Dodoma na Kanda ya Ziwa Mwanza. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga maabara katika Kanda ya Kaskazini, Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara imeendelea kusajili bidhaa zinazozalishwa ndani na zile zinazoingia nchini, na kuendelea na utoaji wa ithibati ya bidhaa za chakula na vipodozi kwa kufanya tathmini na kaguzi za awali wa kiwanda na kufanya kaguzi endelevu za bidhaa sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya *TBS* Dodoma imefunguliwa takribani wiki tatu zilizopita ambayo inahudumia Kanda hi ya Kati, na tunavyoongea sasa hivi inafanya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa bidhaa bandia. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia *FCC* imefanikiwa kutekeleza operesheni maalum za kudhibiti bidhaa mbalimbali ikiwemo pombe bandia. Katika operesheni zilizofanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam, vinywaji bandia pamoja na chupa tupu, na katoni tupu zilikamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vifaa vya uzalishaji na ufungashaji vilikamatwa ikiwemo mashine za kuchapisha maelezo ya bidhaa, kupima vilevi, mashine ya kufunga vifuniko, mizani, ethanoli, vyombo vya kuchanganyia na kuchujia pombe. Aidha, *FCC* imebaini uwepo wa bidhaa nyingine bandia za vipuri na vilainishi ambazo zilikamatwa na watuhumiwa kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Wizara kupitia *FCC* katika kukabiliana na tatizo la bidhaa bandia unalenga kuimarisha uchunguzi wa taarifa za kiintelijensia, utekelezaji wa operesheni za ukaguzi na ukamataji pamoja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imekagua na kuhakiki vipimo 736,746 sawa na 104.5% ya lengo la kukagua vipimo 705,106. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa, vipimo 27,188 vilirekebishwa na vipimo 488 vilikataliwa. Aidha, Wakala iliendelea kufanya kaguzi za kawaida na za kushtukiza ambapo jumla ya kaguzi 3,823 sawa na 127.4% zilifanyika kati ya kaguzi 3,000 zilizopangwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi. Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara *(TanTrade)* iliratibu Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam Mwaka 2025 yaliyofanyika mwezi Juni hadi Julai, 2025, Dar es Salaam. Lengo la maonesho hayo ni kutoa fursa ya kuchochea ukuaji wa biashara na uchumi wa nchi kwa kuwawezesha wazalishaji wa bidhaa na huduma kutangaza na kutafuta masoko endelevu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana kutokana na maonesho hayo ni ununuzi wa papo kwa papo wenye thamani ya shilingi bilioni 7.6 kutokana na jumla ya watembeleaji 385,000 wa maonesho hayo. Mauzo hayo ni sawa na ongezeko la 94.7% ikilinganishwa na mauzo ya papo kwa papo ya shilingi bilioni 3.63 yaliyofanyika katika maonesho ya 48 ya biashara ya Kimataifa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni kupatikana kwa miadi za kibiashara zenye thamani ya shilingi bilioni 4.8 iliyofanyika katika sekta za teknolojia, mifugo, usafirishaji, madini, kilimo, uvuvi na ujenzi, uzinduzi wa Rajamu ya Taifa *(Made in Tanzania)* na kampuni nane zilizosajiliwa kupitia rajamu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukwaa ya Kitaifa na Kimataifa. Wizara imefanikiwa kuratibu ushiriki wa Watanzania 175 katika Maonesho ya Dunia ya *Expo* Osaka Japan 2025, yaliyofanyika Osaka Japan kuanzia Aprili hadi Oktoba, 2025. Kupitia jukwaa hilo, jumla ya wageni 4,514,000 walitembelea banda la Tanzania kuanzia Aprili hadi Oktoba, 2025, ambapo bidhaa 134 za madini na mazao zilinadiwa na kuuzwa. Vilevile, zilisainiwa hati za makubaliano nane kati ya mashirika ya Tanzania na Japan zenye thamani ya shilingi bilioni 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha kitengo cha intelijensia ya masoko na viwanda. Katika mazingira ya sasa ya ushindani wa kibiashara na viwanda duniani, upatikanaji wa taarifa sahihi za uhakika na za wakati kuhusu masoko na teknolojia za viwanda ni suala la muhimu katika maendeleo ya sekta ya viwanda na biashara. Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza viwanda na kuongeza mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kumekuwa na ukosefu wa taarifa za masoko ya Kimataifa kutokujua bidhaa zinazohitajika katika misimu ya mahitaji, viwango vya ubora na vikwazo vya kibiashara na ugumu wa kutofautisha wawekezaji makini na wale wenye nia ya *dumping* pamoja na ukosefu wa taarifa za uwezo wao wa kifedha na kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imedhamiria kuanzisha kitengo cha intelijensia ya masoko na viwanda. Kitengo hicho kitatekeleza majukumu ya kukusanya na kuchambua taarifa za masoko ya Kimataifa, kubaini fursa za bidhaa, mwenendo na mahitaji na vigezo vya kuingia sokoni, kuandaa na kusambaza taarifa za fursa za masoko kwa wafanyabiashara, na kutoa taarifa za tahadhari za haraka kuhusu mabadiliko ya masoko. Kuanzishwa kwa kitengo hicho ni hatua

muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda unaotegemea taarifa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa biashara. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* imefanikiwa kusajili jumla ya kampuni 16,864 kati ya 19,640 zilizokusudiwa, sawa na 86% ya lengo. Majina ya biashara 30,631 yalisajiliwa, kati ya 33,800 yaliyopangwa, ambayo ni sawa na 91% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la alama za biashara na huduma alama 2,804 zilisajiliwa kati ya 3,600 sawa na 78% ya lengo la mwaka. Kwa upande wa maombi ya hataza, wakala ilitoa hataza 44 kati ya 40 zilizolengwa, sawa na 110% ya makadirio. Sambamba na hayo, wakala ilitoa vyeti vya usajili wa viwanda 42 kati ya 65 vilivyokusudiwa ambapo ni 65% ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kurahisisha mazingira ya kufanya biashara nchini, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wadau wengine imeendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali. Sheria zilizofanyiwa mapitio ni pamoja na Sheria ya Makampuni Sura 212, Sheria ya Majina ya Biashara Sura 213, Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura ya 326, Sheria ya Usajili wa Hataza na Sheria ya Alama na Bidhaa Sura 85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba masuala mengine ikiwemo utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala pamoja na uendelezaji wa bunifu kupitia Programu Atamizi, yote hayo yaweze kuingia katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yanavyosomeka katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027. Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Dira 2050, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 - 2030/2031), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Sera na Sheria mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara, Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge, na

Maagizo mbalimbali ya Viongozi. Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele saba kwa kadiri ambavyo vinaonekana na vinasomeka katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki ambacho dunia inabadilika kwa kasi kupitia maendeleo ya teknolojia, uchumi wa kidijiti na matumizi ya taarifa, ni muhimu kwa nchi yetu kuwekeza katika ubunifu na ujasiriamali wa vijana. Kwa sasa, mfumo wa biashara duniani umejikita katika huduma zinazotolewa kidijiti ambapo inategemewa mauzo ya biashara ya kidijiti yatakuwa mara mbili zaidi ya biashara ya bidhaa. Hivyo, kuna kila sababu ya kuhakikisha tunawawezesha vijana ambao wanaingia kwa wingi katika soko la ajira kunufaika na fursa hii inayoendelea kwa kasi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu kazi na namna ambavyo tumejipanga katika hilo yanapatikana kupitia vipaumbele vya Wizara katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 82 hadi 91.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha, ninaomba nitoe shukrani za dhati kwa mara nyingine tena kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Watanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutupatia rasilimali fedha zinazoendelea kuimarisha sekta yetu. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, kwa miongozo anayonipatia katika nyakati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninawashukuru tena viongozi wenzangu wa Wizara ambao ni Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wa kutosha ambao wananipatia katika usimamizi wa Wizara hii. Aidha, sitakuwa muungwana nisipoishukuru Menejimenti ya Wizara, wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wa Wizara na taasisi kwa moyo wa uzalendo na kujitolea wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi, hususan Baraza la Taifa la Biashara, Taasisi ya Sekta Binafsi

Tanzania, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania, Chemba ya Taifa ya Biashara, Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania, Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Wamiliki wa Viwanda na Wajasiriamali wote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninazishukuru benki mbalimbali kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wadau mbalimbali tunaoshirikiana nao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara wakiwemo Washirika wetu wa Maendeleo na wadau wa ndani na nje ya Taifa letu ambao ni *Trade Mark* Africa, *KOICA, UNIDO, JICA* na wengineo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti, Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Kilimo na Mifugo na Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wanatupa ushirikiano katika majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha. Katika mwaka 2026/2027, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 137,812,633,000 kwa Fungu 44. Kati ya fedha hizo, shilingi 104,122,530,000 ni matumizi ya kawaida, na shilingi 33,690,103,000 ni matumizi ya maendeleo. Vilevile, katika shilingi 104,122,530,000 za matumizi ya kawaida, shilingi 78,049,345,000 ni mishahara na shilingi 26,073,185,000 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu inapatikana katika tovuti yetu ya Wizara www.mit.go.tz

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja.

22 MEI, 2026

HOTUBA YA MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (MB.), WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika; kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 24 na 26 Machi, 2026, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/2026. Aidha, ninaliomba Bunge lako likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2026/2027.

2. Mheshimiwa Spika; nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa afya njema na kuwepo hapa siku hii muhimu ya leo.

3. Mheshimiwa Spika; kwa unyenyekevu na moyo wa shukrani, nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Kupitia bunge hili tukufu nimuahidi Mheshimiwa Rais kushirikiana na watendaji wenzangu akiwemo Naibu Waziri, Watumishi wa Wizara na Taasisi pamoja na wadau wote wa Wizara katika kutekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia ili tuweze kufikia malengo mahsusi ya kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara.

4. Mheshimiwa Spika; naomba nitumie tena fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Balozi Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi hawa

wamekuwa wakitoa miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Viwanda na Biashara. Nawashukuru sana.

5. Mheshimiwa Spika; napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kipindi kingine. Hii ni kutokana na utendaji wake mzuri ambao umewapa wananchi wa Zanzibar imani juu yake.

6. Mheshimiwa Spika; ninapenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini na umahiri wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Halikadhalika, nawapongeza watoa hoja wote waliowasilisha hotuba zao kabla yangu. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya Bajeti aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 1 Aprili, 2026. Hotuba hiyo inatoa hali ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa Mwaka 2025/2026 pamoja na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa Mwaka 2026/2027 katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Viwanda na Biashara.

7. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026 Bunge lako Tukufu liliondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge,Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Ismani; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Naomba nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika; Waheshimiwa Wabunge wote; familia; ndugu na jamaa; na wananchi.Tunaomba mwenyezi Mungu aendelee kuwapa pumziko la milele.

8. Mheshimiwa Spika; kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Kondoa Mjini. Kamati hii imekuwa na mchango Madhubuti kwa

Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kupitia maelekezo, maoni na ushauri katika masuala mbalimbali hususan maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

9. ***Mheshimiwa Spika;*** kwa moyo wa shukrani namshukuru Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri na Mbunge wa Mikumi kwa umadhubuti wake na kwa mchango mkubwa anaoutoa katika Wizara yetu. Naibu Waziri ni kiongozi mchapakazi, anayejituma na anayependa kazi yake. Namshukuru, Mheshimiwa Balozi Waziri Rajab Salum, Katibu Mkuu kwa utendaji wake mahiri, Bw. Aristides Robert Mbwasi, Naibu Katibu Mkuu, viongozi wa Bodi, watendaji na watumishi wote wa Wizara na taasisi zote 13 zilizo chini ya Wizara, pamoja na wasaidizi wa ofisi yangu, katibu wangu Bi. Loyce Lubonera, Dereva wangu, Bw. Paul Mtulo na Mwandishi Mwendesha Ofisi yangu, Bi. Pheby Bundala. Nawashukuru kwa utumishi wao.

10. Mheshimiwa Spika; ninapohitimisha salamu za awali na za shukrani, naomba niishukuru familia yangu, Mume Wangu kwa namna anavyonipa utulivu unaonisaidia katika kutimiza majukumu yangu. Namshukuru sana yeye, Watoto wetu na wazazi wangu kwa namna wanavyoniwezesha kufanya majukumu yangu kwa ufanisi. Mwisho kwa hatua hii, nawashukuru sana, wananchi wenzangu wa Jimbo la Mbinga Vijijini, kwa kunipa kura za heshima za kuwa Mbunge wa kwanza mwanamke wa Jimbo letu. Nawaahidi kuwatumikia kwa upendo na moyo thabiti.

11. Mheshimiwa Spika; baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 na mpango wa mwaka 2026/2027.

2. HALI NA MWENENDO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

2.1 Viwanda

12. Mheshimiwa Spika*;* Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara ili kuchochea mageuzi ya uchumi

fungamanishi, jumuishi na shindani unaojengwa katika msingi wa kuongeza thamani ya rasilimali zinazozalishwa nchini na kuimarisha viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa wingi kwa kutumia malighafi za ndani. Jitihada hizo ni utekelezaji wa malengo ya Dira 2025 ambayo yamejielekeza katika kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa muhimu, kuzalisha bidhaa bora, kutoa ajira kwa wingi na kuongeza mauzo nje ya nchi. Kupitia mwelekeo huo, viwanda vipya vimejengwa na vingine vimefanyiwa upanuzi.

13. Mheshimiwa Spika; katika kipindi cha mwaka 2025/2026 jumla ya viwanda vipya vikubwa na vya kati 25 katika sekta mbalimbali vimejengwa na kuanza uzalishaji. Viwanda hivyo vimetoa jumla ya ajira 39,250 ambapo ajira za moja kwa moja ni 7,635 na zisizo za moja kwa moja ni 31,615.

2.1.1 Hali ya Uzalishaji Viwandani

14. Mheshimiwa Spika; hali ya uzalishaji viwandani imeendelea kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika uchumi. Naomba uniruhusu nielezee kuhusu baadhi ya viwanda vinavyozalisha bidhaa muhimu zinazotumika kwa wingi nchini na vyenye uwekezaji mkubwa.

A. Viwanda vya Mabati

15. Mheshimiwa Spika; Tanzania ina viwanda vikubwa vitano (5) vya mabati ambavyo ni Lodhia, MMI Steel, ALAF Limited, Kinglion na GSM Roofing Sheet ambavyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mabati tani 410,000 ya rangi na tani 700,000 meupe kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda hivyo vimezalisha jumla ya tani 350,000 za mabati ya rangi na tani 500,000 ya mabati meupe sawa na asilimia 70 ya uzalishaji wa mabati nchini. Aidha, mahitaji ya mabati ya rangi ni takriban tani 250,000 na mabati meupe ni 380,000. Mabati ya ziada huuzwa katika nchi za Burundi, Rwanda, DRC na Malawi. Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 2,300 na zisizo za moja kwa moja 11,500.

16. Mheshimiwa Spika; kati ya viwanda hivyo vikubwa, kiwanda cha GSM Roofing Sheet kilichopo Dar es salaam ni kipya na kinazalisha mabati ya rangi chenye uwezo uliosimikwa wa

kuzalisha mabati tani 150,000 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 800 na zisizo za moja kwa moja 3,000. Hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda kimezalisha mabati tani 45,000. Pamoja na kukidhi uzalishaji kwa ajili ya matumizi ya ndani ya mabati, Wizara kupitia NDC, inatekeleza mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mabati na kupunguza uagizaji wa malighafi kutoka nje ya nchi kwa kusaini mkataba wa mradi wa Maganga Matitu na kampuni ya Fijuan Hexingwang Industry Tanzania Co. Ltd. Mradi huu unakadiriwa kuwa na hifadhi ya chuma tani milioni 101. Hatua iliyofikiwa ni uingizaji wa mitambo ya uchimbaji na uchakataji wa madini ya chuma. Pindi mradi huo utakapoanza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za chuma, utawezesha uanzishwaji wa viwanda vingine vitakavyoongeza mnyororo wa thamani (*downstream processing industries*).

B. Viwanda vya Saruji

17. Mheshimiwa Spika; Tanzania ina jumla ya viwanda 15 vya kuzalisha saruji vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 13,600,000 za saruji kwa mwaka. Kati ya hivyo, viwanda saba (7) vinazalisha clinker na saruji na viwanda nane (8) vinazalisha saruji pekee. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda vimezalisha jumla ya tani 10,300,000 za saruji ambapo mahitaji ya sasa ni takribani tani 8,500,000 kwa mwaka. Saruji ya ziada huuzwa katika nchi mbalimbali zikiwemo Malawi, Zambia, DRC, Rwanda na Burundi. Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 6,020 na zisizo za moja kwa moja 20,280. Ili kuongeza uzalishaji wa saruji nchini, katika mwaka 2025/2026 kiwanda kimoja (1) kinachozalisha saruji kimejengwa. Kiwanda hicho ni WIH holding Limited kilichopo Mkoa wa Kigoma ambacho kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,900,000 za saruji kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 800 na zisizo za moja kwa moja 3,050. Hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda cha WIH Holding Limited kimezalisha saruji tani 1,500,000.

C. Viwanda vya Sukari

18. Mheshimiwa Spika; Tanzania ina jumla ya viwanda saba (7) vya kuzalisha sukari ambavyo ni Kilombero Sugar Company Limited, Tanganyika Planting Company Limited (TPC - Kilimanjaro),

Kagera Sugar Limited (Kagera), Mtibwa Sugar Estates Limited (Morogoro), Mkulazi Holding Company Limited (Morogoro), Manyara Sugar Limited (Manyara) na Bagamoyo Sugar Limited (Pwani). Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha sukari tani 800,000 kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda vimezalisha jumla ya tani 410,979 za sukari ambapo mahitaji ya sukari ni takriban 550,000. Aidha, viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 28,500 na zisizo za moja kwa moja 95,000.

19. Mheshimiwa Spika*;* katika kuhakikisha nchi inapunguza uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi, viwanda viwili (2) vya Mkulazi Holding Company Limited na Kilombero Sugar Company Limited vimefanya upanuzi ili kuongeza uzalishaji wa sukari nchini. Kufuatia upanuzi huo, Kiwanda cha Kilombero kitakuwa na uwezo wa kuzalisha sukari tani 226,000 kutoka tani 123,000 kwa mwaka ambapo majaribio ya uzalishaji yamekamilika na uzalishaji utaanza mwezi Juni, 2026. Aidha, Kiwanda cha Mkulazi kimeongeza mtambo utakaowezesha kuzalisha sukari ya kiwandani (Industrial sugar). Majaribio ya mitambo yamefanyika na tayari kiwanda kimezalisha tani 256 za sukari ya kiwandani. Kukamilika kwa upanuzi huo, kunawezesha viwanda vyote viwili kuzalisha ajira za moja kwa moja 8,500 na zisizo za moja kwa moja 25,000.

D. Viwanda vya Kubangua Korosho

20. Mheshimiwa Spika; Tanzania ina jumla ya viwanda 70 vya kubangua korosho ambapo kati ya viwanda hivyo, viwanda 50 vinafanya kazi, vinne (4) vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi na viwanda 16 havifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uchakavu wa mitambo na teknolojia kupitwa na wakati. Viwanda vinavyofanya kazi vina uwezo uliosimikwa wa kubangua korosho jumla ya tani 108,549 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 6,900 na zisizo za moja kwa moja 18,000 **(Jedwali Na.1).** Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda hivyo vimebangua jumla ya tani 53,125 za korosho ambazo sawa na asilimia 8.6 ya uzalishaji wa korosho ghafi nchini ambapo kwa mwaka 2025/2026 uzalishaji ulikuwa tani 617,680.

21. Mheshimiwa Spika; katika jitihada za kuongeza ubanguaji

wa korosho nchini, jumla ya viwanda sita (6) vya kubangua korosho vimejengwa mwaka 2025/2026 ambavyo ni Work Point LTD; Ares Trading co.Ltd; Er-Kang (T) Co. Ltd; Sis International Ltd; HK International Ltd; na ECO Broom Enterprises ambavyo vipo katika Mkoa wa Mtwara na Lindi. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kubangua korosho tani 11,400 kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 210 na zisizo za moja kwa moja 605. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya kubangua korosho katika mikoa inayozalisha zao hili. Vilevile, katika kuunga juhudi hizo, Wizara kupitia CAMARTEC imejenga kiwanda darasa cha kubangua korosho katika Wilaya ya Manyoni katika Mkoa wa Singida kwa ajili ya kutoa mafunzo na utaalam wa kubangua korosho.

22. Mheshimiwa Spika; pamoja na ujenzi wa viwanda hivyo, uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda unaendelea ambapo jumla ya viwanda vinne (4) vinaendelea kujengwa katika Mkoa wa Mtwara ili kupunguza uuzaji wa korosho ghafi nje ya nchi. Viwanda hivyo ni kiwanda cha Grand Ruby Group Ltd; MATEAK Holdings Ltd; Tanzania Premium Cashews Ltd; na Akros Cashew Factory. Pindi viwanda vitakapokamilika, vitakuwa na uwezo wa kubangua korosho ghafi tani 153,600 kwa mwaka.

E. Viwanda vya Mbolea

23. Mheshimiwa Spika; Tanzania ina jumla ya viwanda 49 ya kuzalisha mbolea ambapo vikubwa ni viwili (2), vya kati ni 10 na vidogo ni 37 **(Jedwali Na. 2).** Viwanda vikubwa ni Minjingu na Itracom Fertilizer Limited na viwanda vya kati ni YARA Tanzania, ETG Inputs. Ltd, Tanga Mining Co. Ltd, Neelkanth Chemical Ltd, ABM Equipments Ltd, HSSL Lime Co. Ltd, Lavan Investment Limited, Dodoma Cement Co.ltd, Fert Pro Ltd pamoja na Tanzania Biotech Products Ltd (TBPL). Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,793,849 za mbolea kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026, viwanda vimezalisha jumla ya tani 123,203 za mbolea na kutoa ajira za moja kwa moja 2,687 na zisizo za moja kwa moja 9,200.

24. Mheshimiwa Spika; katika kupunguza uagizaji wa mbolea kutoka nje hususan mbolea ya chumvichumvi ambayo pia

hutumika malighafi muhimu katika uzalishaji wa mbolea nyingine hapa nchini, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta mwekezaji mahiri atakayeweza kutumia gesi asilia kuzalisha mbolea hiyo.

F. Viwanda vya Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba

25. Mheshimiwa Spika*;* Tanzania ina viwanda 14 vya kuzalisha dawa za binadamu na vifaa tiba ambavyo ni Zenufa Laboratories (T) Limited; Shelys Pharmaceuticals Limited; Prince Pharmaceuticals Ltd; Kairuki Pharmaceuticals Industry Ltd; Mansoor Daya Chemical Industries; Keko Pharmaceuticals (1997) Limited; Alfa Pharmaceuticals Limited; Katwaza Pharmaceuticals Industry Ltd; A.A Pharmaceuticals Ltd; Sri Balaj Pharmaceuticals Ltd; Bhanji Pharmaceuticals Ltd; Cure Afya Pharmaceuticals Limited; Tanzania Pharmaceutical Industries (TPI) ARV Ltd; na ER-KANG Tanzania. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha asilimia 20 ya dawa na vifaa tiba zinazohitajika hapa nchini. Katika kukabiliana na uagizaji wa dawa kutoka nje ya nchi, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mahsusi ili kuhakikisha sekta hii inaongeza uwekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba angalau kufikia asilimia 60 ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba ifikapo 2035.

26. Mheshimiwa Spika: katika mwaka 2025/2026 jumla ya viwanda 11 vimejengwa na kuanza majaribio ya uzalishaji wa dawa za binadamu na vifaa tiba. Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) vinazalisha maji tiba, viwanda vitatu (3) vitendanishi vya maabara, viwanda vitatu (3) dawa za vidonge na maji na viwanda vitatu (3) vinazalisha vifaa tiba. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha vizio (units) bilioni 3.5 za dawa za binadamu na kutoa ajira za moja kwa moja 4,200 na zisizo za moja kwa moja 21,000. Hadi kufikia Aprili, 2026 viwanda hivyo vimezalisha vizio (units) bilioni 1.2 za dawa za binadamu. Aidha, kiwanda cha kuzalisha dawa za kufubaza virusi vya ukimwi (ARV) cha Tanzania Pharmaceutical Industries (TPI) kilichopo Arusha kimeanza ukarabati ikiwa ni juhudi za kuzalisha dawa hizi hapa nchini.

G. Viwanda vya Mafuta ya Kula

27. Mheshimiwa Spika; Tanzania ina jumla ya viwanda 1,604 vya kuzalisha mafuta ya kula ambapo 1,038 ni vidogo sana, 543 vidogo, tisa (9) vya kati na 14 vikubwa. Viwanda hivi vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mafuta ya kula tani 2,527,739 kwa mwaka na vimetoa ajira za moja kwa moja 10,755 na zisizo za moja kwa moja 36,416. Aidha, viwanda hivyo vinazalisha tani 302,000 za mafuta ambapo mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takriban tani 700,000 kwa mwaka. Hivyo tani 430,000 huagizwa ili kutosheleza mahitaji ya ndani.

28. Mheshimiwa Spika; Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za nchi kujitosheleza na mahitaji ya mafuta ya kula. Juhudi hizo zinajumuhisha kuzalisha mbegu bora na kuzigawa kwa wakulima; kutoa ruzuku ya mbolea; kuendelea kuhamasisha wawekezaji wakubwa kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula; na kuendelea kuboresha teknolojia za wasindikaji wadogo.

29. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026, kiwanda cha Vion Win Ltd cha kukamua na kusafisha mafuta ya kula ya alizeti pamoja na kuzalisha mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo kilichopo Mkoa wa Singida kimejengwa. Kiwanda hicho kimewekeza mtaji wa takriban shilingi bilioni 5.5. Hadi kufikia Aprili, 2026, kiwanda kimetoa ajira za moja kwa moja 70 na zisizo za moja kwa moja 300. Kiwanda kina uwezo uliosimikwa wa kuchakata tani 100 za mbegu za alizeti kwa siku. Aidha, kiwanda cha Mainland Group Agro Process Co. Ltd kilichopo Dodoma kimefanya upanuzi utakaowezesha kiwanda kusindika mbegu za alizeti kiasi cha tani 150,000 kutoka tani 75,000 kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026 kiwanda kimezalisha mafuta ya kula tani 48,000 na kutoa ajira za moja kwa moja 450 na zisizo za moja kwa moja 2,000.

2.1.2 Viwanda Vingine Vipya Vilivyojengwa

30. Mheshimiwa Spika; viwanda vipya vilivyojengwa katika sekta ndogo nyingine ni vifuatavyo:

a) Kiwanda cha Afriport Apparel

31. Mheshimiwa Spika; Kiwanda cha *Afriport Apparel* kilichopo jijini Dar es Salaam ni uwekezaji wa kimkakati unaozalisha nguo maalum za kujikinga mahala pa kazi (protective gears). Kiwanda kimewekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 8.8 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha jozi milioni 10 za mavazi kwa mwaka na kutoa ajira za moja kwa moja 1,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 2,500. Kiwanda kilianza uzalishaji mwezi Februari, 2026 na hadi kufikia Aprili, 2026 kimezalisha jozi 50,000 za mavazi na kutoa ajira za moja kwa moja 200 na zisizo za moja kwa moja 600.

b) Kiwanda cha Giant Group Co. Ltd

32. Mheshimiwa Spika; Kiwanda cha Giant Group Co. Ltd kipo Mkoa wa Pwani na kinazalisha nyaya na vifaa vya umeme. Kiwanda kimewekeza mtaji wa takriban dola za Marekani milioni 15 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha nyaya za umeme tani 4 kwa siku. Hadi kufikia Aprili, 2026, kimezalisha tani 520 na kutoa ajira za moja kwa moja 120 na zisizo za moja kwa moja 250.

c) Kiwanda cha Magodoro cha Federal

33. Mheshimiwa Spika; Kiwanda cha Federal kilichopo Mkuranga, Mkoa wa Pwani, kinazalisha magodoro ya sponji (foam), mito na bidhaa nyingine za malazi. Kiwanda kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 8.7 na kina uwezo wa kuzalisha wastani wa magodoro 1,000 kwa siku. Hadi kufikia Aprili, 2026, kiwanda kimezalisha magodoro 8,000 na kutoa ajira za moja kwa moja 140 na zisizo za moja kwa moja 350.

d) Kiwanda cha Dawa za Mifugo cha FarmBase

34. Mheshimiwa Spika; Kiwanda cha FarmBase kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam, kinajishughulisha na utengenezaji wa dawa za mifugo na virutubisho. Kiwanda kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 10.2 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha dawa za mifugo za maji na unga tani 200,000 kwa mwaka. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya tani 152.7 za dawa za maji na unga zimezalishwa na kutoa ajira za moja kwa moja 95 na zisizo za moja

kwa moja 200. Bidhaa hizo huuzwa nchini na katika nchi za Zambia na Malawi.

e) Kiwanda cha Starlink Gulf Trading Ltd

35. Mheshimiwa Spika; Kiwanda cha Starlink Gulf Trading Ltd kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani, kinazalisha chokaa (white skim wallputty) na kimewekeza mtaji wa shilingi bilioni 15 kikiwa na uwezo wa kuzalisha wastani wa chokaa tani 900 kwa siku. Hadi kufikia Aprili, 2026, kiwanda kimezalisha tani 113,400 na kutoa ajira za moja kwa moja 200 na zisizo za moja kwa moja 360. Bidhaa hizo huuzwa nchini na katika nchi za DRC, Burundi, Zambia na Malawi.

2.2 Biashara

A. Hali ya Biashara Duniani

36. Mheshimiwa Spika; biashara ya Tanzania nje ya nchi imekuwa ikiongozeka mwaka hadi mwaka. Mathalan thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 10,080.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,702.0 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 16. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa mikakati ya kuboresha mazingira ya biashara nchini, utafutaji wa masoko, kuzalisha bidhaa zinazokidhi ushindani nje ya nchi na kupunguza milolongo ya hatua za kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na mazao ghafi ya kilimo kama; ufuta, tumbaku, mbaazi, ngano, mchele maharage, mahindi, kahawa, pamba na parachichi; Mazao ghafi ya Mifugo ni pamoja na, samaki na bidhaa za viwandani ikiwa ni pamoja na dhahabu, kakao, makaa ya mawe, vigae, na mabati.

37. Mheshimiwa Spika; mwaka 2025, bidhaa zilizoingizwa nchini zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 16,031.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 15,684.5 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Ongezeko hilo linatokana na kuagiza kwa wingi bidhaa ambazo hazizalishwi hapa nchini na zinazotumia teknolojia ya juu. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na bidhaa za mitaji (Capital goods), magari, bidhaa za kutengeneza lami, bidhaa za chuma, mashine mbalimbali za

hospitalini, madawa baridi, mafuta ya petroli na gesi na sukari ya viwandani **(Jedwali Na.3)**.

B. Soko la Umoja wa Ulaya (EU)

38. Mheshimiwa Spika; mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda nchi za Umoja wa Ulaya yameongezeka kufikia dola za Marekani milioni 943.8 kutoka dola za Marekani milioni 686.3 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 37.5. Ongezeko hilo limetokana na kuimarika kwa ushiriki wa wafanyabiashara wa Tanzania katika soko hilo, juhudi za Serikali na sekta binafsi katika kuboresha ubora wa bidhaa ili kukidhi viwango vya soko la Umoja wa Ulaya na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za kikaboni (organic products). Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na maharage, tumbaku, samaki, parachichi, kahawa, kakao, asali, mafuta ya alizeti, madini, chai, maua, matunda, pamba, mbogamboga, ngozi na vito vya thamani.

39. Mheshimiwa Spika; kwa mwaka 2025, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Umoja wa Ulaya ilikuwa dola za Marekani milioni 1,260.13 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,267.6 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 0.6. Upungufu huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani wa baadhi ya bidhaa kama vile mafuta ya kula, bidhaa za plastiki na vifaa vya msingi viwandani. Bidhaa zinazoagizwa kwa wingi kutoka Umoja wa Ulaya ni pamoja na mashine na mitambo inayotumiwa viwandani, vifaa vya usafiri, kemikali, dawa za binadamu, vifaa vya umeme, mbolea, plastiki na bidhaa zake **(Jedwali Na.4)**.

C. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

40. Mheshimiwa Spika; mwaka 2025 Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 1,264.6 katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ikilinganishwa na dola za Marekani Milioni 1,163.8 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya biashara nchini na kuimarika kwa uzalishaji wa bidhaa ambazo zina soko kubwa katika Jumuiya ya

Afrika Mashariki. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni vitunguu, samaki, karanga, nyanya, asali, maharage, mbaazi, dagaa, mahindi, ngano, mchele, karatasi, mabati na vigae.

41. Mheshimiwa Spika; mwaka 2025 bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 563.1 ziliagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 527.3 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Ongezeko hilo limetokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani nchini na kupelekea kuongeza manunuzi ya bidhaa za Viwandani kutoka nchi za jirani ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni sabuni za kuogea, vifaa vya mitaji, vyakula vilivyosindikwa, misumari, dawa za viatu, maziwa na vifaa vya usafirishaji **(Jedwali Na.5)**.

D. Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

42. Mheshimiwa Spika; mwaka 2025 thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ilikuwa dola za Marekani milioni 3,545.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,968.0 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 19.4. Ongezeko hilo limechangiwa na mauzo ya bidhaa kama vile madini, samaki, nyanya, vitunguu, maharage, viazi vitamu, ndizi, nanasi, parachichi, machungwa, majani ya chai, mchele, kahawa, vyandarua, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka.

43. Mheshimiwa Spika; bidhaa zilizoagizwa kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 837.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 786.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Bidhaa zilizoagizwa ni pamoja na pombe aina ya *whisky*, mbegu za alizeti, vifaa vya usafi, meza za mbao, magari, kemikali, na juisi mchanganyiko **(Jedwali Na. 6)**.

E. Bara la Asia

44. Mheshimiwa Spika: mwaka 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda baadhi ya nchi za Bara la Asia tunazofanya biashara kwa wingi hususan kwa nchi za China, India na

Japan ilikuwa dola za Marekani milioni 3,213.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,840.3 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 13.1(Jedwali Na. 5). Ongezeko hilo lilichangiwa na uhitaji mkubwa wa bidhaa kama vile ufuta, kakao na parachichi. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na madini, mazao jamii ya kunde, korosho, parachichi, pamba, tumbaku, ufuta, kakao na samaki.

45. Mheshimiwa Spika: uagizaji wa bidhaa kutoka baadhi ya nchi za Bara la Asia ulikuwa na thamani dola za Marekani milioni 10,093 mwaka 2025 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,514.2 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 83. Ongezeko hilo limechangiwa na uhitaji mkubwa wa bidhaa na huduma katika Sekta ya Usafirishaji na Uchukuzi. Bidhaa zilizonunuliwa kwa wingi ni pamoja na magari; pikipiki; mafuta ya gesi na petrol; bidhaa za chuma; dawa na vifaa tiba; matairi; na mabehewa ya treni **(Jedwali Na. 7)**.

i. China

46. Mheshimiwa Spika; katika nchi ya China, Tanzania inanufaika na msamaha wa malipo ya ushuru wa forodha kwa asilimia 98 ya bidhaa zote zinazouzwa kwenye soko la China. Mwaka 2025 mauzo ya Tanzania kwenda nchini China yalikuwa dola za Marekani milioni 512.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 442.96 mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi China zilikuwa ni madini na makinikia, minofu ya samaki, mbegu za ufuta, tumbaku, mafuta ya ufuta, pamba na kahawa.

47. Mheshimiwa Spika; uagizaji uliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 5,643.3 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 4,780.15 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 18.1. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na zana za kilimo; pikipiki za miguu miwili na mitatu; mashine na mitambo; bidhaa za chuma; rola za mabati; transfoma; magari na bomba (**Jedwali Na.8**).

ii. **India**

48. Mheshimiwa Spika; mwaka 2025 mauzo ya Tanzania kwenda India yalikuwa dola za Marekani milioni 938.03 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,637.03 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 42.7. Upungufu huo umechangiwa na kushuka kwa mauzo ya bidhaa za korosho, madini (dhahabu na shaba) na pamba ambazo ziliuzwa kwenye masoko mengine kama vile China. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni korosho; mbaazi; dhahabu; njegere; pamba; na parachichi.

49. Mheshimiwa Spika; mwaka 2025 bidhaa zilizoagizwa kutoka India zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 2,041.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,130.65 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 4.2. Upungufu huo ulitokana na bidhaa kama vile pikipiki kupatikana katika masoko mengine kama vile China. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na mafuta ya petroli; dawa na vifaa tiba; vifaa vya ujenzi; mapazia; pikipiki za miguu miwili na mitatu; na sukari nyeupe (**Jedwali Na. 9**).

iii. **Japan**

50. Mheshimiwa Spika; kwa upande wa Japan, mwaka 2025 mauzo ya Tanzania kwenda Japan yalikuwa dola za Marekani milioni 110.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 99.82 mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamba, kakao, samaki, ufuta, pareto na bidhaa za mkonge na nyuzi.

51. Mheshimiwa Spika; thamani ya bidhaa zilizoagizwa iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 692.4 mwaka 2025 kutoka dola za Marekani milioni 593.2 mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na magari, vifaa vya magari, mitambo, rola ya mabati, baiskeli, matairi ya magari na machine mbalimbali (**Jedwali Na.10**).

2.3 Mchango wa Sekta ya Viwanda na Biashara Nchini

52. Mheshimiwa Spika; Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2025 ulikuwa asilimia 5.9 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2024 **(Jedwali Na. 11).** Pamoja na kushuka kwa mchango wa sekta katika Pato la Taifa, Sekta ya viwanda imeendelea kukua ambapo katika mwaka 2025 imekuwa kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2024 **(Jedwali Na.12).**

53. Mheshimiwa Spika; Mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa kwa mwaka 2025 umeendelea kuwa asilimia 8.6 sawa na mwaka 2024 **(Jedwali Na. 13)**. Aidha, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Biashara ilikuwa asilimia 5.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara **(Jedwali Na. 14)**.

2.4 Sera Zilizofanyiwa Marejeo

54. Mheshimiwa Spika; katika kuboresha mazingira ya ujenzi wa viwanda na ufanyaji biashara, Wizara katika mwaka 2025/2026 imekamilisha mapitio ya sera mbili (2) ambazo ni Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 1996-2020 ambayo kwa sasa inajulikana kama Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025; na Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara ya Mwaka 2003 ambayo kwa sasa inajulikana kama Sera ya Maendeleo ya Jasiriamali Ndogo na za Kati ya Mwaka 2003 (Toleo la Mwaka 2025).

55. Mheshimiwa Spika; Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025 ina lenga kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine; kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati; kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa masoko ya bidhaa za ndani na nje ya nchi; kuwezesha utafiti na ubunifu wa teknolojia za viwanda; na kujumuisha masuala mtambuka katika maendeleo ya viwanda. Aidha, Sera inayosimamia wajasiriamali inalenga kuimarisha miundombinu wezeshi ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati; kuimarisha ukuaji wa jasiriamali; kuongeza matumizi ya teknolojia na ubunifu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati;

kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo na wa kati; kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wa kati; na kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati.

3. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

56. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ilani ya CCM, Mpango Mkakati wa Wizara, Mipango mingine ya Kitaifa, maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Itifaki na makubaliano ya kikanda na kimataifa. Vilevile, Wizara imetekeleza maeneo ya kipaumbele yakiwemo kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda na biashara nchini; na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ya Liganga na Mchuchuma na Magadi soda Engaruka.

57. Mheshimiwa Spika; maeneo mengine ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mitaa ya viwanda (Industrial Clusters) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati; kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi; kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; kuimarisha usimamizi wa ubora na usalama wa bidhaa nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vipodozi; na kuratibu majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa.

3.1 Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026

3.1.1 Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa

58. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026 Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 135,788,232,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 93,900,697,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 41,887,535,000.00 ni za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea shilingi 95,630,301,245.82 sawa na asilimia 70.43 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi

74,603,022,813.73 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 21,027,278,432.09 ni za miradi ya maendeleo.

3.1.2 Fedha za Matumizi ya Kawaida

59. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa shilingi 93,900,697,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,081,317,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi 75,819,380,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea jumla ya shilingi 74,603,022,813.73, sawa na asilimia 79.45 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 14,336,465,376.94 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na shilingi 60,266,651,284.37 kwa ajili ya Mishahara.

3.1.3 Fedha za Maendeleo

60. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa shilingi 41,887,535,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 27,870,710,000 ni fedha za ndani na shilingi 14,016,825,000 ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara ilipokea shilingi 21,027,278,432.09 sawa na asilimia 75.45 ya bajeti ya fedha za ndani za maendeleo.

3.2 Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2025/2026

3.2.1 Maendeleo ya Viwanda

A. Kuendeleza Miradi ya Kimkakati na Kielelezo

i. Mradi Unganishi wa Liganga na Mchuchuma

61. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026, Wizara imekamilisha majadiliano na Mwekezaji wa Kampuni *ya Shudao Investment Group Company Limited (SDIG)* kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma. Mwekezaji huyu mpya ni Kampuni inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambayo imeinunua Kampuni awali ya *Sichuan Hongda Group Company Limited (SHG)* kwa lengo la kutekeleza Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC).

62. Mheshimiwa Spika; kupitia majadiliano hayo, pande zote mbili zimefikia makubaliano ya misingi sahihi ya mgawanyo wa hisa na muundo wa uwekezaji (share holders' structure and financing structure); kiwango cha mtaji wa uwekezaji unaohitajika; muundo shirikishi wa usimamizi na uendeshaji wa mradi; muda wa mikataba ya uwekezaji; uhuishaji wa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi; uandaaji wa modeli ya kifedha ya pamoja; vivutio vya uwekezaji vinavyoendana na sheria za Tanzania; na uongezaji wa thamani kwa madini yote yakiwemo chuma, vanadium, na tatinium hapa nchini. Vilevile, uandaaji wa rasimu za mikataba ya ubia (JVAs) na mikataba ya wanahisa (SHAs) kwa miradi ya uchimbaji na kiwanda cha kutengeneza bidhaa za chuma umekamilika. Kwa ujumla, majadiliano hayo yamekamilika kwa mafanikio makubwa na kwa sasa pande zote zinawasiliana na Mamlaka zao kwa ajili ya hatua za idhini. Hii ni hatua ya kihistoria kwa mradi huu wa kielelezo kwa Taifa letu ambao utakuwa na manufaa makubwa. Aidha, mikataba ya ubia na wanahisa inatarajiwa kusainiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2026/2027 ambapo ujenzi wa miradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu.

63. Mheshimiwa Spika; kutekelezwa kwa mradi huo kutawezesha nchi kuokoa matumizi ya dola za Marekani bilioni 1.22 sawa na shilingi trilioni 3.2 ambazo zimekuwa zikitumika kununua bidhaa za chuma kutoka nje ya nchi ikiwa ni bidhaa ya pili kwa matumizi makubwa ya fedha za kigeni baada ya bidhaa za mafuta ya petroli. Vilevile, utekelezaji wa mradi utaongeza mnyororo wa thamani kwa bidhaa mbalimbali zitakazozalishwa kupitia viwanda vingine vitakavyoanzishwa; na utaondoa au kupunguza uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na mahitaji ya chuma chakavu katika uzalishaji wa bidhaa za chuma.

64. Mheshimiwa Spika; kwa mujibu wa taarifa za awali za moduli (joint financial model) iliyoandaliwa kwa pamoja na wataalam wa Serikali na mwekezaji, makadirio ya mapato ya Serikali kutokana na kodi mbalimbali pamoja na malipo ya mrahaba kwa kipindi cha miaka 25 ni jumla ya Dola za Marekani trilioni 1.99. Aidha, mapato ya mradi yatatokana na mauzo ya umeme, makaa ya mawe, bidhaa za chuma, titanium, vanadium na aluminium sulphate. Vilevile, utekelezaji wa mradi huu utawezesha

kupatikana kwa ajira za moja kwa moja 6,500 na zisizo za moja kwa moja 26,000.

ii. Mradi wa Magadi Soda Engaruka

65. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia NDC imeendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa kimkakati na kielelezo wa Magadi Soda uliopo katika bonde la Engaruka Wilaya ya Monduli kwa kulipia leseni ya uchimbaji, kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi, na kutafuta mwekezaji. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla shilingi bilioni 5.82 sawa na asilimia 98.7 ya fedha ya fidia ililipwa kwa wafidiwa 513 kati ya wafidiwa 594. Zoezi la kukamilisha ulipaji fidia linaendelea kwa wafidiwa 81 waliobaki ambao wanakamilisha nyaraka zao zikiwemo nyaraka za mirathi. Vilevile, Wizara imefanikiwa kupata mwekezaji na kwa sasa, Timu ya Serikali ya Majadiliano (GNT) inaendelea na majadiliano ya mkataba wa ubia na kampuni iliyoshinda zabuni. Kutekelezwa kwa mradi huo kutaokoa fedha za kigeni zaidi ya dola za Marekani milioni 121 zinazotumika kwa mwaka kuagiza malighafi ya magadi soda pamoja na bidhaa zinazotokana na magadi soda kutoka nje ya nchi.

iii. Mradi wa Chuma cha Maganga Matitu

66. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia NDC imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maganga Matitu unaotekelezwa kwa ubia kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Kampuni ya Fujian Hexingwang Industry Tanzania Co. Ltd. Hadi kufikia Aprili, 2026 malipo ya fidia yamefanyika ambapo wananchi 380 kati ya 385 sawa na asilimia 98.7 ya wananchi waliopisha mradi, wamelipwa fidia kiasi cha Shilingi bilioni 4.196. Malipo ya fidia kwa wanufaika waliobaki yatafanyika pindi watakapokamilisha taratibu za uhakiki. Kwa sasa, shughuli za kutekeleza mradi zinaendelea ambapo mitambo ya kiwanda imeanza kuingia nchini.

B. Kuendeleza miundombinu ya msingi katika Kongani ya Viwanda – TAMCO

67. Mheshimiwa Spika; Kongani ya Viwanda ya TAMCO iliyopo Kibaha, Mkoa wa Pwani ni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za

uzalishaji ikiwemo uunganishaji wa mitambo na magari, uzalishaji wa dawa na vifaa tiba, uzalishaji wa bidhaa nyingine pamoja na huduma saidizi. Eneo hilo lina jumla ya viwanda 14 ambapo viwanda 12 vinafanya kazi na viwili (2) vipo katika hatua ya uwekezaji. Hadi kufikia Aprili, 2026, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu muhimu ikiwemo barabara za ndani kwa kiwango cha lami ambapo kiasi cha kilomita 1.8 zimejengwa. Vilevile miundombinu ya umeme imeboreshwa na wawekezaji wanapata umeme wa uhakika. Viwanda vilivyopo katika Kongani ya TAMCO ni Tanzania Biotech Products Ltd (TBPL) ambayo ni kampuni tanzu ya NDC; Hester Bioscience Ltd; Global Packaging (T) Ltd; Motor Hub East Africa Ltd (TATA Holdings); China Boda Ltd; New Force Company Ltd; Konfa Enterprises; Loti Energies; Hero Sound Traders Ltd; UC General Investment Limited; GF Assemblers Ltd; na Fortes Energies Ltd. Viwanda hivyo kwa pamoja vimetoa jumla ya ajira 853.

68. Mheshimiwa Spika; juhudi za Serikali zimeendelea kuvutia wawekezaji zaidi, akiwemo Hyundai Automobile Manufacturing ambaye ameanza maandalizi ya kuanzisha kiwanda cha kuunganisha magari; Goodlife Investment Tanzania anayetarajiwa kuanza uunganishaji wa magari ya umeme (Electric Vehicles); pamoja na Sanda Max Group Limited anayejenga kiwanda cha kuzalisha chakula cha mifugo. Maboresho hayo ya miundombinu yatachochea ukuaji wa uchumi kwa kuongeza fursa za ajira, kukuza mauzo ya nje na kuboresha upatikanaji wa bidhaa kwa gharama nafuu ndani ya nchi.

C. Kuendeleza kiwanda cha Tanzania Biotec Company Limited (TBPL)

69. Mheshimiwa Spika; Tanzania Biotech Products Limited (TBPL) ni kiwanda cha kuzalisha bidhaa za kibaolojia kilichopo Kibaha mkoani Pwani, kinachotumia teknolojia kutoka nchini Cuba kuzalisha bidhaa mbalimbali za kibaiolojia zinazotumika kwenye sekta ya afya, kilimo na mazingira. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na kina uwezo wa kuzalisha hadi lita milioni sita (6) kwa mwaka. Lengo kuu la uanzishwaji wa kiwanda cha TBPL ni kuzalisha Viuadudu kwa ajili ya kutokomeza ugonjwa wa malaria Nchini Tanzania na barani Afrika ifikapo 2030.

70. Mheshimiwa Spika; Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria nchini ambapo katika mwaka 2025/2026 jumla ya shilingi bilioni 10.5 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa viuadudu lita 875,000 katika kiwanda cha TBPL. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya lita 491,361 za Viuadudu zimezalishwa ambapo kati ya lita hizo, lita 124,121 zimechukuliwa na Halmashauri 80 nchini. Aidha, uzalishaji na usambazaji wa viuadudu katika Halmashauri zilizosalia unaendelea. Pamoja na uzalishaji na usambazaji wa viuadudu ndani ya nchi, kiwanda kimeweza kuuza dawa za viuadudu nchi za jirani ikiwemo Uganda zenye thamani ya shilingi milioni 344.07. Hali hii inaashiria kuongezeka kwa imani ya watumiaji na kupanuka kwa soko la dawa hii nje ya Nchi.

71. Mheshimiwa Spika; katika kuhamasisha matumizi ya bidhaa rafiki kwa mazingira zisizo na kemikali hatarishi, kiwanda kinaendelea na uzalishaji wa mbolea-hai pamoja na viuatilifu hai ambavyo hutumika kuua wadudu waharibifu wa mazao. Uhaulishaji wa teknolojia za mbolea-hai umekamilika ambapo kiwanda kimezalisha jumla ya lita 3,475 za aina mbili za mbolea hai (Fosforina - lita 1,464 na Dimargon - lita 2011) ambazo kwa sasa zipo katika hatua za majaribio kwenye mazao ya mahindi, matango, nyanya na mbogamboga na zimeonesha ufanisi mzuri. Hadi kufikia Aprili 2026, kiwanda kimefanikiwa kuuza zaidi ya lita 12,000 za viuatilifu hai vinavyotumika kudhibiti wadudu waharibifu kwenye mazao mbalimbali.

D. Kuendeleza Kiwanda cha Kilimanjaro Mashine Tools (KMTC)

72. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia NDC imeendelea na juhudi za kukiendeleza na kukisimamia kiwanda cha KMTC Manufacturing Limited kilichopo Kilimanjaro. Hadi kufikia Aprili 2026, kiwanda kimefanikiwa kuzalisha jumla ya mashine 14 na vipuri 159 na kutoa ajira za moja kwa moja kwa vijana 36 na zisizo za moja kwa moja 144. Aidha, jumla ya shilingi milioni 505.69 zimepatikana kutokana na mauzo ya mashine na vipuri hivyo. Kiwanda kwa kushirikiana na Bodi ya Mkonge Tanzania kimefanikisha kubuni na kutengeneza mtambo wa kuchakata katani wenye uwezo wa kuchakata *meta* 80 kwa siku na kuajiri vijana 10. Katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa kiwanda, NDC imefanikiwa kutangaza

zabuni ya ununuzi wa mashine ya Steel Grinding Ball Skew Rolling Machine kwa ajili ya kutengeneza golori za kusaga mawe zinazotumika katika vinu katika migodi mikubwa.

E. Kufanya Tathmini ya Viwanda na Kuainisha Fursa za Uwekezaji

73. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TIRDO imeendelea kutekeleza zoezi la tathmini ya viwanda na uainishaji wa fursa za uwekezaji wa viwanda nchini. Tathmini hiyo inaainisha idadi ya viwanda, ajira, uwezo wa uzalishaji, teknolojia zinazotumika nchini na maeneo yenye fursa za uwekezaji ili kuchochea maendeleo ya viwanda na kuziongezea thamani rasilimali za ndani. Zoezi hilo limefanyika katika mikoa miwili (2) na hivyo kuwa na jumla ya mikoa tisa (9). Mikoa hiyo ni Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Manyara, Mwanza na Shinyanga. Aidha, taarifa za viwanda zilizokusanywa kwa mikoa tisa (9) zimeingizwa katika mfumo wa kanzidata za viwanda. Hadi kufikia Aprili, 2026 kanzidata hiyo ina jumla ya viwanda 25,650 ambapo 482 ni viwanda vikubwa, 625 vya kati, 8,980 vidogo na 15,563 ni viwanda vidogo sana.

F. Kuanzisha na Kuimarisha Maabara kwa Ajili ya Utoaji Huduma

74. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TIRDO imeendelea kuimarisha na kuboresha maabara kwa ajili ya utoaji huduma za kitafiti katika maendeleo ya viwanda. Katika mwaka 2025/2026 maabara ya chakula ambayo ilipata ithibati mwaka 2025 iliboreshwa kwa kuongeza wigo wa huduma kutoka huduma tatu (3) hadi sita (6) na wigo wa bidhaa kutoka moja (1) hadi nne (4). Huduma na bidhaa hizo ni pamoja na vyakula vilivyotayari kwa matumizi; nyama na bidhaa zake; samaki na bidhaa zake; na sampuli za usufi wa nyuso (surface swabs). Kuongezeka kwa wigo huo kunaimarisha uwezo wa maabara kutoa huduma jumuishi na za kuaminika zaidi na kupunguza utegemezi wa huduma kutoka nje.

75. Mheshimiwa Spika; vilevile, TIRDO inaendelea na jitihada za kuanzisha Maabara ya Nishati na Madini katika Mkoa wa

Njombe ili kusogeza huduma karibu na maeneo yenye rasilimali na shughuli za uzalishaji. Uamuzi huu unatokana na uwepo wa makaa ya mawe katika maeneo ya jirani kama Ludewa, Mbinga na Nyasa na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za upimaji na uthibitishaji wa ubora wa nishati. Maabara hii itahudumia Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Ruvuma, Mbeya na Rukwa) na hivyo kupunguza gharama na muda wa upatikanaji wa huduma. Kupitia maabara hii, vipimo vya ubora wa makaa ya mawe vitahusisha salfa, majivu, maada fukivu, unyevu na thamani ya joto, pamoja na uchambuzi wa elementi na utambuzi wa madini na kemikali, huku pia ikitoa huduma za upimaji wa nishati mbadala ikiwamo mkaa mbadala na biomasi ili kuhakikisha ubora na uendelevu wake.

76. Mheshimiwa Spika; maabara hiyo inatarajiwa kuwa na vifaa vyenye teknolojia ya kisasa itakayowezesha kutoa huduma stahiki kwa jamii. Hadi kufikia Aprili, 2026, Shirika limefanikiwa kumpata mzabuni wa kusambaza na kusimika vifaa hivyo pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam watakaoendesha mitambo hiyo. Kukamilika kwa maabara hiyo kutachochea ongezeko la thamani ya rasilimali za nishati, kuimarisha ushindani wa bidhaa za ndani na kuchochea uchumi wa viwanda unaozingatia nishati safi na rafiki kwa mazingira.

77. Mheshimiwa Spika; sambamba na hilo, TIRDO imeendelea na mchakato wa kupata Ithibati kwa maabara za TIRDO. Maabara hizo ni Mazingira, kemia, makaa ya mawe, mafuta na gesi. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilitenga kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kupata idhibati ya Maabara ya Mazingira. Hatua iliyofikia katika utekelezaji wa mradi huo ni ukamilishwaji wa mchakato wa manunuzi ya vifaa ambapo mzabuni amepatikana, uandaaji wa nyaraka za ithibati (*quality manual*) pamoja na utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa maabara hiyo. Aidha, mchakato wa kupata ithibati kwa maabara za kemia, makaa ya mawe, mafuta na gesi upo katika hatua za awali.

G. Uvumbuzi, Utafiti na Uendelezaji Teknolojia

78. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia SIDO imefanikiwa kuhawilisha teknolojia nane (8) za kuchakata

mazao mbalimbali. Teknolojia hizo ni utengezaji wa kinu cha kuchoma masalia ya kilimo; mashine ya kutengeneza mkaa mbadala; mashine ndogo ya kusafisha mafuta ya alizeti; mashine za kuzalisha chakula cha samaki; mashine za kusaga mawe yenye madini; mashine za kukamua na kuchuja mafuta ya nazi; mashine za kubangua korosho; na utengenezaji wa *cage* za ufugaji wa samaki kwenye maziwa, mito na bahari.

79. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia SIDO imetengeneza mashine tatu (3) za kuzalisha mkaa mbadala kwa kushirikiana na UNIDO ikiwa ni pamoja na kuleta teknolojia mpya kutoka Japani ambazo ni kiwanda cha kuzalisha kuni bora *(briquttes)* katika maeneo ya Ifakara, Morogoro; Kahama, Shinyanga; na Mwanjelwa, Mbeya. Aidha, Mitambo ya kuchuja madini na mchanga na kifaa cha kutoa mchanga katika madini ndani ya mashimo vimetengenezwa katika mikoa ya Lindi, Mbeya na Shinyanga.

80. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TEMDO inaendelea kusanifu na kuunda vifaa tiba kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya hospitali. Hadi kufikia Aprili, 2026, TEMDO imefanikiwa kusanifu na kutengeneza vifaa tiba vya aina 15 vilivyoko daraja A ambavyo vimepata ithibati toka Mamlaka ya Uthibiti wa Madawa na Vifaa Tiba (TMDA). Vifaa hivyo ni *bedside locker with stainless steel top (wheeled); bedside locker wooden with stainless steel top (wheeled); bedside locker wooden with wooden top and no wheels; bedside locker wooden with wooden top (wheeled); delivery bed; drip stand with bendbase; drip stand with straight base; examination bed with racks for reclining mechanism; hospital working table (mobile operating table); normal hospital bed (adjusted by slotted bar a ratchet like mechanism); normal hospital bed (adjusted by screw mechanism); normal heavy fixed table; hospital folding screen; na theatre trolleys.* Aidha, kufuatia usanifu huo, vifaa tiba mbalimbali vimetengenezwa vikiwemo vitanda sita (6) vya kujifungulia na vitatu (3) vya kawaida; mitambo 13 ya kuchomea taka ngumu za hospitali; na hifadhi kuta 15 (hospital screen).

81. Mheshimiwa Spika; katika jitihada za kutunza mazingira na kuendeleza nishati mbadala, mwaka 2025/2026 TEMDO ilibuni na

kutengeneza mashine ya kukausha vumbi la mbao. Mashine hiyo iliyofungwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale katika Mkoa wa Geita ina uwezo wa kuzalisha tani moja (1) ya kuni mbadala kwa siku. Aidha, TEMDO imekamilisha uundaji wa mtambo wa kutengeneza mkaa na kuni mbadala zinazozalishwa kwa kutumia mabaki ya pumba za mpunga ambao umekabidhiwa kwa Halmashauri hiyo. Vilevile, mtambo wenye uwezo wa kuzalisha tani mbili (2) za mkaa mbadala umesanifiwa ambao kwa sasa upo katika hatua ya utengenezaji wa vipuri. Pia, mtambo mwingine wa kutengeneza mkaa na kuni mbadala umesanifiwa na kutengenezwa na uko tayari kwa ajili ya kuzalisha mkaa mbadala tani moja na nusu (1.5) kwa siku.

82. Mheshimiwa Spika; Wizara, kupitia CAMARTEC, imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za uendelezaji wa teknolojia za kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uchumi wa buluu; na nishati safi ya kupikia. Hadi kufikia Aprili, 2026 CAMARTEC imekamilisha ujenzi wa mitambo miwili (2) ya bayogesi ya ngazi ya taasisi katika kambi za JKT Oljoro na JKT Mafinga. Aidha, CAMARTEC imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa mitambo ya bayogesi katika magereza nane (8) kama awamu ya kwanza kati ya magereza 14 yaliyopangwa kutekelezwa. Magereza hayo ni Mbigiri (Morogoro), Mtego wa Simba (Morogoro), Kingurungundwa (Lindi), Msalato (Dodoma), Ubena (Pwani), Kitai (Ruvuma), Arusha (Arusha), na Bariadi (Simiyu). Lengo la miradi hii ni kutoa nishati safi na endelevu ya kupikia, kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa, kulinda mazingira, pamoja na kuboresha usafi na usimamizi wa taka katika maeneo husika.

83. Mheshimiwa Spika; CAMARTEC inaendelea kufanya tafiti katika teknolojia za makaushio ya mboga, matunda na mazao ya uchumi wa buluu; mashine ya kukamua mafuta ya parachichi kwa mkono; mashine za kubangua korosho kwa mkono; mashine ya kutengeneza siagi ya karanga; mashine ya kusaga magunzi na mabua kwa ajili ya mifugo; pamoja na mashine za kuangua mayai. Kukamilika kwa tafiti hizi kutasaidia kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo na uchumi wa buluu.

84. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TIRDO imeendelea kufanya tafiti na kutoa huduma za kitaalamu kwa viwanda kwa

kubuni na kuendeleza teknolojia za kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora. Tafiti zilizofanyika zilijikita katika uongezaji thamani wa malighafi za ndani, ubunifu wa mitambo midogo na ya kati, pamoja na kuboresha ubora wa bidhaa ili kukidhi viwango vya masoko ya ndani na nje. Hadi kufikia Aprili, 2026 Shirika limeunda mtambo wa bayogesi na mtambo wa mkaa mbadala (ECO-Carbonizer) kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi.

85. Mheshimiwa Spika; Utafiti unaohusu ulinzi wa mlaji katika biashara mtandao unaolenga kuchambua hali ya sasa ya ulinzi wa watumiaji katika masoko ya kidijitali. Matokeo ya awali ya utafiti huo yanaonesha uwepo wa pengo katika mfumo wa kisheria, hususan katika kushughulikia changamoto za soko la kidijitali (digital market). Kutokana na hali hiyo, mapendekezo ya maboresho ya sheria yanaandaliwa na yatawasilishwa kwa mamlaka husika, ikiwamo BRELA, BOT na TCRA, kwa ajili ya hatua zaidi. Aidha tafiti zote zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

3.2.2 Uendelezaji wa Jasiriamali Ndogo na za Kati

A. Kuanzisha na Kuendeleza Viwanda Darasa

86. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia SIDO imeendelea na juhudi za ujenzi wa viwanda darasa kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati. Katika mwaka 2025/2026 SIDO kwa kushirikiana na KOICA imekalimisha ujenzi wa majengo mawili (2) ya mafunzo ya usindikaji wa vyakula na mahali pa kufanyia uzalishaji katika mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro. Hatua inayofuata ni ununuzi wa vifaa na mashine ili majengo hayo yaanze kutumika kwa kazi iliyokusudiwa. Majengo hayo yana uwezo wa kuhudumia wajasiriamali 60 kwa wakati mmoja.

B. Kuhamasisha na Kuendeleza Uanzishwaji wa Kongani Nchini

87. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wajasiriamali wanaojihusisha na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo katika kongani za *Mbeya Rice Group*, Mkoa wa Mbeya; *Singida Municipal Sunflower Oil Processors Association (SIMSOPA)*, Singida; Magugu-Manyara; na Bitale katika Mkoa wa Kigoma. Hadi

kufikia Aprili, 2026 wajasiriamali 95 wamepata mafunzo kuhusu usimamizi wa biashara, uzingatiaji viwango katika uzalishaji na utafutaji wa fursa za masoko ya bidhaa. Aidha, Wizara kupitia SIDO imeendelea kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo, ushauri wa kitaalamu, mikopo na mbinu za utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali katika kongani 20 kwenye Mikoa ya Geita, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Shinyanga, Mtwara na Kagera. Vilevile, Wizara kupitia SIDO imewezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo vipya 296 katika mikoa yote Tanzania na kuchangia jumla ya ajira 1,409.

C. Kutoa Huduma za Kifedha kwa Wajasiriamali

88. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF) unaosimamiwa na SIDO imetoa jumla ya mikopo 829 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.95. Mikopo hiyo imezalisha ajira 1,859 ambapo wanawake ni 957 sawa na asilimia 51 na wanaume ni 902 sawa na asilimia 49 (**Jedwali Na. 15**). Aidha, tangu mfuko ulipoanza kutoa huduma ya mikopo mwaka 1994, hali ya marejesho ya mikopo imekuwa ni ya kuridhisha ambapo wastani wa marejesho ni asilimia 91.1 (**Jedwali Na. 16**). Vilevile, kupitia Programu ya Uwezeshaji Viwanda Vidogo (SANVN Viwanda Scheme), Wizara imewezesha jumla ya wajasiriamali 11 kuunganishwa na Benki ya Azania na kupata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.98. Halikadhalika, kupitia Mfuko wa Dhamana ya Serikali (CGS), jumla ya mikopo 18 yenye thamani ya shilingi milioni 422 ilitolewa na Benki ya CRDB.

89. Mheshimiwa Spika; Vilevile, Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni nne (4) ikiwa ni sehemu ya shilingi bilioni 200 ambazo ni fedha maalum kwa vijana zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya uwezeshaji wa vijana kiuchumi kupitia mikopo. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya maombi 154 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.61 yamepokelewa na taratibu za uchambuzi na uhakiki wa utoaji mikopo hiyo kwa kushirikiana na *CRDB Bank Foundation* unaendelea.

D. Utengaji wa Maeneo kwa Ajili ya Shughuli za Wajasiriamali Wadogo na wa Kati

90. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea na juhudi za kuhamasisha utengaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati katika mikoa yote nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya hekta 624,584 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe na Tanga **(Jedwali Na. 17).**

3.2.3 Mtangamano wa Biashara

91. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kama ifuatavyo:

A. Nchi na nchi

i. *Utekelezaji wa Mkataba wa Mfumo uliorahisishwa wa ufanyaji Biashara kwa ajili ya kusaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati kufanya Biashara za Mpakani kati ya Tanzania, Zambia na Malawi (Simplified Trade Regime-STR)*

92. Mheshimiwa Spika; katika Juhudi za kukuza na kuimarisha biashara ya uwili Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara imeratibu majadiliano na hafla ya utiaji saini wa Mkataba wa Mfumo uliorasimishwa kwa wafanyabiashara wadogo (Simplified Trade Regime – STR) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Malawi iliyofanyika mwezi Februari, 2026 Jijini Lilongwe – Malawi. Mfumo huo unajumuisha utaratibu maalumu wa biashara unaolenga kurahisisha taratibu za forodha na kupunguza vikwazo visivyo vya kikodi - NTBs kwa bidhaa 61.

93. Mheshimiwa Spika; hatua hii itaimarisha na kurahisisha biashara kwa wafanyabiashara wadogo kupitisha mpakani bidhaa zisizozidi thamani ya dola za Marekani 2,000 kwa siku. Mkataba huo umewezesha wafanyabiashara wadogo kufanya

biashara zao kwa urahisi na kupelekea biashara baina ya Tanzania na Malawi kuimarika. Ili kuwa na ufanisi wa utekelezaji wa mkataba huo, Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Taifa ya wafanyabiashara (TNCC) imeendela kutoa Elimu kwa wafanyabishara wadogo wa mpakani. Aidha, mwongozo uitwao ***Kasumulo Business Model*** umeandaliwa ili kutoa utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa mazao ya soya, ufuta na mbaazi baina ya Malawi na Tanzania.

94. Mheshimiwa Spika; kwa upande wa Tanzania na Zambia, nchi hizo zilifanya mkutano wa pili mwezi Desemba 2025 ambapo kupitia mkutano huo, nchi zilikubaliana kuongeza idadi ya bidhaa kutoka 22 hadi 48 zitakazotumika kwenye STR pamoja na nyaraka za forodha (simplified customs document) zitakazotumiwa na wafanyabiashara wanapovuka mpaka wa Tunduma/Nakonde. Kwasasa Serikali inakamilisha taratibu za kusaini Mkataba wa Nyongeza. Utekelezaji wa Mkataba huo unatarajiwa kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Zambia na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi kwa wafanyabiashara wadogo ambao wengi ni wanawake na vijana.

ii. **Mkataba wa Ushirikiano wa Ubia wa Uchumi kati ya Tanzania na Oman**

95. Mheshimiwa Spika; katika kuimarisha uhusiano wa biashara na kuibua fursa za uwekezaji kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Oman, Wizara iliratibu wadau muhimu walioshiriki katika ziara ya biashara nchini Oman mwezi Aprili, 2025. Ziara hiyo ilifungua fursa za ushirikiano zaidi za uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwemo mifugo, kilimo, usafirishaji na maji. Mafanikio yaliyopatikana katika ziara hiyo ni Taasisi za Sekta Binafsi za nchi zote mbili kukubaliana kuongeza ushirikiano na kuhakikisha fursa za biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Oman zinatumika kikamilifu; kubadilishana uzoefu na teknolojia katika sekta za viwanda na biashara; na kuanzisha majadiliano ya kuingia katika Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (Comprehensive Economic Partnership Agreement- CEPA).

96. Mheshimiwa Spika; katika hatua ya utekelezaji, Serikali ya Oman imewasilisha Rasimu ya Hadidu za Rejea zenye nia ya

kuingia makubaliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi (CEPA) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imeshafanya uchambuzi wa kina na kuainisha maeneo ambayo Tanzania itakuwa na maslahi nayo na yale ambayo hayastahili kujumuishwa katika Mkataba unaopendekezwa na kuishauri Serikali ipasavyo. Hadidu hizo za rejea zenye maoni ziliwasilishwa Serikali ya Oman mwezi Novemba 2025. Kuridhiwa kwa maoni hayo kutawezesha hatua inayofuata ya majadiliano kuanza.

iii. Utatuzi wa Changamoto ya Foleni ya Malori katika Mpaka wa Tunduma, Mkoa wa Songwe

97. Mheshimiwa Spika; Wizara ilishiriki kikao cha kujadili utatuzi wa changamoto ya foleni ya Malori katika mpaka wa Tunduma, Mkoa wa Songwe, kilichofanyika mwezi Januari 2026, Jijini Dar es Salaam. Kikao hicho kilijadili changamoto za kibiashara katika mpaka wa Tunduma na kukubaliana mpango mkakati wa kutatua changamoto hizo. Mikakati hiyo ni pamoja na mashirika ya Serikali ambayo yana uwezo mkubwa wa kifedha kuingia ubia na sekta binafsi wa kujenga barabara za kulipia (road tolls) kwa utaratibu wa Sheria ya Ubia wa Umma na Sekta Binafsi; TANROADS kukamilisha ujenzi wa kipande cha barabara ya mzunguko katika mpaka wa Tunduma; kuunganisha mifumo ya forodha baina ya Tanzania na Zambia; kuendelea kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari kavu; na kuharakisha upimaji wa mizigo kwa upande wa Zambia kwa kukamilisha ujenzi wa mdaki (scanner) wenye kasi.

98. Mheshimiwa Spika; mikakati hiyo imeanza kutekelezwa ambapo kazi ya ujenzi wa kipande cha barabara cha kuingia mpakani kwa njia nne chenye urefu wa mita 750 unaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026; usimikwaji wa mdaki (scanner) kwa upande wa Zambia umekamilika na tayari umeaanza kufanya kazi, ambapo mdaki huo una uwezo wa kupima lori moja kwa sekunde 30, tofauti na mdaki wa awali ambao ulikuwa unachukua muda mrefu zaidi; uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA baina ya TRA na ZRA unaendelea kwa sasa upo katika hatua ya majaribio; na uendelezaji wa bandari kavu Tunduma kwa sasa timu ya wataalam wa kampuni ya mwekezaji

(Jiayou International Logistics) ipo eneo la mradi kufanya upembuzi yakinifu ambapo hatua iliyofikiwa ni asilimia 85. Utekelezaji wa mikakati hiyo utarahisisha biashara baina ya Tanzania, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

iv. Uondoaji wa Vikwazo vya Biashara visivyo vya Kiushuru (NTBs)

99. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuratibu majadiliano ya masuala ya biashara na uondoaji wa Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru (Non-Tariff Barriers-NTBs) baina ya Tanzania na nchi za Kenya na Zambia kama ifuatavyo:-

a) Tanzania na Kenya

100. Mheshimiwa Spika; Wizara imefanikiwa kuendelea kutatua vikwazo vya biashara kati ya Tanzania na Kenya kupitia mkutano wa Kamati ya Pamoja ya Biashara (JTC) uliofanyika mwezi Septemba hadi Oktoba, 2025 katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mkutano huo, jumla ya vikwazo vya biashara 14 vilijadiliwa ambapo sita (6) vilihusu malalamiko yaliyowasilishwa na Tanzania na vikwazo nane (8) vilihusu malalamiko yaliyowasilishwa na Kenya. Kati ya vikwazo hivyo 14, vikwazo vitatu (3) vilitatuliwa vilivyohusu ushuru wa bidhaa usio wa haki na tozo kubwa za malipo ya stampu kwenye bia za Tanzania zinapouzwa nchini Kenya. Aidha, changamoto za kusafirisha mbegu kutoka Kenya kuja nchini na tofauti ya gharama ya malipo ya matumizi ya barabara zilitatuliwa.

101. Mheshimiwa Spika; katika ziara ya Mheshimiwa Dkt William Samoei Ruto Rais wa Jamhuri ya Kenya aliyoifanya nchini tarehe 4 - 5 Mei, 2026. Katika ziara hiyo, wakuu wa nchi za Tanzania na Kenya walielekeza kuondolewa kwa vikwazo vyote vya biashara ndani ya siku 30. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara imewasiliana na taasisi zenye changamoto kwa upande wa Tanzania ili kwa pamoja kuweka mikakati ya namna bora ya kushirikiana na nchi ya Kenya katika kuziondoa changamoto hizo.

b) Tanzania na Zambia

102. Mheshimiwa Spika; Wizara ilifanya mkutano wa nne wa Kamati ya Pamoja ya Biashara kati ya Tanzania na Zambia mwezi Agosti, 2025 Nakonde, Zambia. Katika mkutano huo, Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru (NTBs) 10 vilijadiliwa na nchi zote mbili zilikubaliana muda wa kuondoa vikwazo. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2026 masuala ambayo yametekelezwa baina ya pande zote mbili ni pamoja na kusainiwa kwa Mkataba wa Taasisi zinazohusika na masuala ya vipimo kwa nchi zote mbili (Weight and Measures Agency - WMA na Zambia Metrology Agency - ZMA). Mkataba huo ulisainiwa mwezi Desemba, 2025 kwa lengo la kuondoa changamoto ya utofauti wa vipimo. Aidha, Hati ya Makubaliano ya ushirikiano wa Mamlaka za Mapato (Revenue Authorities) kwa ajili ya uwianishaji wa mifumo ya forodha na kukamilika kwa maboresho ya miundombinu upande wa Zambia (Nakonde) inayohusisha usimikaji wa mdaki (scanner) mpya wa kisasa na ujenzi wa maegesho yanayochukua malori 75 ilisainiwa. Aidha, Mkutano wa tano (5) umepangwa kufanyika mwezi Mei, 2026.

103. Mheshimiwa Spika; utatuzi wa NTBs kwa kipindi cha hivi karibuni umesaidia kupunguza muda wa kuondosha mizigo mipakani kupitia utekelezaji wa Himaya ya Pamoja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa upande mwingine utatuzi wa changamoto umewezesha kuendelea na soko la bidhaa kama vile mayai, makaa ya mawe zilizokuwa zimewekewa ushuru wa bidhaa nchini Kenya; kuendelea kwa biashara ya bidhaa za kilimo nchini Malawi ambazo ziliwekewa katazo na nchi hiyo; kuongozeka kwa biashara ya mahindi kwenda nchi jirani kutokana na kutatuliwa kwa malalamiko ya sumu kuvu; kuimarika kwa biashara ya mchele kwenda Uganda na Rwanda kutokana na kuondolewa kwa changamoto iliyokuwa inatolewa na nchi husika kuwa mchele wetu kuchanganywa na mchele kutoka nje ya nchi; na kuruhusiwa mazao ya parachichi na viungo kuingia katika soko la nchi ya Afrika Kusini.

v. Utekelezaji wa Tamko la Uanzishaji wa Kamati ya Pamoja ya Biashara (JTC) kati ya Tanzania na Uturuki

104. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea na jitihada za

kuongeza kiasi cha biashara kati ya Tanzania na Uturuki ili kufika dola za Marekani Bilioni 1, kama yalivyokuwa makubaliano katika kikao cha Wakuu wa Nchi za Tanzania na Uturuki. Makubaliano hayo yalifikiwa wakati wa ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uturuki mwezi Aprili, 2024. Tarehe 23 Julai 2025 Serikali zote mbili zilisaini Tamko la kuanzisha Kamati ya Pamoja ya Biashara (Joint Trade Committee) kwa ajili ya kujadili fursa za biashara zilizopo baina ya Uturuki na Tanzania na kuweka mikakati ya kutumia fursa hizo na hatua nyingine za utekelezaji.

B. Kikanda

i. Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA)

105. Mheshimiwa Spika; katika utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA), Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya biashara kupitia Mpango wa Majaribio ya Biashara (Guided Trade Initiative - GTI) ambapo kampuni za Tanzania zimefanikiwa kufikia masoko mapya na kupata uzoefu wa moja kwa moja katika taratibu za forodha. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya kampuni 40 za Tanzania zimefanya biashara kwa kutumia Vyeti vya Uasili wa Bidhaa vya AfCFTA, ambapo jumla ya vyeti 500 vimetolewa. Kupitia soko hilo, mauzo ya Tanzania kwenda Ghana yalikuwa na thamani ya dola za Marekani Milioni 62.9; Nigeria dola za Marekani Milioni 8; Algeria dola za Marekani Milioni 3.7; na mauzo kwenda Misri yalikuwa ya dola za Marekani Milioni 1.1. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni nyuzi za katani ambazo zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 56, ikifuatiwa na kahawa na viungo ambavyo vilikuwa na jumla ya dola za Marekani milioni 3 na vioo (float glasses) ambavyo vilikuwa na dola za Marekani milioni 2.4.

106. Mheshimiwa Spika; Wizara imekamilisha na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (National AfCFTA Implementation Strategy) mwezi Julai, 2025. Aidha, Timu ya Kitaifa ya kusimamia utekelezaji wa Mkakati huo imeshaundwa ikihusisha wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi. Vilevile, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Hatua kwa

Hatua wa Ufanyaji Biashara chini ya Eneo Huru la Biashara Afrika ambao utasaidia jamii ya wafanyabiashara kujua kwa kina hatua wanazopaswa kuzifuata wakati wa kuagiza na kuuza bidhaa kwenye soko hilo.

ii. **Mkutano Maalum wa 59 wa Baraza la Mawaziri wa EAC na Mkutano wa 25 wa *Wakuu wa Nchi.***

107. Mheshimiwa Spika; Mkutano Maalum wa 59 wa Baraza la Mawaziri wa EAC ulifanyika mwezi Aprili, 2026 jijini Arusha na kufuatiwa na Mkutano wa 25 wa wakuu wa nchi. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kujadili taarifa ya mwaka ya Baraza la Mawaziri wa EAC; uzinduzi wa Mkakati wa saba wa maendeleo wa EAC; uzinduzi wa dhamana ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na masuala mengine. Mikutano hiyo inachangia katika kuchochea maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara nchini, hususan uzinduzi wa Mkakati wa Saba wa Maendeleo wa EAC (2026/27–2030/31) ambao umeweka vipaumbele katika kuimarisha biashara ya kikanda, kuongeza uzalishaji na thamani ya bidhaa na kuboresha ushindani wa bidhaa za viwanda vya ndani na nje ya nchi. Aidha, uzinduzi wa Dhamana ya Forodha ya EAC utarahisisha usafirishaji wa bidhaa ndani ya Jumuiya kwa kutumia dhamana moja hivyo kupunguza gharama za biashara, kuongeza ufanisi wa forodha na kufungua fursa zaidi za masoko kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

108. Mheshimiwa Spika; maendeleo katika kuimarisha Umoja wa Forodha na Soko la Pamoja na tathmini ya Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA), yanaipa Tanzania nafasi ya kulinda na kukuza viwanda vya ndani huku ikinufaika na masoko ya kikanda na kimataifa. Uteuzi wa mwakilishi wa Tanzania katika Tume ya Ushindani ya EAC utaimarisha usimamizi wa ushindani wa haki katika biashara na hivyo kuboresha mazingira ya uwekezaji. Kwa ujumla, maamuzi ya mikutano hiyo yanaongeza ufanisi wa mifumo ya kikanda na kufungua fursa mpya kwa Serikali katika kuimarisha utekelezaji wa sera na mipango ya kukuza viwanda na biashara nchini.

C. Kimataifa

i. Utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara Duniani (WTO Trade Facilitation Agreement – TFA) na Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (NCTF)

109. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (National Committee on Trade Facilitation (NCTF), inaendelea na utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa Shirika la Biashara Duniani ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wadau wa maendeleo kwa ajili ya ufadhili wa miradi iliyoandaliwa na utekelezaji wa Mkataba kwa ujumla. Aidha, Kamati inaendelea kufanya mapitio ya Mpango Mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Kamati wa miaka mitano (National Trade Facilitation Roadmap Review). Maandalizi ya mpango huo yamefikia katika hatua ya kukusanya maoni kutoka kwa wadau.

110. Mheshimiwa Spika; Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara imeendelea kutatua changamoto za wafanyabiashara kupitia kliniki ya wafanyabiashara hasa katika mpaka wa Tunduma. Kupitia kliniki hiyo wafanyabiashara wamepatiwa uelewa kuhusu taratibu za kuvuka Mipakani; kutumia mfumo uliorahisishwa kwa wafanyabiashara wadogo; uondoshaji na upitishaji wa mizigo mipakani na usafirishaji; na taratibu na fursa za biashara ya kikanda. Kupitia mpango huu jumla ya wafanyabiashara 72 wamenufaika na mafunzo hayo.

ii. Mkutano wa Biashara wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo – UNCTAD

111. Mheshimiwa Spika; Mkutano wa Biashara wa UNCTAD ni mkutano ambao hufanyika kila baada ya miaka minne unaowakutanisha Wakuu wa Nchi, Mawaziri wa Biashara na Uchumi, Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa na Wataalam wa masuala ya Biashara kwa lengo la kujadili biashara na maendeleo katika kuwezesha uchumi imara na endelevu ya nchi wanachama. Mkutano wa 16 ulifanyika mwezi Oktoba, 2025 Geneva, Uswisi. Majadiliano katika mkutano huo yalihusu viwango vya usalama wa bidhaa za watumiaji na mapendekezo yakiwa ni

kuimarisha usalama wa bidhaa kupitia mageuzi ya kitaifa na kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa. Vipaumbele muhimu vilivyoafikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti; kuboresha tathmini ya hatari na ukusanyaji wa taarifa; kuimarisha mifumo ya kubadilishana taarifa za kuvuka mipaka; na kuzingatia mahitaji mahsusi ya nchi zinazoendelea.

iii. Uratibu na Uwasilishaji wa Taarifa mbalimbali za Biashara katika Shirika la Biashara Duniani (WTO Notifications)

112. Mheshimiwa Spika; Wizara huwasilisha taarifa mbalimbali zinazohusu biashara katika Shirika la Biashara Duniani (WTO) kupitia mfumo maalum wa *e-ping*. Taarifa hizo zinahusu masuala ya vigezo vya viwango; afya ya wanyama, mimea na usalama chakula; masuala ya ruzuku katika biashara; na ushuru wa mipakani. Hadi kufikia Aprili, 2026 Tanzania imeendelea kufanya vizuri WTO ambapo jumla ya taarifa (notification) 506 ziliwasilishwa katika shirika hilo kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya Nchi. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, Tanzania imefanikiwa kuwa miongoni mwa nchi 10 kati ya nchi 166 wanachama wa WTO zinazowasilisha taarifa za biashara katika shirika hilo katika eneo la Vikwazo vya Biashara vya Kiufundi (Technical Barrier to Trade - TBT). Hali hiyo inaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazozingatia misingi ya uwazi katika biashara Duniani.

3.2.4 Maendeleo ya Biashara

A. Kuboresha Mazingira ya Biashara

113. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea na jukumu la kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini ambapo katika mwaka 2025/2026 Wizara imefanikiwa kudhibiti raia wa kigeni kufanya biashara zinazostahili kufanywa na Watanzania kupitia Tangazo la Serikali Na. 487A la tarehe 28 Julai, 2025. Tangazo hilo linatoa katazo kwa raia wa kigeni kujihusisha na biashara 15 zinazostahili kufanywa na Watanzania. Biashara hizo ni pamoja na uuzaji wa bidhaa kwa jumla na rejareja, huduma za watalii wa ndani, huduma za fedha kwa njia ya simu (Mawakala), saluni, usafirishaji wa mizigo, uuzaji wa vinyago, uchimbaji mdogo wa

madini, uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya redio na runinga, uendeshaji wa viwanda vidogo, kampuni za huduma ya usafi na uuzaji wa nyumba na viwanja.

114. Mheshimiwa Spika; katika utekelezaji wa Sheria ya Katazo hilo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali imechukua hatua madhubuti za kisera, kisheria na kiutendaji ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imezuia uhuishaji wa leseni za biashara 907. Kati ya hizo, leseni 737 ni za biashara za uingizaji na uuzaji wa bidhaa, leseni tano (5) katika huduma za posta na utoaji wa vifurushi ndani ya mipaka ya kitaifa, leseni 119 za uwakala au udalali katika biashara na sekta ya mali isiyohamishika na leseni 46 za huduma ya utoaji na usafirishaji wa shehena. Hatua hii imerejesha imani ya wazawa kwa Serikali kwa namna inavyosaidia kutatua changamoto za kibiashara; imeboresha mazingira ya biashara kwa wazawa na hivyo kuongeza uwekezaji kwenye biashara; na imeongeza uwezo wa ushindaji kwa wazawa kwenye biashara. Katika kuboresha utekelezaji wa katazo hilo, Serikali imefanya marejeo na kuandaa rasimu ya katazo ambayo ipo katika hatua ya uidhinishwaji.

115. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya maombi 373 ya vibali vya kazi kwa raia wa kigeni wanaokuja kufanya kazi nchini katika tasnia ya biashara hayakuidhinishwa kutokana na kutokukidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Vilevile, Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam na Mbeya zimezuia uhuishaji wa leseni za biashara 191 kwa biashara ya uuzaji wa bidhaa kwa jumla, uuzaji wa bidhaa kwa rejareja, uchimbaji mdogo wa madini na biashara ya maghala/stoo ambazo zinamilikiwa na wafanyabiashara/kampuni wasio raia wa Tanzania kwa kuzingatia amri iliyotolewa. Biashara 13 kati ya 191 zilizozuiwa kuhuishwa au kupewa leseni zilikuwa katika eneo la kariakoo.

116. Mheshimiwa Spika; katika jitihada za kuendelea kuimarisha diplomasia ya uchumi, Wizara iliratibu Majadiliano ya Tatu ya Biashara kati ya Tanzania na Japan yaliyofanyika mwezi Novemba, 2025 Jijini Dar es Salaam kwa dhumuni la kuimarisha mahusiano ya biashara na uwekezaji na kutatua changamoto mbalimbali za wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Tanzania

na Japan. Katika majadiliano hayo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali ilitoa ufafanuzi wa changamoto tatu (3) zilizowasilishwa na Ofisi ya Ubalozi wa Japan ambazo zilihusu utoaji wa viza, vibali vya kazi na makazi; taratibu za ukusanyaji wa kodi; na masuala ya ushindani wa haki katika soko.

B. Kukuza Biashara za Watanzania kupitia Kliniki

117. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea na jitihada za kukuza biashara za watanzania kupitia taasisi zake ambapo katika mwaka 2025/2026 Wizara imetoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara msisitizo ukiwekwa katika usajili, leseni, pamoja na mabadiliko ya sheria zinazosimamiwa na BRELA. Elimu hiyo imetolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari, maonesho na mikutano. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wakala ilitoa mafunzo kwa wadau walioshiriki maonesho sita (6) ya kibiashara. Maonesho hayo ni maonesho ya Wakulima Nanenane; Tiba Asili; Biashara Afrika Mashariki; Madini; Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini; na Maonesho ya Tiba Lishe ambapo kupitia maonesho hayo takribani wadau 27,000 walielimishwa.

118. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia BRELA ilitoa elimu kupitia kliniki za biashara zilizofanyika katika mikoa mbalimbali kwa nyakati tofauti, zikiwemo kliniki ya biashara katika Mkoa wa Mwanza wakati wa michezo ya SHIMIWI, kliniki ya biashara katika Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa maonesho ya Wiki ya Huduma kwa Mteja pamoja na kliniki za biashara wakati wa michezo ya SHIMMUTA katika Mkoa wa Morogoro. Kwa upande wa vyombo vya habari, BRELA ilitoa elimu kupitia vipindi nane (8) vya luninga, vipindi 20 vya redio, pamoja na uchapishaji wa taarifa 23 katika magazeti.

119. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TanTrade imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za usaidizi kibiashara kupitia kliniki za Biashara ambapo jumla ya wadau 986 walihudumiwa katika majukwaa mbalimbali ya maonesho. Kupitia kliniki hizo jumla ya changamoto 192 ziliwasilishwa ambapo 191 zilipatiwa ufumbuzi kupitia TanTrade na SIDO; kampuni 137 zilisajiliwa na BRELA na BPRA; kampuni 107 zilipata elimu ya uzalishaji bora na alama za ubora kupitia TBS na WMA. Kupitia kliniki hizo, wadau 32 walipata

ufahamu wa taratibu za vibali vya kemikali kupitia GCLA; wafanyabiashara 45 waliunganishwa na masoko ya kitaifa na kimataifa; kampuni 41 zilishauriwa kuhusu mashine, vifungashio na mikopo; kampuni 79 zilipata elimu ya kodi na kampuni saba (7) zilipata TIN kupitia TRA; na kampuni tano (5) ziliunganishwa na kampuni ya Islamabad kutoka Pakistani kwa ajili ya kuuza tani 300 za maharage.

C. Kutayarisha Viwango vya Kitaifa Katika Sekta/Nyanja Mbalimbali

120. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imekamilisha viwango muhimu pamoja na viwango mbalimbali katika Sekta ya Kilimo, Chakula na Uhandisi. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya viwango 230 vilitayarishwa. Aidha, jumla ya viwango 499 vipo kwenye hatua za mwisho za maandalizi ambapo vitakamilika ndani ya mwaka 2025/2026.

D. Kutoa Leseni ya Ubora Kwa Bidhaa Katika Sekta Mbalimbali Zikiwemo Bidhaa za Wajasiriamali Wadogo

121. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya leseni 856 za nembo ya ubora ya TBS zilitolewa sawa na asilimia 85.6 ya lengo la kutoa leseni 1,000 kwa mwaka. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 349 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa mbalimbali kama vile siagi ya karanga, asali, maji ya kunywa, pombe kali (spirit), vifungashio, mchele na pombe nyingine. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

E. Kusajili Majengo, Maeneo ya Uzalishaji, Uuzaji na Usambazaji wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi

122. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TBS imeendelea na huduma za kusajili majengo yanayohifadhi bidhaa za chakula na vipodozi kwa lengo la kuhakiki ubora na ufanisi wa maeneo hayo ili kuendelea kulinda afya za walaji. Hadi kufikia Aprili 2026, TBS imesajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa

bidhaa za chakula na vipodozi 31,598 sawa na asilimia 87.8 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 36,000 kwa mwaka. Kati ya maeneo yaliyosajiliwa, maeneo 27,295 yanajihusisha na chakula na maeneo 4,303 yanajihusisha na vipodozi.

F. Kusajili Bidhaa za Chakula na Vipodozi

123. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia TBS imesajili bidhaa za chakula na vipodozi 2,070 ambavyo ni sawa na asilimia 86.3 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 2,400 kwa mwaka. Kati ya bidhaa hizo, bidhaa 1,406 ni za chakula na bidhaa 664 ni za vipodozi.

124. Mheshimiwa Spika; katika kuhakikisha bidhaa za chakula na vipodozi zina ubora unaotakiwa, Wizara kupitia TBS imesogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kuanzisha ofisi katika kanda tisa (9); ujenzi wa maabara katika kanda ya kati Dodoma na kanda ya ziwa Mwanza. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga maabara katika kanda ya kaskazini Arusha. Vilevile Wizara imeendelea kusajili bidhaa zinazozalishwa ndani na zile zinazoingia nchini; na kuendelea na utoaji wa ithibati ya bidhaa za chakula na vipodozi kwa kufanya tathmini na kaguzi za awali wa kiwanda na kufanya kaguzi endelevu za bidhaa sokoni.

G. Kukagua na Kutoa Vibali kwa Bidhaa Zitokazo Nje ya Nchi

125. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya vyeti vya ubora 128,430 vimetolewa kwa shehena za bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambayo ni sawa na asilimia 91.7 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 140,000 kwa mwaka. Kati ya vibali hivyo, vibali 40,225 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nje ya nchi na vibali 88,205 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nchini. Aidha, jumla ya magari 50,919 yaliyotumika nje ya nchi yalikaguliwa sawa na asilimia 101.8 ya lengo la kukagua magari 50,000 kwa mwaka.

H. Kuthibitisha Kampuni Chini ya Mifumo ya Ubora na Uongozi

126. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya kampuni 15 zilithibitishwa kuwa na mifumo yenye ubora wa kimenejimenti

sawa na asilimia 93.8 ya lengo la kuthibitisha kampuni 16 kwa mwaka.

I. Kupima Sampuli za Bidhaa Mbalimbali na Kufanya Ugezi kwa Vifaa/Mashine Mbalimbali

127. Mheshimiwa Spika; katika kusimamia ubora wa bidhaa, Wizara kupitia TBS hupima ubora wa bidhaa kwa kupitia sampuli zinazoletwa kwenye maabara. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya sampuli 40,444 zilipimwa katika maabara mbalimbali za TBS kwa lengo la kuhakiki ubora ambayo ni sawa na asilimia 101.1 ya lengo la kupima sampuli 40,000 kwa mwaka. Aidha, Shirika hupima bidhaa za wazalishaji ili kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa hizo kabla ya matumizi.

128. Mheshimiwa Spika; vilevile, Shirika limefanya ugezi (calibration) wa vifaa/mashine mbalimbali ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya vifaa 12,444 vilifanyiwa ugezi ambavyo ni sawa na asilimia 103.7 ya lengo la kufanya ugezi wa vifaa 12,000 kwa mwaka. Lengo la kufanya ugezi wa mitambo au vifaa mbalimbali vinavyotumika katika uzalishaji wa bidhaa ni kuhakikisha usawa/usahihi wa vipimo wakati wa matumizi ya vifaa hivyo.

J. Kuweka Kinasaba Katika Kusimamia Ubora wa Bidhaa

129. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TBS imeendelea kutekeleza jukumu la kuweka kinasaba kwenye mafuta ambapo hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya lita bilioni 4.35 za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ziliwekewa kinasaba sawa na asilimia 90.8 ya lengo la kuweka kinasaba katika lita bilioni 4.8 za mafuta kwa kipindi cha mwaka. Lengo la kuweka kinasaba ni kuendelea kudhibiti ubora wa mafuta pamoja na upotevu wa mapato ya Serikali kwa kuuza mafuta yasiyolipiwa kodi katika soko la ndani. Aidha, mafuta ambayo hayawekewi kinasaba ni yale yanayosafirishwa kwenda nchi jirani na mafuta yenye msamaha wa kodi yanayotumika kwenye miradi maalum.

K. Kupata Ithibati ya Umahiri ya Kiwango cha Kimataifa cha ISO/IEC 17020

130. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2025/2026, TBS, ilifanikiwa kupata ithibati ya umahiri (accreditation) ya kiwango cha kimataifa cha ISO/IEC 17020 katika ukaguzi wa bidhaa ambayo ilitolewa na taasisi ya Huduma za Umahiri ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika yaani SADCAS. Hatua hiyo imepelekea TBS kuwa taasisi ya kwanza nchini na ya pili kwa ukanda wa Afrika Mashariki kupata ithibati hiyo. Ithibati ya umahiri wa mfumo wa ukaguzi katika kiwango cha kimataifa ni hatua muhimu na ya kimkakati inayoiwezesha nchi yetu kuepuka vikwazo vya kiufundi katika biashara, kuaminika kwa matokeo ya udhibiti na kurahisisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi na hivyo kukuza uchumi wa Taifa.

L. Udhibiti wa Bidhaa za Bandia

131. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia FCC imefanikiwa kutekeleza operesheni maalum za udhibiti katika bidhaa mbalimbali ikiwemo pombe bandia. Katika operesheni zilizofanyika katika mkoa wa Dar es Salaam, jumla ya chupa 4,251 za vinywaji bandia pamoja na chupa tupu 286 na katoni tupu 250 zilikamatwa. Aidha, vifaa vya uzalishaji na ufungashaji vilikamatwa, ikiwemo mashine za kuchapisha maelezo ya bidhaa, kipima kilevi, mashine ya kufunga vifuniko, mizani, ethanoli, vyombo vya kuchanganyia na kuchujia pombe. Aidha, FCC imebaini uwepo wa bidhaa nyingine bandia za vipuri na vilainishi ambazo zilikamatwa na watuhumiwa kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Mkakati wa Wizara kupitia FCC katika kukabiliana na tatizo la bidhaa bandia unalenga kuimarisha uchunguzi wa taarifa za kiintelijensia, utekelezaji wa operesheni za ukaguzi na ukamataji pamoja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika.

132. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) mwaka 2024/2025 ilifanya utafiti na kubaini uwepo wa mwenendo wa unywaji holela wa pombe miongoni mwa jamii unaoweza kusababisha athari za kiafya, kiuchumi na kijamii. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, katika mwaka 2025/2026,

Wizara kupitia TBS imeendelea kutoa elimu kwa jamii kwa kushirikiana na Idara zingine za Serikali (Maendeleo ya Jamii, Afya) juu ya athari za matumizi holela ya pombe. Matarajio ni kuhakikisha wananchi wanatumia kwa usahihi bidhaa za pombe zinazokidhi matakwa ya ubora na usalama. Elimu hiyo imetolewa katika mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza. Hivyo, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika kudhibiti mienendo hiyo.

M. Kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Hataza na Vyeti vya Usajili wa Viwanda

133. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imefanikiwa kusajili jumla ya kampuni 16,864, kati ya 19,640 zilizokusudiwa, sawa na asilimia 86. Majina ya Biashara 30,631 yalisajiliwa kati ya 33,800 yaliyopangwa, ambayo ni sawa na asilimia 91 ya lengo. Katika eneo la Alama za Biashara na Huduma, alama 2,804 zilisajiliwa kati ya 3,600, sawa na asilimia 78 ya lengo la mwaka. Kwa upande wa maombi ya Hataza, Wakala ilitoa Hataza 44 kati ya 40 zilizolengwa, sawa na asilimia 110 ya makadirio. Sambamba na hayo, Wakala ilitoa Vyeti vya Usajili wa Viwanda 42 kati ya 65 vilivyokusudiwa, ambavyo ni asilimia 65 ya utekelezaji.

134. Mheshimiwa Spika; katika kurahisisha mazingira ya kufanya biashara nchini, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wadau wengine imeendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali. Sheria zilizofanyiwa mapitio ni pamoja na Sheria ya Kampuni Sura ya 212, Sheria ya Majina ya Biashara Sura ya 213, Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura ya 326, Sheria ya Usajili wa Hataza Sura ya 217, na Sheria ya Alama za Bidhaa Sura ya 85. Mapitio ya Sheria hizi zote yamekamilika na zipo katika hatua za uidhinishwaji.

N. Kutoa Leseni za Biashara kundi 'A' na za Viwanda

135. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia BRELA imefanikiwa kutoa jumla ya Leseni za Viwanda 512 kati ya 437 zilizopangwa, sawa na asilimia 117 ya lengo. Aidha, Leseni za Biashara kundi "A" 19,110 zilitotolewa kati ya 21,582 zilizokusudiwa,

ikiwa ni asilimia 89 ya utekelezaji. Mafanikio haya yanadhihirisha jitihada endelevu za Serikali katika kuimarisha na kurahisisha usimamizi na udhibiti wa taratibu za biashara zinazozingatia matakwa ya kisheria. Kutokana na maboresho yaliyofanyika katika mifumo ya usajili wa biashara na leseni, mteja anaweza kukamilisha taratibu za usajili na kupata cheti cha jina la biashara ndani ya siku moja, leseni siku mbili na kampuni siku tatu za kazi.

O. Kufanya Kaguzi Elimishi za Leseni za Biashara Kundi 'A' na Viwanda

136. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia BRELA imefanya kaguzi elimishi tatu (3) kati ya hizo mbili zilifanyika kwenye eneo la Leseni za Biashara kwa wafanyabiashara wa kigeni katika Soko la Kariakoo, Jijini Dar es Salaam. Jumla ya biashara za kigeni 37 zilikaguliwa, kati ya hizo, biashara 36 zilikuwa na leseni halali za biashara na biashara moja (1) ilikuwa na leseni ya biashara iliyokwisha muda wake. Kati ya biashara zilizokaguliwa, biashara 12 zilikuwa na leseni za kundi 'B' na 24 kundi 'A'. Aidha, ukaguzi wa tatu (3) ulifanyika mkoa wa Pwani. Hatua zilizochukuliwa kwa biashara ambazo hazina Leseni ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kufanya biashara kwa kufuata Sheria za Nchi na walipatiwa Leseni.

137. Mheshimiwa Spika; vilevile, kaguzi elimishi kwa Wamiliki Manufaa (Beneficial Ownership) wa kampuni zilifanyika Jijini Dar es Salaam na Arusha ambapo kampuni 632 zilitembelewa. Kati ya kampuni hizo, kampuni 398 sawa na asilimia 63 zilikuwa zimewasilisha taarifa za wamiliki manufaa na kampuni 562 sawa na asilimia 89 zilikuwa zimelipa ada za mwaka (annual return).

P. Kuendelea Kuboresha na Kuimarisha Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA kwa Ajili ya Kuboresha Utoaji wa Huduma

138. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia BRELA imeendelea kuimarisha ulinzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa kufanikiwa kukamilisha mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kujikinga na Majanga ya kimtandao. Sambamba na hilo, BRELA imetoa elimu kwa watumishi 119 kuhusu ulinzi wa taarifa mtandaoni na namna

ya kuzuia uharibifu katika mfumo unaotokana na majaribio ya udukuzi wa taarifa. Aidha, Wakala imeendelea kufanya maboresho katika mifumo ya Usajili kwa njia ya Mtandao (Online Registratioin System - ORS) na Tanzania National Business Portal – TNBP, Industrial Property Automation System – IPAS na kuifungamanisha na mifumo mingine ya Serikali inayosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Lengo likiwa ni kuleta urahisi wa huduma kufikiwa na wateja na kuondoa kero zinazoathiri kasi ya utekelezaji wa majukumu ya usajili kwa njia ya mtandao.

Q. Kutoa Leseni na Kufanya Ukaguzi wa Ghala

139. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), imetoa jumla ya leseni 367 za Waendesha Ghala na leseni mbili (2) za Wakaguzi wa ghala katika msimu wa mwaka 2025/2026. Aidha, Bodi imefanikiwa kukagua jumla ya ghala 734 za kuhifadhia mazao kabla ya msimu kuanza na wakati msimu unaendelea. Vilevile, Bodi imefanikiwa kuratibu uuzwaji wa kilo 953,913,595 za mazao ya korosho, mbaazi, ufuta, dengu, choroko, kakao, na soya yenye thamani ya shilingi trilioni 2.14 **(Jedwali Na.18).**

R. Kufanya upanuzi wa Utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Kuongeza Bidhaa za Kilimo na Zisizo za Kilimo Katika Mfumo

140. Mheshimiwa Spika; Bodi imeendelea kuongeza wigo wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Sekta mbalimbali za uzalishaji nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026 mfumo una bidhaa 15 za kilimo ambazo ni Korosho, Ufuta, Mbaazi, Dengu, Choroko, Mahindi, Mpunga, Mchele, Vitunguu swaumu, Maharage, Chai, Kahawa, Kakao, Karanga na Mhogo mkavu na moja (1) isiyo ya kilimo ambayo ni Asali. Katika kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, Bodi imewezesha kufungwa kwa kamera za CCTV katika ghala 54 katika mikoa ya Lindi, Pwani na Mtwara. Zoezi hili linaendelea kutekelezwa katika maghala yote yanayotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala nchini.

141. Mheshimiwa Spika; ili kuboresha uwazi na ujumuishi katika utekelezaji wa shughuli za mfumo wa stakabadhi za ghala, Bodi imeendelea kufanya usaili wa waendesha ghala kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Bodi za Mazao, Soko la Bidhaa Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, vyama vya msingi (AMCOS), Ofisi ya Mkoa na Halmashauri katika utaratibu mzima wa upatikanaji wa Waendesha Ghala Mahiri. Zoezi hili limekuwa hatua muhimu katika kujenga uwazi na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mfumo na hata kurahisisha utatuzi wa changamoto pale zinapojitokeza.

142. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia WRRB imeendeleza jitihada za kuongeza bidhaa mbalimbali nchini katika mfumo wa stakabadhi za ghala na ujumuishi wa sekta binafsi kwa kushughulikia kikwazo cha waweka mali ghalani kukosa mikopo kutoka taasisi za fedha kwa kutumia stakabadhi za ghala. Ili stakabadhi za ghala zitumike kama dhamana kwenye taasisi za fedha, kunahitaji Mameneja Dhamana wa taasisi za fedha kuwa na weledi wa utoaji wa dhamana katika stakabadhi za ghala. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa tarehe 17 Aprili 2026 Benki Kuu ya Tanzania ilirasimisha utaratibu wa Meneja Dhamana chini ya mfumo wa stakabadhi za ghala kwa kutoa Mwongozo kwa taasisi za fedha kuwa na Mameneja Dhamana wenye leseni kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala.

143. Mheshimiwa Spika; katika kuongeza ufanisi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala inaendelea kuunganisha mifumo yake na mifumo ya wadau wengine kama vile Soko la Bidhaa (TMX), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Bodi ya Korosho. Muunganiko huu utaongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuwa kichocheo cha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati zitakazotumika katika soko.

144. Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Bodi imeendelea kuwa kichocheo cha uzalishaji na ufanyaji wa biashara kwa mikoa ambayo haikuwahi kuuza bidhaa ya korosho kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Mkoa wa Singida umeuza zao la korosho kupitia mfumo huu katika msimu wa 2024/2025 ambapo uliuza tani 128.7 (kwa mara ya kwanza) na msimu wa 2025/2026 tani 541.12 ikiwa ni

ongezeko la asimilia 320.12. Hii inaashiria kuwa mfumo huu unakuwa kichocheo katika kufanya biashara ya bidhaa na kuwakomboa Watanzania walio wengi kwa kuwa zao hili lilizoeleka kuwa ni zao la Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma.

145. Mheshimiwa Spika; Bodi imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Bodi imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda kwa kuhamasisha muunganiko baina ya taasisi zinazofanya kazi za usimamizi wa mfumo huu katika ukanda wa Afrika Mashariki. Muunganiko huu ni nyenzo muhimu ya kukuza biashara kati ya Tanzania na nchi jirani, ikizingatiwa kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi zinazozalisha kwa wingi katika ukanda huu. Hii itarahisisha bidhaa za Tanzania zinazouzwa chini ya mfumo wa stakabadhi za ghala kuwa na wigo mpana wa ushindani katika ukanda huu.

S. Kuimarisha Ushindani wa Kibiashara Nchini

146. Mheshimiwa Spika; Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara, kupitia TanTrade, imeendelea kuimarisha uwezo wa wadau wa biashara ili kuongeza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji, uongezaji thamani na upanuzi wa masoko. Katika kipindi hicho, jumla ya wadau wa biashara 1,865 waliwezeshwa kupitia mafunzo ya uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa biashara, masoko pamoja na uongezaji thamani wa bidhaa. Kati yao, washiriki 1,317 walipata mafunzo katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Rukwa, Songwe, Njombe na Mtwara kuhusu usimamizi wa biashara, namna ya kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi, matumizi ya fursa za Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa. Aidha, wazalishaji 115 wa viungo walipatiwa mafunzo katika Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga. Vilevile, wanafunzi 433 wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) walipatiwa mafunzo kuhusu fursa za biashara zilizopo nchini na katika masoko ya kikanda.

147. Mheshimiwa Spika; TanTrade, imeendelea kuimarisha utambulisho wa bidhaa za Tanzania katika Rajamu ya Taifa (Made in Tanzania) ambapo rajamu hiyo imetekelezwa rasmi na

kuanza kutumika katika masoko ya ndani na nje. Hadi kufikia Aprili, 2026, kampuni 20 zilisajiliwa kutumia rajamu hiyo na bidhaa 58 zilikidhi vigezo vya matumizi yake. Rajamu hiyo ilinadiwa katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, 2025 na katika Mkutano wa 27 wa SADC na kuongeza muonekano wa bidhaa za Tanzania kimataifa.

148. Mheshimiwa Spika; Mamlaka imeendelea kuboresha upatikanaji wa taarifa za biashara ambapo taarifa za bei zilikusanywa kutoka masoko nane (8) ya mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Taarifa hizo zilisambazwa kwa jumla ya wadau 75,103 kupitia TanTrade Biashara App, tovuti na mitandao ya kijamii. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya watumiaji 1,460 walikuwa wamejisajili rasmi katika TanTrade Biashara App na kufanikiwa kufuatilia mwenendo wa bei katika masoko 67 nchini. Aidha, tathmini ya fursa za bidhaa za nafaka, nyama na matunda ilifanyika katika masoko ya AfCFTA na EAC ambapo fursa zilionekana zaidi katika nchi za DRC, Uganda, Rwanda, Comoro na Kenya. Taarifa hizo zilisambazwa kwa wafanyabiashara ili kuongeza ushindani wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya kikanda.

T. Kutafuta Masoko ya Bidhaa za Tanzania Nje ya Nchi

149. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea na jitihada za kutafuta na kupanua masoko kwa bidhaa na huduma za Tanzania zinazozalishwa nchini katika masoko ya kimataifa; kutangaza fursa za biashara, uwekezaji na miradi ya kimkakati ya nchi, na kusimamia matukio ya ukuzaji biashara katika kutangaza bidhaa na huduma yaliyoratibiwa na sekta binafsi na Umma kwa lengo la kuimarisha mwenendo wa tasnia ya ukuzaji biashara nchini. Kupitia jitihada hizo, Wizara imefanikiwa kuratibu matukio ya ukuzaji biashara na kuwezesha ushiriki wa wafanyabiashara nchini ili kupata masoko ya bidhaa na huduma zitolewazo kupitia uratibu na ushiriki wa maonesho; majukwaa ya biashara; mikutano na makongamano; na kupitia mpango wa kuanzisha kitengo cha Intelijensia ya Masoko na Viwanda kama ifuatavyo:

i. Maonesho

150. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade) iliratibu Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, mwaka 2025 (49th DITF) yaliyofanyika mwezi Juni hadi Julai, 2025 Dar es salaam. Lengo la maonesho hayo ni kutoa fursa ya kuchochea ukuaji wa biashara na uchumi wa nchi kwa kuwawezesha wazalishaji wa bidhaa na huduma kutangaza na kutafuta masoko endelevu ndani na nje ya nchi. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na maonesho hayo ni ununuzi wa papo kwa papo wenye thamani ya shilingi bilioni 7.06 kutokana na jumla ya watembeleaji 385,500 wa maonesho hayo. Mauzo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 94.7 ikilinganishwa na mauzo ya papo kwa papo ya shilingi bilioni 3.63 yaliyofanyika katika Maonesho ya 48 Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, mwaka 2024.

151. Mheshimiwa Spika; mafanikio mengine ni kupatikana kwa miadi ya kibiashara yenye thamani ya shilingi bilioni 4.8 iliyofanyika katika sekta za teknolojia, mifugo, usafirishaji, madini, kilimo, uvuvi na ujenzi; uzinduzi wa Rajamu ya Taifa "Made in Tanzania", na kampuni nane (8) zilisajiliwa kutumia rajamu hiyo. Kampuni hizo ni *Airplanes Africa Limited*, Yusuph Maiko Lehemu (TingaTinga), African Uji Mix, Amir Hamza (T) Ltd, *Tanfoam ltd, Bakhresa Food Products Ltd*, *Soosung Engineering Co.ltd* na Jitegemee Holding Co. Ltd; kupatikana kwa ajira za muda mfupi 22,593 katika kutoa usaidizi wa huduma mbalimbali wakati wa maandalizi ikiwemo ufundi na ujenzi wa miundombinu na mabanda ya biashara, usafirishaji, migahawa, mapambo na upagaji.

152. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia Tan trade ilisimamia na kuratibu maonesho ya *Tanzania Poultry Show* yaliyofanyika katika Jiji la Dar es Salaam mwezi Oktoba, 2025 ambapo jumla ya kampuni 54 za ndani na nje ya nchi zilishiriki. Kati ya kampuni hizo, kampuni za ndani zilikuwa 30 na 24 za nje. Kampuni hizo zilitoka katika nchi 11 ambazo ni Tanzania, Uholanzi, Ufaransa, India, Ujerumani, Ubelgiji, Kenya, Canada, Hungary, Malawi, na Afrika Kusini. Kupitia maonesho hayo, wadau wa biashara walipata elimu ya teknolojia ya ufugaji wa kuku na ndege wafugwao, namna bora ya ufugaji, elimu ya bima pamoja na elimu ya

mikopo kwa wafanyabiashara wa kati na wadogo. Vilevile, TanTrade iliratibu maoesho ya EACLC *Shopping Festival* yaliyofanyika mwezi Agosti, 2025 katika Jiji la Dar es salaam. Kupitia maonesho hayo, jumla ya wafanyabiashara 200 wakiwemo wajasiriamali wadogo walishiriki na kutangaza bidhaa na huduma zao.

153. Mheshimiwa Spika; Wizara kwa kushirikiana na iliyokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu iliratibu ushiriki wa wajasiriamali katika Maonesho ya 25 ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki maarufu kama "Nguvu Kazi au Jua Kali" yaliyofanyika Nairobi nchini Kenya mwezi Novemba, 2025. Kupitia maonesho hayo zaidi ya wajasiriamali wadogo na wa kati 300 walipata fursa ya kutangaza bidhaa zao. Kutokana na ushiriki huo, jumla ya mikataba saba (7) ya kibiashara ilisainiwa katika bidhaa za magari, vikapu, nguo, korosho, viungo na nafaka; na mauzo yenye thamani ya shilingi 271,000,000 yalipatikana.

154. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia SIDO ilihamasisha wajasiriamali 1,366 kushiriki katika maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Maonesho ya Madini, Maonesho ya Wiki ya Chakula na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wajasiriamali hao. Kupitia maonesho hayo, wajasiriamali walikutanishwa na watoa huduma kwa lengo la kuongeza wigo wa soko la bidhaa zao ili kupata wateja wapya; kubadilishana uzoefu na wajasiriamali wengine; na kuunganishwa na wakulima pamoja na taasisi mbalimbali.

ii. Majukwaa ya Kitaifa na Kimataifa

155. Mheshimiwa Spika; Wizara imefanikiwa kuratibu ushiriki wa Watanzania 175 katika Maonesho ya Dunia ya Expo Osaka Japan 2025 yaliyofanyika Osaka - Japan kuanzia mwezi Aprili hadi Oktoba, 2025. Kupitia jukwaa hilo, jumla ya wageni 4,514,000 walitembelea banda la Tanzania kuanzia mwezi Aprili hadi Oktoba, 2025 ambapo bidhaa 134 za madini na mazao zilinadiwa na kuuzwa. Bidhaa hizo ni pamoja na madini (Tanzanite, Ruby, Garnet), viungo vya chakula, korosho, bidhaa za mkonge na karanga, karafuu, asali, mwani, kahawa na chai. Aidha, miradi ya uwekezaji katika maeneo ya nishati, reli/usafirishaji, kilimo, afya na

uchumi wa buluu ilitangazwa. Vilevile, mauzo ya papo kwa papo ya shilingi milioni 300 yalifanyika; na kusainiwa kwa hati za makubaliano nane (8) kati ya Mashirika ya Tanzania na Japan zenye thamani ya shilingi bilioni 38.

156. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TanTrade iliratibu ushiriki wa kampuni saba (7) za Kitanzania katika maonesho ya *China International Import Expo (CIIE),* yaliyofanyika Novemba, 2025 Shanghai China. Kampuni hizo ni *Chrises Real Solutions Company Limited, Tingatinga Art Cooperative Society, Swahili Honey, Riyami Resources, Investment Business and Seaweed Development, Tanzanite Love Company Limited* pamoja na *EACLC*. Katika maonesho hayo, bidhaa za madini, mwani, kahawa, asali, parachichi, kokoa, mvinyo, vipodozi na sanaa za mikono zilioneshwa pamoja na kupokea mahitaji ya bidhaa tani 2,000 ikiwemo soya zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6.

iii. Mikutano na Makongamano

157. Mheshimiwa Spika; Wizara imefanikiwa kushiriki katika Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Korea lililofanyika mwezi Novemba 2025. Katika kongamano hilo, jumla ya washiriki 74 walishiriki ambapo kati yao washiriki 59 ni kutoka Tanzania na washiriki 15 ni kutoka Korea. Kongamano hilo liliandaliwa kwa lengo la kuunganisha waagizaji kutoka Korea na wazalishaji wa Tanzania. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na kongamano hilo ni pamoja na kusainiwa kwa hati ya makubaliano kati ya KOIMA na TPSF kwa lengo la kuendeleza mashirikiano ya biashara na uwekezaji; na kupatikana kwa kampuni sita (6) za Tanzania ambazo zinaendelea na mazungumzo ya kibiashara na kampuni kutoka KOIMA-Korea. Makubaliano hayo ni kati ya kampuni za METEL na MEDIPROTECH; KOLMAR BNH, G&S Clearing and Forwading Ltd na CMT Global Logistics; Natureripe Kilimanjaro Ltd na MEDIPROTECH; KOLMAR BNH, TANZANEX Co. Ltd na C.S for life; National Ranching Co. Ltd (NARCO) na Highland Innovation Co. Ltd; pamoja na Union Meat.

iv. Kuanzisha Kitengo cha Intelijensia ya Masoko na Viwanda

158. Mheshimiwa Spika; katika mazingira ya sasa ya ushindani wa

kibiashara na viwanda duniani, upatikanaji wa taarifa sahihi, za uhakika na za wakati kuhusu masoko na teknolojia za viwanda ni suala la muhimu katika maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Biashara. Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza viwanda na kuongeza mauzo nje ya nchi. Hata hivyo, kumekuwapo na ukosefu wa taarifa za masoko ya kimataifa; kutokujua bidhaa zinazohitajika katika misimu ya mahitaji, viwango vya ubora na vikwazo vya kibiashara (tariffs & NTBs); na ugumu wa kutofautisha wawekezaji makini na wale wenye nia ya "dumping", pamoja na ukosefu wa taarifa za uwezo wao wa kifedha na teknolojia. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imedhamiria kuanzisha Kitengo cha Intelijensia ya Masoko na Viwanda.

159. Mheshimiwa Spika; kitengo hicho kitatekeleza majukumu ya kukusanya na kuchambua taarifa za masoko ya kimataifa; kubaini fursa za bidhaa, mwenendo wa mahitaji na vigezo vya kuingia sokoni; kuandaa na kusambaza taarifa za fursa za masoko kwa wafanyabiashara; na kutoa taarifa za tahadhari za haraka kuhusu mabadiliko ya masoko. Kuanzishwa kwa kitengo hicho ni hatua muhimu katika kujenga uchumi wa viwanda unaotegemea taarifa sahihi.

I. Kusimamia na Kuimarisha Mifumo ya Ufanyaji Biashara

160. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TanTrade imehuisha taratibu za uondoshaji wa bidhaa saba (7) kupitia Bandari ya Dar es Salaam, ambazo ni parachichi, mihogo, ngozi, kokoa, viungo, nafaka na uyoga. Bidhaa hizo zimewekwa katika Mfumo wa Trade Portal (trade.tanzania.go.tz) ili kuongeza uwazi, kupunguza muda wa kufuata taratibu na kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wafanyabiashara wa ndani na nje. Aidha, taarifa za taasisi wezeshi mbili (2) za Zanzibar ambazo ni *Zanzibar State Trade Corporation* na *Zanzibar Seaweed Company*; na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda zilihuishwa katika mfumo huo ili kuboresha usomaji wa mifumo na kuimarisha utoaji wa huduma za biashara ya kimataifa.

J. Kuchunguza Mashauri ya Ushindani

161. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeshughulikia mashauri 43 ya ushindani sokoni. Kati ya mashauri hayo, mashauri 38 yanahusu miungano ya kampuni ambayo haikutolewa taarifa FCC na mashauri matano (5) yanahusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko. Kati ya mashauri 38 yanayohusu miungano ya kampuni ambayo hayakutolewa taarifa FCC, uamuzi wa mwisho umetolewa kwenye mashauri manne (4), mashauri 18 yameshatolewa uamuzi wa awali na uchunguzi kwenye mashauri 16 bado unaendelea. Kwa upande wa matumizi mabaya ya nguvu ya soko, uchunguzi kwenye mashauri manne (4) yanayohusiana na uzalishaji na usambazaji wa madaftari, sarufi, sigara na bia yanaendelea na uamuzi wa awali umetolewa kwenye soko la usambazaji wa vinywaji baridi nchini.

162. Mheshimiwa Spika; kati ya mashauri matano (5) yanayohusu makubaliano yanayokatazwa na Sheria ya Ushindani, (FCC) inaendelea na hatua ya utekelezaji (Enforcement) katika mashauri mawili (2) yanayohusu soko la uzalishaji na usambazaji wa nondo na soko la uingizwaji na usambazwaji wa magari mapya nchini na inatarajia kutoa maamuzi ya mwisho kwa Wadau wa mashauri hayo. Pia FCC imekamilisha uchunguzi kwenye soko moja (1) la uzalishaji na usambazaji wa saruji nchini na inatarajia kutoa maamuzi ya awali kwa Waadawa husika. Mashauri mawili (2) yanayohusu masoko ya mbolea na kakao yapo katika hatua ya uchunguzi na ukusanyaji wa taarifa unaendelea.

K. Kuchunguza Maombi ya Miungano ya Kampuni

163. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeshughulikia jumla ya maombi ya Miungano ya Kampuni 62, maombi hayo yalitoka katika sekta za uzalishaji (13); utalii (3); madini (5); bima (8); usafirishaji (6); nishati (4); Michezo (4): benki (2); Afya (4); kilimo (6); ardhi na nyumba (2); mawasiliano (4); Ujenzi (1). Kati ya maombi hayo, maombi 37 yaliidhinishwa bila masharti baada ya Tume kujiridhisha kuwa miungano hiyo haitakuwa na athari hasi za kiushindani. Maombi

manne (4) yaliidhinishwa kwa masharti mahsusi ili kuhakikisha kampuni zinazoungana haziathiri ushindani sokoni.

164. Mheshimiwa Spika; kwa upande wa maombi 21 yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi na yanatarajiwa kutolewa maamuzi katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025/2026. Miungano hii imeendelea kuleta faida katika ukuaji wa sekta mbalimbali kwa kukuza mitaji na teknolojia, kuwezesha upatikanaji wa masoko na kuongeza ajira kwa watanzania. Mathalan, kununuliwa kwa hisa asilimia 65 za Hospitali ya Regency na kampuni ya Tasakhtaa Hospital Limited imesaidia kukua kwa mtaji na upanuzi wa soko katika Sekta ya Afya. Vilevile, FCC kwa kushirikiana na BRELA, ilifanya upekuzi wa jumla ya kampuni 1,214 katika Kitabu cha Msajili wa Makampuni. Lengo la upekuzi huo ni kujiridhisha kuwa kampuni hizo zilizofanya mabadiliko ya muundo wa udhibiti wa kampuni, yalitekelezwa bila kuathiri utekelezaji wa vifungu vya Sheria ya Ushindani.

L. Kuendelea Kuchukua Hatua dhidi ya Bidhaa Bandia na Kumlinda Mlaji

165. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia FCC imeendelea na juhudi za kupambana na bidhaa bandia na kumlinda mlaji dhidi ya mienendo potofu, hadaifu na kandamizi katika soko la bidhaa na huduma. Hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia FCC imeshughulikia malalamiko 63 ya walaji wadogo ambapo malalamiko 45 yalipatiwa ufumbuzi na malalamiko 18 yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za utatuzi; imesajili na kuthibitisha mikataba 27 inayoandaliwa na upande mmoja (SFCC) kwa lengo la kuondoa masharti kandamizi kwa walaji; imefanya kaguzi za kushtukiza 31 ambapo bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 4.74 zilikamatwa kwa kuvunja Sheria ya Alama za Bidhaa ya 1963 (kama ilivyorekebishwa). Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na vipuri vya magari, vilainishi vya magari, pombe kali, vyandarua, dawa za viatu na betri. Vilevile, imeendelea na ukaguzi wa kila siku wa mizigo (cargoes) ya bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Bandari na Bandari kavu zote (ICDs) na vituo vya pamoja vya mipakani. Kati ya mizigo ya bidhaa 4,791 iliyokaguliwa, mizigo ya bidhaa 418 ilikamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa Sura ya 85.

166. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia FCC imeendelea kutekeleza mkakati unaohusisha matumizi ya teknolojia za ukaguzi wa bidhaa, utoaji wa elimu kwa umma na kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za serikali, sekta binafsi na wananchi ili kuhakikisha udhibiti endelevu wa bidhaa bandia, kulinda afya ya wananchi, kuongeza mapato ya Serikali na kuimarisha ushindani wa haki katika soko.

M. Kutoa Maamuzi ya Mashauri ya Rufaa Yanayowasilishwa Katika Baraza la Ushindani

167. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) imepokea na kutoa maamuzi ya mashauri 25 yaliyokuwa tayari kwa ajili ya usikilizwaji. Mashauri hayo yanajumuisha rufaa zinazotokana na maamuzi ya mamlaka mbalimbali za udhibiti na ushindani nchini, ikiwemo mashauri yanayohusu ukiukwaji wa sheria za ushindani, matumizi mabaya ya nguvu ya soko, miunganiko ya kampuni (mergers and acquisitions), bidhaa bandia, migogoro ya leseni na tozo za huduma zinazodhibitiwa na mamlaka za kisekta. Matokeo ya maamuzi ya mashauri hayo yameongeza na kuchangia uwajibikaji katika soko; uwajibikaji kwenye ushindani katika sekta ya viwanda na biashara; kampuni kuongeza umakini katika kufuata sheria za nchi; kuongezeka kwa uwazi na ushindani wa bei katika kampuni mbalimbali nchini; ufanisi katika uzalishaji; usambazaji wa huduma na bidhaa; kukuza ubunifu; na kumlinda mlaji.

N. Usimamizi na Uhakiki wa Vipimo Vitumikavyo na Viingiavyo Nchini

168. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) imekagua na kuhakiki vipimo 995,884 sawa na asilimia 112.5 ya lengo la kukagua vipimo 885,307. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa, vipimo 30,512 vilirekebishwa na vipimo 713 vilikataliwa. Aidha, Wakala iliendelea kufanya kaguzi za kawaida na za kushtukiza ambapo jumla ya kaguzi 4,192 sawa na Asilimia 104.8 zilifanyika kati ya kaguzi 4,000 zilizopangwa kufanyika.

169. Mheshimiwa Spika; vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni Pampu za kuuzia mafuta ya nishati; *Flowmeters* zitumikazo kupimia mafuta kwenye bohari na maghala ya kuhifadhia mafuta; tenki za kusafirishia mafuta na tenki za kuhifadhia mafuta; mita za maji; mizani inayotumika kupimia bidhaa mbalimbali; vipimo vya urefu; na malori yabebayo kokoto, mchanga na vifusi. Vilevile, uhakiki na ukaguzi ulifanyika kwenye maeneo mbalimbali yakiwemo masoko ya nafaka, vituo vya mafuta, bohari/maghala ya mafuta, sehemu za kuuzia mbao, bucha na maduka ya kuuzia bidhaa mbalimbali.

170. Mheshimiwa Spika; kaguzi na ufuatiliaji wa uhakiki wa vipimo vinavyotumika katika ushushaji wa mafuta jamii ya petroli pamoja na mafuta ya kula ulifanyika. Kupitia kaguzi hizo, jumla ya meli 116 zilizoingia nchini zenye jumla ya lita bilioni 7.97 zilikaguliwa ambapo kati ya lita hizo, lita bilioni 2.43 zilikuwa petroli, lita bilioni 4.95 dizeli, lita bilioni 0.35 mafuta ya taa na lita bilioni 0.25 mafuta ya kula. Aidha, taarifa inayotokana na ukaguzi hutumiwa na Mamlaka nyingine za Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya utozaji wa kodi, EWURA kwa ajili ya upangaji wa bei za mafuta, Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa ajili ya wanunuzi na wauzaji wa mafuta pamoja na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

O. Ukaguzi wa Bidhaa Zilizofungashwa Kwenye Maeneo ya Mipakani, Bandarini na Viwandani

171. Mheshimiwa Spika; Wakala imeendelea kufanya kaguzi za bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya mipaka ya kivipimo ya Sirari Mkoa wa Mara; Mtukula, Kagera; Namanga, Arusha; Holili na Tarakea, Kilimanjaro; Tunduma, Songwe; Horohoro, Tanga; Kasumulu, Mbeya; Manyovu, Kigoma; Kwala, Pwani; Mbweni, Dar es Salaam; na maeneo ya viwandani. Ukaguzi huo ulilenga kuhakiki usahihi wa kiasi/ idadi iliyotamkwa (declared quantity). Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya shehena 13,458 zenye bidhaa 16,768 zilikaguliwa na kuhakikiwa, ikilinganishwa na lengo la shehena 16,180 zenye bidhaa 17,774 zilizokadiriwa kuingia nchini. Vilevile, kulifanyika uhakiki wa bidhaa zinazozalishwa na kufungashwa na viwanda vya ndani, ambapo jumla ya bidhaa 18,296 zilikaguliwa ikilinganishwa na lengo la kukagua bidhaa

17,990.

172. Mheshimiwa Spika; bidhaa ambazo hazikidhi matakwa/vipimo adhabu hutolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 46 cha Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 ambapo, hupigwa faini na kuamriwa bidhaa hizo kuteketezwa kwa kukatwakatwa mbele ya wakaguzi, kisha kurudishwa kwa mzalishaji ili zitengenezwe upya kwa vipimo sahihi. Aidha, watuhumiwa wanaofikishwa mahakamani hupewa adhabu kwa mujibu wa Kifungu cha 45 cha Sheria hiyo au kutaifishwa kwa bidhaa hizo kwa mujibu wa Kifungu cha 50.

P. Kuboresha Mazingira ya Utendaji Kazi pamoja na Ununuzi wa Vifaa vya Kisasa vya Uhakiki wa Vipimo

173. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi ya WMA kwa kuanza mchakato wa ujenzi wa Ofisi za Wakala katika mikoa ya Lindi na Songwe. Hadi kufikia Aprili, 2026, usanifu na michoro ya majengo umekamilika. Hatua inayofuata ni kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Sambamba na hilo, Wakala imenunua vifaa vya kisasa vya uhakiki wa vipimo ikiwa ni pamoja na vifaa vya TEHAMA (Laptop 35, Desktop 28, Scanner 2, Multifuctional printer 20, Photocopier 2, Colour printer 1). Vilevile, Wakala imekamilisha ununuzi wa vifaa vya kitaalam ambavyo ni:- *Digital Thermometer 1, CNG Dispensing Pump Verifier 2, Electronic Balances 31, Mass comperator 2, Flow Meters 4, Proving Tanks 11, Preasure Gauges 9, Portable Legal Metrology Test Kit for Field Inspectors 40,* na *Legal Metrology Test Kits for Verifying High-Precision Balances 20.* Upatikanaji wa vifaa hivyo utaongeza wigo wa uhakiki wa vipimo katika maeneo mapya na kuweza kutoa huduma kwa karibu zaidi.

Q. Kukabiliana na Changamoto ya Lumbesa

174. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia WMA, ina jukumu la kusimamia na kuhakikisha matumizi sahihi ya vipimo katika biashara na uchumi ili kulinda Wakulima, Wauzaji, Wanunuzi na Wasafirishaji wa mazao shamba. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa biashara ya mazao ya kilimo nchini, na imebaini kuendelea kuwepo kwa vitendo vya

ufungashaji na uuzaji wa mazao hayo kinyume na taratibu za Sheria ya Vipimo Sura ya 340, maarufu kama "*Lumbesa.*" Sheria, hiyo pamoja na mambo mengine inaeleza kuwa mazao yaliyofungashwa kwa namba/idadi/uzito hayapaswi kuzidi kilogramu 100 pamoja na kiasi himilivu cha asilimia 5 (Tolerance limit of +5 %) na imeelekeza wauzaji/wanunuzi wa mazao kutumia mizani ambayo kwa mujibu wa Sheria inapaswa kuhakikiwa na Wakala wa Vipimo angalau mara moja kwa mwaka.

175. Mheshimiwa Spika; katika jitihada za kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imefanya jitihada mbalimbali kwa kufanya operesheni tisa (9) katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Mbeya, Iringa, na Njombe. Kupitia operesheni hiyo, magari 2,500 yanayosafirisha mazao yalikaguliwa, kati ya hayo magari 2,419 yalikuwa na mazao yaliyofungashwa kwa uzito unaoruhusiwa yaani usiozidi kilogramu 100 na magari 81 yalikutwa na makosa kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura ya 340 na hatua stahiki zilichukuliwa kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kutozwa faini ya papo kwa papo na kuamriwa kufungasha upya.

176. Mheshimiwa Spika; operesheni hizo ni endelevu na zinafanyika mikoa yote Tanzania Bara kupitia Ofisi za Mikoa za Wakala wa Vipimo zilizopo nchi nzima ili kutokomeza kabisa changamoto hiyo. Vilevile, Serikali imesogeza huduma ya uhakiki wa vipimo kwa wananchi kwa kuweka vituo vya muda 5,050 katika maeneo ya ofisi za Kata, Mitaa na Vijiji. Aidha, baadhi ya Halmashauri za miji na Wilaya kama vile Mpanda, Kasulu na Kibondo zimetunga sheria ndogo za ushuru wa mazao zikisisitiza upimaji wa mazao kufanyika kwa kutumia mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo.

R. Kuboresha Miundombinu ya Kufundishia na Kujifunzia katika Chuo cha CBE

177. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) inaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa 10 la *Metrology Complex* katika Kampasi ya Dar es Salaam. Hadi kufikia Aprili, 2026 ujenzi umefikia asilimia 93, ambapo shilingi bilioni 8.88 zimetumika kati ya shilingi bilioni10.39 zilizotengwa kwa hatua ya

kwanza. Jengo litakapokamilika litakuwa na kumbi 29 za mihadhara zenye uwezo wa kubeba wanafunzi 4,160, hivyo kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

178. Mheshimiwa Spika; ujenzi wa miundombinu umeenda sambamba na maboresho ya mitaala na programu ili kuongeza kiwango cha udahili. Wizara kupitia CBE imeboresha mitaala ili kukidhi mahitaji ya soko na maendeleo ya teknolojia, ikisisitiza elimu ya vitendo kupitia Programu ya Uanagenzi, ambapo wanafunzi watatumia nusu ya muda darasani na nusu kazini kupata uzoefu halisi wa kazi. Hadi kufikia Aprili, 2026 mitaala mipya nane (8) imeidhinishwa na kufanya jumla ya mitaala iliyopitishwa kufikia 71. Aidha, mitaala mingine 28 ipo katika hatua za maandalizi na uthibitishaji. Ongezeko la mitaala hiyo limepelekea kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi na hivyo kuhitaji miundombinu toshelevu ya kufundishia na kujifunzia. Mathalan, mwaka wa masomo 2023/2024 udahili ulikuwa wanafunzi 20,029 ikilinganishwa na wanafunzi 24,957 katika mwaka wa masomo 2025/2026 sawa na ongezeko la wanafunzi 4,928.

S. Uendelezaji wa Bunifu Kupitia Programu Atamizi

179. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TEMDO imeendelea kuwasaidia wajasiriamali wabunifu kwa kuwawezesha kupata huduma kama vile maeneo ya kufanyia kazi; mashine na mitambo; ushauri wa kiufundi; na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili wakue na kufikia viwango vya kujitegemea. Hadi kufikia Aprili, 2026 wajasiriamali wabunifu watano (5) ambao ni *Bivac Co. Ltd, Rest Food Process Ltd, Upendo Food Process Ltd, Simba and Alice Food Process Ltd* na *Neema Nafaka Products* wameendelea kuzalisha bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo kwenye kiatamizi cha TEMDO katika Mkoa wa Arusha ambapo ajira 220 zimezalishwa. Kati ya ajira hizo, ajira za moja kwa moja ni 100 na ajira zisizo za moja kwa moja ni 120. Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa ni pamoja na siagi ya karanga, unga lishe, vyakula lishe, biskuti na virutubisho mbalimbali.

180. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara kupitia SIDO imekamilisha jumla ya mawazo bunifu nane (8) kati ya 24 na yapo kwenye majaribio ya kufanya biashara (commercialization)

chini ya uangalizi wa SIDO. Mawazo bunifu hayo ni utengenezaji wa kifaa cha kuuza maji kwa kuweka sarafu; utengenezaji wa taulo za kike zenye uwezo wa kutumika tena; utengenezaji wa vichocheo (booster) za mbolea kwa kutumia mabaki ya nywele za binadamu; akili unde inayoendesha vifaa vya kielektroniki vya nyumbani; utengenezaji wa sabuni za asili na mimea; utengenezaji wa vifaa vya maabara ya shule kwa ajili ya mafunzo ya sayansi kwa vitendo; utengenezaji wa mikate na bidhaa nyingine zilizorutubishwa; na utengenezaji wa mabegi ya shule yenye *solar charge*. Aidha, mawazo bunifu 16 yaliyosalia yanaendelea kuatamiwa katika mkoa wa Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa, Singida na Morogoro.

181. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia TIRDO ina jumla ya wabunifu 23 wanaoatamiwa ambapo kupitia wabunifu hao, kampuni 10 tayari zimeanzishwa na kusajiliwa rasmi. Kampuni hizo ni *Plant Biodefender Ltd (Moshi), PREYO Company Ltd, Innovex Solutions and Merchants, H.O.P Electronics Technologies, Innovasie Company Ltd, Albetus Technologies, Ammacom Technologies Co. Ltd, Survey Fish Market Company, Munny Chocolate Company Ltd,* na *Kaypee Motors Ltd.* Wabunifu hao wamewezeshwa kwa kupewa maeneo ya uzalishaji kupitia mpango wa uatamiaji. Aidha, Shirika linaendelea kuwasaidia katika kuboresha ubora wa bidhaa, kuthibitisha viwango na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili waweze kupata mitaji ya kuendeleza shughuli zao.

182. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia CBE imeendelea kutoa mafunzo ya atamizi za biashara kwa lengo la kutoa mazingira bora ya kukuza bunifu za kibiashara; na kuwajengea vijana uwezo wa kiutendaji na kuwaunganisha na fursa za soko, mitaji na ushauri wa kitaalamu ili kusaidia ukuaji na maendeleo ya biashara hususan biashara changa (Start-ups). Mafunzo hayo yamegawanyika katika hatua tatu (3) ambazo ni hatua kabla ya atamizi (pre- incubation); atamizi (incubation) na baada ya atamizi (post- incubation). Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya bunifu 773 zimesajiliwa katika atamizi za biashara na teknolojia za chuo. Kati ya hizo, 278 sawa na asilimia 36 zipo katika hatua ya maandalizi; 75 sawa na asilimia 9.7 zipo kwenye atamizi; na 420 sawa na asilimia 54.3 zipo katika hatua ya baada ya atamizi.

T. Elimu na Mafunzo

183. Mheshimiwa Spika; katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Wizara imetoa elimu na mafunzo kwa umma na wajasiriamali. Elimu iliyotolewa ilihusu viwango na udhibiti ubora; urasimishaji wa biashara; matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala; matumizi sahihi ya vipimo; na teknolojia. Elimu na mafunzo yaliyotolewa katika maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Teknolojia ya Kuongeza Virutubisho Kwenye Vyakula

184. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imetoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati 78 wanaojihusisha na usindikaji wa vyakula hususan unga wa mahindi, mafuta, chumvi na ngano katika mikoa ya Simiyu na Shinyanga. Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha wajasiriamali hao wanatumia teknolojia ya uongezaji wa virutubishi katika vyakula hivyo ili viweze kukidhi soko la ndani na nje. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wajasiriamali kuhusu ujasiriamali, uendeshaji biashara na ujuzi maalum wa kiufundi katika uzalishaji.

185. Mheshimiwa Spika; mafunzo mengine yalilenga masuala ya KAIZEN, utengenezaji sabuni, batiki, vipodozi, usalama viwandani, ufungashaji na usimamizi wa mikopo ambapo Wanawake 5,604 sawa na asilimia 68 na Wanaume 2,638 sawa na asilimia 32 walishiriki. Kutokana na mafunzo hayo jumla ya biashara ndogo na za kati 646 zilirasimishwa katika maeneo ya usindikaji vyakula, utengenezaji sabuni na utengenezaji batiki. Halikadhalika ushauri kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara ulitolewa kwa wajasiriamali kwa ushirikiano na Mamlaka za Serikali za Mitaa, BRELA, TBS, GCLA na TRA.

ii. Mafunzo na Semina Kuhusu Viwango na Udhibiti Ubora

186. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TBS imeendelea kutoa elimu kwa wazalishaji wa bidhaa za viwandani, wasindikaji na umma wa watanzania kuhusu dhana nzima ya viwango na ubora. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya wadau 1,215 wa sekta tano (5) ndogo za vifungashio, matofali, vipodozi, unga wa mahindi na vyakula vya mifugo walipewa mafunzo juu ya

masuala ya viwango ambayo ni sawa na asilimia 67.5 ya lengo la kutoa mafunzo kwa wadau 1,800 kwa mwaka mzima. Mafunzo hayo yalifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Singida, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Rukwa, Songwe, Mbeya na Ruvuma. Aidha, Shirika limeendelea kutoa mafunzo hayo kwa wajasiriamali wadogo (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima ya kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama ili kuwezesha kukidhi ushindani wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

iii. Ugani na Mafunzo ya Zana za Kilimo na Teknolojia za Vijijini

187. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea na shughuli za ugani na mafunzo yenye lengo la kukuza matumizi ya teknolojia mbalimbali kwa maendeleo ya viwanda. Wizara kupitia CAMARTEC imetoa mafunzo ya matumizi ya teknolojia za viwandani kupitia Vitovu vya Teknolojia za Kihandisi (VITEKI) vya Maswa na Karatu, ambapo hadi kufikia Aprili, 2026 vijana 78 wamepata elimu ya kutumia mashine za kupura mazao (mtama, mahindi, mbaazi na alizeti) na kukamua mafuta ya alizeti. Pia, kupitia Kiwanda Darasa cha Kubangua Korosho Manyoni, vijana 16 hususan wanawake wamefundishwa kubangua na kufungasha korosho kwa ajili ya soko la ndani na nje. Vilevile, mafunzo ya kuchakata siagi ya karanga yametolewa kwa wajasiriamali wanne (4) katika Kiwanda Darasa cha Nzega.

iv. Uhamasishaji Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala

188. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia WRRB imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Hadi kufikia Aprili, 2026 Bodi imefanikiwa kutoa elimu kwa wadau wa mfumo 1,488,584 kupitia mikutano ya wadau, ushiriki wa maonesho na makongamano ya kitaifa na kimataifa, kurasa za mitandao ya kijamii na vyombo vya Habari. Kati ya wadau hao, wadau 1,487,608 walipata elimu kupitia mitandao ya kijamii, wadau 289 kupitia maonesho ya Sabasaba, wadau 200 kupitia maonesho ya Nane Nane, na wadau 487 kupitia mikutano ya wadau mbalimbali.

i. Elimu kuhusu Haki katika Ushindani wa Soko

189. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara kupitia FCT imefanya semina katika mikoa 10 ya Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Shinyanga, Kigoma, Mtwara, Lindi, Dodoma na Dar es Salaam na kuwajengea uwezo wadau 3,000 kutoka sekta ya biashara/wawekezaji, wakulima, watoa huduma, walaji na watumishi wa umma. Mafunzo hayo yalilenga kuongeza uelewa katika masuala yanayohusu ushindani wa kibiashara; udhibiti wa soko; na matumizi ya mfumo wa kusajili mashauri kwa njia ya kieletroniki.

ii. Elimu kwa Umma Kuhusu Matumizi Sahihi ya Vipimo

190. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia WMA imeendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, Umoja wa wamiliki wa Viwanda vya Alizeti Kongwa, wafanyabiashara, wasafirishaji, mafundi miundo na wauzaji wa mafuta. Elimu hiyo imetolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo programu 100 za luninga (TV), stori za Blogu 230, maonesho matano (5) ambayo ni Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Saba Saba), Nanenane, Maonesho ya Madini Geita, Maonesho ya TCIAA Mwanza, na Maonesho ya Usafirishaji Dar es Salaam. Aidha, jumla ya wadau 3,970 walitembelea mitandao ya kijamii na kupata mafunzo hayo.

iii. Elimu Kuhusu Usindikaji wa Nafaka, Vipodozi na Uzalishaji wa Bidhaa Bora za Ngozi

191. Mheshimiwa Spika; Wizara kupitia TIRDO ilitoa mafunzo kwa wadau wa viwanda Wadau hao ni pamoja na wajasiriamali 20 wa utengenezaji wa mkaa (*briquette),* wadau 41 wa uzalishaji bora wa mkaa mbadala na uhakiki wa ubora, wadau 94 wa usindikaji wa nafaka na vipodozi kutoka katika viwanda 94 katika Manispaa za Tabora na Mpanda, Katavi na wadau 23 wa uzalishaji wa bidhaa bora za ngozi kutoka mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Kilimanjaro na Morogoro. Aidha, huduma za kitaalam zilitolewa kwa viwanda mbalimbali ikiwemo Tanzania Pharmaceutical Industries Limited (TPI), MSD Makambako na Kilimanjro International Leather kwa kusimamia ujenzi wa kiwanda

hicho na kuwezesha kufanya majaribio ya awali, hatua iliyochangia kuimarisha ubora wa uzalishaji, kuongeza tija na ushindani wa bidhaa za viwandani nchini.

iv. Mafunzo ya Muda Mfupi kwa Wajasiriamali

192. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Aprili,2026, Wizara kupitia CBE imetoa mafunzo ya kozi 20 za muda mfupi kwa wajasiriamali 1,240 katika mikoa ya Mwanza (440) na Mbeya (800). Mafunzo hayo yalihusu Utunzaji wa Taarifa za Kifedha (Financial Records Keeping) na Elimu ya Mlipa kodi (Tax payment edeucation). Lengo la mafunzo ni kuwajengea uwezo wajasiriamali ili waweze kusimamia na kukuza shughuli zao kwa ufanisi zaidi, ikiwemo usimamizi wa biashara na ukuzaji wa mitaji.

4. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027

193. Mheshimiwa Spika; Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2026/2027 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: Dira 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 - 2030/2031); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025; Sera na Sheria mbalimbali; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2026/2027 - 2030/2031; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge na maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

4.1 Vipaumbele

194. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2026/2027, Wizara itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

a. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ya Viwanda;

b. Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kongani (Industrial Clusters) na mitaa ya viwanda (Industrial Estates) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati;

c. Kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara kupitia ubunifu na matumizi ya teknolojia za kisasa, elimu na mafunzo ya ujuzi.

d. Kuimarisha upatikanaji wa fedha na mitaji kwa wajasiriamali na wazalishaji viwandani;

e. Kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa Sekta binafsi;

f. Kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; na

g. Kuanzisha na kuendeleza mawazo ya biashara na bunifu (Innovation and Business Hubs) kwa vijana kwa lengo la kuchochea uchumi.

195. Mheshimiwa Spika; naomba nikazie na kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu Mpango wa Wizara ninayoisimamia wa kuanzisha Vituo vya Ubunifu na Ukuzaji wa Biashara kwa Vijana (Innovation and Business Hubs) kama nyenzo muhimu ya kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa. Vituo hivyo ni muhimu vitakavyowawezesha vijana wenye mawazo bunifu ya biashara kupata mazingira rafiki ya kubuni, kukuza na kuendesha biashara zenye ushindani katika soko la ndani na la kimataifa.

196. Mheshimiwa Spika; katika kipindi hiki ambacho dunia inabadilika kwa kasi kupitia maendeleo ya teknolojia, uchumi wa kidijitali na matumizi ya maarifa, ni muhimu kwa nchi yetu kuwekeza katika ubunifu na ujasiriamali wa vijana. Aidha, kwasasa, mfumo wa biashara duniani umejikita katika huduma zinazotolewa kidijitali ambapo inategemewa mauzo ya biashara ya kidijitali yatakuwa mara mbili zaidi ya biashara ya bidhaa. Hivyo, kuna kila sababu ya kuhakikisha tunawawezesha vijana ambao wanaingia kwa wingi katika soko la ajira kunufaika na fursa hii inayoendelea kwa kasi duniani.

4.2 Kazi Zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi

197. Mheshimiwa Spika; vipaumbele vilivyoainishwa vitatekelezwa na Wizara na Taasisi zake kama ifuatavyo:

4.2.1 Sekta ya Maendeleo ya Viwanda

A. Idara ya Mendeleo ya Viwanda

198. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo katika kuendeleza viwanda:-

a. Kuanzisha na kuendeleza miundombinu ya viwanda;

b. Kufanya tafiti katika sekta za vipaumbele za viwanda; na

c. Kuendelea kukamilisha kanzidata ya viwanda.

B. Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC)

199. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Shirika limepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

a. Kuendelea na utekelezaji wa miradi kielelezo (flagship projects) ya Makaa ya mawe ya Mchuchuma, Chuma cha Liganga na mradi wa Magadi Soda Engaruka;

b. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya Kimkakati ikiwemo mradi wa chuma Maganga Matitu, na Makaa ya mawe Katewaka na kulipia leseni za uchimbaji;

c. Kuendelea na uboreshaji wa Kiwanda Mashine na Vipuri cha KMTC;

d. Kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za kibaiolojia katika kiwanda cha TBPL;

e. Kuendelea na ufufuaji wa kiwanda cha Mang'ula kwa kushirikiana na wawekezaji mahiri;

f. Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu kwenye kongani za viwanda na kuanzisha kongani kubwa na ya kisasa ili kuvutia wawekezaji zaidi;

g. Kuendeleza mashamba ya miti ya mpira kwa ajili ya kuzalisha malighafi za viwanda na kutunza mazingira; na

h. Kujenga jengo la Ofisi Dodoma.

C. Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)

200. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Shirika limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a. Kuanzisha Kituo cha Taarifa za Viwanda (NIIMS), ubashiri wa teknolojia na viatamizi kwa wabunifu wa teknolojia;

b. Kufanya tafiti za mnyororo wa thamani wa madini adimu kwa maendeleo ya viwanda katika mikoa ya Kagera (Kyerwa), Singida (Iramba) na Dodoma (Mpwapwa);

c. Kuendelea na ukamilishaji wa ithibati za maabara na kuboresha maabara za kemia, makaa ya mawe, nguo na ngozi, nishati pamoja na mafuta na gesi;

d. Kuanzisha maabara ya nishati na madini katika Mkoa wa Njombe pamoja na maabara ya upimaji wa majiko ya kupikia;

e. Kujenga kiwanda darasa cha vifaa vya kielektroniki kinachotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini; na

f. Kujenga mtambo wa *biogas* asilia ya ubadilishaji wa taka Jijini Dar es Salaam katika masoko ya mabibo, Ilala Boma na Temeke - Sterio kuwa gesi ya petroli iliyosindikwa (LPG).

D. CAMARTEC, SIDO NA TEMDO

201. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia CAMARTEC, SIDO na TEMDO kwa pamoja imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

a. Kuanzisha kiwanda darasa cha kuchakata chikichi Kigoma;

b. Kuwezesha upatikanaji wa masoko na fedha/mikopo 3,000 kwa wajasiriamali;

c. Kutoa mafunzo na uendelezaji ujuzi kwa wajasiriamali 21,200;

d. Kuanzisha kongani za viwanda katika wilaya moja kwa kila mkoa Tanzania Bara;

e. Kutoa huduma za kihandisi kwenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kwa lengo la kuongeza ufanisi, matumizi bora ya rasilimali, ubora wa bidhaa na uwezo wa ushindani; na

f. Kutafiti, kubuni, kuendeleza na kuunda mitambo, mashine na vifaa pamoja na teknolojia mbalimbali na kuhamasisha utengenezaji wake kibiashara na matumizi yake katika shughuli za uzalishaji mali ili kukuza uchumi.

4.2.2 Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

202. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo: -

i. Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa kongani za wajasiriamali wadogo na kati nchini;

ii. Kuhamasisha uendelezaji wa miundombinu katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wadogo na kati;

iii. Kuhamasisha urasimishaji wa shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati; na

iv. Kuhamasisha wajasiriamali wadogo na wa kati kuchangamkia masoko ya ndani na nje ya Nchi.

4.2.3 Sekta ya Biashara

A. Idara ya Mtangamano wa Biashara

203. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027 Wizara imepanga kuimarisha ushirikiano wa biashara baina ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa kwa ajili ya kuongeza ushindani wa sekta ya biashara kwa kufuata kanuni na miongozo ya mtangamano wa biashara kwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

a. Kusimamia na kuratibu majadiliano ya ushirikiano wa biashara kati ya Nchi na Nchi;

b. Kusimamia na kuratibu majadiliano ya biashara na utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda ya Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Eneo Huru la Biashara la Utatu (EAC-SADC-COMESA -TRIPARTITE);

c. Kusimamia na kuratibu majadiliano ya biashara na utekelezaji wa Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO);

d. Kuimarisha utendaji wa kamati za uwezeshaji biashara na kutatua changamoto za biashara; na

e. Kubaini fursa za biashara na masoko kwa bidhaa na huduma nje ya nchi kupitia majukwaa na jumbe za biashara.

B. Idara ya Maendeleo ya Biashara

204. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuendeleza Biashara:-

a. Kuboresha mazingira ya biashara nchini;

b. Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na mazao ndani na nje ya nchi kwa kuratibu matukio ya ukuzaji biashara ikiwemo maonesho na misafara ya kibiashara;

c. Kufanya intelijensia ya masoko (market inteligence) kuhusu upatikanaji wa fursa za masoko ya mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini;

d. Kuimarisha na kuboresha huduma na mifumo ya upatikanaji wa taarifa za mazao, biashara na masoko;

e. Kuratibu mwenendo wa ufanyaji biashara za mipakani ikiwa ni pamoja na urasimishaji wa biashara hizo; na

f. Kuratibu uanzishwaji wa vituo vya kuendeleza mawazo ya biashara na bunifu (Innovation and Business Hubs) kwa vijana.

C. Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

205. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2026/2027, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limepanga kutekeleza yafuatayo:-

a. Kutayarisha viwango 520 vya Kitaifa Katika Sekta/Nyanja Mbalimbali;

b. Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 1,200 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo;

c. Kusajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 50,000;

d. Kusajili bidhaa 2,600 za chakula na vipodozi;

e. Kukagua na kutoa vibali 142,000 kwa bidhaa zitokazo nje ya nchi ambapo kati ya hizo, vibali 42,000 ni kwa bidhaa zitakazokaguliwa nje ya nchi na vibali 100,000 ni kwa bidhaa zitakazokaguliwa nchini;

f. Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 54,000 za magari yaliyotumika yanayoingizwa nchini;

g. Kupima sampuli 46,000 za bidhaa mbalimbali;

h. Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 15,000;

i. Kuweka kinasaba katika lita 5,200,000,000 za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa;

j. Ujenzi wa maabara na ofisi katika kanda ya kaskazini (Arusha); na

k. Kuendelea na udhibiti wa bidhaa zisizo na viwango.

D. Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)

206. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

a. Kusajili kampuni 22,586, majina ya biashara 38,870 alama za biashara na huduma 4,186, maombi ya hataza 98 na kutoa hataza 46;

b. Kutoa Leseni za Biashara kundi 'A' 25,875 na za Viwanda 564 pamoja na vyeti vya usajili wa Viwanda 75;

c. Kufanya kaguzi elimishi 8 za Leseni za Biashara kundi 'A' na Viwanda;

d. Kuendelea kuboresha na kuimarisha mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma; na

e. Kujenga jengo la Ofisi Dodoma.

E. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)

207. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Bodi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimalisha utendaji wa Mfumo wa Stakabadhi za ghala kwa kusimamia Ubora wa bidhaa zinazoingia na kutoka ghalani pamoja na utendaji wa waendesha ghala, wakaguzi wa ghala na meneja dhamana;

ii. Kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala; na

iii. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa cheti cha ithibati ya ubora wa kimataifa (ISO).

F. Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade)

208. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

a. Kuimarisha na kuunganisha masoko ya ndani, kikanda na kimataifa;

b. Kuongeza ushindani wa kampuni za Tanzania (MSMEs/viwanda);

c. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za biashara na intelijensia ya masoko; na

d. Kuimarisha uwezeshaji wa biashara (trade facilitation)

G. Wakala wa Vipimo (WMA)

209. Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wakala wa Vipimo inatarajia kutekeleza majukumu yake kupitia vipaumbele vifuatavyo:

(i) Kutoa elimu ya matumizi ya vipimo sahihi kwa wananchi;
(ii) Kufanya kaguzi na uhakiki wa vipimo; na
(iii) Kuboresha utoaji wa huduma kupitia mageuzi ya kidijitali.

H. Tume ya Ushindani (FCC)

210. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza malengo yafuatayo:

a. Kuboresha hali ya ushindani sokoni;
b. Kuimarisha ulinzi wa mlaji;
c. Kuimarisha ulinzi wa Alama za Bidhaa nchini; na
d. Kuendelea na udhibiti wa bidhaa bandia sokoni.

I. Baraza la Ushindani (FCT)

211. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2026/2027, Baraza la Ushindani (FCT) litatekeleza malengo yafuatayo:-

a. Kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri ya rufaa 50 yanayowasilishwa katika Baraza;
b. Kufanya utafiti wa kisheria na kiuchumi kuhusu ushindani wa kibiashara na udhibiti wa Soko; na
c. Kuwajengea uwezo Wadau na jamii kwa kuwaongezea uelewa kuhusu shughuli za Baraza, haki na Wajibu katika ushindani wa Soko.

J. Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE)

212. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka 2026/2027, Chuo cha Elimu ya Biashara kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a. Kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 10 la Vipimo na Viwango kwa awamu ya pili katika Kampasi ya Dar es Salaam;

b. kujenga madarasa katika eneo la Nzuguni - Kampasi ya Dodoma;

c. kujenga ukumbi wa mihadhara katika Kampasi ya Mwanza, kujenga vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Kampasi ya Mbeya; na

d. Kufanya mapitio ya mitaala iliyopo na kuandaa mipya.

5. SHUKRANI

213. Mheshimiwa Spika; ninapohitimisha, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa mara nyingine tena kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano waTanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupatia rasilimali fedha zinazoendelea kuimarisha sekta yetu. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb,) kiongozi wa shughuli za serikali bungeni kwa miongozo anayonipatia katika nyakati zote. Vilevile, nawashukuru sana viongozi wenzangu wa Wizara ambao ni Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri na Mbunge wa Mikumi, Balozi Waziri Rajab Salum, Katibu Mkuu pamoja na Aristides Robert Mbwasi, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wa kutosha ninaoupata kutoka kwao katika usimamizi wa Wizara hii. Aidha, sitakuwa muungwana nisipoishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa moyo wa uzalendo na kujitolea wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu.

214. Mheshimiwa Spika; naomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi; hususan Baraza la Taifa la Biashara – TNBC; Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania – TPSF; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania - CTI; Chemba ya Taifa ya Biashara – TNCC; Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania - TWCC; Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania-JWT; Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo - JWK; Wamiliki wa Viwanda na Wajasiriamali wote Nchini. Aidha, nazishukuru Benki mbalimbali kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Vilevile, nawashukuru wadau mbalimbali tunaoshirikiana nao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara wakiwemo Washirika wetu wa Maendeleo na wadau wa

ndani na nje ya Taifa letu ambao ni Trade Mark Africa, KOICA, UNIDO, JICA na wengineo.

215. Mheshimiwa Spika; kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

6. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027

216. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2026/2027, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 137,812,633,000 kwa Fungu 44. Kati ya fedha hizo, shilingi 104,122,530,000 ni matumizi ya kawaida, na shilingi 33,690,103,000 ni matumizi ya maendeleo. Katika shilingi 104,122,530,000 za matumizi ya kawaida, shilingi 78,049,345,000 ni mishahara na shilingi 26,073,185,000 ni matumizi mengineyo. Aidha, fedha zote za maendeleo ni za ndani.

217. Mheshimiwa Spika; hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara www.mit.go.tz.

218. Mheshimiwa Spika; naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Judith Kapinga. Hoja yako imeungwa mkono. Ninashukuru sana kwa taarifa hiyo kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea tuna mgeni mmoja kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, Ndugu Sabri Mubarak Salum, Mkurugenzi wa *United Traders,* karibu sana ndugu yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Waziri kuwasilisha taarifa hiyo ya Wizara ya Viwanda na Biashara sasa ninamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo aweze kuwasilisha taarifa yake. Mheshimiwa Mariam Ditopile kwa niaba ya Mwenyekiti.

MHE. MARIAM D. MZUZURI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo (Fungu 44) kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba taarifa yote ya Kamati iwekwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ili kuonyesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
(b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026;
(c) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
(d) Sehemu ya nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na
(e) Sehemu ya tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawanda ya uchambuzi. Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara inagusa Fungu 44 ambayo ni Wizara yenyewe ikiambatana na baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, ninaomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Fungu hilo tarehe 24 na 26 ya mwezi Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ufafanuzi wa jumla. Katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 24 na 26 ya Mwezi Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) zilizohusu pamoja na mambo mengine, Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hiyo umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni:-

(a) Taarifa ya fedha zilizovuka mwaka wa fedha 2024/2025;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025, hadi Februari, 2026;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa za Fedha zilizovuka mwaka 2024/2025. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) iliomba kibali cha kuvuka na jumla ya shilingi bilioni 2.32 ili kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo katika miradi yake miwili inayosimamiwa na *SIDO*

na *CAMARTEC*. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.752 ni kwa ajili ya *SIDO* na shilingi milioni 570.57 ni kwa ajili *CAMARTEC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2026, shilingi milioni 885.17 zilitumika na shilingi bilioni 1.43 zilikuwa bado hazijatumika kutokana na taratibu mbalimbali za manunuzi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Viwanda na Biashara fungu 44 liliidhinishiwa shilingi bilioni 93.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 18 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 75.81 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2026, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 58.7 sawa na 62.5% ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jedwali namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kwamba hadi kufikia Februari, 2026, fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni 62.5% ya jumla ya fedha iliyotengwa, ilhali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafike 66.6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa zimefika kiwango cha 61% ya jumla ya fedha zilizotengwa, ilhali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafikie 66.6%. Fedha za mishahara zilizopokelewa zimefikia kiwango cha 62.9% ya jumla ya fedha iliyotengwa, ilhali kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafike 66.6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ulikuwa pungufu kwa 4.1% ya lengo, ambapo Wizara ilipokea 62.5% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inaashiria hatari ya kutokamilika kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2026, jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara endapo hatua hazitachukuliwa kabla ya kufikia mwisho wa mwaka wa fedha unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa shilingi bilioni 41.88 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 27.87 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 14 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Wizara ilipokea shilingi bilioni 20 sawa na 48.6% ya fedha zilizotengwa, ambapo kiasi hicho ni fedha za ndani na hakukuwa na fedha za nje zilizopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa kiasi hicho cha fedha za maendeleo kilichopokelewa kinajumuisha shilingi bilioni nne kilichotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni sehemu ya fedha alizotoa kwa ajili ya vijana kupitia Wizara mbalimbali kiasi cha shilingi bilioni 200. Mchanganuo wa fedha hizo za maendeleo ni kama inavyoonekana katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi kufikia Februari, 2026, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo imepatikana kwa 48.6%. tu, ingawa katika kipindi hicho upatikanaji wake ulitakiwa kufikia 66.6%. Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa 73.1% na kuvuka lengo sawa na ongezeko la 6.5%. Hakuna fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwezesha vijana nchini. Ninaomba kurudia, Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwezesha vijana nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya fedha hizo, shilingi bilioni nne zilipelekwa Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuwezesha vijana katika sekta ya viwanda kupitia *SIDO*. Hatua hii inaonesha dhamira ya kweli ya Serikali katika kukuza uchumi wa vijana, kuhamasisha ubunifu, kujenga uwezo wa kujiajiri na kuanzisha biashara endelevu. Uamuzi huu ni chachu muhimu ya maendeleo ya vijana na unaendelea kuimarisha dira ya Tanzania ya kujenga uchumi shindani unaojumuisha wananchi wote, hasa vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa inayotegemewa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo hufanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea miradi miwili inayotekelezwa chini ya Wizara hii. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo: mradi wa kwanza, ni mradi wa ujenzi wa jengo la vipimo na viwango, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa jengo la vipimo na viwango lenye ghorofa kumi ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuboresha na kupanua miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na kuimarisha mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu una thamani ya shilingi bilioni 26.39 ambapo unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza inagharimu shilingi bilioni 10.39 na awamu ya pili inagharimu shilingi bilioni 16 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya NMB. Ujenzi huu umefikia 93% na ulitakiwa kukamilika tarehe 23 Mei, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utakapokamilika unatarajia kuleta manufaa mengi ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 5,594 kwa wakati mmoja, kuimarisha mafunzo kwa vitendo na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilibaini kuwa zipo changamoto nyingine zinazokabili chuo hicho ikiwemo uhaba wa miundombinu mingine kama vile hosteli ambapo Kamati ilielezwa kuwa ni 3.57% tu ya wanafunzi hukaa hosteli. Changamoto hii ya makazi inaleta kadhia ya makazi kwa wanafunzi, hususan wa kike ambao kwa kiasi kikubwa huathiriwa na mwingiliano na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili ni utekelezaji wa mradi wa kituo cha uhakiki Misugusugu - Kibaha kwa taasisi ya Wakala wa Vipimo kwa kifupi *WMA*. Wakala wa vipimo *(WMA)* ilianzisha mradi wa ujenzi wa kituo cha kisasa cha uhakiki katika eneo la Misugusugu. Eneo hili lina ukubwa wa hekta 2.4 na ujenzi wa kituo hiki umekamilika na umegharimu shilingi bilioni 7.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa kituo hiki ni utekelezaji wa azma ya Serikali kusogeza huduma za vipimo karibu na wananchi, wadau wa kibiashara pamoja na kuimarisha miundombinu ya uhakiki nchini. Aidha, kituo kinalenga kufanya uhakiki wa matanki ya magari yanayosafirisha vimiminika, mita mpya za umeme na dira za maji kabla ya kufungwa kwa wateja. Lengo la uhakiki huo ni kuhakikisha vifaa hivyo vinakidhi viwango vilivyowekwa na vinatoa matokeo sahihi ya matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vipimo inakabiliwa na changamoto mbili ikiwemo mwitikio hafifu kutoka kwa baadhi ya wazabuni wanaouza mita za nishati ya umeme katika kutekeleza takwa la kisheria la kuhakikisha mita hizo zinahakikiwa na wakala kabla ya kuwasilishwa kwa taasisi nunuzi, na madai ya muda mrefu ya malipo ya huduma za uhakiki wa dira za maji kutoka kwa baadhi ya kampuni zilizopewa zabuni ya dira za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati. Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya Wizara hiyo. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa, Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri wa Kamati kuzingatiwa kwa sehemu kubwa, ipo sehemu ya ushauri ambayo utekelezaji wake haujakamilika. Mfano wa ushauri huo ni kuhusu ukamilishaji wa Mradi wa Magadi Soda Engaruka na mradi wa Liganga na Mchuchuma. Maelezo ya Mtoa Hoja yanaonyesha kuwa bado timu za majadiliano ya mikataba ya ubia na kampuni zilizoshinda zabuni yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni kuhusu upatikanaji wa umeme wa uhakika viwandani ambapo Mtoa Hoja alieleza kuwa Serikali inaendelea kupeleka njia maalumu za umeme *(dedicated lines)* katika maeneo ya viwanda. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa maagizo yenye mwendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Machi, 2026 Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Mapato na matumizi ya Viwanda na Biashara yaani Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi huo ulilenga kujihakikishia iwapo mpango na makadirio hayo pamoja na mambo mengine umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 pamoja na Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025/2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu 44, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya shilingi bilioni 104.12 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 78 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 26 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi hicho ni ongezeko la 10.88% ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: makadirio ya fedha za matumizi ya kawaida kwa ujumla yameongezeka kwa 10.88% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha ulioisha. Makadirio ya fedha za matumizi mengineyo *(OC)* yameongezeka kwa 44.19% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Makadirio ya fedha za mishahara yameongezeka kwa 2.94% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza bajeti ya Wizara hii kwani kwa kufanya hivyo kutawezesha kukuza uchumi wa viwanda wenye ushindani unaotegemea matumizi ya rasilimali za ndani, teknolojia, ubunifu na nguvu kazi yenye ujuzi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba sekta ya viwanda imepewa nafasi ya kimkakati katika Dira 2050 ya Taifa kama moja ya sekta za kipaumbele zinazochochea mageuzi makubwa ya uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi ya miradi ya maendeleo; katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Viwanda na Biashara yaani Fungu 44 inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya shilingi bilioni 33.69 sawa na punguzo la 19.57% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambazo ni fedha za ndani. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika jedwali namba nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zimepungua kwa 19.57% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha, lakini hakuna fedha za nje za miradi ya maendeleo zilizopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yamepungua ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Hali hii inakwamisha mkakati wa Wizara unaolenga kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya viwanda. Licha ya Wizara kutotenga fedha za nje, Kamati inaona ipo haja ya Wizara kuendelea kuandaa na kuwasilisha maandiko mbalimbali kwa washirika wa maendeleo ili kuhakikisha inapata fedha za nje zitakazosaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaona kuwa kutokana na upatikanaji wa fedha za nje za maendeleo kuwa wa kusuasua, ipo haja ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya viwanda ili kufikia azma ya Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Kufuatia majadiliano ya kina baina ya Kamati na Wizara hii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ili kusaidia utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kuwa sekta ya viwanda imepewa nafasi kubwa ya kimkakati katika Dira ya Taifa 2050 kama moja ya sekta za kipaumbele zitakazochochea mageuzi makubwa ya uchumi wa Taifa, jambo linalopelekea kuwa na uhitaji mkubwa wa fedha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuona umuhimu wa kuiongezea bajeti Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kutekeleza azma yake ya kuleta mageuzi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa fedha za maendeleo siyo ya kuridhisha. Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kunasababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua na mingine kutotekelezwa kabisa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokukamilika kwa muda mrefu kwa miradi ya Liganga na Mchuchuma pamoja na mradi wa Magadi Soda Engaruka kumepelekea kuchelewa kwa maendeleo ya viwanda. Kuendelea kutegemea bidhaa kama vile chuma, kemikali na mali ghafi nyingine kutoka nje ya nchi, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi na za haraka kuhakikisha miradi hii inaanza kutekelezwa mapema iwezekanavyo. Kukamilika kwa miradi hii kutakuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha uchumi wa viwanda, kuongeza ajira na kutumia rasilimali za nchi kwa maendeleo ya Taifa;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya viwanda nchini kunaathiri kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya viwanda. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha Mfuko huu. Aidha, Kamati inashauri, taasisi zilizopo chini ya Wizara hii kuchangia

fedha kwenye Mfuko huu ili kuongeza mtaji ikizingatiwa kwamba Mfuko huu unaweza kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha uzalishaji, kuongeza ajira na kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya tozo katika biashara zinaathiri ushindani wa bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, jambo linalopelekea kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na kudhoofisha ukuaji wa viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo Wizara ya Fedha, kufanya tathmini ya kina kuhusu tozo mbalimbali na athari zake katika biashara ili kubaini namna zinavyoathiri ushindani wa bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo itasaidia kuboresha mazingira ya biashara, kuongeza ushindani wa viwanda vya ndani na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa huku tukiheshimu *regional commitments* na *bilateral agreement* mfano Tanzania na nchi ya Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko ya wananchi juu ya thamani halisi za matumizi ya huduma za muda wa maongezi na bando za *internet*. Kwa msisitizo, ninaomba nirudie hapa, kumekuwepo na malalamiko ya wananchi juu ya thamani halisi za matumizi ya huduma za muda wa maongezi na bando za *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara kupitia Wakala ya Vipimo (*WMA)* kuanza jukumu la kuhakiki vipimo vinavyotumika kwenye muda wa maongezi na bando za *internet* ili wananchi waweze kupata thamani halisi ya huduma wanazolipia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mwitikio hafifu kutoka kwa baadhi ya wazabuni wanaouza mita za nishati ya umeme katika kutekeleza takwa la kisheria la kuhakiki mita hizo kwa Wakala wa Vipimo (*WMA)* kabla ya kuwasilishwa kwa taasisi

nunuzi, jambo linaloathiri usahihi wa Ankara, yaani bili na kuibua malalamiko ya walaji na kudhoofisha uadilifu wa mifumo ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kushirikiana na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha mita zote mpya za umeme zinawasilishwa kwa ajili ya kuhakikiwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo kabla ya kusimikwa kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya lumbesa bado haijapata suluhu ya kudumu, jambo linalopelekea baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kuendelea kutumia mfumo huu na kupelekea kuwanyonya wakulima na kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kushirikisha mamlaka zote zinazohusika na vipimo ili kupata suluhu ya kudumu. Usimamizi wa pamoja utasaidia kubaini chanzo cha tatizo na kuweka mkakati madhubuti ya kulidhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa bidhaa feki sokoni unasababishwa na ukosefu wa udhibiti wa kutosha wa mamlaka husika, jambo linalopelekea Serikali kukosa mapato, kuathiri uwekezaji na kuleta athari kwa watumiaji. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha ukaguzi wa bidhaa mipakani na sokoni sambamba na kuziongezea nguvu mamlaka husika kwa kuziongezea rasilimali watu na fedha ili kuimarisha ukaguzi nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe kuwa mifumo ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo inasomana ili kuwezesha mnyororo mzima wa uzalishaji na biashara unafuatiliwa kwa ufanisi. Hatua hiyo itasaidia Serikali kupata taarifa sahihi kuhusu uzalishaji wa mazao, usindikaji wa viwandani, usafirishaji na mauzo ndani na nje ya nchi. Vilevile, itasaidia kuongeza ufanisi wa usimamizi wa uchumi na kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la biashara ndogondogo za wazawa kufanywa na raia wa kigeni nchini kumeathiri kwa kiasi

kikubwa ushindani kwa wafanyabiashara wazawa, kupungua kwa nafasi za ajira na kujiajiri na kushuka kwa ukuaji wa bidhaa za ndani. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha utekelezaji wa Sheria za Bidhaa na Uwezeshaji kwa kudhibiti vibali vya biashara kwa wageni katika sekta ndogondogo za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa *hostel* katika Vyuo vya Elimu ya Biashara, kwa kifupi *CBE,* umesababisha 3.57% tu ya wanafunzi katika vyuo hivi ndio hukaa *hostel,* jambo linalofanya wanafunzi wengi kuishi nje ya vyuo na kusababisha wengi wao ambao wana umri wa chini ya miaka 18, hususan wanafunzi wa kike, kupata changamoto mbalimbali ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa *hostel* ili kupunguza changamoto zinazowakabili wanafunzi hao katika vyuo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Ninapenda kukushukuru wewe binafsi, lakini ninachukua fursa hii pia, kumshukuru sana Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa dhati kabisa ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, tukiongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Deo Mwanyika, ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninapenda kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, na Waziri wa Viwanda na Biashara, akisaidiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo. Kwa kweli tunawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa wanaoupatia Kamati ambayo kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, mtu mahiri, Balozi Waziri Rajab Salum, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu, Bwana Aristides Robert Mbwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninamshukuru sana Katibu wetu wa Bunge, kaka yangu, Ndugu yetu Baraka Leonard kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge. Kipekee Makatibu Kamati wanaotusaidia katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, yaani Fungu 44 kwa mwaka wa fedha 2026/2027, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU – 44 KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 **MAELEZO YA JUMLA**

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha

2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla ili kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;
(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na
(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

1.2 Msingi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Msingi wa taarifa hii unatokana na majukumu ya Kamati ambayo yapo kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(a) na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekekezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilifanya uchambuzi na kupata maudhui ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge yanayohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kazi hiyo ilifanyika kuanzia ya tarehe 12 hadi 14 Machi 2026 katika Mikoa ya Dar Es Salaam na Pwani. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara inagusa **Fungu 44** ambayo ni Wizara yenyewe ikiambatana na baadhi ya taasisi zilizo chini ya wizara hiyo. Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa fungu hilo tarehe 24 na 26 ya Mwezi Machi 2026.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/ 2026

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 24 na 26 ya Mwezi Machi, 2026. Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara **(Fungu 44)** zilizohusu pamoja na mambo mengine Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hiyo umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni;

(a) Taarifa ya fedha zilizovuka Mwaka wa Fedha 2024/2025
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya kawaida na Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari 2026;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2.2 Uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara inajumuisha fungu moja – **Fungu 44.**

2.2.1 Taarifa ya Fedha zilizovuka Mwaka 2024/2025

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Viwanda na Biashara (**Fungu 44**) iliomba kibali cha kuvuka na jumla ya **Shilingi 2,323,391,970** ili kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo katika miradi yake miwili inayosimamiwa na SIDO na CAMARTEC,kati ya fedha hizo **Shilingi 1,752,821,741** ni kwa ajili ya SIDO na **Shilingi 570,570,229** ni kwa ajili CAMARTEC**.** Hadi kufikia Februari 2026, **Shilingi 885,173,570** zilitumika na **Shilingi 1,438,214,400** zilikuwa bado hazijatumika kutokana na taratibu mbalimbali za manunuzi kuendelea.

2.2.2 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida


Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Viwanda na Biashara - **Fungu 44** iliidhinishiwa **Shilingi 93,900,697,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,081,317,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 75,819,380,000.00** ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 58,704,127,320.73** sawa na asilimia **62.5** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 47,672,881,443.79** sawa na asilimia **62.9** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 11,031,245,876.94** sawa na asilimia **61.0** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 1**

Jedwali Na. 1: Fungu 44 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2025/2026

Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya kawaida kwa Mwaka 2025/2026 - Fungu 44			
Matumizi	**Kilichoidhinishwa**	**Kilichopokelewa**	**Asilimia**
Mishahara	75,819,380.000	47,672,881,443.79	62.9
Matumizi Mengineyo (OC)	18,081,317,000	11,031,245,876.94	61.00
Jumla Kuu	**93,900,697,000**	**58,704,127,320.73**	**62.5**

Chanzo: *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati



Chanzo: *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2026:-

(i) Fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni **asilimia 62.5** ya jumla ya fedha iliyotengwa ilihali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafikie **asilimia 66.6**

(ii) Fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa zimefika kiwango cha **asilimia 61** ya jumla ya fedha iliyotengwa ilihali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafikie **asilimia 66.6**

(iii) Fedha za mishahara zilizopokelewa zimefikia kiwango cha **asilimia 62.9** ya jumla ya fedha iliyotengwa ilihali katika kipindi hicho ilitakiwa mapokezi hayo yafikie **asilimia 66.6**

Mheshimiwa Spika uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ulikuwa pungufu kwa **asilimia 4.1** ya lengo, ambapo Wizara ilipokea **asilimia 62.5** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hali hii inaashiria hatari ya kutokamilika kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2026 jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara endapo hatua hazitachukuliwa kabla ya kufikia mwisho wa mwaka wa fedha unaondelea.

2.2.3 Upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa **Shilingi 41,887,535,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 27,870,710,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 14,016,825,000** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Wizara ilipokea **Shilingi 20,377,278,432.09**, sawa na **asilimia 48.6** ya Fedha zilizotengwa, ambapo kiasi hicho ni fedha za ndani na hakukuwa na fedha za nje zilizopokelewa.


Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa kiasi hicho cha fedha za maendeleo kilichopokelewa kinajumuisha **Shilingi 4,000,000,000** kilichotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni sehemu ya fedha alizotoa kwa ajili vijana kupitia wizara mbalimbali kiasi cha **Shilingi 200,000,000,000**. Mchanganuo wa fedha hizo za maendeleo ni kama invyoonekana katika **Jedwali Na. 2.**

Jedwali Na. 2: Fungu 44 - Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mtiririko wa fedha za Miradi ya Maendeleo hadi Februari, 2026			
MIRADI	**Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2025/2026**	**Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2026**	**Asilimia ya Fedha zilizopokelewa**
Fedha za Ndani	27,870,710,000	20,377,278,432.09,	48.6

Fedha za Nje	14,016,825,000	0	0
Jumla	**41,887,535,000**	**20,377,278,432.09,**	**48.6**

Chanzo: *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati



Chanzo: *Randama ya Wizara 2026/2027*-Fungu 44 na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba hadi kufikia Februari 2026;

(i) Fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo imepatikana kwa **asilimia 48.6** ingawa katika kipindi hicho upatikanaji wake ulitakiwa kufikia asilimia 66.6

(ii) Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa **asilimia 73.1** na kuvuka lengo sawa na ongezeko la **aslimia 6.5.**

(iii) **Hakuna fedha za nje zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa **Shilingi 200,000,000,000** kwa ajili ya kuwezesha vijana Nchini.

Sehemu ya fedha hizo **Shilingi 4,000,000,000** zilipelekwa Wizara ya Viwanda na Biashaa ili kuwezesha vijana katika Sekta ya Viwanda kupitia SIDO. Hatua hii inaonyesha dhamira ya kweli ya Serikali katika kukuza Uchumi wa vijana, kuhamasisha ubunifu, kujenga uwezo wa kujiajiri na kuanzisha biashara endelevu. Uamuzi huu ni chachu muhimu ya maendeleo ya vijana na unaendelea kuimarisha Dira ya Tanzania ya kujenga Uchumi shindani unaojumuisha wananchi wote hasa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa inayotegemewa zaidi**.**

2.2.4 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Katika ziara hiyo Kamati ilitembeleamiradi miwili inayotekelezwa chini ya Wizara hii. Miradi hiyo ni kama ifuatayo;-

(a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Vipimo na Viwango, Chuo cha Elimu ya Biashara-CBE

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa jengo la Vipimo na Viwango (Metrology Complex) lenye ghorofa 10 ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuboresha na kupanua miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na kuimarisha mafunzo kwa vitendo. Mradi huu una thamani ya **Shilingi 26,398,228,771.45** ambapo unatekelezwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza inagharimu **Shilingi 10,398,228,771.45** na awamu ya pili inagharimu **Shilingi 16,000,000,000** ambazo ni mkopo kutoka Benki ya NMB. Ujenzi huu umefikia asilimia 93 na ulitakiwa kukamilika 23, Mei 2026. Mradi huu utakapokamilika unatarajia kuleta manufaa mengi ikiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa kuhudumia jumla ya wanafunzi 5,594 kwa wakati mmoja, kuimarisha mafunzo kwa vitendo na kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa chuo. Aidha Kamati ilibaini kuwa zipo changamoto nyingine zinazokikabili chuo hicho ikiwemo uhaba wa miundombinu mingine kama vile hosteli ambapo Kamati ilielezwa kuwa ni **asilimia 3.57** tu ya Wanafunzi hukaa Hostel.

Changamoto hii ya makazi inaleta kadhia ya makazi kwa Wanafunzi hususan Wanafunzi wa kike ambao kwa kiasi kikubwa huathiriwa na mwingiliano na Jamii.

(b) Utekelezaji wa mradi wa Kituo cha Uhakiki Misugusugu-Kibaha. (Wakala wa Vipimo)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Vipimo (WMA) ilianzisha mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Uhakiki katika eneo la Misugusugu. Eneo hili lina ukubwa wa heka 2.4 na ujenzi wa Kituo hiki umekamilika na umegharimu **Shilingi 7,300,000,000.** Kuanzishwa kwa kituo hiki ni utekelezaji wa azma ya Serikali kusogeza huduma za vipimo karibu na wananchi, wadau wa kibiashara, pamoja na kuimarisha miundombinu ya uhakiki nchini. Aidha, kituo kinalenga kufanya uhakiki wa matenki ya magari yanayosafirisha vimimikia, Mita mpya za Umeme na Dira za Maji kabla ya kufungwa kwa wateja, lengo la uhakiki huo ni kuhakikisha vifaa hivyo vinakidhi viwango vilivyowekwa na vinatoa matokeo sahihi ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Vipimo inakabiliwa na changamoto mbili ikiwemo mwitikio hafifu kutoka kwa baadhi ya wazabuni wanaouza Mita za nishati ya umeme katika kutekeleza takwa la kisheria la kuhakikisha Mita hizo zinahakikiwa na Wakala kabla ya kuwasilishwa kwa taasisi nunuzi na Madai ya muda mrefu ya malipo ya huduma za uhakiki wa Dira za Maji kutoka kwa baadhi ya makampuni yaliyopewa zabuni ya Dira za Maji.

2.2.5 Hali ya Uzingatiaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati

Mheshimiwa Spika, Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na ushauri wa Kamati kuzingatiwa kwa sehemu kubwa, ipo sehemu ya ushauri ambayo utekelezaji wake haujakamilika. Mfano wa ushauri huo ni kuhusu ukamilishaji wa mradi wa Magadi Soda-Engaruka na mradi wa Liganga na

Mchuchuma. Maelezo ya mtoa hoja yanaonesha kuwa bado timu za majadiliano ya Mikataba ya Ubia na Kampuni zilizoshinda zabuni yanaendelea. Ushauri mwingine ni kuhusu upatikanaji wa umeme wa uhakika Viwandani ambapo mtoa hoja alieleza kuwa Serikali inaendelea na kupeleka njia maalumu za umeme (dedicated lines) katika maeneo ya viwanda. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa maagizo yenye muendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Machi, 2026 Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara – **Fungu 44** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi huo ulilenga kujihakikishia iwapo Mpango na Makadirio haya Pamoja na mambo mengine umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025- 2030.


3.1 Makadiriro ya Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, **Fungu 44 -** Wizara ya Viwanda na Biashara, inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya **Shilingi 104,122,530,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 78,049,345,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 26,073,185,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 10.88** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo ilikuwa ni **Shilingi 93,900,697,000**

Jedwali Na. 3: Ulinganisho wa Fedha za Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027

Ulinganisho wa Bajeti Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027				
Matumizi	**2025/2026**	**2026/2027**	**Ongezeko/ Pungufu**	**Asilimia**
Mishahara	75,819,380,000	78,049,345,000	2,229,965,000	2.94
Matumizi Mengineyo (OC)	18,081,317,000	26,073,185,000	7,991,868,000	44.19
Jumla	**93,900,697,000**	**104,122,530,000**	**10,221,833,000**	**10.88**

Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati



Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo;-

(i) Makadirio ya fedha za matumizi ya kawaida kwa ujumla yameongezeka kwa **asilimia 10.88** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa fedha ulioisha.

(ii) Makadirio ya Fedha za Matumizi mengineyo (OC) yameongezeka kwa **asilimia 44.19** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa fedha ulioisha.
(iii) Makadirio ya fedha za Mishahara yameongezeka kwa **aslimia 2.94** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

Mhesimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii kwani kwa kufanya hivyo kutawezesha kukuza uchumi wa viwanda wenye ushindani, unaotegemea matumizi ya rasilimali za ndani, teknolojia, ubunifu na nguvu kazi yenye ujuzi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba sekta ya viwanda imepewa nafasi ya kimkakati katika Dira 2050 ya Taifa kama moja ya sekta za kipaumbele zinazochochea mageuzi makubwa ya Uchumi wa Taifa.


3.2 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Viwanda na Biashara **(Fungu 44)** inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya **Shilingi 33,690,103,000** sawa na punguzo la **asilimia 19.57** Ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka unaoisha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambazo ni fedha za ndani na hakuna fedha za nje zilizotengwa. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.**

Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027

Ulinganisho wa bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026/2027			
MIRADI	**Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2025/2026**	**Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2026/2027**	**Ongezeko / Punguzo %**
Fedha za Ndani	27,870,710,000	33,690,103,000	20.87
Fedha za Nje	14,016,825,000	0	100
Jumla	**41,887,535,000**	**33,690,103,000**	**-19.57**

Chanzo: *Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati*



Chanzo: *Randama ya Wizara 2026/2027-Fungu 44 na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

(i) Fedha za ndani kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maeondeleo zimepungua kwa **asilimia 19.57** ilkilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha.
(ii) Hakuna fedha za nje za miradi ya maendeleo zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yamepungua ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2025/2026. Hali hii inakwamisha mkakati wa Wizara unaolenga kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya Viwanda. Licha ya Wizara kutotenga fedha za nje. Kamati inaona ipo haja ya Wizara kuendelea kuandaa na kuwasilisha maandiko mbalimbali kwa washirika wa maendeleo ili kuhakikisha inapata fedha za nje zitakazosaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha Kamati inaona kuwa kutokana na upatikanaji wa fedha za nje za maendeleo umekuwa wa kusuasua ipo haja ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda ili kufikia adhma ya Tanzania ya Viwanda.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kufuatia majadiliano ya kina baina ya Kamati na Wizara hii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Kutokana na ukweli kuwa Sekta ya Viwanda imepewa nafasi kubwa ya kimkakati katika Dira ya Taifa 2050 kama moja ya sekta za kipaumbele zitakazochochea mageuzi makubwa ya Uchumi wa Taifa jambo linalopelekea kuwa na uhitaji mkubwa wa fedha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuona umuhimu wa kuiongezea Bajeti Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutekeleza azma yake ya kuleta mageuzi ya kiuchumi.

(b) Hali ya upatikanaji wa fedha za maendeleo si ya kuridhisha. Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua, na mingine kutotekelezwa kabisa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio.

(c) Kutokamilika kwa muda mrefu kwa mradi ya Liganga na Mchuchuma pamoja na mradi wa Magadi Soda Engaruka kumpelekea kuchelewa kwa maendeleo ya viwanda, kuendelea kutegemea bidhaa kama vile chuma, kemikali na malighafi nyingine kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi na za haraka katika kuhakikisha miradi hii inaanza kutekelezwa mapema iwezekanavyo. Kukamilika kwa miradi hii kutakuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha Uchumi wa viwanda, kuongeza ajira na kutumia rasilimali za Nchi kwa maendeleo ya Taifa.

(d) Kutokuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Nchini kunaathiri kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya Viwanda. Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha Mfuko huu. Aidha Kamati inashauri Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii kuchangia fedha kwenye Mfuko huu ili kuongezesha mtaji ikizingatiwa kwamba Mfuko huu unaweza kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha uzalishaji, kuongeza ajira na kukuza Uchumi wa Taifa.

(e) Baadhi ya tozo katika biashara zinaathiri ushindani wa bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi jambo linalopelekea kuongeza gharama za uzalishaji na kudhoofisha ukuaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za serikali kufanya tathmini ya kina kuhusu tozo mbalimbali na athari zake katika biashara ili kubaini namna zinavyoathiri ushindani wa bidhaa za ndani dhidi ya bidhaa zinazoingizwa toka nje ya nchi. Hatua hiyo itasaidia kuboresha mazingira ya biashara, kuongeza ushindani wa viwanda vya ndani na kuchochea ukuaji wa Uchumi wa taifa.

(f) Kumekuwepo na malalamiko ya wananchi juu ya thamani halisi za matumizi ya huduma za muda wa maongezi na bando za intaneti. Kamati inasishauri Wizara kupitia Wakala wa Vipimo WMA kuanza jukumu la kuhakiki vipimo vinavyotumika kwenye muda wa maongezi na bando za intanet ili wananchi waweze kupata thamani halisi ya huduma wanazolipia.

(g) Kumekuwa na mwitikio hafifu kutoka kwa baadhi ya wazabuni wanaouza Mita za Nishati ya Umeme katika kutekeleza takwa la kisheria la kuhakiki mita hizo kwa Wakala wa Vipimo (WMA) kabla ya kuwasilishwa kwa taasisi nunuzi jambo linaloathiri usahihi wa Ankara (*Bill),* kuibua malalamiko ya walaji na kudhoofisha uadilifu wa mifumo ya mapato. Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kushirikiana na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha Mita zote mpya za umeme zinawasilishwa kwa ajili ya kuhakikiwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo kabla ya kusimikwa kwa watumiaji.

(h) Changamoto ya lumbesa bado haijapata Suluhu la kudumu jambo linalopekea baadhi ya wafanyabiashara wasio

waaminifu kuendelea kutumia mfumo huu na kupelekea kuwanyonya wakulima na kuikosesha serikali mapato. Kamati inaishauri Serikali kushirikisha mamlaka zote zinazohusika na vipimo ili kupata Suluhu ya kudumu. Usimamizi wa Pamoja utasaidia kubaini chanzo cha tatizo na kuweka mkakati Madhubuti ya kulidhibiti.

(i) Uwepo wa bidhaa feki sokoni unasababishwa na ukosefu wa udhibiti wa kutosha wa Mamlaka husika jambo linalopelekea Serikali kukosa mapato, kuathiri uwekezaji na kuleta athari kwa watumiaji. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha ukaguzi wa bidhaa mipakani na sokoni sambamba na kuziongezea nguvu mamlaka husika kwa kuwaongezea rasilimali watu na fedha ili kuimarisha ukaguzi nchi nzima.

(j) Serikali ihakikishe kuwa mifumo ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo inasomana ili kuwezesha mnyonyoro mzima wa uzalishaji na biashara unafuatiliwa kwa ufanisi. Hatua hiyo itasaidia serikali kupata taarifa sahihi kuhusu uzalishaji wa mazao, usindikaji wa viwandani, usafirishaji na mauzo ndani na nje ya nchi. Vilevile itasaidia kuongeza ufanisi wa usimamizi wa Uchumi na kuongeza mapato ya taifa.

(k) Tatizo la Biashara ndogo ndogo za Wazawa kufanywa na Raia wa Kigeni nchini kumeathiri kwa kiasi kikubwa ushindani kwa Wafanyabiashara Wazawa, kupungua kwa nafasi za ajira na kujiajiri na kushuka kwa ukuaji wa bidhaa za ndani. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha utekelezaji wa Sheria za bidhaa na uwezeshaji kwa kudhibiti vibali vya biashara kwa Wageni katika sekta ndogo ndogo za kibiashara.

(l) Uhaba wa Hosteli katika Vyuo vya Elimu ya Biashara (CBE)umesababisha asilimia 3.57 tu ya Wanafunzi katika vyuo hivi ndio hukaa hostel, jambo linalopelekea wanafunzi wengi kuishi nje ya Vyuo na kupelekea wanafunzi hususan wanafunzi wa kike ambao wengi wao wana umri chini ya miaka 18 kupata changamoto mbalimbali ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwaajili ya ujenzi wa Hosteli ili kupunguza changamoto zinazowakabili Wanafunzi hao katika vyuo husika.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

5.1 Maelezo ya Kuhitimisha

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kwa kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa:-

1. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo,Mb - Mjumbe
5. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Tauhida Galos Cassian, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Marcus Msigwa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobelo, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Dkt.Rita Enerpher Kabati, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde Mb - Mjumbe
14. Mhe. Magreth Baraka Ezekiel, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Abubakar Alli Omari, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Khalfan Issa Mohamed, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Khamis Hamad Yussuf, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amour Seif Abdalla, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khalid Mussa Nsekela, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb) - Waziri wa Viwanda na Biashara na Mhe. Dennis Lazaro Londo (Mb) – Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu. Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Mheshimiwa Balozi Waziri Rajab Salum, akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu Bwana. Aristides Robert Mbwasi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuwaongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44), kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Ufugaji kwa kuwasilisha Taarifa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa zote mbili zimeshawasilishwa na sasa ni wakati wa uchangiaji, lakini kutokana na ratiba yetu ya leo na hoja iliyopo Mezani, wachangiaji ni wengi, tutatumia dakika saba kwa kila Mbunge.

Tunaanza na Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mheshimiwa Eric James Shigongo na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby ajiandae.

MHE. KHALID M. NSEKELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuweza kuchangia Bajeti hii nzuri ya

Viwanda na Biashara. Kwanza ninatoa pongezi kubwa sana na nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake wenye maono, hasa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara hapa nchini kupitia falsafa yake ya uchumi shirikishi, uchumi jumuishi na diplomasia ya uchumi kwa sababu, chini ya uongozi wake tumeona *improvement* kubwa sana, hasa katika uwekezaji na mazingira bora kabisa ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Taifa lolote ambalo linaweza kujenga uchumi wenye nguvu na wa msingi bila kuwa na sekta madhubuti ya viwanda na biashara. Hapa tunapojadili Bajeti ya Viwanda na Biashara, tunajadili msingi mzima wa Uchumi wa Taifa letu, lakini tunatambua ndiyo msingi wa ajira, Mapato ya Serikali na kukuza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba kutoa pongezi kwa uongozi wa Wizara, Mheshimiwa Waziri, dada yangu Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote chini ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi, kama Mjumbe wa Kamati, nimeshiriki, tumezunguka, tumejionea kazi kubwa ambayo inafanywa na Wizara hii. Tumetembelea sehemu nyingi sana. Katika mustakabali mzima wa kutengeneza ushindani wa haki, ulinzi wa bidhaa, ubora wa bidhaa na kumlinda mlaji na mazingira mazima ya biashara, ni lazima sasa Serikali ione umuhimu wa kuzipa nguvu na kuziongezea uwezo taasisi hizi ambazo ziko chini ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hizi zinafanya kazi kubwa sana. Ukiangalia *TBS*, *FCC*, na Wakala wa Vipimo wanafanya kazi kubwa sana, lakini kazi zao ili ziweze kuonekana, na watu wazione, ni lazima sasa ziongezewe nguvu na zipewe mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano *TBS,* wanaangalia ubora wa bidhaa, lakini kwa mbali unaweza ukahisi labda *TBS* wanafanana na Wakala wa Vipimo ingawa ni vitu viwili tofauti. Wakala wa Vipimo anaangalia viwango vya upimaji wa bidhaa, kwa mfano

tu, suala dogo kwenye nondo. Ukiangalia, ni ngumu kujua kwamba, nondo ile kweli ni kiasi kile kile? Ni kiwango kile cha nondo kinachotakiwa? Achilia mbali ubora, lakini Wakala wa Vipimo ndiyo anaweza kujua hicho kitu. Ukiangalia simenti, ukibeba ni nzito utahisi ni kilo 50, lakini bila Wakala wa Vipimo huwezi kujua kwamba mfuko huu wa sementi ni kilo 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia Wakala wa Vipimo umeanza toka enzi za mkoloni, muda mrefu sana. Maana yake ni kulikuwepo na lengo mahsusi la kuanzisha huu Wakala wa Vipimo. Kwa hiyo, ninaomba upewe nguvu. Ninatoa rai kwa hizi taasisi, sasa ni muda muafaka zifanye kazi kwa mfumo wa *KPI,* zitembee, ziende vijijini, zimfikie mkulima, zitoe elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoongelea lumbesa, mkulima ajue lumbesa siyo kwenye viazi wala ndizi, lakini hata kwenye kahawa; kule Kyerwa kuna lumbesa. Ndoo zinakatwa katikati, zinachomwa, zinaongezwa zinakuwa zaidi ya debe, kwa hiyo, ni muda watembee, waongeze uwezo. Wakala wa Vipimo upewe nguvu, wawe na mamlaka ya kufanya maamuzi ya kumfunga mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni uzalishaji. Uchumi ulioko duniani sasa hivi, vita ya uchumi siyo tena kwenye mambo ya silaha, ni uwezo wa nchi kuzalisha. Sisi hapa tumeona mazingira mazuri yamewekwa na Mheshimiwa Rais na uongozi wake mzuri, wawekezaji wanakuja, sasa uzalishaji unafanyika, viwanda vingi vinajengwa hapa, lakini changamoto tuliyonayo ni kwenye ulinzi wa viwanda vyetu ambavyo viko hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameongea Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, dada yangu, Mheshimiwa Mariam. Tumetembelea viwanda vingi sana, wamewekeza nguvu, wameweka *machinery* zenye bei kubwa sana, lakini changamoto waliyonayo kulingana na ushindani wa watu ambao wana-*import the same* bidhaa ni kwamba wanashindwa kushindana kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kumaliza hapa, atuambie ni mkakati gani

anauleta wa kulinda biashara za ndani, hasa viwanda vinavyozalisha kwa kuweza kuweka *import duty* ya kutosha kwa watu wanao-i*mport the same product*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, mimi ni kijana, siwezi kumaliza bila kumgusia Kijana wa Tanzania. Tanzania ina vijana wengi wazuri na wana mawazo makubwa sana ya biashara. Mheshimiwa Rais ameona, amewatengea Wizara na ameona kwamba, ni muhimu sasa kuwekeza kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara akae karibu sana na Wizara ya Vijana, watengeneze mfumo wa kuzilinda, kuziongeza nguvu na kuzilea *startups* za vijana ambao wanaanza biashara kwa sababu, tumeona biashara nyingi sana zinaanza lakini zinafia katikati, hasa za vijana. Maana yake ni zinakosa *support* kutoka kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa ichukue *risk* ya kwanza, halafu Serikali hiyo hiyo imlee kijana anayeanza biashara na kum-*connect* na mwekezaji baada ya kuona kwamba, anaanza kusimama. Vilevile ni lazima tuwe na mfumo wa *mentorship* kwa vijana ambao wanaingia kwenye biashara, ili tuwalee wasipoteze mtaji. Wanapochukua mikopo kutoka benki, tuilee, mpaka tuhakikishe kwamba wanasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, mimi ninatoka Kyerwa, wilaya ambayo inazalisha kahawa kwa wingi, lakini ni wilaya ambayo iko mipakani. Tunapoongelea mipaka, siyo kama ni ramani ya mwisho wa nchi yetu, lazima tuangalie mipaka hii kama fursa na lango la kufanya biashara. Sisi pale kwetu Kyerwa tuna mpaka wa Mrongo, tunapakana na nchi ya Uganda na Rwanda moja kwa moja, lakini ninasisitiza na ninaomba Wizara, tuje na mfumo ni jinsi gani tunaenda kufanya biashara ya mipakani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tuna biashara kubwa ya mazao kama ndizi, maharage, kahawa, na kila kitu kiko pale, lakini hatuna *logistics* nzuri. Tukiweka *logistics* nzuri tukapata maghala na soko *cross border* ile ya masoko, biashara kubwa

itafanyika pale mpakani na uchumi wa wananchi wa Kyerwa kwa ujumla utapanda juu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mchango huo, ninashukuru sana, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khalid Nsekela. Nilimtaja Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby na Mheshimiwa Simai Mohamed Said ajiandae.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu. Ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutumikia nchi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wetu wa kuchangia ni mchache, kama sitamaliza, basi nitaleta mchango wangu mwingine kwa maandishi. Nchi yetu kiviwanda imekua. Tuna viwanda takribani 49,000. Nchi yetu kiuwekezaji imekua, nafikiri katika mwaka 2021, uwekezaji katika nchi yetu ulikuwa ni dola za Marekani bilioni 1.5, lakini leo tuna Dola za Marekani bilioni 6.5. Kwa hiyo, hiyo ni dalili kwamba, hatuko palepale, tunasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, tukiangalia *speed* yetu ya ukuaji tunakwenda, lakini hatukimbii kwa kasi ambayo nilikuwa ninaitarajia. Hapa mkononi mwangu nina karatasi moja, ninaomba niisome kwa muda mfupi tu, halafu baada ya hapo niendelee na mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja aitwaye Kitojo wa Tengere kutoka Chuo Kikuu cha Arusha aliandika andiko, ninaomba ninukuu maneno yake halafu baada ya hapo niendelee. Alisema, kwenye utangulizi wake;

"*The objective of this study was to examine industrialization in Tanzania and the need to include the disadvantaged people in the development process. This study used documentary review*

methodology. The study found out that industrialization is key to economic growth, if not properly managed it tends to marginalize the poor people. This caused for social inclusion policy measures, the study therefore recommends that if industrialization is to benefit the disadvantaged, the poor, then agriculture has to be industrialized." (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niyatafsiri maneno kwa kifupi. Mtafiti huyu alisema ya kwamba, suala la kujenga viwanda ni jambo jema, lakini lisipofanyika kwa uangalifu, linaweza likawafanya watu wengi walio masikini katika nchi kutengwa na uchumi. Akashauri, ili kufanya watu maskini wanufaike na suala la viwanda, lazima suala la kilimo liweze kuwa *industrialized*. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anahusisha kwamba, suala la kilimo na viwanda lazima liunganishwe. Wizara hii ya Viwanda na Biashara ifanye kazi kwa pamoja na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inanipeleka mimi mwaka 1959, ambapo nchi yetu na nchi ya Taiwan zilikuwa kwenye uchumi wa kulingana, lakini Taiwan wakaamua ya kwamba, sisi kama nchi tutalima, baada ya kulima tutauza mazao nje, lakini baadaye tutaacha kuuza mazao nje, tutaanza kutengeneza bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa nchi yetu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, rafiki mkubwa wa Mao Zedong akaenda Taiwan akajifunza, akaja Tanzania akasema Tanzania ilime, tukalima. Tanga wakalima katani, Mwanza wakalima pamba, chai ikalimwa Mufindi, kila mkoa ukawa na zao lake na viwanda vikaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa ni uamuzi wa busara sana na zaidi ya hayo, bado Mheshimiwa Rais wetu wa kwanza akaanzisha taasisi kama *Bard of External Trade,* ambayo baadaye imekuja kuwa *TanTrade,* akaja akaanzisha *TIRDO*, akaanzisha *TEMDO*, akaanzisha *CAMARTEC*, akaanzisha *SIDO*. Lengo lake ni *TIRDO* wafanye utafiti wa viwanda, *TEMDO* watengeneze *machinery* ndogondogo kwa ajili ya watu wetu kuwa na viwanda vidogovidogo nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Baba wa Taifa lilikuwa ni kuanzisha viwanda vidogovidogo nyumbani, baadaye akaanzisha *SIDO* kwa ajili ya kuratibu viwanda hivyo. Ndani ya *SIDO* akaweka Mfuko unaitwa *NEDF*. *NEDF* maana yake ni *National Entrepreneurship Development Fund;* kuwasaidia watu waweze kununua mashine, ili baada ya kulima tusiuze mazao, tutengeneze bidhaa tuuze nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo ilikuwa ramani ya Baba wa Taifa. Miaka mingi baadaye *TIRDO* ipo, *TEMDO* ipo, *CAMARTEC* ipo na *TanTrade* ipo, lakini hazina nguvu za kutosha kufanya kazi zake. Nimesimama hapa kuiomba Serikali na kumwomba Mheshimiwa Waziri, waziwezeshe taasisi hizi ziwe na uwezo kifedha kutimiza majukumu yake. *TanTrade* watafute masoko ya mazao nje ya nchi kidigitali na wakitafuta, bado tubadilishe mazao yetu kuwa bidhaa tuuze nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili na la muhimu sana ni uwezeshaji wa wazawa kiuchumi. Tulitunga Sheria Mwaka 2004, Mheshimiwa Rais Mkapa alitunga Sheria ya Uwezeshaji wa Wazawa Kiuchumi *(National Entrepreneurship Empowerment Act)*. Dada yangu, Mheshimiwa Beng'i Issa yuko hapa ndani, lengo lake ilikuwa ni kuwawezesha wazawa washikilie uchumi wa nchi yao. Leo ninapozungumza, wazawa wako kando ya uchumi wao, uchumi unaingia mikononi mwa wageni. Hawafurahii jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa leo kuomba, tulitunga Sheria ya Manunuzi hapa ndani kwamba, biashara yoyote ambayo ni ya shilingi bilioni 50 kushuka chini, isifanywe na mgeni. Nimesimama hapa leo, bado biashara zinafanywa na wageni, wanasajili kampuni *BRELA*, wanajiita wao ni wenyeji, lakini ni wageni. Ninaomba sana tufanye kile kinachowezekana kuhakikisha kwamba, Watanzania wanashikilia uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kariakoo leo, maduka yanafungwa. Ndugu zetu, siwezi kuwataja majina, ninawaona wamo humu ndani, sitaki kutaja jina la mtu yeyote, wanatoka kule kwao wanakuja Kariakoo wanajifunza biashara gani inatoka, halafu wanaenda kule wanazungumza kwenye viwanda,

wanakuja nao wanafungua maduka. Wakifungua maduka wanauza bei ndogo kuliko watu wetu, biashara zinafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, tuko hapa kuwalinda watu wetu. Tusikubali biashara za watu wetu zifungwe. Tufanye kila kinachowezekana kuwasaidia watu wetu wabaki kwenye biashara. Mwisho wa siku wawekezaji wataondoka, watatuachia nchi yetu. Mkibadilisha Sera za Kodi leo, watahamia nchi nyingine, Mheshimiwa Tale atabaki. Mwezesheni Mheshimiwa Tale ashikilie uchumi wa nchi yake, yuko hapa siku zote na ataendelea kubaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi ni benki zetu ziwawezeshe watu wetu, na zaidi ya yote hayo, Serikali mfanye kila kinachowezekana kuwaambia wananchi wafahamu fursa zilizoko ndani ya nchi yao. Watu hawafahamu fursa zilizoko ndani ya nchi yao, wanashtukia kuna bomba la mafuta, hawajui ndani ya bomba la mafuta kuna nini? Kuna biashara fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye kile kinachowezekana ili Watanzania wajue fursa zilizopo na wawezeshwe kushindana na wageni. Wageni wanakuja hapa na mikopo ya *interest* 5% kushuka chini. Mimi nikienda Benki yangu *CRDB* ninapewa 15% mpaka 22%, nitashindana vipi na mgeni? Tukienda kwenye tenda atanishinda tu, bei yake itakuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwasaidie watu wetu, tuwawezeshe. Tumesaini mkataba wa *African Continental,* soko moja la Afrika *(Continental Free Trade Agreement),* tunawapeleka watu wetu kushindana na nchi nyingine, lakini tufahamu kwamba, nchi hazifanani uchumi. Kuna *economic disparity*, Mimi siwezi kulingana hata siku moja na Mmisri kwenye nguo; na kiwanda cha maziwa cha Kenya hakiwezi kulingana na *Tanga Fresh.* Lazima akija Mkenya hapa na maziwa, *Tanga Fresh* atakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwawezeshe watu wetu kushindana na wawekezaji wanaokuja. Hatukatai wageni, tunawataka waje nchini kwetu, hakuna nchi itakayoendelea bila

investors, waje; lakini nchi yetu itulinde, hakuna nchi isiyolinda watu wake. Tusipofanya hivyo, baada ya miaka michache biashara zitakuwa zimefungwa, hakuna walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tuna haki ya kufaidi matunda ya Taifa letu. Wazee wetu walipigania uhuru wa nchi yetu; sisi tuwe watu wa kwanza, wageni waje, hatukatai; wawekeze mitaji. Wasije hapa na biashara ndogondogo za kuuza nyanya Kariakoo, kuuza yeboyebo Kariakoo, hao sio wawekezaji tunaowataka.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka watu waje wawekeze mitaji mikubwa, waajiri watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Eric Shigongo. Nilimtaja Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Simai Mohammed Said na Mheshimiwa Mariam Ditopile wajiandae.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji. Kwanza kabisa niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya; lakini ninataka niwaambie, kwamba hii wizara tunapoichangia kwenye biashara ina maana sisi tunachanganya. Wasije wakasema huyu kataja madini, huyu kaenda wapi, kwa sababu biashara ni biashara. Awe mkandarasi ni biashara, awe wapi ni biashara; kwa hiyo humu sisi tunaogelea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Wakala wa Vipimo. Eneo hili la Wakala wa Vipimo ni muhimu sana. Lazima niseme ukweli, ni lazima tumpongeze Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Vipimo, anafanya kazi nzuri. Kwa sababu kuna kipindi walikuwa wanapima sasa hadi madebe ya viazi. Watu wake walikuja pale

Jimboni kwangu Gairo wanapima madebe ya viazi, madebe ya nyanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima anapokwenda kununua kule shamba haendi kununua kwa mzani, wewe unataka apige teke madebe apime kwa mzani, kitu ambacho hakiwezekani. Ninashukuru tulimweleza Mkurugenzi jambo hilo na mwenyewe akamshuhudia mama pale Dumila ananunua kwenye madebe, mbogamboga na nyanya kwa hiyo hilo suala ameliacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja zito sana linaendelea kwenye hii nchi na yeye mwenyewe ni shahidi. Nimpongeze Katibu naye alilichukulia kidogo hatua; lakini nataka niwashauri. Sasa hivi viwanda, hasa kwa wageni, ukiangalia viwanda vya Watanzania vya nondo vinatengeneza nondo ambazo zina ujazo sahihi na wa kipimo, lakini viwanda vya wageni wakitengeneza nondo badala ya milimita 12 inakuwa na milimita 11; badala ya urefu wa futi 40 unakuwa na urefu wa futi 38 au 37. *Square pipe* ikiwa labda imeandikwa milimita tano ujue ina milimita tatu, urefu badala ya futi sita ina futi 5.7. Sasa, kutokana na vitu kama hivi nyumba za ghorofa zinaanguka huko; vitu vinaanguka kwa ajili ya hivi viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa wanakamata lakini sasa kosa linalofanyika ni kwenda kukamata watu wenye maduka wanaouza. Wewe unaenda kumkamata mtu Dodoma, unamkamata mtu Dar es Salaam muuzaji, unamkamata Mwanza mtu mwenye duka; kwa nini usiende kudhibiti kwenye kiwanda? Sababu muhimu wanayotoa; mimi sina duka, wasije wakasema jamaa anatetea biashara yake, maana mimi ni mfanyabiashara, sina duka. Sasa sababu wanayotoa, wanasema huyu aliandika *order* anataka milimita 11; hii siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mwizi mmoja alitokea hapa; mimi ni mfanyabiashara; akitokea mwizi, kama ndugu yangu nilikuwa najadiliana naye hapa Kampala, Mbunge wa Katavi; akitokea mwizi mmoja wengine wote watafuata ili wafanye biashara, lakini mwenye kiwanda ana sheria zinazomwongoza kwenye kiwanda. Kama nondo milimita 12 we

kazi yako ni kutengeneza milimita 12, kama milimita 16 wewe ni milimita 16. Hata hivyo, wamewapiga wafanyabiashara 20,000,000 au 15,000,000 wa sehemu tofauti. Mbona wanaenda kupima dukani badala ya kwenda kupima viwandani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo inatokea kama wakati ule wa viroba vile vya pombe, kuna aliyejinyonga Dodoma hapa kakutwa na viroba vya 1,000,000,000, wameenda kuvipiga kibiriti badala ya kuzuia kwenye *production*. Sheria inakuja inaenda kumuumiza mtu wa dukani kabla ya kwenye *production*. Kwa hiyo tuangalie kwenye viwanda, viwanda siyo wanapiga faini ya 20,000,000 funga kiwanda na huyo ni mhujumu uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo hapa viwanda vya nondo, vimejaa, ni vingi; na wao wenyewe ni mashahidi kwa sababu tayari wamekwishakamata, wanaona; nondo zote *fake, fake. fake, square pipe fake,* kwa hiyo tuangalie kwenye hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni viwanda vya matunda. Jamani hii nchi ina matunda yanaoza huko majimboni kwetu, halafu viwanda vya juisi vinaweka picha la embe ehee inawekwa picha sijui ya nanasi halafu mle kemikali, hakuna tunda hata moja. Viwanda na Biashara waliangalie hili. Viwanda ni *fake*. Mgonjwa anaenda hospitali anaambiwa akanywe juisi ya matunda anaenda kunywa sumu badala ya kula matunda; hiki kitu hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye mitaji; hii mitaji twende kwenye uwekezaji; hawa watu wa biashara ndio wanaotakiwa kutoa ushauri. Mgeni anakuja anatoa dola 500,000 eti huyo mwekezaji hivi Watanzania wangapi wenye dola 500,000, si ni wengi hapa? Halafu anakuja na *briefcase* anaenda kuchukua ukandarasi wa barabara. Akichukua ukandarasi wa barabara hana hata mia aliyokujanayo Serikali tena imetunga sheria inampa ka-*advance*. Akimaliza kupewa *advance* akichelewa kulipwa anadai *penalty* halafu sheria imetungwa na Watanzania. Hivi hii nchi ina rushwa ya aina gani? Hivi watu mbona hawajitambui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mimi kama, *anyway,* ngoja 2030 na mimi nitagombea hapo…

MBUNGE FULANI: *(Alizngumza bila kutumia kipaza sauti)*.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Subiri; utakuwa Makamu wa Rais, usiwe na wasiwasi, tutaleta sheria ya kunyonga watu, ninaona hapa ndipo watu watakapokaa vizuri, kweli kabisa. Yaani tunatunga sheria wenyewe halafu mzawa akija anaomba huo huo ukandarasi hapewi, huo ukandarasi mzawa hapewi na hata mia hapewi; lakini akija mgeni unampa kabisa tena, unamwongezea tena na fedha; yaani *briefcase*. Haanzi kazi na ukimpa unaweza ukampa 20,000,000,000 analima lima pale anasema anataka nyingine *certificate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana wanatenda biashara zao, kutenda bei ndogo kwa sababu wanajua watawapiga *penalty*. Utakuta kuna kampuni inadai *penalty* tu 100,000,000,000 au sijui bilioni ngapi. Tuangalie tuwe makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu, Mheshimiwa Waziri ameanza vizuri sana, lakini na uzalendo alionao Naibu Waziri, Katibu Mkuu waende, wao wanatakiwa waende kila sehemu yenye biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija pale kwangu Gairo ma-*broker* wa madini wale wazawa sasa hivi hawafanyi kazi; ametaja hapa madini; kila sehemu kuna Mchina kila ukizunguka hapa kuna Kamchina kapo, ukikaangalia hata 80,000 hakana, kapo kule nako kanafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Kariakoo wanauza hadi makopo, wanauza hiki sasa hizi ndiyo biashara? Nenda kafanye wewe kazi huko sehemu hizo kama utapata. Hii nchi tusipoangalia wageni wataongezeka mwishowe tutakuja kuangalia tumebadilika rangi tunakuwa Weusi, lakini tuna nywele za singa tutakuja kuwa kama kile kisiwa kinaitwa Mauritius. Mauritius hawajulikani Waafrika, Wachina; hata hawaeleweki utakuta mweusi ana nywele za singa. Maana tusipoangalia tutakuwa hivyo na tumekuwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo viwanda utasema hiki ni kiwanda; kama kiwanda cha *tiles,* vile vya *tiles* vile vya Wachina pale, kinachukua mawe kinatengeneza yanakuwa *tiles.* Lakini viwanda vingine ukiliangalia hata limashine lile *JD* la *diesel* linauzwa 300,000, mtu tayari anakwambia ni kiwanda, halafu ni mgeni. Hivi, kwani ukimpa Musukuma hiyo kazi haiwezi? Ukimwambia Musukuma alete kiwanda kama hicho, au Njelu hapa hawezi? Ataweza; halafu ndiyo wanatuletea sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watu wanalima alizeti, viwanda vya alizeti hivyo badala walete mashine ya mafuta waje wananchi wetu wauze alizeti kwa wingi, hawaleti viwanda kama hivyo. Baadaye tutakaa tutaona kwenye bajeti wanaleta, ujue tayari watu wamekwishakula rushwa huko. Utasikia, sasa hivi mafuta ya nje tunapunguza 10%, ujue tayari dili limeshapigwa huko watu wale hela. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo mtu akileta mafuta mengi utasikia ahaa sasa hivi tunaona kidogo tunalinda viwanda vya ndani hakuna kuleta nje wengine hawaleti. Sasa hii jamani tuangalie, mama mna kazi ya ziada kuweni wazalendo. Leo hapa tunaweza tukaogopa watu lakini kesho na kesho kutwa mimi ninajitoa katika Wabunge nisije nikaambiwa katika Bunge lile palikuwa na watu kazi yao ndiyo mzee, mimi ninajitoa kwenye ndiyo mzee. Enhee ndiyo, tuseme ukweli, ni lazima twende kwenye ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitoongea kitu cha uongo, hiyo ni sumu kwangu; lakini kwenye ukweli hatuwezi kuacha kuongea ukweli. Tuwalinde watu wetu wa ndani wa viwanda, Watanzania walindwe bila kuangalia Mtanzania huyu ana rangi gani awe Mrundi, awe Mwarabu, awe Msomali au awe mnini, awe Mswahili au awe nani walinde viwanda vya Tanzania kwa sababu hivi ndiyo vitakavyonyanyua benki zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shigongo amezungumza hapa, hawa watu wote wanaowapa hizi kazi wanaweka fedha nje, benki za Tanzania hazina fedha...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. AHMED M. SHABIBY: Bado nilikuwa ninaendelea, lakini kama muda umekwisha, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ahmed Shabiby, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Simai Mohammed Said, Mheshimiwa Mariam Ditopile na Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel wajiandae.

MHE. SIMAI MOHAMMED SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote tukawa wazima wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende kwenye hoja moja kwa moja kwa sababu ya muda. Hoja yangu mimi sitailenga katika masuala ya viwanda, nitazungumza zaidi katika biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, sekta ya biashara, kama mzungumzaji aliyepita, ni biashara mtambuka ni sekta mtambuka. Utalii ni biashara, kilimo ni biashara, kuuza duka ni biashara; na maeneo mengi. Sisi Wazanzibari tunategemea biashara; na katika kuchangia mchango wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilizungumza umuhimu wa *coast* yetu hii kutoka Pemba, Tanga, Unguja, Lindi, Mtwara; umuhimu wa *coast* hii kuiangalia ni njia gani tutaisaidia katika maeneo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wazanzibari katika mkakati wetu wa kupunguza umaskini kuelekea 2050 tumechagua maeneo matatu; biashara, huduma na utalii. Sekta hizi tatu ni muhimu sana na zote zinategemea biashara. Sasa, Mheshimiwa Waziri asijifunge katika kuangalia maeneo ya biashara, ni lazima awe *visionary,* maana yeye ni sawasawa na *epicenter,* mtu wa katikati. Maeneo yote anayoangalia, hawezi akakataa akasema sekta ya utalii yeye hahusiki, hawezi akakataa akasema sekta ya kilimo yeye hahusiki, biashara ni biashara na ni lazima tuangalie. Ukiangalia kwa upande wa huku *Western Tanzania*, Kigoma ukija zako mpaka Songwe, ukienda kule Wilaya ya Misenyi, Mutukula wanafanya biashara Soko la Ujirani la Mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa ninataka niseme kitu cha msingi. Kama sisi tunataka biashara na Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla akili zetu tuzipeleke huko huko. Mimi juzi mtu ananiuliza wewe uko wapi! Uko wapi, niko wapi na mimi sijaona niko wapi? Haya sasa hivi watu kuanza na michakato ya kuanzisha makundi ya urais. Akili zetu sisi ziwe ni moja, ni lazima tumheshimu Mwenyekiti wetu *Comrade* Samia Suluhu Hassan. Tukubali kwamba yeye ndiye alama ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwape Wabunge wenzangu wapya tulioingia humu ndani. Mimi ndiye niliyekuwa ninaitwa Simai, ndiye niliyekuwa mtu mmoja muhimu, nambari moja, wa marehemu Edward Lowassa, mamvi Zanzibar. Wengi tuliokuwa tuko chini tuliamini kwamba Mheshimiwa Lowassa atakamata kiti cha Urais; leo ninatoa hii siri; Mheshimiwa Lowassa tulikuwa tupo chumbani katika hoteli ninampigia shati pasi aliniambia; ni lazima umheshimu Mwenyekiti wa CCM, ni mtu muhimu sana. Yeye mwenyewe alimpenda sana Mwenyekiti wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninachotaka kusema ndugu zangu, Wabunge wenzangu wapya tusikubali sisi mtu kutuchanganya, mtu akaja sisi akatuambia lolote katika safari ya kuelekea 2030. Sisi tusimame moja na *Comrade* Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti, alama yetu na ndiye anayetuunganisha sisi sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yeyote ambaye anahisi yeye anaweza akapata kiti cha Urais kwa kutomheshimu Mwenyekiti hutoboi, hutoboi. Kwa hiyo ninachokisema hapa akili zetu sisi Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge tufanye kazi sasa hivi ya kumsaidia Mwenyekiti wetu na Serikali zetu ili tuweze kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, vijana wetu wapate ajira. Tusifikiri kwenda kujenga mahoteli, kuanza kuweka wajumbe kwa ajili ya mwaka 2030 hatafika kokote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba, tunataka biashara. Sisi Wazanzibari hatutaki kuchanganywa kuelekea 2030; sisi tunataka tumheshimu Mwenyekiti wetu, tunataka biashara. Kama nilivyosema sekta hii ni mtambuka;

Zanzibar tume-*identify tourism, trade and services.* Kwa hiyo wakati ukifika 2030 tutakuja kukutana, lakini sisi tunataka biashara. Kwa hiyo hoja yangu ninayoisema ni kwamba Waheshimiwa Mawaziri na sisi Waheshimiwa Wabunge wapya akili zetu twendeni katika biashara mambo ya siasa 2030 tuachane nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu lilikuwa ni hilo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Simai Mohammed Said. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri na Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel ajiandae.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa fursa hii. Nitangulie kuunga mkono hoja, lakini pia kuungana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Kilimo na Mifugo katika maoni na ushauri waliotoa kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane pia na wenzangu kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niseme tu kwamba ninamuunga mkono mchangiaji aliyepita Mheshimiwa Simai ingawa sauti kidogo, sasa aanze kulamba asali kwa vile anavyopiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sisi tunasimama na Dkt. Samia Suluhu Hassan, yako aliyoahidi mazito kwenye sekta ya viwanda na biashara pamoja na uwekezaji, hayo ndiyo Watanzania wanasubiri kuyasikiliza 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wachangiaji wenzangu pia kumshukuru na kumpongeza sana Waziri wetu Mheshimiwa Judith Kapinga; kwa kweli tunarudia tena, kama huko nyuma nilivyochangia wakati wa Mjadala wa Hotuba ya Wizara ya Elimu, lakini tumemwona Jemedari Ulega, hii ndiyo namna gani Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi inaweka viongozi ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu Mheshimiwa Judith tutampa ushirikiano kama Mbunge mwenzetu, lakini ni dua kwa

Mwenyezi Mungu; na sisi tunamwombea aendelee kuwa mnyenyekevu na msikivu. Ameianza vyema safari yake ya kisiasa na hakika atafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Londo pia amepita sehemu nyingi ndani ya Serikali yetu na pia uwakilishi wake pale Jimboni, naye ni mtu mtulivu sana aendelee kushirikiana na Waziri wake pamoja na Watendaji wote. Hakika Wizara hii wataenda kutimiza zile ndoto na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa menejimenti niwapongeze wakurugenzi wa taasisi zote; na ninaomba ku-*declare interest* tu kati ya Wizara ambazo zina wakurugenzi wengi akina mama ni hii Wizara ya Viwanda na Biashara. Yuko dada yangu Katunzi pale *TBS*, wapo *FCC* tunavyoona *fairness* inakuja ni mwanamama yuko anakaimu pale. Kipo chuma, Profesa kwenye chuo nilichosoma mimi pale *CBE,* kwa kweli kama kuna mwingine nimemsahau anawawakilisha akina mama, wote wanafanya kazi nzuri sana huku wakiongozwa na Mheshimiwa Judith.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu amekuja, Balozi alikuwa Katibu wa Rais; amepita *TEA* huko, amepitia kwa Makamu wa Rais na hata Mheshimiwa Rais alisema wakati anamwapisha. Kwamba 'mwanangu Waziri ninakutoa uende ukakue zaidi.' amemlea, amemwezesha anataka akaone anakuwa sehemu ya kuacha alama kwenye uongozi wake wa Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Kamati imeongea, tumeshangaa kuona kwamba hakuna fedha za miradi ya maendeleo kutoka nje. Mheshimiwa Waziri amtumie Katibu Mkuu, ni Balozi huyu, lakini amekaa Ikulu, amezunguka nchi nyingi, tuna uhakika sisi kama Kamati wakija huko mbeleni watakuja kutueleza kwamba kuna wadau wamekaa nao na kuna kafungu kanakuja, hasa kwenye ule Mfuko tulioomba wa Kuendeleza Viwanda Nchini. Kwa hiyo, nimpongeze sana, maana wanasema kuna mtu kupata kazi na kuna kazi kupata mtu. Kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara basi kazi imepata mtu, lakini na kijana makini pia Naibu Katibu Mkuu wake kaka yangu Robert waendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sana kugusia, ametangulia Mjumbe mwenzangu wa Kamati, kuongelea suala la umuhimu wa taasisi hizi mbili ambazo zinahakikisha siyo tu mlaji ama bidhaa inakuwa bora bali pia inahakikisha mlaji anapata kipimo sahihi cha bidhaa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko nong'onong'o mitaani kwamba tunataka kuunganisha Taasisi ya *TBS* na *TMDA,* sisi kama Kamati kwa kweli tumeliona hilo na tumesema hapana. Hizi taasisi mbili zote ziwepo, zote ziwezeshwe kwa sababu kila mmoja analo jukumu lake ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuangalia nchi nyingine huko hata Kenya tu hapo jirani. *TBS* anasimamia *national standards,* anaenda kudhibiti ule ubora lakini huyu Wakala wa Vipimo anaenda kuhakikisha kama maziwa haya ubora wake ni huu; je, hiyo lita moja ya maziwa unayoletewa mlaji ndiyo hiyo lita moja kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shabiby ameongelea kuhusu, tumeona mfuko wa *cement* wa kilogramu 50 *WMA* inaenda kukamata watu mtu kaweka kilogramu 47. Hebu kilogramu tatu tatu tu zile au hata nusu kilogramu kwenye mifuko 1,000 ni kilo ngapi? Ndiyo maana tunapata *disaster* za majengo kuanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kuwaonea wananchi hawa ambao Mheshimiwa Rais anawawezesha wanapata hela wanataka wapige chini nyumba za tembe wajenge za matofali, wanapata bidhaa zisizo bora kwa sababu usimamizi unakuwa siyo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaunga mkono uwepo wa taasisi zote mbili ziende sambamba na tunaomba kwa...

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa inatoka wapi?

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa.

TAARIFA

MHE. KIJA L. NTEMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, sijaelewa maana ya tembe labda Mheshimiwa Mbunge anisaidie ili nijaribu kuelewa nyumba ya tembe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Ditopile.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ya tembe ni nyumba zile ambazo zinajengwa na majani na kadhalika. Eeh na pia ni *crown* siyo kirauni. Mtani wangu huyu anajua kwa nini nimemwambia hivyo. Taarifa ninapokea na ninafikiri nimempa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna gani tunaenda mbele kwa ajili ya taasisi hizi? Tunashauri Mheshimiwa Waziri akae na timu yake ili sasa ni muda mwafaka kwa mijadala hii, tuwe na sera ya ubora, kwa maana *National Quality Policy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi waliotangulia wameongelea suala la kulinda uwekezaji wa ndani. Sisi kama Bunge tumekuwa tukipiga kelele na kweli tunaipongeza Serikali imefanya kazi kubwa. Wanakuja wageni wanafanya kazi za wanyonge, za wazawa ambao tunatakiwa tuwalinde.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu uliliwa, ningaomba nimalizie.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mariam.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize hoja yangu kidogo tu kwa sababu nililiwa muda wangu na taarifa. Samahani lakini.

MWENYEKITI: Sekunde 30.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hamna shida. Kwa hiyo, tunaomba tulinde wazawa wetu, lakini kwenye

zile bidhaa ambazo zinaingizwa nchini na hazitozwi kodi na tuna kampuni zinazozalisha, kama Kamati tulienda Tanga kwenye Kiwanda cha *Neelkanth Chemicals*. Kwa kweli bidhaa ile ya *Calcite Calcium Carbonate* imefika muda Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha twende tuka-*impose tax* ya *product* hii inayoingia kutoka nje ya nchi ili tulinde bidhaa ambazo zinazalishwa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Asma Mwinyi na Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya ajiandae.

MHE. ASMA ALI MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na amani aliyeniwezesha nikasimama siku hii ya leo na mimi nikaweza kuunga hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea siku hii ya leo. Pia, ninachukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka na kudumisha utulivu uliosababisha ukuaji wa viwanda hapa nchini kwetu na biashara na ustawi wa biashara na viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua vile vile fursa hii kumshukuru pia, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, naye pia kwa jitihada nzuri ambazo anazifanya katika kuboresha uchumi huu wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana Wizara ya Viwanda (Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote) kwa kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini pia ninaomba nijikite katika viwanda vya ndani hususan wale ambao wanatengeneza taulo za kike. Kutokana na kuwa ni kiongozi mwanamke, mama, ninaelewa umuhimu wa hizi bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa hizi za hedhi salama hapa Tanzania kuna takribani viwanda vya ndani vitano mpaka nane ambavyo vipo hapa ndani, lakini viwanda hivi vinavyotoa hizi taulo za kike hapa nchini zimekuwa zinakabiliwa na changamoto kubwa sana kutokana na bidhaa ambazo zinatoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa hizi ambazo zinatoka nje ya nchi zinaonekana kwamba imekuwa ni rahisi kununua na kuleta hapa ndani badala ya kuweza kutengenezwa hapa hapa. Hii ni changamoto ambayo Mheshimiwa Waziri ninaomba uiangalie vizuri na tuangalie jinsi gani ambavyo tunaweza kuwanyanyua viwanda hivi ili iwe rahisi kutengeneza hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa hizi zinaonekana kwamba zimechukua takribani 60% mpaka 70% za hizi hedhi salama zinazotoka nje ya nchi na 30% mpaka 40% za hapa ndani. Unaona jinsi gani ilivyokuwa kuna changamoto hii ilivyokuwa iko kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, hizi huwa haziji kwa bei rahisi kitu ambacho kimefanya wanawake wengi ambao wenye kuishi maisha duni na hususan watoto wetu, mabinti wetu wa shule ambao hasa wako vijijini wanashindwa kuweza kumudu kununua pedi hizi. Hizi huja katika 1,500 mpaka kiwango cha 4,000, ambayo mtu wa kawaida ni ngumu kwake kuweza kununua kitu ambacho kimesababisha mabinti wetu, wanawake wengi kwenda kutumia njia mbadala ambazo siyo nzuri kwa afya ya jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuwapongeza sana Serikali kwa juhudi ambazo zimefanya katika kujaribu kukuza sekta hii ya ndani, kama vile kuondoa kodi *(VAT)* katika *product* ambayo imemalizika ya hizi hedhi salama lakini pia, kutoa kodi katika malighafi. Hivyo ninaomba (ninaona muda wangu umekwisha) kwa haraka tu ninaomba kuipa ushauri Serikali vitu vifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza motisha kwa viwanda ambavyo vinafanyika hapa nchini ili kupunguza kodi na pia

kuwawezesha wao kuweza kupata mitaji kwani kwa sasa hivi mtu ambaye anataka kwenda kuanzisha kiwanda kuna mtaji unakuwa una *rate* kubwa sana na mashine pia kuzileta nchini *cost* yake ni kubwa sana. Kwa hiyo, hii ni sehemu mojawapo ambayo waangalie. Pia tuongeze kusambaza hizi taulo za kike kwa wanafunzi wetu shuleni ili ipate kusaidia kuwasaidia watu wa viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kushauri Serikali kuongeza katika ubunifu na ustadi. Kufanya *study* ambayo zile *raw materials* ambazo tunaweza tukatumia hapa Tanzania zinazokuwa *produced* hapa Tanzania, ili ziweze kutengeneza hizi taulo za kike ambazo zitasaidia kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninapenda suluhisho la kisera ya kisheria kuanzisha *Menstrual Leave Policy*, ambayo kwa wale akina mama wenye maumivu makali walau wapate siku moja au mbili bila kuandikiwa barua kutoka kwa daktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Asma Mwinyi. Nilimtaja Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya.

MHE. ALI HAIDAR MADEWEYYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii na makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Nijielekeze moja kwa moja kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Waziri Rajabu, kwa imani kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za makusudi katika kulihudumia Taifa hili la Tanzania. Tunaona mara kwa mara anaposafiri anasafiri na wawekezaji kwa ajili ya kukuza biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijielekeze katika Shirika la *TanTrade*. Ukweli ambao usiofichika *TanTrade* ndiyo roho

ya biashara hapa Tanzania. Sasa wakati umefika kuifanya *TanTrade* iweze kujitegemea. *TanTrade* inahitaji iwe na mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Serikali duniani ina majukumu ya msingi ya kuhudumia wananchi wake lakini lazima Serikali hii ya Mama Samia ijikite kutengeneza matajiri. Hawa matajiri jamani wanatengenezwa. Kupitia *TanTrade* tunaweza tukaiwezesha *TanTrade* kutengeneza matajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu kwamba ukiangalia kwa mfano kama China, kuna kitu wanaita *Export Guarantee Fund* au wengine wanasema *Export Credit Guarantee Scheme*. Hapa ndipo tunapotengeneza matajiri. Tuifanye *TanTrade* kuwa na huu mfumo. Mwisho wa siku tunapompa huu mfuko tuje tumsimamie, tumwambie umetengeneza matajiri wangapi na wale matajiri watakuja ku-*reflect* kwenye kulipa kodi pamoja na kutengeneza ajira. Leo *TanTrade* imekuwa kama mkiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tumeshuhudia *TanTrade* kutoka 2021 mpaka 2025 imetoka kwenye makusanyo ya shilingi 250,000,000 mpaka shilingi 300,000,000. Leo *TanTrade* inakusanya kupitia mifumo iliyowekwa pale ya sabasaba na mambo mengine ya maonesho, inafika shilingi 10,000,000,000 mpaka shilingi 11,000,000,000. Yule mama aliyeko pale anajitahidi sana kufanya kazi. Shida iliyopo Mheshimiwa Waziri kunakuwa na maneno maneno kwenye Wizara. Hapa ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, wako baadhi ya wakurugenzi wake pale ndani uwezo wao mdogo; huo ndiyo ukweli, wanaleta fitina. Kuweni sana katika hili kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaiomba sana Wizara ya Biashara, hapa Serikali lazima ifanye *coordination*. Leo tunashuhudia kuna *BBT*, kuna *COPRA*, kuna *TPHPA*. Hawa wote, *COPRA* ana-*deal* na masuala ya mazao, *export*. *TPHPA* ukitaka kusafirisha biashara za kilimo. Sasa tutakuwa na wasimamizi wangapi wakati tunayo pale *TanTrade*? Hebu waende wakakae kama Serikali wakubaliane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana sasa hivi tukimtaka Waziri atupe *data* za wafanyabiashara wanavutana. Haziji katika

realistic. Kwa hiyo, lazima wafanyabiashara wasimamiwe kupitia hii *TanTrade*. Ikiwa ni mazao basi tuipeleke kwenye *TanTrade*. Tunajua *TanTrade* wana-*export* mazao mangapi kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo *TPHPA* bado *TanTrade* tukiiwezesha tunaweza tukafanya hivyo vitu kabisa kabisa, badala ya kuwa sasa kila mtu anasimamia biashara. *TanTrade* ni mwarobaini wa *solution* ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi, tulikaa muda mrefu hapa tumeshuhudia *TanTrade* ime-*develop master plan*. Baada ya muda mfupi tutaona pale Sabasaba panakwenda kubadilika. Tulikaa muda mrefu sana, sisemi kwamba Ma-*DG* waliopita hawakufanya kazi; si kweli, lakini huyu ameupiga mwingi tumpe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho si kwa umuhimu, tuna changamoto. Sisi pale Zanzibar tunafanya biashara nyingi tu tofauti halali. Sasa kuna ongezeko limeongezeka pale la mafuta ya kula. Ni ukweli usiofichika biashara inayokuja Zanzibar tunatumia kama Wazanzibari lakini vilevile iliyokuwa ya ziada tunafanya *u-turn* lakini inapoingia nchini lango la *TRA* ni moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mafuta ya kula yametoka kwa dumu moja kutoka shilingi 10,000 mpaka shilingi 27,000. Kaka yangu Mwenda hebu liangalie hili lakini na Wizara ya Biashara hizi tena zisije zikawa ndiyo kero mpya za Muungano. Mheshimiwa Waziri hebu liangalieni hili na sisi ni ndugu zenu. Si tatizo, tulisema hapa tutengeneze matajiri, siyo ubaya tukitengeneza matajiri pia kutoka Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninaunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Madeweyya. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi hii na shughuli zetu za *session* hii zimeishia hapa kwa mujibu wa ratiba, isipokuwa nina tangazo la wageni waliopo Bungeni muda huu.

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni Menejimenti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Menejimenti ya Wizara ya Viwanda na Biashara siwaoni. *(Makofi)*

Tuna wakurugenzi wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Wapo pale. *(Makofi)*

Tuna Mameneja Mikoa wa *SIDO* na wadau wa Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wawakilishi wa taasisi za kifedha na wadau wa viwanda chini ya Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania *(CTI)*. Karibuni sana wadau wetu. *(Makofi)*

Wadau wa Chemba za Biashara na Viwanda za Sekta Binafsi nchini *(Private Sectors)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wadau wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania wakiambatana na mtangazaji wa kipindi cha biashara *East African TV Media*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Viongozi na wafanyabiashara, machinga Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)*. Karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri wetu wa Viwanda na Biashara. Hao ni viongozi wa CCM kutoka Wilaya ya Kilosa. Karibuni sana viongozi wetu wa CCM kutoka Kilosa. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Londo, ni wadau wa Sekta ya Biashara kutoka kampuni za Waikiki, *Makutano Group* na *Green Culture*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wageni 15 wa Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, wafanyabiashara na wachimbaji

kutoka Nyamtondo-Katoro, Mkoani Geita. Karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna tangazo hapa. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi, tarehe 23 Mei, 2026, kutakuwa na mchezo wa kirafiki kati ya Timu ya Mpira wa Miguu ya *Bunge Sports Club* na Timu ya Dar es Salaam *Gymkhana Veteran Club*. Mchezo huo utachezwa saa 10 jioni katika Kiwanja cha Jamhuri Dodoma. Waheshimiwa wote mnaombwa kufika bila kosa ili kushiriki na kutia hamasa ya ushindi katika mchezo huo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumaliza matangazo hayo, ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.57 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Naibu Spika *(Mhe. Daniel B. Sillo)* Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano hoja iliyopo mbele yetu. Tunaanza na Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mheshimiwa Abubakar Mohammed Mussa, ajiandae.

Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mheshimiwa Magreth, tunakusubiri.

MHE. MAGRETH B. EZEKIEL: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa nafasi hii adhimu ya kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani ni kwa sababu nilikuwa nakimbiakimbia kwa hiyo, sikupata muda wa kutulia na kupanga vitu vyangu. Kwa hiyo, ninaomba muda wa dakika tatu ili niweze kuwa na utulivu kama kuna mwongeaji mwingine anaweza akaendelea. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mheshimiwa Abubakar Mohammed Mussa ajiandae.

MHE. ABUBAKAR MOHAMMED MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Allah Subhanahu Wata'ala*, kwa kutujaalia uzima wa afya na leo hii kukutana ndani ya Bunge letu hili Tukufu na kuchangia hoja hii ya kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni mwezi tano, *Dhul-Hijjah* ninawatakia kila la heri wenzangu waliofunga katika kuelekea *Idd el Hajj*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ndiyo mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi wake mnono alioupata katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 29. Hata hivyo, nimpongeze Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Nchimbi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Spika wa Jamhuri ya Bunge la Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, pia ninakupongeza na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. Pia nimpongeze Spika wa Baraza la Wawakilishi, ndugu Zubeir Ali Maulid na yeye kwa kuongoza vizuri Baraza la Wawakilishi kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bila ya kuwasahau wananchi ambao ndiyo wamenituma hapa Bungeni, wananchi wa Jimbo langu la Mtoni. Ninawaambia nipo hapa na nitaendelea kuwawakilisha na ninawaahidi sitawaangusha. Bila ya kumsahau mke wangu kipenzi pamoja na watoto wangu ambao wamenivumilia katika kipindi kirefu cha uchaguzi na mpaka kufikia hapa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanangu na mke wangu wamekubali kugawana mapenzi baina yao na wanajimbo wa Jimbo la Mtoni, niwashukuru sana kwa kukubali hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Waziri wa Viwanda na Biashara, dada yangu Mheshimiwa Judith Kapinga, pamoja na Naibu Waziri, pamoja na *cabinet* yake nzima kwa kuandaa mambo mazuri katika Wizara yetu hii, Wizara ambayo ndiyo uti wa mgongo wa maisha yetu sisi ya kila siku wanadamu, Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu nilizokuwa nazo, mwaka wa fedha 2020/2021 kipindi ambacho Mama Samia, anaingia madarakani Wizara hii ilikuwa na bajeti ya shilingi 81,000,000,000, lakini leo hii tuliposimama hapa tunazungumzia Wizara hii, tunaijadili hapa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, jumla ya bajeti ni shilingi 137,000,000,000. Ambayo sawa na ongezeko la shilingi 56,000,000,000, hii inaonesha dhahiri kwamba Mama Samia Suluhu Hassan, yupo *serious* katika kukuza sekta hii ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuthibitisha hilo, Wizara ya Viwanda na Biashara imeboresha mazingira ya kufanya biashara nchini kupitia mpango wa *blueprint*. Sambamba na hilo Wizara imefanya mageuzi ya sera na sheria za uwekezaji ili kuvutia mitaji

mikubwa kutoka nje na ndani ya nchi; mfano kupitishwa kwa Sheria mpya ya Uwekezaji *(Tanzania Investment Act, 2022)* pamoja na kuanzishwa kwa sheria mpya ya maeneo maalumu ya kiuchumi *EPZ* na *SEZ*: na uwekezaji wa kawaida ili mwekezaji apate huduma zote sehemu moja kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarika kwa diplomasia ya uchumi na ziara za kimataifa za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia zimeboresha imani ya uwekezaji wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia wakati Mama Samia, anaingia madarakani nchi yetu ilikuwa na viwanda 52,000, lakini sasa hivi nchi yetu ina viwanda 80,179, hii uone kwamba Mama Smia, jinsi gani ameupiga mwingi katika kuhakikisha sekta ya Viwanda na Biashara inakuwa. Katika viwanda hivyo 80,179; kufikia mwaka huu 2026 viwanda vikubwa vimekuwa 1,522 sawa na ongezeko la viwanda 27 katika nchi yetu. Viwanda hivi 27 ambavyo ni vikubwa tu vimeweza kuajiri watu wasiopungua 189,000, hii inaonesha dhahiri kwamba Mama Samia amekuja kuhakikisha kwamba vijana wanapata ajira na kuweza kuondokana na umaskini, hiyo ndiyo azma yake Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mazuri yote hayakosi kuwa na misukosuko. Kuna kadhia ambayo inaendelea kutokea katika sehemu ambazo vinajengwa viwanda ndani ya nchi yetu. Wakati wawekezaji wanakwenda kujenga viwanda kuna *authority* mbalimbali, wakati hawa watu wanaanza kujenga huwa wanajitokeza na kuanza kuwa-*harass* mara watu wa *fire*, mara watu wa *NEMC*, mara watu wa *OSHA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli hii inaleta kadhia. Niwashauri Serikali wakati mwekezaji anapewa kibali cha kujenga kiwanda chake, ninaomba kuandaliwe semina kwa wawekezaji hawa ili waelezwe kwamba, ukitaka kujenga kiwanda ndani ya Tanzania uwe na moja, mbili, tatu, nne kwa ajili ya kuondoa usumbufu kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo.... ninaomba nimalizie.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, malizia.

MHE. ABUBAKAR MOHAMMED MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *VAT deferment* pamoja na *duty remission*. Hivi vitu vimekuwa vikichanganya sana wafanyabiashara ndani ya nchi yetu. Leo hii ukienda upande wa *TRA* kuna watu wamepewa barua, wameitwa kule kwa ajili ya kwenda kupewa penati walipe hii, *VAT deferment* pamoja na *duty remission*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasababisha aidha viwanda kufa au kusababisha uzorotaji wa uzalishaji ndani ya nchi yetu. Ninaomba sana Waziri wa Viwanda pamoja na Waziri wa Fedha wakae pamoja walizungumze suala hili na waache kuwasumbua watu badala yake wawape elimu juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hata Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wata'ala*, amesema: *Wamakunna mu'adhdhibiina hatta nab'atha rasula*...

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. ABUBAKAR MOHAMMED MUSSA: ...sitaweza kuwaadhibu umma mpaka niwaletee Mtume. Kwa nini wanaadhibu watu bila kuwapa semina?

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. ABUBAKAR MOHAMMED MUSSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa; atafuatiwa na Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete; Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel, ajiandae.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze

kuchangia maoni yangu katika bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kipekee ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri lakini na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lililopita, Bunge la Kumi na Mbili, nimekuwa mjumbe wa kamati hii ya Viwanda na Biashara kwa muda wa miaka mitano na *professional* ni *line* yangu ambayo nimeisomea. Kwa hiyo, ninataka kutoa ushauri kwa baadhi ya mambo machache ambayo ninadhani yanaweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza juzi wakati ninachangia kwenye Wizara ya Uchukuzi, nilisema sasa *TISEZA* na Wizara ya Viwanda na Biashara wajikite kwenye kupunguza msongamano hasa wa Bandari kavu Dar es Salaam. Kwa sababu viwanda vingi vya nchi hii *more than 50%* vipo Dar es Salaam. Sasa na sisi tunapozidi kuchukua maeneo ya uwekezaji tunaongeza huko huko, maana yake tunaongeza msongamano wa makontena na hatimaye foleni zinakuwa nyingi, lakini na gharama pia kwa sababu tutashindwa kutumia reli yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikasema ushauri mkubwa tuone *along the rail* hii ambayo tumeijenga ya *SGR* kama tutaanza kupata maeneo, wawekezaji wenye viwanda wanachohitaji wapate usafiri wa kupeleka mizigo bandarini na kuitoa ili waweze kusafirisha vizuri. Kwa hiyo, ninaamini hili walione waweze kutafuta maeneo mazuri kwa ajili ya kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, jambo lingine ambalo nimekuwa nalo, hata katika Bunge lililopita ni *issue* ya kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu vya ndani, *(local content)*. Wenzetu jirani zetu wa Uganda wana kauli moja inaitwa, *buy Uganda, build Uganda*. Kwa hiyo, chochote ambacho kinapatikana ndani ya nchi yao wanakipa *priority* ya kwanza *no matter* mfadhili ni nani, *no matter what* lazima kinunuliwe kitu cha ndani kwanza. Wanaenda nje endapo hakuna bidhaa ile ndani ya nchi yao, ndiyo hapo wanapotoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka tulitembelea *TEMDO last time* Arusha. Wale watu wanazalisha vitanda vizuri vya kutumia hospitalini lakini ukija hapa *MSD* wanaagiza vitanda China, wanaagiza vitanda wapi, vyenyewe vinachukua muda mrefu sana wakati taasisi ya Serikali inazalisha hivi vitu hapa na bado kule wanapopeleka wanatoa *advance* kwa pesa hii ambayo tunaikusanya halmashauri na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake unakuta bidhaa inachelewa kwa muda mrefu wakati hapa *TEMDO* taasisi ya Serikali iliyopo chini ya Wizara yetu ya Viwanda na Biashara wangeweza kuzalisha mpaka majokofu ya kuhifadhia maiti kwenye mochwari, wanazalisha. Kwa hiyo, tulione hili tuweze kutumia bidhaa zetu za ndani, tulinde pesa ya kigeni ambayo inatolewa nje ya nchi, lakini tutengeneze ajira kwa ajili ya watu wetu. Kwa hiyo, hilo tulione liweze kutusaidia zaidi kwenye viwanda vyote kama ni viwanda vya kutengeneza bidhaa nyingine; *cement* na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapowezekana kwenye *Finance Bill* tuone kama kitu kinazalishwa ndani tuna haja ya kuongeza *importation* ya kodi ikawa kubwa zaidi ili viwanda vya ndani tuvilinde. Anayeangalia anatengeneza faida ni mfanyabiashara aone je kuagiza nje au kuagiza ndani wapi anapata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kweli, ni aibu leo tunakuwa tunataja viwanda lakini bado *Finance Bill* au tunayoruhusu hapa bado *duty* tunaweka chini zaidi mtu anatoa vitu nje ana-*compete* na viwanda vya ndani, yeye bado ana *incentive* ya *export* kule hatuwezi kushindana naye. Ukiangalia gharama za uzalishaji; umeme na vitu vingine kwetu bado ni gharama *in comparison* na nchi nyingine kule wanapotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulione hili tusaidie watu wanaowekeza ndani ili tunapozungumza huko nje tukavutie wawekezaji waje waone kwamba kuna *incentive* za ziada na wanapowekeza hapa watalindwa na hatimaye wataajiri Watanzania na watalipa kodi kihalali ili waweze kwenda sawa na *competition* inayofanyika huko nje. Hiyo ni sehemu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ipo habari ya *WMA*; ninataka hili jambo nilieleze kwa kina kidogo kwa sababu kumekuwa na suala la utata hata kwenye uzalishaji wa nondo. Mtu anaweza akasikia kuna nondo za milimita 11, nyingine milimita 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, nondo zinazalishwa kwa *standard*, iwe *TBS*, iwe yoyote yule anayezalisha anafuata *standard*. Sasa *standard* tunazozalishia nondo ni *base standard 44, 49* ya 2005. Tuna *grade* ya *TBS* ya Tanzania ambayo ni *TZS* 142 na zimeeleza kwamba *thickness* za nondo, *standard* ambayo zinazalisha ni milimita nane, 10, 12, 16, 20, 25 na 32. Hatuna milimita 11 kwenye *standard*. Sasa kinachotokea ni nini, hizi milimita kwa tani zinaonesha kabisa kama ni nondo ya milimita nane, tani moja ni nondo 210 zenye urefu wa mita 12. Kama ni milimita 20, tani moja ni nondo 34, kila kitu kinajulikana kipo hapa na hii ndiyo *standard* inayotuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *it is a shame* baadhi ya wazalishaji unakuta anazalisha nondo anapunguza *thickness* inakuwa milimita 11 ili a-*compete* na mwingine anayezalisha kwa kufuata *standard*. Kinachotokea ni nini, kiwandani nondo zinauzwa kwa tani, kila mmoja atalipa kwa tani, lakini mwingine anaambiwa kwa tani moja wewe unapata *piece* 104, wewe kwa tani moja unapata *piece* 94, zimeshaongezeka *piece* 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati kule mtaani kinachouzwa kinauzwa nondo moja inauzwa kwa *piece*. Sasa mfanyabiashara yoyote anayeuza mtaani kwa *end user* atataka apate *piece* nyingi kwa kila tani, kwa hiyo, matokeo yake ndiyo haya masuala tunaenda kujenga kule unakuta ghorofa linanguka, madaraja yanaharibika kwa sababu ya vitu hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *the unfair bad;* wakandarasi wanapata shida sana kwa sababu hujengi daraja ukapata *certificate* bila kupeleka hii nondo kwenda kupimwa *University of Dar es Salaam* au *DIT*. Sasa unapopeleka nondo ina milimita 11 pale wanakukatalia wanakwambia hii nondo haija-*meet the standard*. *By that time* umeshalaza nondo za shilingi 200,000,000 au 300,000,000 chini na wewe ni mfanyabiashara umenunua

kiwandani bila kujua. Kwa hiyo tungeomba *adherence* ya *standard* ambazo zimewekwa ifuatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba *WMA* wapewe meno: tena kama ingewezekana hawa sijui wafanye taasisi kamili kabisa ili waweze kusimama. Maana kumekuwa na *agenda, agenda* hapa za kusema waunganishwe na *TBS*, wafanye nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayaunganisha mashirika yaliyofeli kushindwa kufanya kazi. Huwezi kuchukua *WMA* leo waliosaidia hata kwenye *meter* za maji: sisi ni wafanyabiashara wa *meter* za maji. Kipindi tunawapa *meter* zikifanyiwa *pre-verification* of *conformity* kwenye nchi ya *origin*, *meter* zilikuwa zinafeli lakini leo *meter* inatoka kiwandani wanakuambia wameipima ipo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaifikisha *WMA* inafeli, kinachofanywa inafanyiwa *calibration*, inapimwa tena ina-*meet the standard*. Sasa haya mambo yote tukitaka tulundikwe *TBS* ndugu yangu hatutaweza. *TBS* tunawapa kukagua magari hapa ndani, miaka kama minne iliyopita, mzigo ukawa mkubwa akashindwa. Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia mwenyewe akasema yaanze kukaguliwa kule yalipokuwa yanakaguliwa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoomba taasisi hizi tuzisaidie kwenye madaraka haya tuliyozipa, kama zinahitaji mtaji zipewe mtaji, zifanye kazi, lakini tukianza kuziunganisha unganisha tunapoteza ubora. *TBS* ni msimamizi wa *standards*, *its* Tanzania *Bureau of Standards*. Tumwache asimamie *standards* lakini hawa wengine wafanye *adherence* ya *standard* ili waone kama kuna sehemu kuna kosa hawa wawili wakishirikiana hiki kimeandikwa hivi, hiki kimeandikwa wataweza kusababisha mlaji wa mwisho apate faida anayoitegemea kutokana na pesa anayoitoa. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ahsante.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja kwa sababu ya muda, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete; atafuatiwa na Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, ajiandae.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa, kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona akiendelea kupeleka fedha nyingi ili wizara hii iendelee kufanya vizuri. Pia, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara mdogo wangu Judith Kapinga kwa kazi kubwa, kazi nzuri, tunamwona namna anavyopambana. Kwanza Mheshimiwa Waziri ni msikivu, mnyenyekevu na anamsikiliza kila Mbunge akiwa na uhitaji yeye pamoja na Naibu Waziri mnafanya kazi vizuri. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Rais amewapa Katibu Mkuu mzuri ambaye ni mwelewa na anaifanya kazi yake vilivyo kwa kuhakikisha anamsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua sekta ya viwanda na biashara ndiyo *engine* ya uchumi wa Taifa letu. Kwa namna hiyo mimi ninatamani kuiona sekta ya viwanda na biashara inaendelea kufanya vizuri hasa kuhakikisha inatengeneza viwanda au inatawanya viwanda ndani ya mikoa yetu kutokana na rasilimali zinazopatikana katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu viwanda vingi vimekuwa vikilundikwa sehemu moja, ukienda pale Dar es Salaam, ukienda Pwani, ukienda Tanga kuna viwanda; lakini kuna maeneo tofauti tofauti ya nchi yetu ndani ya mikoa yetu ambayo tunaweza tukatawanya viwanda na vijana

wakapata kazi huko huko kwenye mikoa yetu kulingana na rasilimali zinazopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pale Mkoa wa Mara hakuna viwanda, kulikuwepo na viwanda kipindi cha nyuma kulikuwa na Kiwanda cha *Mutex*, kulikuwa na Kiwanda cha Samaki, kulikuwa na Kiwanda cha Maziwa lakini kulikuwa na viwanda mbalimbali mpaka hivi sasa ninavyoongea hakuna kiwanda hata kimoja kinachofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mara kuna rasilimali za kutosha, sisi tuna ziwa lakini sisi ni wafugaji, lakini sisi ni wakulima Mkoa wa Mara, lakini bado sisi ni wachimbaji wa madini. Unapotawanya viwanda vya maziwa, vya samaki na vya madini tunatengeneza ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mlundikano wa kutoka mikoani na kwenda pale Dar es Salaam, kwenda Tanga, kwenda Pwani, hautakuwepo bali tutaendelea kuwekeza kule. Kwanza, tutainua pato la mikoa yote ambayo tumewekeza, lakini pato la mwananchi na pato la mtu mmoja mmoja ili kusudi waweze kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua Mheshimiwa Waziri ni msikivu, ninaomba aangalie maeneo kulingana na rasilimali zinazopatikana aweze kupeleka viwanda. Ukiangalia pale Tarime Mjini ni mji ambao umechanganyika na watu wengi, kuna mpaka Wakenya lakini pia kuna rasilimali za kutosha, akitengeneza pale *Special Economic Zone* pale Tarime Mjini atakuwa amewasaidia sana wananchi wa Mkoa wa Mara, wananchi wa Tarime kwa kuwekeza pale *Special Economic Zone* na pale Musoma Mjini vivyo hivyo, lakini pia na Bunda na maeneo yanayozunguka pale Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo nikiwa ninamaanisha watu wengi sasa hivi wanatamani wajiinue kutokana na rasilimali walizonazo, wajiinue kutokana na viwanda vitakavyotengenezwa. Tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema vizuri kwamba anakwenda kuweka kongani za viwanda kwa kila wilaya. Sasa kwa mantiki hiyo

twende tukaweke ili kusudi tusiandike tu kwenye makaratasi bali twende kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo sasa ninaomba niwapongeze Wakala wa Vipimo *(WMA)*. Tumewaona mara nyingi wakipima mita za maji, hiyo inamgusa mwananchi, wakipima mita za umeme, zinamgusa mwananchi, lakini wakienda mpaka kwenye pampu za mafuta zinamgusa mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuniambia hao ni akina nani? Mimi nitasema hao ni marafiki wa wananchi hivyo tunatamani hawa marafiki wa wananchi waendelee kupewa nguvu na ninawaomba Wakala wa Vipimo *(WMA)*, waende sasa moja kwa moja kwa kupima muda wa maongezi; hii imekuwa ni changamoto kubwa kwa wananchi wetu. Sasa hivi mwananchi anaweka labda bando la shilingi 2,000 anaambiwa siku saba, ni siku moja tu anaambiwa bando limekwisha. Kwa hiyo, tukitumia hivyo vipimo vitatusaidia sana na mwananchi atajua kwa muda huu ninaoongea niko sahihi kwa sababu bando langu limekwisha kihalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea ninaomba pia niwaombe hawa Wakala wa Vipimo, wamekuja na mfumo mmoja wa kuendelea kupima kitu kinaitwa lumbesa, ninafikiri wanalifahamu hii. Hii imekuwa ni changamoto hasa kule vijijini na hapa niwapongeze kwanza wamefanya vizuri, wamefika ndani ya mikoa saba na ndani ya mikoa saba wamefanya vizuri; bado baadhi ya mikoa hawajafika washushe elimu ili kusudi ile elimu iwafikie wananchi. Hapa ninaomba washirikiane na Wizara ya Kilimo, TAMISEMI ili waweze kuhakikisha mazao yote yanapita kwenye vipimo na hapa tutakuwa tumemsaidia mwananchi, lakini tumesaidia na halmashauri zetu ziweze kupata pia mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwapongeza sana sana Wizara hii kwa namna wanavyofanya. Mimi kama Mjumbe wa Kamati nimeenda kutembelea Kiwanda cha *Neelkanth* pale Tanga ni kiwanda kinachofanya vizuri sana. Changamoto waliyonayo baada ya kuwa sisi tumewaita wamewekeza fedha

nyingi sana pale na wamenunua mitambo miwili ya zaidi ya 5,000,000,000. Mtambo mmoja unafanya kazi, mtambo mmoja umefungwa; nilisikitika sana na umefungwa kwa sababu uzalishaji umekuwa mdogo, kemikali inayozalishwa inatoka nje ya nchi na inatoka nje ya nchi bila hata ya kuwekewa *VAT*, haina *VAT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoweza kumwomba Waziri, lakini kuiomba Serikali yangu iangalie ni namna gani inaweza kuwalinda hawa wawekezaji wa ndani, kusudi wanapowekeza basi waone manufaa ya kuwekeza kwenye nchi yetu, tofauti na hapo tutawapoteza, watafunga biashara hatutawasaidia. Ni pamoja na kuendelea kuwalinda wafanyabiashara wa ndani, wafanyabiashara wa ndani wanapata changamoto kubwa sana. Ninaona umewasha taa ukiamini kwamba muda wangu umekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chomete. Nimtaje Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel, atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

MHE. MAGRETH B. EZEKIEL: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia ningependa kwa kuanza kusema yafuatayo; "Tanzania, Tanzania, Nchi yangu Tanzania nakupenda kwa moyo wangu wote, jina lako ni tamu sana, nilalapo nakuota wewe na niamkapo ni heri mama we, Tanzania, Tanzania nakupenda kwa moyo wangu wote."

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza wajibu wake kama kiongozi wa kutupa maono (*vision)* ya kitaifa 2050 inayotuonyesha ni nini tufanye ili kupata maendeleo ya Taifa letu. Pia, ningependa kumshukuru Makamu wa Rais Mheshimiwa Balozi

Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuendelea kutukumbusha sisi vijana kila iitwapo leo kwamba tuna wajibu thabiti wa kulitumikia Taifa kuhakikisha uchumi wetu na biashara zetu na hali na ustawi wa Watanzania kwa ajili ya masilahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda vilevile kumshukuru Waziri Mkuu kwa sababu katika kila harakati anazopata za kuongea na Watanzania na kutatua kero zao, kipaumbele chake kimekuwa kuelewa hali halisi ya maisha ya Mtanzania na namna gani hizo suluhu zitaenda kuleta wepesi wa yeye kuendelea na maisha yake. Vilevile, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, dada yangu Mheshimiwa Judith Kapinga, kiukweli amekuwa ni mtu ambaye ni mwalimu mzuri sana kwangu wa biashara na uongozi na si hivyo tu ni mtu mwenye ubunifu na maono mapana na makubwa ya kuleta mapinduzi makubwa ya biashara na uchumi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru na kumpongeza vilevile Naibu Waziri kaka yangu kwa kuwa yeye pia na Wizara nzima ya Viwanda na Biashara ni watu wenye weledi na ufahamu kwamba tunaishi katika nyakati gani za *geopolitics and geoeconomics*. Waheshimiwa Wabunge, wote mimi nimeanza kwa kusema: "Tanzania Tanzania nchi yangu Tanzania nakupenda sana" kwa sababu tunaishi katika dunia ambayo ulinzi wa Taifa upo katika uchumi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kuomba ni kwamba bajeti hii, nitaunga mkono kwa asilimia mia moja, lakini kama kijana wa Taifa hili bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara inapaswa iongezwe na inapaswa kuwa ni bajeti kubwa kuliko bajeti nyingine katika nchi yetu na ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunaishi katika dunia ambayo *we need to survive*. Zamani kwenye *theory of evolution* kulikuwa na *evolvement of human species* kutoka kwenye nyakati mbalimbali na *that time DNA,* ndiyo ilikuwa kitu kinacho-*stand* kwa sababu sisi humo wote tuliopo ni *product* ya *natural selection* kwamba *genetics* ambazo zina nguvu zinaweza ku-*survive the test of time*. Vilevile, tunaishi kwenye dunia ambayo tunahitaji

DNA ya *business and economics* na *DNA* yetu ya *business and economics* tunapata katika mlango gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata katika falsafa ya kuelewa kwamba maendeleo ya nchi, uchumi na biashara ya nchi yetu haiwezi ikaja ndani ya siku moja. Leo tutambana Mheshimiwa Waziri na kumwambia mambo mengi, lakini tuna jukumu tunapokaa katika Bunge hili si kujadili biashara na uchumi wa leo bali kujadili uchumi na biashara ya nchi yetu miaka 10 au 20 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo ninamaanisha nini? Ninamaanisha kwamba kwa vijana wetu wa Kitanzania tunapaswa kuelewa hesabu ya uchumi. Hesabu ya *GDP* ni *population times labour times production,* lakini vilevile ukienda kwenye hesabu ya mafanikio yaani *in terms of national success* tunaongelea suala la *vision plus execution times consistency,* lakini vilevile tukienda kwenye *index* nyingine ya uchumi inaongelea *population*, *productivity, infrastructure* na *innovation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda zaidi kwenye kutengeneza *wealth* tunaangalia kitu kinachoitwa *capital times time, times compound growth.* Tunachokosa kwenye Taifa letu ni *value addition* ya *compound growth;* leo mfanyabiashara anatumia miaka 20 kutengeneza biashara, lakini akifa amekufa na ujuzi wake, amekufa na biashara yake, amekufa na mtaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vijana wetu wa Kitanzania uzalendo mkubwa ni kulitumikia Taifa kuhakikisha uchumi na biashara na uendelevu wa sisi kama Watanzania na hilo tutalipata vipi? Tutalipata katika kuhoji na kuwa na maswali sahihi kwa Serikali yetu. Mapinduzi ya kiuchumi yanapaswa kufanywa na sisi vijana na siku zote tunasema *change is inevitable* haijalishi utakubali, haijalishi utakataa, lakini tunapaswa kuelewa kwamba mabadiliko yanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile watoto wanavyokaa na wazazi wao wanakwenda ku-*present business ideas* ni vilevile tunapaswa kufanya kazi na Serikali yetu. 60% ya Waheshimiwa

Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri, ninamkumbuka baba yetu Vangimembe Lukuvi aliwahi kuniambia mimi maisha yangu yote nimeitumikia nchi yangu. Vilevile, sisi tunapaswa kuwa na utashi, tumeingia katika *age* ya *super intelligence* na ukuaji wa kiuchumi kwa mataifa mengine, tutumie teknolojia. Tunapoleta mapendekezo yetu na Serikali inapokea na mengine tunaambiwa tusubiri, hatujaambiwa hapana tumepewa muda wa kutengeneza ramani kwa ajili ya maendeleo yajayo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kugusia ninataka kuongea na jamii zetu na familia zetu kwa wazazi wengi kwa Taifa letu, tumeweka desturi pale ambapo mtu anaoa au anaolewa anachangiwa pesa na jamii nzima; huyu shangazi atatoa, mjomba atatoa, kila mtu atatoa kitu Fulani, lakini kwa nini tusipunguze hiyo michango ya harusi tukafanya *early investment* kwa vijana wetu? Kwamba badala ya kunichangia mimi Magreth milioni 30 au 50 kwenye harusi yangu kwa nini ninapotoka chuo mzazi wangu au jamii yangu isichangishe…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MAGRETH B. EZEKIEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba dakika moja nimalizie; kwa nini familia na jamii isinichangie katika kutengeneza hiyo biashara na kampuni na kesho au kesho kutwa itakuwa na maslahi mapana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi na Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali ajiandae.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara. Awali ya yote, ninaomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Wizara husika na Waziri na Naibu wake na timu nzima. Kitu ambacho kinatia faraja ni kuona Liganga na Mchuchuma

hatimaye ime-*mature*. Kwa hilo wanastahili pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wakati yupo kwenye *summit* ya *Nuclear Energy*, Rwanda aliongelea kuhusiana na suala la *energy* kwamba tutaongeza megawati, lakini tutatumia pia *nuclear* na hilo jambo tunastahili kumpongeza, ana maono ya mbali. Kwa kuwa bila nishati ya umeme hakuna kiwanda, hakuna kiwanda kabisa. Kwa hiyo nitoe pongezi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma agano jipya (Biblia) na nikasika sehemu moja ilikuwa kwenye Luka 17:11-19; Yesu alienda kwenye kijiji kimoja akakutana na wananchi kama 10 walikuwa wanaumwa ukoma, wakamwomba awaponye na wakapona, lakini aliyerudi kwenda kumshukuru alikuwa mmoja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasimama hapa kushukuru wakati *session* hii ya bajeti inaendelea kuna vitu mimi niliviomba kwenye Bunge lako Tukufu; niliomba shule kidato cha tano na sita Nanguruwe, tumefanikiwa. Kuna mradi wa maji Shilingi 222,000,000 kupitia Wizara ya Nishati *(TPDC)* tumefanikiwa; tulikuwa na barabara mbovu ambayo ilikuwa inaelekea Msimbati, *TANROADS* wanaiboresha. Sisi, Wananchi wa Mtwara Vijijini tunasema *Alhamdullilah Rabil Alamin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 Mtwara iliahidiwa tutakuwa tumepewa kiwanda cha mbolea 2016, kampuni ilikuwa inaitwa *Helm* ya Kijerumani ilikuwa tayari kuwekeza Dola za Kimarekani 2,000,000,000, Kata ya Msangamkuu na hekta 400 zilikuwa zimetengwa pale, lakini hiyo mipango ilikuwa kwenye makaratasi haiku-*mature*. Sasa ninaomba nikumbushe kwamba kuna mwekezaji mwingine pia anataka kuwekeza kwenye kiwanda cha mbolea na yeye yupo tayari kuwekeza Dola za Kimarekani 627,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda amwangalie huyo mwekezaji maana yake asipopata *raw material* atakimbilia Ethiopia, kwa hiyo nisisitize sana hilo. Pia, kuna

mwekezaji mwingine ambaye anataka kuweka *gas to liquid*, kuchakata gesi kwenda kwenye *diesel*, kampuni ya *Rocky Mountain* na yeye anataka kuwekeza kiwanda hicho Mtwara. Kwa hiyo, niombe sana, la sivyo hao wawekezaji watakimbia na hivyo viwanda havitajengwa. Ni ahadi ya viongozi wengi sana waliopita kwamba gesi itakapotokea Mtwara *as a raw material* viwanda vitamwagika pale, Mtwara itabadilika kuwa Dubai, bado hiyo Dubai hatujaiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee suala lingine la riba. Mfanyabiashara yeyote ambaye anataka kuanzisha biashara au kiwanda ataangalia *capital*. Sasa ninaomba niongelee uhalisia, Wizara ya Fedha, *CBR* ni *Central Bank Rate*, riba kuu ya *BOT* ni asilimia 5.75 ambapo taasisi za kifedha huwa zinaenda zinakopa pale, lakini twende kwenye uhalisia, Tanzania tunayo makundi matatu, moja ni wafanyabiashara, wakulima na watumishi wa umma. Sasa angalia hizi *interest rate* wanazopata hawa watu. Ukimwangalia mkulima anapewa *single digit,* asilimia tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwangalia mfanyabiashara anapewa 14% mpaka 20% na ukimwangalia mtumishi wa umma naye anapewa 14% mpaka 20%. Sasa tujiulize, *where is that fairness?* Kwanza hapo hakuna *fairness.* Tuangalie tulete usawa, riba hizo zipungue. *BOT* inatoa 5.75, taasisi za kifedha angalieni, tuje kwenye *single digit,* ili watu waweze kupata mikopo ya riba nafuu na tuweze kujiendeleza. Tufanye ustawi kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia na hili, ninaomba nitoe ushauri tu; simu hizi ukiziangalia vizuri zina *semiconductors,* zina *capacitors*. *Raw materials* za kutengeneza vitu hivi, nchi hii tunazo na nitatoa mfano wa uhalisia mdogo tu; *South Africa* wamewekeza kwenye *tech factories* na huwezi amini, karibu shilingi trilioni 13.5 ndiyo fedha inayozunguka pale na inasaidia kwenye pato lao la kitaifa kwa 12.5%. Kwa hiyo, *it's high time* sasa hivi tujikite huko kwenye *tech factories* kwa sababu, ndiyo ulimwengu unaelekea huko. Sisi tumebakia kwenye viwanda hivi hivi vya mabati, misumari na nondo. Tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya muda, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Nimemtaja Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas ajiandae.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza, ninaomba niwapongeze sana Watendaji wa Wizara hii na nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutupa vijana ambao hawajui kusinzia, ambao siku zote utawaona Tanzania nzima wakizunguka, wakizindua na kukagua miradi mbalimbali. Hawa ni Mheshimiwa Judith pamoja na Dennis Londo. Mungu awabariki, kazi yenu ni nzuri sana na awatie nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza ni kuhusu fedha zinazotolewa katika Wizara hii. Bunge lako kipindi kilichopita lilipitisha fedha za maendeleo, siku zote ninaangalia fedha za maendeleo kwa sababu, fedha za matumizi mengine watu wataendelea kulipwa mshahara. Fedha za maendeleo zilizopitishwa zilikuwa shilingi 41,887,535,000, lakini mpaka Februari ilikuwa zimepitishwa shilingi 20,377,218,432.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli kutokutoa fedha katika Wizara hii ni hatari sana. Leo Waziri amesimama hapa, ameliomba Bunge lako Tukufu apitishiwe shilingi 33,690,103,000, hii ni pungufu kuliko bajeti iliyopita. Bajeti iliyopita fedha hazikutolewa zote, lakini leo ameomba pungufu ya zaidi ya 19.7%.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara ambayo tunaitegemea. Ni ya kimkakati ya kukuza uchumi, ili tuweze kufikia malengo ya Dira ya 2050. Kwa namna hii tunafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo tunaitegemea kukuza ajira na uchumi. Wizara hii ndiyo tunaitegemea tufikie malengo ya Liganga na Mchuchuma. Kwa fedha hizi, tunatarajia *KMTC, TIRDO, TEMDO* na *CAMARTEC* ziweze kusimama na kufanya

kazi zake zenyewe kibiashara kwa sababu, bado tuna Bajeti ya Taifa. Tuone uwezekano wa kuiongezea Wizara hii, ambayo ni moyo wa uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu kulinda biashara za wazawa na viwanda vya ndani. Ni kweli, biashara za ndani pamoja na viwanda vimeshindwa ushindani na changamoto kubwa ni hii ya kuingiza vifaa vya viwandani na *products* za viwandani kutoka nje kwa bei ndogo. Ukiangalia gharama ya kuzalisha vitu ndani ya nchi yetu ni kubwa; gharama za umeme na tozo nyingi, hebu tuwasaidie. Watu wametoa mfano mmoja wa kiwanda kama hicho kinachotengeneza malighafi, kwa ajili ya kutengeneza simenti. Tunataka simenti ipatikane kwa bei ndogo, ili wananchi wetu wajenge makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kama hicho cha *Neelkanth,* sisi Tanzania mahitaji yetu kwa ajili ya *raw materials* ni tani 5,549,901, lakini uwezo wa kusindika wa kiwanda kimoja unafikia tani 7,000,104 na zinashindwa kufanya kazi kwa sababu, bidhaa zenye *quality* kama hiyo zinaingizwa ndani ya nchi kwa gharama ndogo kabisa. Ninaiomba Serikali yanapotokea mazingira kama hayo, kwanza wachukue ushuru wa forodha hata zaidi ya 25%, wa *tax VAT,* wachukue *excise duty*, ili kwamba, gharama za kuingiza aidha, zilingane au ziwe juu ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi. Viwanda vyetu vya ndani ni sharti vipatiwe nishati tena kwa bei nzuri kwa sababu, wanashindwa uzalishaji pamoja na miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu *TANTRADE*. *TANTRADE* ni maonesho ya wafanyabiashara, kama ilivyo Nane Nane na ni jukumu muhimu sana kwa wafanyabiashara. Katika jukwaa hili wafanyabiashara mbalimbali wakikutana wanapata *exposure,* wanajifunza kutoka kwa wengine, lakini wanapata soko la kupeleka bidhaa zao. Sasa hii ingeboreshwa, kama ambavyo kwa kweli, Waziri amesimamia maboresho mengi yamefanywa, ikiwemo digitali ya kuomba fursa ya kuingia kwenye maonesho kwa kufanya *booking online* pamoja na mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiomba ni maonesho haya yafanyike sawa na maonesho ya Nane Nane, yafanyike katika kanda zote, yasiwe *centered* Dar es Salaam pekee yake. Yafanyike Njiro kwenye uwanja wa Nane Nane, yafanyike hapa Dodoma; hapa Dodoma tuna *experience,* kuna kitu kinaitwa *Syria Exhibition,* ambayo mara nyingi wanaonesha maonesho yao hapo *Area C* kwenye ukumbi wa vijana. Ni fursa nzuri sana kwa wafanyabiashara kwa hiyo, ninaomba katika kanda zote maonesho haya yafanyike, ili kukuza biashara ya wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni *FCC,* hii ni Tume ya Ushindani. Wameongea wenzetu, *FCC* inatakiwa ilinde biashara ya ndani na ilinde afya ya walaji wa Tanzania. Tumesema kuna biashara kwa mfano, wenzetu Wachina kuja kufanya biashara ya umachinga siyo sawa, si ushindani kwa wafanyabiashara wetu wa ndani. Vijana wetu wakafanye kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu *FCC* watusaidie sasa kuona ushindani wa wenzetu wa nje kuja kufanya biashara namna gani ndani na kulinda afya ya walaji, nchi yetu imekuwa dampo. Kuna bidhaa zinaingizwa huku, kwa mfano mitumba; kuna mitumba ya nguo inaletwa huku imechoka; kuna mitumba ya vifaa vya ndani, kuna sufuria, vikombe, sahani, zimechoka; kuna friji zimechoka hadi zinakutu, nyingine hata mende unaweza ukakuta. Kwa nini *FCC* isitusaidie kutupa heshima sisi Watanzania? Kuondoa hizi bidhaa sokoni kwa sababu zinaharibu ushindani huku ndani!

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu *WMA,* wanafanya kazi nzuri sana na tumeona mabadiliko. Kwa mfano, wakulima pamoja na vyama vya ushirika sasa hivi wamekubali kwenda kutumia mizani. Wametusaidia hata mizani ya barabarani kulinda barabara zetu na kila kitu na tumeomba sasa hivi *TANESCO*, Wakala wa Maji na Mamlaka ya maji, hizi zabuni mnazozitoa kwa *supplier* wa kuleta hizo *meter,* hakikisheni zimepita kwa *WMA,* ili…

(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, unga mkono hoja.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

MHE. HAIDERALI H. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Allah *(S.W.T)* kunijalia afya njema, ili niweze kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu. Ninachukua nafasi hii kukushukuru kunipatia nafasi niweze kuongea machache, ili tuweze kujenga nchi yetu kwa pamoja, lakini nina kila sababu ya kumpongeza jemedari wetu Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye amesimama kila wakati na Watanzania kipindi cha shida zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka vizuri kabisa nchi hii ilikuwa na uhaba wa sukari, lakini mama alitoa msamaha wa kodi na akahakikisha sukari inafika, ili Watanzania waweze kunufaika na zao hilo. Isitoshe kikatokea kipindi ambapo kulikuwa na uhaba wa mafuta, bei ikapanda sana; akaweza kwa makusudi kabisa kusamehe kodi na tozo mbalimbali, ili bei ya mafuta iweze kushushwa. Hayo yote yanahitajika dira kubwa na Watanzania wala hawajakosea kumpa kura 98% na ushee kwa sababu, anastahili na hao walioisoma namba tunawakaribisha kwa heshima zote tujenge nchi yetu pamoja sasa, Chama Cha Mapinduzi kina Serikali tawala tayari madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana dada yangu, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Judith, *you have done a very great job. Well done!*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemshuhudia, tumemwona na wafanyabiashara wamempokea kwa mikono miwili. Dada yetu hajapumzika, kutoka siku ametangazwa unaona anafanya ziara za kila aina; yupo katika viwanda, yupo katika biashara, viwanda mbalimbali tumemshuhudia. Ninachukua pia nafasi hiyo, pamoja na kumpongeza kwamba, kuna mahali nina kiwanda hapa hapa Dodoma, ninamkaribisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha msamaha wa kodi ya *VAT* kwenye kiwanda cha kuzalisha na kukamua mafuta ya alizeti, lakini msamaha huo unatolewa kwa mwaka mmoja tu, hiyo ni changamoto. Ni changamoto kwa sababu, kiwanda kikitengenezwa, kukijenga, kukikuza na kukileta mpaka kifike hapa nchini inaweza ikachukua zaidi ya miaka miwili; hatua hii ilichukuliwa makusudi, ili iweze kulinda zao la alizeti na wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yamefanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, ili kulinda Watanzania na wajasiriamali waweze kunufaika na viwanda vidogovidogo, pamoja na vikubwa, waweze kuzalisha na kutumia kilimo chao wenyewe na kukikuza. Ninaomba kwamba, angalau msamaha huo ungetolewa kwa miaka mitano, ili wawekezaji waweze kuji-*program* vizuri na waweze kuendeleza sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ninamalizia. Kama tunavyojua wote kwamba, halmashauri zetu zinatoa 10 ya mkopo kwa vijana, wanawake na walemavu. Sasa, mkopo huu mara nyingi vikundi hivyo kuna wengine wanarudisha, wengine hawarudishi; kwa mfano, kwetu Ilongero tumeweza kutoa shilingi 330,000,000 mwaka huu, lakini halmashauri nyingine zimetoa zaidi kufuatana na mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishauri Serikali kwamba, badala ya kutoa fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara ingeweza kukaa na makundi hayo, tungekuwa na *program* maalum, tuweze kuwanunulia mashine au uwekezaji wa aina yake, ili fedha za Serikali zibaki mikono salama na wao waweze kukuza biashara zao na kodi ya Serikali iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, ninaomba nikushukuru sana. Ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga ajiandae. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi, aliyenipa uhai siku hii ya leo, niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninapenda kuwapongeza viongozi wa Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa kwa juhudi zao mbalimbali wanazofanya kuhakikisha sekta zao zote zinafanya kazi kwa uaminifu na uadilifu. Napenda kuchukua fursa hii fupi kupongeza sana taasisi hizi ikiwemo *SIDO*, ikiwemo *TBS*, *CAMARTEC* na taasisi nyingine kama vile *TANTRADE, TIRDO, TEMDO* na *BRELA*. Mwisho sijawasahau stakabadhi za ghala ambao juzi tu wametimiza miaka 20 katika kufanya kazi zao, ambapo kazi hizo zinawasaidia sana wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kwa mfano, taasisi hii ya *WMA* inahitajika nchi nzima ifanye kazi kuwasaidia wananchi huko waliko kwenye vijiji kwa sababu, uwezo wa kufanya hivyo na utaalamu wanao. Taasisi hii inaonekana umuhimu wake, kinachohitajika ni kuwaongezea watumishi na rasilimali fedha, ili waweze kuwafikia wananchi vijijini huko waliko waweze kufanya kazi zao. Kwa mfano, inahitajika kupimwa mita zote za maji na mita zote za umeme, kazi hii tunawapongeza Wizara ya Maji; mita za maji zinapimwa, lakini mita za umeme bado kuna changamoto. Kuna haja sana sasa watu wanaoshughulikia mambo ya umeme kuhakikisha zile mita kabla hawajamfungia mwananchi inakuwa imepimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana *CDE* kwa juhudi na ubunifu wanaoufanya. Tunawapongeza kwa jengo la ghorofa 10, ambalo wanalijenga kule, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu, uwekezaji ni muhimu katika Taifa. Tunahimiza kila siku tuwe na wawekezaji wa kutosha wenye maslahi ya kuwasaidia wananchi, ya kuwekeza kwenye viwanda na mambo mengine. Anapoanza mtu mmoja au mwekezaji mmoja akafanya vizuri na akaona ule

uwezeshaji anaoupata kwa taasisi na Serikali ndiyo na wengine wanafuata, wanakuja kuwekeza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna changamoto nyingi kwa wawekezaji kwenye masuala ya viwanda, lakini ninasema moja tu, kuna kiwanda kikubwa kule Tanga kinatumia malighafi za ndani ya nchi. Kina uwezo wa kuzalisha *metric ton 30,000* kwa mwaka, lakini mahitaji yetu ya ndani ya nchi ni kati ya *metric ton 20,000* na *24,000* tu. Kuna haja gani ya kuagiza kutoka nje? Wakati wanao uwezo zaidi wa kuzalisha na ziada na wakauza nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utakuta mitambo imekaa haifanyi kazi, watumishi wale wamekaa hawafanyi kazi na kwa sababu hiyo sasa, wanakosa kuongeza idadi ya vijana wa kuwaajiri. Mitambo ile miwili ingefanya kazi kwa wakati mmoja, ongezeko la vijana wanaohitaji ajira lingekuwa kubwa na tungepunguza kwa kiasi upungufu wa ajira katika nchi. *Calcium bicarbonate* inasaidia kuzalisha kwenye mambo ya plastiki na mpira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea na mchango wangu; bidhaa zinazoingizwa kutoka nje. Bidhaa hizi zinazoingizwa kutoka nje ni lazima sasa wale wawekezaji na wafanyabiashara ambao wanakuja kufanya hizi biashara ambazo nyingine hata mwanafunzi wa darasa la saba anaweza kufanya au wananchi tu wa kawaida, tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili halihusu Wizara ya Biashara pekee yake, linahusisha taasisi nyingi ambazo ikiwemo uhamiaji, uwekezaji na taasisi nyingine ambazo zinamfanya yule mgeni kuwekeza hapa na kufanya biashara. Kwa hiyo ni lazima hizi taasisi zikashirikiana kuhakikisha, hadi leseni inatoka ametimiza vigezo na masharti yanayohitajika ili kutoa fursa kwa wananchi wetu waweze kuwekeza, waweze kufanya biashara, waweze kuuza vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kupitia mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha ile changamoto kubwa, lile jambo lililokwama kwa

muda mrefu wa Liganga na Mchuchuma sasa linakwenda kupatia ufumbuzi wa uhakika. Ninawapongeza sana Wizara ya Biashara kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kuanzia watangulizi wao waliopita akina Mheshimiwa Jafo na sasa dada yangu pale kuliendeleza hili na sasa linafikia ukingoni. Ni jambo kubwa sana na ni jambo la kupongezwa na ndiyo hayo mambo anayoyataka Mheshimiwa Rais kuweka tabasamu kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la Liganga na Mchuchuma litakwenda kuweka tabasamu kwa sababu tutapata malighafi, tutaongeza uchumi, tutapata fedha za kigeni na fedha za kigeni zitaongeza dawa kwenye hospitali. Vilevile, tutajengea zahanati. Tunakwenda kujikomboa kiuchumi kwa hakika kabisa. Hili ni la kupongezwa kwa nchi yetu, tumepiga hatua kubwa sana kimaendeleo. Hapa la kufanya ni kusisitiza na kuhamasisha zaidi, jambo la mwisho la kuweka saini likamilike. Haya mambo yaanze kufanyika kwa maslahi ya nchi na wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa; viwanda vinasaidia kutatua changamoto ya ajira kwa vijana; biashara inakwenda kutatua changamoto ya ajira kwa vijana, lakini pia kupitia viwanda tunapata masoko ya uhakika kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Ni vyema sasa tukaangalia kwa karibu zile changamoto za kodi, za tozo na malipo mbalimbali, kuhakikisha kwamba zinafanyiwa kazi ili kiwe kivutio kwa wawekezaji wa ndani waweze kuwekeza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, si vibaya wahitimu wetu wa vyuo mbalimbali ambao wamepata ujuzi wa kutengeneza vitu mbalimbali, ni vyema sasa tukatafuta namna ya vijana hawa kukopesheka ili waanzishe viwanda vidogovidogo kama vya watu 10/10, 20/20 kutokana na ujuzi wao ili tuweze kukwamua hili tatizo la ajira linalotukabili ndani ya nchi kwa maslahi ya vijana wetu, kwa maslahi ya nchi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Devotha Daniel na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Ijumaa wakati ninachangia Wizara ya Maliasili na Utalii nilikuwa *so stranded,* lakini leo ninachangia nikiwa na nuru yenye furaha. Wananchi wangu wanavuna kwenye Jimbo la Katavi siasa imetulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Mheshimiwa Rais huyu amefanya mageuzi makubwa sana upande wa viwanda. Leo ukipita Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine viwanda vinaota kama uyoga. Mheshimiwa Rais, popote alipo tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimpongeze Waziri, dada yangu Judith Kapinga. Ninampongeza sana dada yangu kwa kazi nzuri anayoifanya. Wakati anateuliwa, moja ya watu waliokuwa na mashaka kidogo ni mimi, lakini ameni-*surprise;* anafanya kazi nzuri sana dada yangu. Hongera sana. Kazi yetu sisi Wabunge ni kumuunga mkono na kuendelea kumwombea kwa Mungu afanye kazi, atimize wajibu wake. Yeye na Naibu wake, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu wa tatu wa kumpongeza kwenye Wizara, ndugu yangu, Katibu Mkuu Waziri. Ninampongeza sana, anafanya kazi nzuri. Sisi ndugu zake tuna imani kubwa sana naye. Tunaamini, kazi yetu kubwa nyingine ni ya kuendelea

kumwombea. *Shots* ni nyingi, lakini ninaamini atavuka, Mungu wa mbinguni atamsimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze alipoishia kaka yangu Mheshimiwa Shabiby. Wizara hii inafanya kazi kubwa sana. Kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Judith ataifanya na wananchi wa Tanzania watamkumbuka ni kulinda wafanyabiashara wa ndani. Leo kila sehemu unayokwenda, hatukatai wawekezaji wa kigeni; lakini wawekezaji hawa wanaokuja na *briefcase*, Mheshimiwa Judith apambane nao, ni hatari kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongea Mheshimiwa Ahmed Shabiby hapa, wanakuja na fedha ambazo hazizidi dola 500,000 ambazo mwananchi wa kawaida wa Kitanzania anaweza kuwa nazo. Ukienda kule Katavi kwenye madini wamejaa wenyewe, mitaji yao ni ya kawaida. Kila sehemu unayokwenda unawakuta wenyewe wamejaa. Hakuna kitu ambacho Taifa hili linaweza kumkumbuka dada yangu kama kulinda wafanyabiashara wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la pili walilonalo Wizara ya Viwanda; Wizara ya Viwanda ndilo eneo pekee linaloweza kutusaidia kupunguza tatizo la ajira kwenye nchi hii. Wahamasishe uwekezaji mkubwa wa viwanda kwenye nchi hii. Ninaamini tukifanya *proper investment* ya viwanda kwenye nchi hii ndani ya miaka mitano upungufu wa ajira utakuwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la tatu ni kuhusu Wakala wa Vipimo. Hawa wanafanya kazi kubwa sana, sana sana; lakini ninaomba nishauri wapanuliwe wigo, wafike mpaka kwenye huduma za mawasiliano. Huku kwenye huduma za mawasiliano kuna shida kubwa. Ameongea Mheshimiwa Ghati hapa, huku dada yangu awe *serious*, kuna makateli wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ananunua bando la wiki, ndani ya siku mbili bando limekwisha, anaongeza tena. Hajui vocha zimeenda wapi, hajui bando limeishia wapi. Hawa *WMA* wakifika na huku watakuwa wametusaidia ili mlaji apate kile

ambacho anastahili, tofauti na ilivyo sasa. Kwenye bando na vocha malalamiko ni mengi kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la nne ni kuhusu kuvilinda viwanda vya ndani. Ni lazima tukubaliane, kwamba bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje ambazo viwanda vya ndani vinaweza kuzizalisha ni lazima viwe na kodi. Ukija kwa mfano, kuna dawa ambazo zinaingia nchini, hizi wanaita *calcium carbonate,* viwanda vinavyozalisha bidhaa hizi hapa nchini viko zaidi ya vitano, kikiwemo Kiwanda cha *Neelkanth* cha Tanga. Wajumbe wa Kamati na Kamati imeongelea vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Mheshimiwa Waziri lazima aweke mpango wa makusudi wa kuhakikisha mwekezaji anapokwenda kuwekeza anategemea atapata *result*. Sasa hawa watu wakienda wanakuja kushindanishwa na bidhaa ambazo zimetoka nje hazina kodi hazina ushuru, wanagushi, wanafeli; matokeo yake wawekezaji watakuwa wanakuja, wanafungua viwanda mwisho wanaishia katikati wanaondoka. Tutakuwa hatumsaidii Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe dada yangu aje Katavi. Kule Katavi kuna viwanda vingi vya kati vinafanya vizuri sana. Tunafanya kazi kubwa kwenye hivi viwanda kwa ajili ya kufanya *value addition* kwenye mazao yetu. Hawa watu wanahitaji kujengewa uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam, Pwani na maeneo mengine viwanda viko vya kutosha, aje na huku pembezoni ili tunapojenga viwanda, hususan kwenye Jimbo la Katavi, tutawekeza vizuri na wale watu watawekeza vizuri, tutaondoa ongezeko la watu kutoka vijijini kukimbilia mijini kwa sababu kule napo kutakuwa kuna *infrastructure* na watu watafanya shughuli zao na manufaa yataonekana, tofauti na ilivyo sasa ambapo tuna *base* eneo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la nne na la mwisho, ninampongeza sana dada yangu, sana sana. Nimpongeze kwa kazi nzuri anayoifanya; lakini nimwombe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana...

MHE. THOMAS K. MAGANGA: ...apambane na hawa wafanyabiashara wa kigeni. Wanakuja na shilingi 200,000 baada ya shughuli zao kukamilika wanaondoka, wanatuachia vitoto havieleweki rangi gani, mwisho wa mwisho ni matatizo tu kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Devotha Daniel, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, ajiandae.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Pia ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumeona dhamira yake kwenye sekta hii ya viwanda na biashara. Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana dada yangu na rafiki yangu sana, Mheshimiwa Judith Kapinga, pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa waliyoifanya. Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wake, ninawapongeza sana. *You have done a very grateful job; I have seen you everywhere* wakitangaza viwanda na mimi ni mdau wa viwanda. Nimefurahi sana na ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nimwombe Waziri wa Viwanda; wananchi wa Mkoa wa Kagera wamenituma. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda; Mkoa wa Kagera tuna viwanda ambavyo vimekufa na viwanda hivi nitavitaja. Tuna kiwanda cha *TANICA* ambacho kinasuasua; tuna Kiwanda cha *BUKOP* ambacho tunaona kimekufa na matumaini ya wananchi wa Mkoa wa Kagera wanamwangalia yeye. Pia tuna kiwanda cha Pepsi, kiwanda hiki kilichangia uchumi mkubwa sana ndani ya Mkoa wa Kagera, lakini leo hii kiwanda hiki kimekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo pia kiwanda kule Maruku na hiki kiwanda ni kwa ajili ya chai. Kiwanda hiki ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera. Nimwombe, kwa sababu tunavyotengeneza viwanda, tunakwenda kutengeneza ajira za Watanzania na tunakwenda kuinua uchumi wa Mkoa wa Kagera. Kama tunavyofahamu, Mkoa wa Kagera ni mkoa ambao uko mpakani, umepakana na Uganda, Rwanda na Burundi na *DRC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe, kwa sababu mkoa wetu uko mpakani mwa hizi nchi na tumeona biashara kubwa zikifanyika, ukienda pale mpakani Murongo, utaona jinsi gani wananchi wanavyofanya *trade* na Uganda. Niombe sana sisi Watanzania tusibaki kuwa watazamaji kwenye hili suala; kwa sababu hii mipaka inabidi tutambue nini sababu inayosababisha upande wetu, hatufanyi biashara kama tunavyofanya Uganda, kama tunavyofanya Burundi na kama tunavyofanya *DRC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwomba sana Mheshimiwa Waziri, siku akipata muda twende Kagera tukazungumze na wawekezaji, wana hamu ya kumwona, wanamsubiri na wanamtamani. Hivi ninavyozungumza, Mkoa wa Kagera tunazalisha kahawa 50% ndani ya Tanzania. Kahawa hiyo tunao wazalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wazalishaji wa ndani ni Watanzania wenzetu, kama tulivyosema tuhakikishe kuwa hawa Watanzania wanafanya kazi katika mazingira mazuri. Tunafahamu kwenye biashara ya viwanda *what we need the more* ni *rates* ambazo zinakuwa nzuri kwa wawekezaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe jambo moja Mheshimiwa Waziri wa Viwanda. Tunafahamu kabisa kuwa tuna Benki ya Maendeleo. Hii benki ya maendeleo ya *TADB* ni benki ambayo imewekwa kwa ajili ya kuwasaidia wawekezaji. Niombe, tuwa-*finance* wafanyabiashara wa viwanda ambao tayari wamewekeza fedha nyingi kwenye viwanda hivyo vya kuchakata kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ninaomba niombe ombi moja ambalo nitamwomba sana Waziri wa Viwanda akisaidiana na Waziri wetu wa Mifugo na Uvuvi. Wananchi wa Mkoa wa Kagera wanamwomba Mheshimiwa Waziri atuletee kiwanda kwa ajili ya kutengeneza chakula cha samaki; kwani wananchi wale wamepata vizimba na vijana wako tayari kufanya biashara hiyo ya samaki. Leo hii wananchi hao wanakwenda Mwanza kununua chakula. Hii ina-*add cost* kwa biashara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, kwamba siku akipata muda Wabunge wetu wa Mkoa wa Kagera ni wachapakazi wataambatana naye ili tukainue uchumi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga hoja mkono na nimwombe aendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge jioni hii. Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tuna wanafunzi 89 na Walimu watano wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato ya Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula na Mheshimiwa Moses Charles Bujaga, ajiandae.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye aliwahi kusikika akitamka kwamba amechoka kusikia wimbo wa Liganga na Mchuchuma. Pia ninampongeza Mheshimiwa Judith Kapinga Waziri na Naibu wake na wasaidizi wake wote, akiwemo Katibu Mkuu na Dkt. Nicholaus Mkurugenzi wa *NDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii imekuwa ni wimbo wa siku nyingi sana; imesemwa sana. Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamesemea Liganga na Mchuchuma, waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Njombe wamesemea. Vilevile, nimepitia *Hansard* Waheshimiwa Wabunge wote walionitangulia Ludewa,

ambao ni tisa, wamesemea sana Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Wimbo huu sasa leo unakwenda kufika mwisho. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa jitihada na uzalendo mkubwa ambao wameuonyesha katika kupigania rasilimali muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unaongeza sana mapato ya kodi, mapato ya kodi ambayo ni *corporate tax*. Vilevile kupitia ule mrabaha tutapata mapato mengi sana kupitia kodi ya zuio, kupitia leseni za biashara, halmashauri itapata mapato mengi. Vilevile, tunapata fedha za kigeni nyingi sana ambazo zitakuja kuchangamsha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia tunaona kwamba Liganga ina tani 126,000,000 za chuma, lakini ndani ya chuma kuna *titanium* na kuna madini yanaitwa *vanadium*. Ukiangalia hii *titanium* inatumika kwa ajili ya kutengeneza vipuri vya ndege, *Airbus*, *Bombardier*, vifaa mitambo ya kijeshi lakini vilevile vifaa vya matibabu. Hii *titanium* bei yake ni zaidi ya mara 20 ya bei ya chuma chenyewe. Kwa hiyo, haya mapato yote yatakwenda kuchangamsha sana pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitachangia Sekta ya Viwanda, mchango wake kufika 36% kwenye *GDP*...

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

TAARIFA

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninataka nimpe kaka yangu taarifa kwamba, pamoja na faida nyingi alizozitaja uwepo wa makaa ya mawe na chuma yatatumika pia kwenye Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* kwa ajili ya kujenga vipuri na kuzalisha chuma kamili hapa nchini. Kwa hiyo badala ya sisi kuagiza chuma nje ya nchi tutaagiza

hapa kutokana na uwepo wa makaa na chuma cha Liganga na Mchuchuma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, unapokea taarifa?

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninapokea taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu nilizonazo Serikali ilikuwa inaagiza chuma chenye thamani ya 3,000,000,000,000 karibia kila mwaka. Tumejenga *SGR* tumeagiza chuma chote nje ya nchi, tumejenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, chuma tunatoa nje ya nchi. Kwamba chuma ndiyo msingi wa viwanda vyote hapa nchini. Chuma kilichopo kule hizi tani 126,000,000 kwa eneo dogo tu ambalo lilifanyiwa utafiti kinatosha kulisha viwanda vitakavyojengwa palepale Liganga, lakini vilevile viwanda ambavyo vipo hapa nchini; na chuma kingine kinaweza kikauzwa kama malighafi nje ya nchi. Hii itaingiza fedha nyingi za kigeni ambazo zitakuja kuchangamsha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huu vilevile utafanya vijana wetu wengi, Watanzania wengi waweze kupata teknolojia mpya na ya kisasa *(technology transfer)*; wale watakaoajiriwa pale; kwa sababu inaonekana kuna ajira zaidi ya 6,500 za moja kwa moja; Hii ni Liganga. Bado ile Maganga Matitu kuna ajira zaidi ya 1,000 ambazo zitakwenda pale, ambapo Watanzania mbalimbali wakiwemo wananchi wa Ludewa watakwenda kupata ajira; na tunajua kwamba ajira ni changamoto kubwa sana kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema pia kwamba chuma ndiyo msingi wa viwanda. Kwa hiyo utachangia mapato yanayotokana na viwanda kwenye pato la Taifa kuongezeka kwa 36% mchango wake kwenye *GDP*. Vilevile sekta ya madini mchango wake utaongezeka kwa asilimia kati ya mbili hadi tatu kwa sababu sasa hivi tumeshavuka 10% kwenye *GDP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mradi huu unao umuhimu mkubwa sana. Kwa hiyo, niwapongeze sana wenzetu wa Serikali kwa kuangalia *multiplier effects* za miradi hii na sasa inakwenda kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba sasa Wizara mbalimbali Serikalini zifanye mawasiliano ili Wizara ya Ardhi iende kule Ludewa ikaandae mpango kabambe *(master plan)* ya matumizi ya ardhi. Huu mradi ni mkubwa ambapo inakadiriwa zaidi ya shilingi 6,000,000,000,000 zitakwenda kuwekezwa pale (6.9 hadi saba). Kwa hiyo kutakuwa na mji mkubwa sana wa viwanda. Kwa hiyo, ni budi sasa Wizara ya Ardhi ianze sasa kwenda kuandaa *master plan* (mpango kabambe) wa matumizi ya ardhi ya maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kule kuna Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Bonde la Mto Ruhuhu kule Ibumi, Masimavalafu, Ngelenge – Ilela na Kipingu. Kwa hiyo, miradi kama hii itasababisha upatikanaji wa chakula cha kutosha kwa ajili ya kulisha wale watumishi watakaokuwa kule. Vilevile, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na yenyewe pia iweze kuandaa mipango kwa ajili ya ugeni mzito ambao utakuwa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi inalo jukumu kubwa sana la kuhakikisha zile barabara zinaboreshwa na kujengwa kwa kiwango cha zege kama ambavyo Serikali imeshaanza. Imeshakamilisha kilomita zile 50 za Mawengi hadi Lusitu, lakini vilevile sehemu ya Lusitu hadi Njombe imekwama kwa muda mrefu sana miaka karibia mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa kanisani kule padre mmoja ananiuliza kwamba sisi watu wa Ludewa tumeikosea nini Serikali? Kwa nini barabara inaachwa inakuwa na mashimo kiasi hiki, wananchi wanahangaika wanateseka. Kwa hiyo, maneno haya kutoka kwa viongozi wa dini ni mazito sana. Maana yake nini? Maana yake uwekezaji unavyokuja kuna mitambo mikubwa ambayo itapelekwa kule Liganga na Mchuchuma itahitaji barabara ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili bidhaa ziweze kutoka huko na kwenda kwenye masoko maeneo mbalimbali, barabara hii ninaomba Serikali iipe kipaumbele kwa sababu itakuwa na *multiplier effects* kubwa sana kwenye uwekezaji huu ambao unakuja Ludewa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na sehemu ile inayoanzia Mawengi mpaka Manda pale napo kilomita 111 napo Serikali itafute fedha ili wawekezaji waweze kuwa ni sehemu ya kivutio. Kwa sababu kuna wawekezaji wengine wako kule wanaitwa *HWTZ* nao wanahangaika umeme, umeme ambao unafika Ludewa hakuna kituo kile cha kupoozea umeme. Kwa hiyo sekta sasa ya nishati nayo lazima sasa tukae pamoja sekta zote serikalini tufanye mawasiliano na kuanza kujenga hizi barabara na kuboresha miundombinu ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Charles Bujaga na Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma ajiandae.

MHE. MARIAM A. MUNGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwapongeza sana Wizara ya Viwanda na Biashara kwa usimamizi mahiri wa sekta hii muhimu katika kukuza uchumi wetu. Sote tunafahamu kwamba biashara ndiyo moyo wa uchumi na ili tuweze kuendelea kufikia malengo yetu ya Dira ya *Vision* 2050, (Dira ya 2050) ni lazima tuwekeze zaidi au tuwekeze kwa ukubwa zaidi kwenye biashara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia katika maeneo mawili: eneo la masoko, lakini vilevile eneo la *research and development* au utafiti na maendeleo maeneo ambayo nadhani ni muhimu sana katika kukuza biashara ya nchi yetu na uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Nilivyokuwa ninamsikiliza kwenye hotuba yake alisema kwamba wanaanzisha Kitengo cha Utafiti wa Intelijensia ya Masoko. Ninapongeza sana hatua hii kwa sababu ninaamini hiki ni kitengo muhimu sana katika kutafuta masoko ya biashara zetu. Nilikuwa ninaomba kushauri kidogo yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo hiki kwa sababu tayari katika mashirika au taasisi ambazo zipo chini ya Wizara hii tuna Shirika letu au Taasisi yetu ya *TanTrade* (Mamlaka ya Usimamizi wa Biashara) na wale nadhani ndiyo wenye jukumu la kusimamia masoko. Kwa hiyo, ninaomba kushauri kitengo hiki kikiwa chini ya taasisi hii ya *TanTrade* itakuwa rahisi zaidi kwa sababu wao tayari watakuwa wana mifumo ambayo wanaitumia kwa ajili ya kutafuta haya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kushauri katika huu upande wa *TanTrade* wawezeshwe zaidi, lakini vilevile wapewe uhuru. Ninakumbuka hapo nyuma *TanTrade* ilikuwa ina kitengo cha biashara kwa nchi za nje walikuwa wanakiita *Trade Centres*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uingereza kwa mfano kutumia balozi zetu kulikuwa kuna ofisi pale ya *Tanzania Trade Centre*. Sina uhakika kama bado vipo kwa sababu sijavisikia kwa muda mrefu na wala sijafahamu vilikuwa katika nchi ngapi. Kwa hiyo, ninaomba kushauri kwamba kama tutarudisha zile *trade centres* zilikuwa zina umuhimu kwa sababu ilikuwa ni sehemu ya wafanyabiashara wale *locals* kukutana na wafanyabiashara wa Tanzania. Vilevile, bidhaa za Tanzania zilikuwa zikifika katika nchi kama Uingereza zikifika pale inakuwa rahisi kupata masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kushauri *TanTrade* ikirudisha hizo *trade centres* iweze kutumia Watanzania wanaoishi nje ya nchi kwa sababu wale wanakuwa ndiyo wanajua zaidi nini kinahitajika na masoko yanapatikana sehemu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kuipongeza sana Wizara kwa kuanzisha chini pia ya *TanTrade* nimeona wameanzisha ile *Brand Tanzania* (kui-*brand* nchi yetu nje ya nchi) kwa kutumia nembo ya *Made in Tanzania*. Hili siyo geni kwa

sababu linafanyika nchi nyingine Kenya wana kampeni yao ya *Make it Kenya*, South Africa wanayo kampeni kama hiyo na nchi nyingine tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi Tanzania tangu ile kampeni imezinduliwa, ninadhani mwishoni mwa mwaka 2024 imekuwa bado haijapata ile *momentum*. Ninaomba kushauri kwamba sasa ile kampeni isiishie tu Wizara ya Viwanda na Biashara, tuibebe iwe ni kama kampeni ya nchi nzima. Yaani tuhakikishwe kwamba kila kinachotoka hapa nchini hata kama ni pini, gunia kiwe kimekuwa *labelled* kwamba kinatokea Tanzania. Hii itasaidia sana hata tutakapopeleka biashara zetu katika soko huru la Afrika kujulikana zinatokea wapi na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nilikuwa ninaomba pia kushauri kwamba hatuwezi kukuza biashara bila ya kufanya utafiti na uchunguzi. Wizara ya Viwanda na Biashara pia ina taasisi ile inaitwa *TIRDO*. Sasa hii Taasisi ya *TIRDO* ni ya muhimu sana na ina vipaji (mimi niliwahi kwenda kuitembelea miaka mingi, miaka zaidi ya 10 huko nyuma). Pale *TIRDO* kuna vipaji na kuna wanasema nini, *innovation;* kuna uzinduzi mwingi sana. Nilikuwa ninaomba kushauri ile taasisi iwezeshwe zaidi ili iweze kukua lakini ifanye kazi kwa karibu na taasisi ambazo zinatafuta masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hii *TanTrade* sasa hivi kama tunavyofahamu dunia nzima tunaenda kwenye teknolojia hii ya akili mnemba. Kwa hiyo pale *TIRDO* tutakuwa tuna wataalamu ambao wanaweza kusaidia katika kutafuta au kutengeneza *systems* za masoko ambazo zitatumika na taasisi nyingine katika kutafuta biashara na hatimaye kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia hayo tu. Niipongeze sana Wizara tena kwa kazi nzuri wanayofanya. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yao, wanafanya kazi nzuri sana na wana majukumu makubwa ya kusimamia taasisi nyingi licha ya Wizara wanasimamia taasisi hizi zaidi ya 12 hadi 14 na wanaendelea vizuri. Kwa hiyo, sisi tunawapongeza na kuwatia moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Moses Charles Bujaga atafuatiwa na Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma na Mheshimiwa Rashid Habib Ali ajiandae.

MHE. MOSES C. BUJAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia. Kwa maslahi ya muda kipekee kabisa nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Judith, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Mheshimiwa Naibu wake ndugu yangu Mheshimiwa Londo kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia, pongezi zangu ziende kwa Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara Ndugu yangu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya uzalishaji ni vya muhimu sana katika uchumi wa Taifa lolote lile. Viwanda vya uzalishaji kwa Tanzania mpaka sasa hivi vinachangia pato la Taifa kwa asilimia saba mpaka nane. Watu wa uchumi wanatuambia viwanda vya uzalishaji, ajira ya mtu mmoja kwenye kiwanda cha uzalishaji inasaidia ajira zingine tano kwenye sekta zingine. Kwa hivyo inaonesha ni umuhimu kiasi gani sekta ya viwanda vya uzalishaji ilivyo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri ametoa hotuba yake jana ya bajeti sijamsikia anavyoweza kuunganisha sekta zingine za uzalishaji na kuongeza thamani hasa zao la pamba. Kule Mwanza, Shinyanga, Simiyu na mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa ni wazalishaji wakubwa wa zao la pamba na tumesema kwamba tutaanzisha kongani ya kuongeza thamani ya zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ekari 1,000 zimechukuliwa pale Wilaya ya Misungwi kwenye Bandari Kavu ya Fela na tayari ekari 300 zimekwishalipiwa fidia. Kwenye kongani hiyo tunatarajia tuwe na viwanda vya kuchakata nyuzi na kuzalisha majora. Kwenye kongani hiyo tunatarajia tuwe na viwanda vya kuzalisha mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri dada yangu Mheshimiwa Judith katika hotuba yake na katika randama sijaona akizungumzia jambo lolote la kuongeza thamani ya zao la pamba. Tanzania tunazalisha pamba na 80% yote tunasafirisha kwenda nje kama pamba ghafi. Sasa eneo hili ni la muhimu sana na ningemwomba dada yangu Mheshimiwa Judith atakapokuwa anafanya majumuisho aje azungumze aseme katika sekta ndogo ya pamba kama Wizara yake inaitazamaje, ana mkakati gani wa kuweza kusogeza wawekezaji katika kuongeza thamani ya zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ninataka kulizungumza; Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amezungumza kuhusu mafuta ya kula. Amefanya tathmini nzuri sana kwamba viwanda vilivyopo ndani ile *installed capacity* ni kuzalisha mafuta tani 2,500,000 na ameonesha kwamba tuna upungufu mpaka sasa hivi wa kufikia tani 400,000 za mafuta. Pia, amesema vizuri sana kwamba tasnia ya viwanda vya mafuta wanazalisha ajira karibu 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni jambo zuri, lakini ninataka nimtahadharishe dada yangu Mheshimiwa Judith, mafuta yanayoingia kupitia Zanzibar yataua viwanda vyetu hivi. Mafuta yanayoingia kupitia Zanzibar bila utaratibu ambao umedhibitiwa yataua uwekezaji ambao tumeweka katika kilimo cha alizeti na yataua uwekezaji ambao tumeweka katika kilimo cha michikichi kule kule Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana dada yangu ajue kwamba viwanda hivi ndivyo ambavyo vinabeba hali halisi ya chakula. Viwanda vya mafuta ni *food security,* kwa hiyo avitazame kwa jicho la karibu sana. Mafuta yanayoingia Zanzibar ama kodi zozote ambazo zitasababisha viwanda vyetu vya mafuta vikatetereka, ni muhimu sana dada yangu aangalie jambo hili lisiruhusiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu linahusu mfumo wa stakabadhi ya ghala. Kazi nzuri inafanywa na maafisa wa stakabadhi ya ghala akiwemo ndugu yetu Bangu, lakini kuna jambo moja ningeomba lifanyike; wakae na wafanyabiashara wa

mazao jamii ya mikunde wa Wilaya ya Kwimba na Misungwi ili waangalie changamoto zao wanazokutana nazo mara kipindi msimu unapokwisha wapate vibali vya kuweza kuuza mazao yanayokuwa yamebaki katika maghala yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mazao yanayobaki katika ghala baada ya msimu hawa wauzaji wanapata changamoto kubwa sana. Hawawezi wakasafirisha kwa urahisi na wakisafirisha wanapigwa faini ya shilingi 500 kwa kilo. Sasa urasimu huu uondolewe. Ndugu yangu Bangu wewe ni mtu ambaye anaelewa masuala haya kwa uzuri sana. Hebu nimwombe akae na wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni la pongezi kwa kazi ambayo aliifanya dada yangu. Mheshimiwa Judith alikuja Wilaya ya Kwimba akatembelea maghala ambayo tunaweka mazao jamii ya mikunde. Uhamasishaji ule alioufanya tuliupokea kwa mikono miwili. Tunamwomba mara nyingine tena dada yangu badala ya kuishia Hungumalwa aje katika Jimbo la Sumve. Tulikubaliana aje atembelee maghala ya kule, lakini bado hajaniambia ni lini atakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Habib Ali, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde ajiandae.

MHE. EDIBILY K. KINYOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii, Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais kwanza kwa kufungua biashara zetu na Mataifa mengine na hatimaye Kimataifa kidogo biashara tunafanya vizuri. Ametengeneza uhusiano na mataifa mengine kitu ambacho kilipelekea mpaka uwekezaji kutoka nje kwa maana ya *FDI* kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *FDI* inakaribia *2.2% of GDP* ya Taifa letu, lakini pia imeongezeka kutoka kwenye *1.7%,* 2021 na hiyo ni 2024 ambapo ilikuwa na *2.2%. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia juhudi wanazozifanya Wizara. Niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wetu pale kwanza kwenye upande wa uwekezaji wa Liganga na Mchuchuma. Kwa kweli, hili nalo linahitaji pongezi nyingi kwa sababu ni jambo ambalo nimesikia mimi tangu nasoma nikiwa sekondari, nimetoka sekondari nimeenda *advance* na chuo. Yaani mpaka sasa ni jambo ambalo lilikuwa bado tunasikia tu Liganga, Liganga tuna *deposit* ya kutosha kule, lakini bado utekelezaji wake ulikuwa unakuwa mgumu. Kwa hiyo nipongeze kwa juhudi zilizofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda mbali kwenye mchango wangu, ninaomba nikumbushe tu Waheshimiwa Mawaziri hapo, pale kwangu nina uwekezaji wa kiwanda cha *cement,* mwekezaji anaitwa *Teseco Limited*. Yule mwekezaji amepewa lile eneo ni zaidi ya miaka mitatu sasa, lakini lile eneo hajawahi kuliendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimekwishaongea na Mheshimiwa Waziri na niliuliza swali. Serikali imesema kwamba wanafanya tathmini ya kina, lakini imechukua miaka mitatu na mpaka sasa wanaendelea kusomba malighafi pale. Wanasomba mawe na kuyapeleka Burundi. Sasa hali hiyo imeharibu Barabara ya kutoka Mgombe kwenda Kagera Nkanda ile barabara haipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inaleta shida kwa wananchi wetu na inaleta inaongeza mpaka bei ya nauli, yaani kutoka pale kuja mjini mwananchi anatumia zaidi ya 20,000 kwenda na kurudi na wakati ni karibu siyo mbali kilomita 37. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie hilo na *of course* nimekuwa nikiongea naye mara kwa mara kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie kuhusiana na mchango wangu kwenye sekta hii. Sekta hii kwenye uchumi wetu ina-*compose almost* 19.7% kwenye uchumi wetu. Sekta ya viwanda ukiacha sekta ya biashara pembeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye viwanda ukija kwenye shughuli za msingi huku tunakopata *raw materials* uchumi wetu una 42.9% huku ndipo tunapata malighafi. Kwa hiyo, uchumi wetu umejikita sana kwenye shughuli nyingi za msingi ambazo ni kilimo yaani shughuli zinazohusisha ardhi, uchimbaji wa madini na vitu vingine mazao ya msitu, ndiyo uchumi wetu umejikita hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa Dira yetu tunalo lengo kubwa la kuhakikisha tunakuwa na uchumi stahimilivu. Sasa ili tuwe na uchumi stahimilivu tunahitaji tupambane kuboresha sekta yetu hii ya viwanda yenye 19% inayochangia kwenye uchumi wetu. Hapa ninaomba, nimshauri Mheshimiwa Waziri, kwamba tujikite zaidi kwenye viwanda ambavyo vinaenda kuwagusa na vinagusa maisha ya wananchi wetu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi lazima viwe ni viwanda ambavyo vinahusisha sekta ya kilimo. Tuwe na viwanda vingi ambavyo vitakwenda kubeba malighafi zinazotoka kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hapa katikati kuna viwanda vingi vilikuwa vimeanzisha kwa takwimu ya *NBS* 2002, tulikuwa na viwanda zaidi ya 50 kwenye uzalishaji wa nguo, lakini mpaka tunavyozungumza *NBS* wanasema vile viwanda vimebaki 23 tu. Pia kwa mujibu wa *NBS* 2011 mpaka 2016 inaonekana mpaka 2024 viwanda hivi uzalishaji wake unashuka kwa 17% yaani maana yake viwanda vingi vimekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 tulikuwa tumeajiri, viwanda hivi vilikuwa vimeajiri wafanyakazi zaidi ya 12,000 lakini sasa hivi 2016 ndani ya mwaka mmoja tu vilikuwa vimebaki na wafanyakazi 9,000 tu pekee yake. Maana yake tuna vijana wengi wanaokosa kazi, lakini pia viwanda hivi havifanyi kazi vizuri. Kwa hiyo, nimshauri Mheshimiwa Waziri ahakikishe anaongeza nguvu

kuhakikisha tunafufua viwanda vyetu vinavyochukua na kuongeza thamani mazao yetu yanayotokana na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nishauri kwenye biashara urari wa biashara zetu na mataifa mengine. Hapa bado hatujafanya vizuri kwa sababu ukiangalia kwa mujibu wa takwimu na ripoti iliyotolewa na Wizara ya Fedha, hali ya uchumi Juni, 2025 ikiwa na vyanzo vya *BOT* na *TRA,* lakini pia na *NBS* inaonyesha 2024 tulikuwa na *negative* ya 14,000,000,000,000 dhidi ya urari wa biashara na mataifa mengine lakini pia 2023 *negative* ya 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nishauri tuongeze nguvu kuongeza thamani ili tuweze kufanya vizuri kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Rashid Habib Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri ajiandae.

MHE. RASHID HABIB ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, awali ya yote, ninaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu wata'ala,* muumba mbingu na ardhi pamoja na vyote vilivyomo katika mbingu na ardhi, akaumba pia mataifa mbalimbali na kila Taifa akalijalia kwa kulipa neema yake ya uchumi ili liweze kujiendeleza Taifa hilo kutokana na neema hizo ambazo Mungu amezipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata masikitiko makubwa punde hivi kusikia kauli ya ndugu yangu, kaka yangu ambaye ametoka kuchangia na niweke wazi, nilitaka kumlima taarifa, lakini bahati nzuri nina wakati wa kuchangia ninadhani hoja yangu itajielekeza huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nina masikitiko makubwa na masikitiko yangu moja ya Wizara ambazo kwamba zinaumiza na zinadumaza biashara na uchumi wa Zanzibar, ni Wizara hii ya

Viwanda na Biashara ambayo kuwa leo hii tunasimama kuipitishia bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Aprili 2026, Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi aliongoza kikao cha Kamati ya Pamoja Zanzibar, *Golden Tulip Hotel*. Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kikao hicho kikijumuisha na kikijulikana kama Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa kikao hiki hakina mamlaka yoyote ya kikatiba na maazimio ya kikao hiki yasipotekelezwa, hatuna popote pa kwenda kuhoji kwamba kwa nini yale mliyofikiana hamkuyatekeleza moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao hiki kilitoka na maazimio ya kwamba eti sukari ya Zanzibar iruhusiwe kuuzwa Tanzania Bara kwamba leo hii Wazanzibari kuuza sukari yao Tanzania Bara ni mpaka waruhusiwe na Watanzania Bara wakati nchi hii ni nchi ambayo kwamba tunaiita ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana hapa kutokana na Kamati hii kuwa haina mamlaka ya kikatiba wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha hoja yake hii ya hotuba ya mipango na bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika hotuba yake yote, ukurasa wa 39, Mheshimiwa Waziri alisema hapa kwamba kuna kipengele alichosema cha kuondoa vikwazo vya kibiashara, lakini kutokana na kuwa Mheshimiwa Waziri hatambui Kamati hii na hajui kinachoendelea kwenye Kamati hii hakuna neno Zanzibar limeandikwa katika kipengele kile bali vikwazo vya kibiashara vilivyokwenda kuondoshwa, ametaja sehemu mbili (a) ni Kenya na (b) Zambia kana kwamba hiki kilichofanyika Zanzibar hakijui wala hakuambiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba hakijui kwa sababu chombo hiki kilichotumika kutoa maamuzi haya hakina mamlaka ya kikatiba na ndiyo maana Wazanzibari tunashindwa

kabisa kwenda kuhoji kwamba kwa nini makubaliano haya hamkwenda kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina dhamira ya dhati juu ya suala hili ilipeleke kwenye vyombo huru vya kikatiba ambavyo kuwa ni Bunge na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa ajili ya kuundiwa sheria mahsusi ambayo kuwa itaondoa kadhia hii iliyodumu kwa muda mrefu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Taarifa.

MHE. RASHID HABIB ALI: Na kama wana…

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Taarifa.

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Mzungumzaji anayeendelea kuchangia anajenga hoja yake vizuri sana na hoja zake zinaeleweka. Hata hivyo, ninataka nimpe taarifa kwamba tunao utaratibu ambao tumejiwekea kama nchi wa kushughulikia masuala yanayohusu hoja za Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006 tulipitisha utaratibu wa kuwa na Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia hoja zote za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka huo wa 2006, Kamati ya Pamoja imekwishapokea hoja 25 na katika hizo imeshughulikia hoja 23 na zimebaki hoja mbili tu. Katika hoja 23 ambazo

zimeshughulikiwa ni pamoja na hoja hii ya sukari inayozalishwa Zanzibar kuruhusiwa kuuzwa kwenye soko la Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Aprili tulipitisha hoja hii tuliiondoa miongoni mwa hoja ambazo zinaonekana kwamba ni tatizo, hivi sasa hoja hii haipo na kwenye Bunge hili tutakapokuwa tunajadili *finance bill* jambo hili litajitokeza na kwamba hapatakuwa na kikwazo hicho tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, tumefanya hivyo kwenye hoja zote za bidhaa ikiwemo pia hoja ya bidhaa ya maziwa ilikuwa hivyo na tumekuwa tukitatua hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utaratibu wetu huu wa kutatua hoja za Muungano upo ni utaratibu wa ndani na unaokubalika. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Habib Ali taarifa unaipokea?

MHE. RASHID HABIB ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme wazi taarifa hii sipokei na ninaomba unilindie muda wangu kwa sababu utaratibu si sheria na utaratibu si katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunahitaji chombo cha kikatiba na kwa sababu hizo ndiyo maana Wizara ikashindwa kutambua hata kusema kwamba pia tumeondosha kizuizi cha sukari ya Zanzibar. Wametajwa Wakenya wametajwa Wazambia lakini sisi ndugu zao wameshindwa kututaja kwamba kikwazo cha sukari ya Zanzibar kimeondoshwa. Kwa hiyo hoja hii sipokei.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ni kuhusu tozo ama kodi ya pamoja. Mfumo wa kodi ya pamoja unaojulilikana kama kwa jina la *VAT*. Mfumo huu unatuumiza sisi Wazanzibari ambao kwamba tunakuwa tuna biashara ndogo ndogo tofauti na biashara kubwa za Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar inapaswa kuachwa huru kwa ajili ya kuandaa, Zanzibar inapaswa iwe huru kuandaa mipangilio yake, kuandaa… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako…

MHE. RASHID HABIB ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante ninamalizia, ninaomba sekunde 30 kwa ajili ya kumalizia.

NAIBU SPIKA: Malizia sentensi hiyo unayoongea.

MHE. RASHID HABIB ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia. Kwamba Zanzibar inapaswa iwe huru kwa ajili ya kuandaa mipango yake ya kodi na sera zake kwa ajili ya kodi na isiwe sera hizi zote zinapangwa kwa ajili ya Tanzania Bara, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri na mtoa hoja ajiandae.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu kabisa ya kuchangia moja ya Wizara muhimu ambazo Waheshimiwa Wabunge wamekwishaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Mheshimiwa Judith Kapinga pamoja na Dennis Londo kushika nafasi katika Wizara hii ya muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuwapa hongera vilevile nimpe pole Mheshimiwa Ado nilikuwa ninamwonea huruma anataka kujificha, inashindikana, akashika kichwa ndiyo hivyo endelea kuvumilia. Unapoambiwa utaratibu si sheria kuna utaratibu mwingine ni sheria. Kwa mfano kaunda suti haichomekewi na unaona yule hajachomekea pale kwa sababu ni utaratibu siyo sheria, lakini utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara muhimu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza lakini Wizara hii ikichukua hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo wamezichangia hapa ni hoja nzito ambazo zinaweza kusaidia kui-*push* hii Wizara ili iweze kufanya mabadiliko makubwa ambayo yataleta mageuzi makubwa katika biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni lazima isomane na Wizara zingine, kwa mfano tunapozungumzia habari ya biashara, habari ya uwekezaji, lazima Wizara ya Viwanda na Biashara iende sambamba na Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Wakikaa wote pamoja wanaweza kusuka kitu kikaja kuwa msaada mkubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumempongeza sana vilevile Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo analea taasisi zake ndogo zilizoko chini ya Wizara yake. Wakurugenzi wote wamepongezwa na nikiri hapa ni Mjumbe wa Kamati inayosimamia hii Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini wameona wajumbe wengi wanazungumza sana kuhusu *WMA*, kuhusu taasisi ambazo ziko chini ya hiyo Wizara, *TBS* na mambo mengine? Siku tulipofanya ziara kuwatembelea wakala wa vipimo, tulikuta wamekamata maroli manne yakiwa na nondo ambazo hazijafikia ujazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kama kwa siku ile walikuwa wamekamata maroli manne mangapi yalikuwa yamewapita na hizo nondo ziko wapi sasa hivi? Maana yake zimeshafika kwa mlaji, zimekwishajenga haya majengo na tunasubiri hayo majengo yaje yatuponde.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana wanaona wenzao kwa niaba ya Kamati tunawaambia Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana hizi taasisi zikawekewa nguvu ili ziweze kufanya kazi barabara za vipimo na ziweze kuzuia. Kwa sababu vinginevyo itakuwa ni shida; zimekamatwa nondo malori manne, nondo zile hazijafikia milimita zilizoandikwa mle. Maana yake ni kwamba

zingepita zile zingekuwa zimeshajenga tayari baadhi ya nyumba za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapiga kelele ili hizi taasisi ziwezeshwe, ziwe na nguvu ya kusimamia kikamilifu sheria za nchi. Haya mambo tutakapoyasimamia walaji wa mwisho watanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, usipoipima mita moja ya umeme ikakupa umeme sahihi mita ya kiwandani, maana yake hicho kiwanda kina uwezekano wa kutumia umeme bure, halafu mita hiyo isipopimwa ikawa inachaji umeme mwingi ikifungwa nyumbani kwa Mheshimiwa Anne Kilango hapa itamchaji shilingi 500,000 wakati nyumba ya kawaida siyo kiwanda. Hii inakuwa siyo sawa ndiyo maana tunapiga kelele taasisi hizi ziwezeshwe ili ziweze kufanya kazi yake barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimezungumzwa na Kamati yetu ilitembelea Tanga. Nami ninamwomba Waziri na Naibu wake kwenye hiki Kiwanda cha *Neelkanth*, waende wao wenyewe, kuona ni kuamini. Waende wakatembee wajionee kwa macho watafanya maamuzi kwa sababu hawashindwi kufanya maamuzi wanapotembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunawashauri fikeni, nendeni mfanye maamuzi pale ili muone nini mnaweza kusaidia kile kiwanda kiweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunapozungumzia viwanda vya ndani tunazungumzia ulinzi wa viwanda vya ndani, tunazungumzia habari ya ajira, tunazungumzia habari ambayo itawawezesha vijana wetu kupata kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii viwanda vingi kwa nini vinapenda kukaa kwenye maeneo ya Pwani? Viwanda vingi vinakaa pwani kwa sababu ya bandari. Urahisi wa usafiri, urahisi wa kupata malighafi, maana yake sisi tukitaka kuvivuta vije kwenye mikoa yetu huku ni lazima Wizara iweke upendeleo maalumu. Tufanye mazingira yawe rafiki ili hawa wawekezaji waweze kusogea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira kuwa rafiki maana yake nini? Tuboreshe barabara zetu, tuboreshe maji, tuboreshe upatikanaji wa umeme, tuwavutie wawekezaji ili wasogee kwenye mikoa yetu. Kwa kufanya hivyo tunajikuta nchi nzima inanufaika na uwepo wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini viwanda vyetu tuvitenge basi. Tuelewe viwanda gani ambavyo vinashabihiana na Wizara ya Kilimo, viwanda gani vinashabihiana na Wizara ya Mifugo, tuangalie tuna uharibifu mkubwa sana wa ngozi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama wengi wanatumia pochi za ngozi, wakina baba wengi tunavaa viatu vya ngozi. Lakini sisi wenyewe tunazalisha ngozi kiasi gani kuingia kwenye hilo la utengenezaji wa hizo bidhaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunakuwa walaji tu badala ya sisi kuzalisha. Tukizisimamia vizuri bidhaa zetu utajikuta mifugo inatuletea faida kubwa sana. Je, tuna viwanda vingapi ambavyo vinashabihiana na Wizara ya Uvuvi? Vingapi ambavyo vinafanya kazi? Nini tufanye hivi kuviboresha spidi ya hizi ya hivi viwanda iwe kubwa ili upatikanaji wa ajira uwe mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapozungumzia habari ya biashara tumejiandaaje? *AFCON* inatupa nafasi kiasi gani ya kufanya biashara? Leo hapa tunasema tunatumia sukari tani kadhaa kwa mwezi, tunatumia mafuta tani kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *AFCON* itatuletea wageni wanaweza wakatumia nusu ya hivyo vitu ambavyo sisi tunasema tunatumia kwa mwezi. Tumejiandaaje? Ili kuja kuteka hilo soko la biashara wakati wageni watakapojaa hapa Tanzania; hilo ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka nilizungumze hapa ni lazima tuhakikishe hili suala la lumbesa, tunalizungumza tu lumbesa, mimi ninawapa mwarobaini. Tunahangaika na gunia. Gunia siyo kipimo! Gunia ni kifungashio. Watu wajanja gunia lenyewe wanalibana. Wakishalibana gunia halikupi zile kilo ambazo zimetajwa. Watanzania ni wajanja na sisi

tuendelee kufuatilia na kuzuia ili kutenda haki kwa watu. Gunia linaweza likafungwa na kishungi na bado lisiwe lumbesa, bado lisifikie hizo kilo mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina uzoefu, kuna watu wanakuja kununua ufuta kwa wananchi wetu. Anakuja na ndoo yake, hataki atumie ndoo ya mwenyeji. Ile ndoo imeunguzwa moto halafu imetanuliwa. Inaingia zaidi ya kilo ishirini na tano. Anasema ya kwenu mimi situmii! Kwa hiyo dawa yake ni moja. Kila zao lipimwe kwenye mzani. Unataka mahindi, mzani! Mahindi mabichi, mzani! Tikiti, mzani! Kila kitu mzani! Ukiweka mzani umeondoa hiyoo! Tusihangaike na lumbesa kuhangaika na kishungi, kile kishungi hakitoi matokeo sahihi kwamba huo mzigo umezidi au haujazidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tunazungumza kuhusu baadhi ya kodi. Baadhi ya kodi zimekuwa tatizo, hazitoi fursa sawa. Hebu wafanye utafiti tuone, hivi kodi hii tunayoitoza, Uganda wanatoza? Kodi hii tunayoitoza, Kenya wanatoza? Unaweza kukuta kuna kodi ni kikwazo kikanda. Kwa hiyo, hata kuzikusanya zinakuwa na tatizo. Wenzako kule hawatozi, wewe ukitoza wafanyabiashara wanakimbilia kule. Wenzako kule wanatoza, wewe usipotoza unapoteza hela. Kwa hiyo, ni muhimu sana tukatengeneza na wataalamu wetu wakatembelea baadhi ya nchi kwenda kuangalia mifumo ya kikodi, tuone kodi gani ni rafiki, kodi gani siyo rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ADONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali kwa ujumla kwa kazi kubwa iliyofanyika, ilichochea ukuaji wa sekta za viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri yafuatayo: kwanza uzalishaji wa dawa na vifaa tiba; kwa kuwa bidhaa za afya ni muhimu kwa ajili ya kujenga Taifa lenye afya bora. Tukijenga uwezo mkubwa wa kuzalisha bidhaa za afya nchini italipunguzia Taifa uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi ambao hutumia fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mipango na Uwekezaji na Wizara ya Afya zishirikiane katika kupitia sera na sheria za sekta mbalimbali kwa nia ya kuondokana na changamoto, kuwezesha na kuandaa mazingira mazuri zaidi ikiwemo miundombinu ya uwekezaji katika uzalishaji dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni vizuri Wizara ya Viwanda na Biashara ikakubaliana na Wizara ya Afya kuhusu lengo au malengo ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba ni kufikia asilimia ngapi ya mahitaji ya bidhaa hizo kwa nchi. Kuna utofauti wa malengo kati ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi za Misri, Bangladesh, China na India zimepiga hatua kubwa katika eneo hili la uzalishaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kutokana na kutenga maeneo maalum ya viwanda vya bidhaa hizo yenye miundombinu na kuweka vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi kwa muda maalum. Ni vizuri tukajifunza kutoka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda; uanzishaji wa Mfuko huu utasaidia kuwezesha mazingira na kuchochea uanzishaji wa viwanda na kuleta ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu Tume ya Ushindani Tanzania *(FCC);* Serikali iongezee uwezo wa rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi vya kisasa ili iweze kudhibiti vizuri uingizaji na usambazaji wa bidhaa duni na bandia pamoja ukuaji wa biashara haramu ya mitandao unaoendelea kuathiri ushindani wa haki kwa wazalishaji wa ndani na wafanyabiashara wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *FCC* iendelee kushirikiana/kuimarisha ushirikiano na taasisi nyingine za udhibiti katika kupambana na bidhaa ambazo hazikidhi mahitaji ya sheria. Pia kuimarisha utoaji elimu kwa wananchi ili kuwajengea uelewa wa bidhaa duni na bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, uzalishaji wa sukari nchini; Serikali ikae kwa pamoja na wazalishaji wa sukari nchini ili kufanya tathmini na kukubaliana nao mikakati ya kuongeza uwezo wao wa kuzalisha bidhaa hiyo kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani. Viwanda vya sukari vimekuwa vikilalamika kuhusu ushindani wa sukari kutoka nje unaathiri uwezo wao wa kukidhi mahitaji ya soko la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Serikali ifanye mapitio ya uwepo wa taasisi nyingi za udhibiti na zinazotoza tozo na ushuru kwa wawekezaji na wafanyabiashara na kuathiri ukuaji wa biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Serikali iwekeze *CAMARTEC* kwa kukipatia mitambo ya kisasa pamoja na maabara za kisasa za kufanyia majaribio ya teknolojia. *CAMARTEC* iwezeshwe zaidi ili iweze kushirikiana na halmashauri katika kuimarisha kilimo na kukuza uchumi vijijini. Uwekezaji ufanyike zaidi katika vifaa vya kisasa na miundombinu kwa *TEMDO* na *SIDO* ili kuzijengea uwezo zaidi wa kufanya kazi na halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS);* tangu udhibiti wa bidhaa za chakula ulipohamishiwa *TBS* kutoka kwa iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* sasa *TMDA* mwaka 2019, taasisi hiyo ya *TBS* imekuwa haifuatilii magonjwa yatokanayo na matumizi ya chakula *(food borne disease)*. Ufuatiliaji huu ungesaidia kubaini kama baadhi ya magonjwa yanatokana na matumizi ya vyakula fulani kwa mfano sumu, kuvu kutoka katika baadhi ya nafaka husababisha magonjwa. Baadhi ya milipuko ya magonjwa husababishwa na matumizi ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapenda kutoa ushauri kwa Wizara ya Viwanda na Biashara juu ya kulinda na kuendeleza viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi; kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa wasaa wa kuchangia katika Wizara ya Viwanda na Biashara kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mapenzi makubwa naipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara; hasa Mheshimiwa Judith Kapinga pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dennis Londo. Ninawapongeza pia watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kuanzia Katibu Mkuu Ndugu Waziri Rajabu Salum, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Arstides Mbwasi pamoja na watumishi wote walioko chini yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi kwa Wizara ni kwa sababu ya maandalizi makini ya bajeti ya Viwanda na Biashara yenye maono, iliyoandaliwa kwa weledi na inayoakisi mahitaji halisi ya kila Mtanzania katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri; kulinda na kuendeleza viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa kutoka nje ni jambo muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa kama Tanzania, lakini ulinzi huo unatakiwa ufanywe kwa njia yenye usawa ili viwanda visibweteke, wananchi wapate bidhaa bora na uchumi ukue kwa muda mrefu. Njia muhimu zinazoweza kusaidia kuongeza ufanisi wa viwanda vya ndani na kuvilinda dhidi ya bidhaa zinazofanana kutoka nje ni kama ifuatavyo:

Kwanza, kuboresha ubora wa bidhaa za ndani; hii ndiyo nguzo kuu ya ushindani. Bidhaa za ndani zikawa bora, wananchi watazipendelea hata bila kulazimishwa. Njia za kufanya hivyo ni:-

(i) Kuongeza matumizi ya teknolojia za kisasa viwandani;

(ii) Mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu uzalishaji bora;

(iii) Kuimarisha viwango vya ubora kupitia *Tanzania Bureau of Standards;* na

(iv) Kufunga mashine zinazopunguza gharama na kuongeza ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida zake ni bidhaa za ndani hushindana kimataifa; wateja huamini bidhaa za ndani na viwanda hupata masoko mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kupunguza gharama za uzalishaji; bidhaa nyingi kutoka nje huwa nafuu kwa sababu ya uzalishaji mkubwa na gharama ndogo. Hivyo, Serikali inaweza kusaidia kwa kupunguza kodi kwa malighafi za viwandani; kutoa umeme wa uhakika na bei nafuu; kuboresha barabara, reli na bandari; na kupunguza urasimu wa leseni na vibali. Kwa mfano, kiwanda kinapotumia umeme wa gharama kubwa, bidhaa yake huwa ghali kuliko ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuweka kodi au tozo kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje; hii ni njia inayotumiwa na nchi nyingi kulinda viwanda vya ndani. Aina za ulinzi ni kuongeza ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazofanana na za ndani; kuweka kiwango maalum cha bidhaa zinazoingia; kuzuia bidhaa duni zisizo na viwango; lakini pia kodi isiwe kubwa kupita kiasi; na ulinzi uwe wa muda huku viwanda vikijengewa uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatari; ulinzi wa kupindukia unaweza kuongeza bei kwa wananchi, kuleta bidhaa za magendo, kufanya viwanda vya ndani vibweteke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kukuza matumizi ya bidhaa za ndani; wananchi wakiamini bidhaa za ndani, viwanda hukua haraka. Njia ya kutumia ni Kampeni za "Nunua bidhaa za Tanzania"; Serikali kununua bidhaa za ndani kwanza; na maduka makubwa kupewa motisha kuuza bidhaa za ndani. Faida zake ni

ajira huongezeka; fedha hubaki ndani ya nchi; na viwanda huongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kutoa mikopo na mitaji kwa wazalishaji wa ndani; viwanda vingi vinakosa mtaji wa mashine, malighafi, upanuzi wa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho; benki kutoa mikopo nafuu kwa viwanda; Serikali kuunda mifuko maalum ya viwanda; na kuvutia wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kuwekeza katika malighafi za ndani; nchi ikiwa na malighafi lakini bado inaagiza kutoka nje, gharama huongezeka. Tanzania ina uwezo mkubwa katika pamba, ngozi, mazao ya kilimo, madini, gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, malighafi hizi zikichakatwa ndani huongeza thamani, huongeza ajira na hupunguza uagizaji wa bidhaa za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kupambana na bidhaa bandia na magendo; bidhaa nyingi kutoka nje huingia bila kulipa kodi, ikiwa duni na ikiwa bandia. Hii huua viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua muhimu ni kuimarisha mipaka; ukaguzi mkali bandarini; adhabu kali kwa wakwepa kodi; na ufuatiliaji wa ubora sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, kuimarisha Soko la Afrika Mashariki na Afrika *(East African Community* na *African Continental Free Trade Area)* vinaweza kusaidia viwanda vya Tanzania kupata soko kubwa zaidi. Faida zake ni uzalishaji mkubwa hupunguza gharama; viwanda hupata wateja wengi; na mauzo ya nje huongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, kuongeza utafiti na ubunifu viwanda visivyobuni bidhaa mpya hupitwa na ushindani. Ni muhimu ushirikiano kati ya viwanda na vyuo vikuu; kuongeza tafiti za teknolojia; na kuboresha vifungashio na ubunifu wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, kuwa na sera imara na endelevu; wawekezaji wanahitaji mazingira yenye utulivu. Hivyo basi Serikali inapaswa kuepuka kubadilisha sera mara kwa mara; kutoa mwongozo wa muda mrefu wa viwanda; na kusikiliza sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kulinda viwanda vya ndani siyo tu kuongeza kodi kwa bidhaa za nje. Njia bora zaidi ni kuongeza ubora; kupunguza gharama za uzalishaji; kuboresha teknolojia; kukuza matumizi ya bidhaa za ndani; na kuweka mazingira mazuri ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mifano ya nchi duniani kama sehemu ya somo kwa Tanzania katika sekta ya viwanda; nchi nyingi duniani zimefanikiwa kujenga viwanda vyao kwa kutumia mchanganyiko wa ulinzi wa viwanda vya ndani; uwekezaji mkubwa; elimu; teknolojia; na sera thabiti za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano muhimu ambayo Tanzania inaweza kujifunza kutoka kwa nchi nyingine za nje kama ifuatavyo; China – kutoka nchi maskini hadi "kiwanda cha dunia." China ni mfano mkubwa wa mafanikio ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, walifanya nini kulinda viwanda vya ndani mwanzoni; kwanza waliongeza ushuru kwa bidhaa nyingi kutoka nje; na pili walizuia bidhaa ambazo zingeua viwanda vya ndani. Walifanya nini kuiga na kujifunza teknolojia; kampuni za nje zilipowekeza China, zililazimika kushirikiana na wazawa. Wachina walijifunza teknolojia haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, walifanya nini katika miundombinu mikubwa; kwanza walijenga reli, bandari, umeme na miji ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, walifanya nini kukuza uzalishaji mkubwa? Bidhaa zilipotengenezwa kwa wingi gharama zilishuka na bei zikawa nafuu duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, somo kwa Tanzania; viwanda haviwezi kukua bila umeme, reli, bandari na sera thabiti. Hivyo Serikali lazima iwe na mpango wa muda mrefu wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *South Korea* kutoka umaskini hadi teknolojia kubwa; *South Korea* miaka ya 1960 ilikuwa maskini kuliko baadhi ya nchi za Afrika, leo ni moja ya mataifa makubwa ya teknolojia duniani. Je, walifanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali kusaidia kampuni za ndani. Kampuni kama Samsung na Hyundai yalisaidiwa kwa mikopo nafuu, ulinzi wa soko na motisha za kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, elimu ya ufundi; walitoa elimu kali ya sayansi, teknolojia na uhandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulenga mauzo ya nje; walitengeneza bidhaa kwa ajili ya dunia nzima, si soko la ndani pekee. Hapa somo kwa Tanzania ni elimu ya ufundi ni muhimu sana na viwanda vikikosa wataalamu, haviwezi kuwa vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya India kukuza viwanda na teknolojia; India ilitumia nguvu kubwa katika teknolojia, dawa na viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, walifanya nini? Kwanza kutoa nafasi kwa wazalishaji wa ndani. Kwa kufanya hivyo walipunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha sekta ya teknolojia; leo India ni kubwa katika programu za kompyuta, dawa na huduma za kiteknolojia. *Programme* ya *Make in India* ilisisitiza uzalishaji wa ndani, ajira na uwekezaji wa viwanda. Somo kwa Tanzania; teknolojia na ubunifu vinaweza kuleta mapinduzi makubwa ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Ethiopia mfano wa Afrika; Ethiopia imejaribu kukuza viwanda hasa vya nguo, ngozi na viatu. Walifanya nini? Kwanza walijenga maeneo maalum ya viwanda;

walitoa umeme wa bei nafuu; na walivutia wawekezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ni siasa, migogoro, na utegemezi wa wawekezaji wa nje. Somo kwa Tanzania; maeneo maalum ya viwanda yanaweza kusaidia sana; na utulivu wa kisiasa ni muhimu kwa maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazoikabili Tanzania katika viwanda; kwanza Tanzania ina fursa kubwa, lakini pia changamoto kadhaa ikiwemo gharama kubwa za uzalishaji, umeme, usafirishaji, na mikopo yenye riba kubwa; bidhaa nyingi kutoka nje na baadhi huwa nafuu, za magendo, au zenye ruzuku kutoka nchi zao; teknolojia ndogo; viwanda vingi bado vinatumia mashine za zamani; na ukosefu wa mitaji; wazalishaji wengi wadogo hawawezi kupanua biashara; lakini pia soko dogo la bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengine bado wanaamini bidhaa za nje ni bora zaidi. Aidha, elimu ya ufundi haitoshi. Pia sekta ya viwanda inahitaji wahandisi, mafundi, wabunifu na wataalamu wa mashine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa hatua kwa hatua kwa Tanzania ni hatua ya kwanza; kuimarisha nishati, umeme wa uhakika, gesi asilia, na nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili; kuwekeza katika elimu ya ufundi. Vyuo vya ufundi, teknolojia, na uhandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya tatu; kulinda viwanda vya kimkakati. Kwa mfano, nguo, dawa, usindikaji wa chakula, na vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya nne; kuongeza thamani ya malighafi badala ya kuuza pamba ghafi, ngozi ghafi, korosho ghafi, na ichakatwe ndani kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya tano; kupambana na magendo kwa mifumo ya kidigitali, ukaguzi, na kodi za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya sita; kukuza "*made in Tanzania*" bidhaa za ndani zijengwe kwa ubora, vifungashio vizuri, na matangazo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya saba; kukuza ushirikiano wa Afrika. Soko la Afrika lina watu zaidi ya bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho kuu; nchi yoyote haiwezi kuwa tajiri kwa kutegemea kuagiza bidhaa, kuuza malighafi pekee; au biashara ndogo tu. Nguvu ya uchumi mkubwa hutokana na viwanda, teknolojia, elimu, uzalishaji, na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina rasilimali nyingi, watu wengi, soko, amani, na nafasi nzuri ya kijiografia. Tanzania ikiwekeza kwa umakini katika viwanda, inaweza kuwa moja ya nchi kubwa za viwanda Afrika katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha mazingira ya kuwa na Tanzania yenye viwanda. Nchi yetu miaka iliyopita ilikuwa ina viwanda vingi sana kama vile *URAFIKI, MWATEX* na kadhalika ambavyo vilizalisha ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kila Mtanzania aliyefanya kazi kwenye viwanda hivyo alionekana kuwa mtu mwenye hadhi na kuheshimika kwenye jamii yetu. Tunatamani leo ambapo tuna viwanda zaidi ya 80,000 hadhi ya wafanyakazi wa viwandani ionekane kama nyakati zile za viwanda vya *MWATEX* na *URAFIKI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya kuwa na viwanda ni makubwa, lakini kero za wafanyakazi wa viwandani ni kubwa ikiwemo kucheleweshewa malipo ya stahiki zao, kutolipwa michango ya pensheni mazingira magumu ya kufanya kazi na kadhalika. Serikali ijikite kwenye kukagua vizuri viwanda vilivyopo kwani vingine havikidhi haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza uwepo wa viwanda vya ku-*assemble* magari na ninaomba tuone uwezekano wa kufufua kiwanda cha *General Tyre* kwani sasa hivi nchini uhitaji wa matairi ni mkubwa na kuna matairi yanayoletwa nchini hayana uimara, jambo ambalo linasababisha gharama kubwa kwa wenye magari ya biashara kutokana na matairi kupasuka kabla ya wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina madini ya viwanda ikiwemo madini yanayotengeneza *gypsum* na chaki katika Kijiji cha Makangaga, Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi. Ninapendekeza Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Madini kuanzisha kiwanda kikubwa cha kutengeneza bidhaa hizo hususan kwenye eneo hilo ili kuweza kuongeza thamani ya madini hayo. Kwa kufanya hivyo itazalisha ajira kwa vijana na kuweza kuwanufaisha moja kwa moja wananchi wa Kilwa na Mkoa wa Lindi kwa ujumla hasa ukizingatia kwamba Mkoa wa Lindi bado hauna viwanda vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Sasa nimwite Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri, Mtoa Hoja ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na afya njema aliyotujalia katika kutekeleza majukumu yetu kwa Watanzania. Pia, nitumie nafasi hii kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anachukulia sekta hii ya biashara, nimshukuru kwa uteuzi wangu kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii nyeti ya Viwanda na Biashara. Wizara ambayo imebeba hatima ya Watanzania wengi katika mnyororo wa biashara na thamani ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, lakini pia Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na Mawaziri wake, hasa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi ambaye anashughulikia uratibu wa

Bunge, ambaye kwa kipindi chote hiki amekuwa akitupa ushirikiano yeye na Naibu wake dada yangu Mheshimiwa Ummy Nderiananga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru Waziri wangu, dada yangu, Mheshimiwa Judith Kapinga kwa ushirikiano ambao amekuwa akinipa tangu nimefika kwenye Wizara hii. Nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote; na hasa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Zungu pamoja na wewe ukiwa Naibu wake na Wenyeviti wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchangia katika mtazamo chanya wa hotuba yetu, nimeona michango mingi ya Wabunge ikijikita katika mtazamo huo chanya. Hasa wakiwakilisha kundi kubwa la wapiga kura ambao ni wafanyabiashara, wazalishaji wa bidhaa, lakini pia wakulima wao ambao wanajikita katika shughuli za kuongeza thamani katika maeneo yao ya uchaguzi. Nia yetu kama Wizara ni kuendeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kama Dira ya 2020 – 2050 inavyotuelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuunga mkono hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Waziri wa Viwanda na Biashara, pamoja na kuunga mkono bajeti hii ambayo imewasilishwa katika Bunge lako Tukufu. Bajeti hii imebeba dhamira kuu yenye vipaumbele ambavyo vimejikita katika kuendeleza utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati, hasa ya viwanda; Kongani za viwanda; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuboresha mazingira wezeshi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mitaa ya viwanda, kongani kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuchochea maendeleo ya viwanda pamoja na kuzingatia ubunifu wa matumizi ya teknolojia ya kisasa; elimu ya mafunzo ya ujuzi, kuimarisha upatikanaji wa fedha na mitaji kwa wajasiriamali na wazalishaji wa viwandani; kuboresha mazingira ya biashara na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi; kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini na kuanzisha na kuendeleza

mawazo ya biashara ya kibunifu kwa vijana kwa lengo la kuchochea uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama michango ya Wabunge wengi ambayo imeelekezwa kuhusiana na ulinzi wa viwanda vyetu, ulinzi wa wafanyabiashara wetu, uchocheaji wa mitaji, kuimarisha biashara za ndani, lakini pamoja na hayo kuangalia namna gani tunaenda kuhamasisha miradi midogo midogo ama viwanda vidogo vidogo vya kati ili kuchochea viwanda vikubwa kuja kuwekeza ambavyo vinaenda ku-*complement* viwanda vya kati na vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ninaomba sasa nielekeze mchango wangu kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa hoja za baadhi ya Wabunge kuhusiana na bajeti yetu ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi, tunafahamu changamoto na malalamiko ya wananchi wetu hasa kwenye suala zima la thamani halisi ya matumizi ya huduma za muda wa maongezi, hasa bando za *internet* na muda wa simu. Kamati imezungumza, lakini Wabunge wamezungumza kupitia michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge ambao wamezungumzia suala la vipimo ni Mheshimiwa Shabiby, Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, Mheshimiwa Ghati, Mheshimiwa Yustina Rahhi, Mheshimiwa Khadija Aboud, Mheshimiwa Kampala Maganga, na Mheshimiwa Lusinde. Wamezungumza kwa mapana kuhusiana na jukumu la Wakala wa Vipimo kulinda imani ya Mtanzania, lakini pia kumpa thamani Mtanzania ya fedha yake anaponunua huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo inaendelea na vikao mbalimbali na *TCRA,* lakini pia na Msajili wa Hazina. Tuna maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Wizara yetu na Wizara ya Mawasiliano, lakini pia na Msajili wa Hazina kukaa kuona namna bora ambayo tunaenda kutekeleza Sheria ya Vipimo kwa maana ya bando na *internet* kupitia Wakala wa Vipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa kwa mapana yake ni suala la mita za umeme. Wananchi wamekuwa wakilalamika kwamba wanacholipia hakilingani na huduma wanazopata. Sote ni mashahidi na Wabunge wamezungumza hili kwa uzito na hisia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mawakala kuleta mita zao kwa Wakala wa Vipimo kupima kuangalia ubora wake ni sheria, si ombi. Kwa hiyo mawakala ambao wana-*supply* hizi mita kwa *TANESCO* bila kufuata sheria hii, wanavunja sheria. Kwa hiyo, jukumu letu sisi ni kusimamia sheria na ninaomba niliahidi Bunge lako kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri kwamba tunaenda kusimamia kikamilifu kuona kwamba haki ya Mtanzania na thamani ya fedha yake inaenda kulindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa kwa hisia kubwa ni suala zima la vipimo ambalo linazungumziwa hasa lumbesa. Lumbesa imekuwa tatizo kubwa na lumbesa imechukuliwa kama kielelezo cha dhuluma dhidi ya mkulima lakini ninaomba niseme kwamba lumbesa si kipimo, ni kifungashio kama Mheshimiwa Lusinde alivyozungumza. Dhuluma anayofanyiwa mkulima, ni pamoja na kuongeza uzito wa hicho kifungio kuchukua nafasi ya kipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lumbesa si dhuluma tu, ni uhujumu uchumi. Kwa maana hawa wanaofanya hivi wanafanya kwa makusudi kukwepa mapato ya Serikali, kulipia ushuru wa Serikali kwenye Serikali zetu za mitaa lakini pia linahatarisha afya ya hao wanaobeba magunia haya kwa sababu uzito wake haulingani na ukubwa wa kifungashio hicho. Aidha, umechakachuliwa ama hauzingatii vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara tuna maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba tukae na wenzetu wa Wizara ya Kilimo, tukae na wenzetu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, TAMISEMI, ili kwa pamoja tuwe na mkakati wa pamoja wa kuhakikisha kwamba lumbesa inafika mwisho. Kwa maoni yetu, suala hili litafika mwisho kama halmashauri zetu zitahakikisha kwamba zinatenga maeneo ya masoko, na zitatumia mizani

katika kupima mizigo na zitatoza ushuru kulingana na mizigo na siyo magunia kwa maana gunia ni kifungashio na siyo kipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni suala la biashara za mipakani. Tanzania, ina bahati, tunapakana na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini pia tunapakana na nchi za *SADC*. Mikoa ambayo inapakana na jumuiya hizi kwetu sisi tunaiangalia kama mikoa ya kimkakati. Tumejipanga kuiangalia kwa jicho la tofauti, tumejipanga kutumia mikoa hii kama *frontiers* za kuhakikisha kwamba tunaenda kuwekeza kama soko, ama kama viwanda, ama kama *entry* ya biashara katika nchi ambazo tunapakana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kwa kuangalia maeneo ya mikoa ambayo inapakana na Jumuiya ya *SADC* na *East Africa*, inaenda kutuongezea sisi ari, inaenda kutuongezea sisi ama kutupa nafasi kwa halmashauri zetu na mikoa yetu kujipanga na tathmini tumefanya kuhakikisha kwamba tunajua kila mkoa unahitaji kiwanda cha aina gani kuongeza thamani ya mazao yao, lakini pia kuhakikisha kwamba tunakuwa masoko ya bidhaa ambazo majirani zetu wanahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo linaenda kutuongezea sisi hali ya ushindani katika jumuiya ambazo sisi ni wanachama. Lakini pamoja na hayo, inaenda kutupa sisi *leverage* katika suala zima la biashara himilivu, kwa maana tunaweza tuka-*export*, lakini pia tukaimarisha masoko yetu kwa ajili ya bidhaa ambazo zinahitajika katika nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ingawa si kwa umuhimu, ninaomba nitumie nafasi hii baada ya maelezo haya kusema kwamba ninaunga mkono hoja na ninaomba kwa dhati Waheshimiwa Wabunge, kuunga mkono hoja, bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Waziri wa Viwanda na Biashara na mtoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote ninaomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kuwepo hapa siku ya leo. Kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa, ninaomba uniruhusu nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukiangalia mwelekeo wa bajeti yetu ya Viwanda na Biashara kwa miaka mitatu nyuma, huwezi kuacha kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anaipendelea sekta yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia uniruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. Mwugulu Lameck Nchemba, kwa nyakati tofautitofauti amekuwa akituelekeza na kutushauri namna ya kuenenda katika sekta yetu ya viwanda na biashara. Ninyi ni mashahidi mlimsikia katika suala la lumbesa, lakini pia mlimsikia katika masuala ya stakabadhi za ghala na namna ya kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiongozi wetu huyu wa shughuli za Serikali Bungeni anatusaidia sana katika sekta yetu ya viwanda na biashara na sisi tutaendelea kupokea maelekezo yake kwa weledi mkubwa katika kuyatekeleza kwa maslahi ya sekta yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Spika, wewe Mheshimiwa Naibu Spika Wenyeviti wa Bunge, lakini vilevile Wajumbe wa Kamati yetu ya Viwanda na Biashara, Kilimo na Mifugo, wakiongozwa na Mwenyekiti kaka yangu Mheshimiwa Mwanyika, pamoja na Makamu Mwenyekiti ndugu yangu Mheshimiwa Mariam Ditopile. Vilevile, kwa hatua hii, ninaomba uniruhusu niwashukuru sana, Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia bajeti yetu kwa upendo, kwa ufanisi mkubwa, mmetupa mapendekezo, lakini vilevile wametuelekeza namna ya

kuenenda kwa ajili ya kuboresha sekta yetu ya viwanda na biashara. Tunataka kuwahakikishia, yale waliyotuchangia leo tumepokea kwa moyo mkunjufu, tumepokea kama maelekezo, na tutaenda kuyafanyia kazi kwa sababu ninyi na sisi tunajenga nyumba moja ya kuhakikisha tunaendelea kuimarisha viwanda, tunahakikisha uendelevu wa viwanda na kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba uniruhusu niweze kujielekeza kwenye hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezieleza siku ya leo. Novemba, 2025, Mheshimiwa Rais ndipo aliniamini niweze kumsaidia katika sekta ya viwanda na biashara. Wakati ule, mimi na wenzangu ndani ya sekta, tulikubaliana namna ya kuenenda ili kusaidia kuchochea mageuzi ya kiuchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya masuala ambayo tulikubaliana yatakuwa kipaumbele katika kuyafanyia kazi, ni kuhakikisha miradi ambayo ni vipaumbele, miradi ambayo ni vielelezo, ambayo ipo katika sekta yetu ya viwanda na biashara inafanyiwa kazi na ni lazima ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati wakati anaeleza hapa, alieleza bado umuhimu wa Serikali kuhakikisha tunautekeleza Mradi wetu wa Liganga na Mchuchuma. Ndani ya sekta yetu ya viwanda na biashara iko miradi mikubwa mitatu, ambayo ni muhimu sana katika mageuzi ya kiuchumi ya Taifa letu na mradi wa kwanza ni Mradi wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndoto ya Dira ya 2050 ni kuhakikisha tuna uchumi wa viwanda ambao una ushindani. Uchumi wa viwanda una vijenzi vingi lakini uti wa mgongo wa uchumi wa viwanda ni sekta ndogo ya chuma, (*steel)*. Viwanda vyenye mitaji mikubwa (*capital intensive industries*) ambavyo ndivyo kote duniani vinachangia kwa kiasi kikubwa mageuzi ya kiuchumi, vinategemea uimara katika chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aina ya viwanda hivi ambavyo hata hapa nchini tunavyo, ikiwemo Viwanda vya *cement* pamoja na viwanda vya mabati, vina mchango mkubwa sana katika kusaidia kubadilisha uchumi wetu kutoka kwenye uchumi wa matumizi kwenda kwenye uchumi wa uzalishaji. Namna pekee ambavyo tutaendelea kuongeza uwepo wa viwanda hivi na kupanua uwepo wa viwanda hivi kwa masilahi ya mageuzi ya kiuchumi ya Taifa letu, ni iwapo tutakuwa tuna miradi ambayo itasaidia upatikanaji wa chuma nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema hapa Mheshimiwa Kamonga kwamba ukitaja Mradi wa Liganga na Mchuchuma, kila mmoja huwaga anasema *same old story* na wana haki ya kusema hivyo kwa sababu mradi huu upo kwenye vitabu kuanzia enzi za Mpango wa Pili wa Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa mwaka 1969, lakini miaka 57 baadaye, sintofahamu ya kuanza kwa Mradi wa Liganga na Mchuchuma inafutwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu majadiliano yamekamilika na yamekamilika kulingana na taratibu za kisheria ambazo zinatuongoza ndani ya nchi yetu. Masuala yote ya muhimu, ikiwemo mrabaha, ikiwemo uongezaji wa thamani, kwa madini ambayo yanapatikana pale katika Mradi wetu wa Liganga na Mchuchuma, yote yamewekwa kwa mujibu wa taratibu na sheria zetu za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuma cha Liganga kina *composition* ya madini mengi lakini madini matatu ndio yana *composition* ya juu kidogo. Chuma kuna *composition* ya 51.25%, lakini vilevile madini ya *vanadium* kuna *composition* ya 0.49%, na madini ya *titanium* yana *composition* ya 13.38%. Kwa mantiki hiyo, kwa hatua hii ya awali tumefanya modeli za kifedha, *(joint financial model)*, ambazo zinatuonyesha mafanikio ya mradi huu kwa miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu zetu za miaka mitatu nyuma, ambayo tumekuwa tukiagiza chuma, mwaka 2023 tuliagiza tani milioni 1.175 za chuma zenye thamani ya shilingi

3,000,000,000,000. Mwaka uliofuata wa 2024 tuliagiza tani milioni 1.41 zenye thamani ya shilingi trilioni 3.73, lakini Mwaka ulioisha Disemba 2025, tuliagiza tani milioni 1.82 zenye thamani ya takribani shilingi trilioni 3.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunakubaliana Mradi wa Liganga na Mchuchuma utakapoanza utatuletea mageuzi makubwa ya kiuchumi. Linalotupa faraja ni *models* zetu za kifedha zinatuambia, kwenye kiwanda cha chuma tutaweza kuzalisha takribani tani milioni 2.9 za chuma kwa mwaka, vilevile bidhaa za chuma takribani tani 1,000,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia uchumi wa shilingi 1,000,000,000,000 itakapofika 2050. *Joint financial models* zetu zinatwambia tukitekeleza mradi huu kwa kadiri ambavyo tumeupanga, basi mapato yetu yatafikia shilingi trilioni 1.9 ndani ya miaka 25 ijayo kwa hiyo, ambacho ninataka kuwapa moyo Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla ni zimepita awamu nyingi ambapo stori za Liganga zilikuwa nyingi, lakini kwa Awamu hii ya Sita, Liganga haitakuwa stori tena, tunaenda kuanza utekelezaji. Tunamalizia *feasibility study,* ili kuweza kuanza hatua za utekelezaji wa mradi huu. Yote haya yamefanyika kutokana na msingi mzuri ambao ameuweka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, Novemba 2024, Mheshimiwa Rais alifanya ziara kwenda China na ule ndiyo ulikuwa msingi wa mafanikio ya Mradi wa Liganga. Sisi ndani ya sekta tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuifanikisha kazi hii na kuturahisishia utekelezaji wa majadiliano ambayo yamekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Liganga na Mchuchuma, mradi mwingine muhimu kwa mageuzi ya uchumi wa Taifa letu ni Mradi wa Maganga Matitu unaohusisha uzalishaji wa chuma ghafi. Mradi huu utakapoanza uchimbaji kuanzia mwaka ujao wa fedha, tutakuwa tuna uwezo wa kuchimba chuma tani 1,000,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tuna uwezo vilevile wa kuzalisha chuma ghafi tani 300,000 kwa mwaka. Waheshimiwa Wabunge chuma ghafi ni *raw materials* kwenye viwanda vyetu ambavyo vinatumia chuma chakavu. Mradi huu utakapoanza kuanzia mwaka ujao wa fedha, sasa hivi tayari mkandarasi yuko *site,* tutakuwa tuna chuma ghafi kwa ajili ya kusaidia viwanda vyetu ambavyo sasa hivi vinategemea chuma chakavu. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutupa maelekezo, ambayo yametusaidia kuanza utekelezaji wa Mradi wa Maganga Matitu, ambao tunategemea kuanzia mwaka ujao wa fedha tutaanza uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine wa tatu ambao ni muhimu sana kwa mageuzi ya uchumi wa Taifa letu ni Mradi wa Engaruka. Mradi huu unahusisha uchimbaji wa *soda ash* na uko kule Arusha kwenye Jimbo la Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi tunaagiza kutoka nje *soda ash*. Kwa mwaka tunatumia Dola za Kimarekani 121,000,000 na matumizi yetu ya ndani ni takribani tani 600,000 kwa mwaka. Tutakapoanza utekelezaji wa mradi huu tutakuwa tuna uwezo wa kujitosheleza sisi wenyewe kwa ndani. Kwa wasiofahamu, *soda ash* ni *raw material* nzuri sana kwa sababu, ndiyo inayotumika kwenye viwanda vyetu vya *glass* (viwanda vya vioo) na viwanda vya vigae. Vilevile inaweza ikatumika katika bidhaa za chakula na dawa pamoja na sabuni kwa hiyo, ni mradi muhimu sana wa kuweza kutusaidia kupunguza kuingiza *raw materials* kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu tulipata mwekezaji ambaye tumefanya naye majadiliano, lakini kwa sababu, sisi ndani ya sekta tunayo azma ya kuhakikisha miradi hii inaanza kutekelezeka, kama ambavyo tumefanya vizuri kwenye Liganga na Mchuchuma, Maganga Matitu na Mradi wa Engaruka. Tunaenda kujiridhisha kama majadiliano yana sura na taswira ya kiuchumi, ambayo sisi tunaitaka. Kama tukijiridhisha haya na sura hiyo, tutasitisha majadiliano na tutatangaza upya mradi huu kwa sababu, majadiliano yamechukua muda mrefu na tunaanza kujiridhisha kwamba, sisi na mwekezaji hatupo kwenye sura moja inayotazama mageuzi ya kiuchumi ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaahidi ndugu zangu ambao wako katika Mradi wa Engaruka, ambao tayari Mheshimiwa Rais ametupatia fedha na tumeanza kulipa fidia kule, tutafanyia kazi na hatutaruhusu kurudishwa nyuma na mwekezaji yeyote, ambaye hana azma njema kwa miradi yenye mageuzi ya kiuchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kuhusiana na miradi ya kimkakati, ambayo wote watakubaliana na mimi kwamba, ni muhimu sana, Kamati na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameelezea, sasa ninaomba nijielekeze kwenye hoja ambayo Wabunge wameielezea kuhusiana na kulinda viwanda vya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wamezungumza hapa kuhusiana na tozo na kodi ambazo zipo kwenye bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, bidhaa ambazo pia, zinazalishwa katika Taifa letu. Ninaanza kwa kusema ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, viwanda vya ndani vinafuata mnyororo wa thamani ambao unataka wawekezaji kwenye kuingia gharama kubwa za uwekezaji *(capital investment)* kwa hiyo, ni muhimu sana pale tunapoweka tozo na kodi kuangalia uwiano ambao utaleta usawa, ili bidhaa zetu za ndani ziweze kuwa na ushindani sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunakubaliana kwamba, tozo na kodi ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu, lakini kwa ajili ya uendelevu wa biashara tozo na kodi ni muhimu ziwe rafiki kwa mazingira ya biashara, zisilete urasimu, ziwe zina uwiano na ziwe zinachochea uzalishaji na ukuaji wa sekta binafsi. Nitatoa mfano; kuna kiwanda cha *textile* (nguo) ambacho sitakisema leo kwa sababu maalum, kiwanda kile kimeajiri Watanzania 2,500 kimewekeza kwa wakulima 5,000 wa pamba na kinanunua marobota tani 30,000 kila mwaka kwa thamani ya zaidi ya shilingi 25,000,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaingiza bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo *material* yake ni *plastic* kwa hiyo, ni bei ya chini. Huyu mwekezaji wa ndani hawezi ku-*compete* kwenye soko la aina hiyo kwa hiyo, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge,

yapo mambo ambayo ni lazima tuyaangalie upya kwenye masuala ya kulinda viwanda vyetu vya ndani. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, yeye ameunda Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi, ambayo inafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ndani ya Sekta ya Viwanda na Biashara tumefanya mapitio ya kwanza ya tozo na kodi kupitia mpango wa kwanza wa kuboresha mazingira ya biashara MKUMBI *One*. Sasa hivi tukiratibiwa na Wizara ya Uwekezaji tunafanya maboresho ya mazingira ya biashara, MKUMBI *Two,* kuhakikisha pamoja na jitihada zinazoendelea tozo na kodi ambazo siyo rafiki kwa viwanda vya ndani tunazipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua hii kuna biashara inabadilika kila siku kwa hiyo, mambo yaliyotokea miaka 10 nyuma siyo yanayotokea sasa hivi, lakini kwa sababu, biashara kila siku inakuwa na sura mpya na inakua kwenye Soko la Dunia inatulazimisha mara kwa mara kuangalia upya sekta yetu. Kuhakikisha yale masuala yanayokwamisha yasichukue muda mrefu, tuyachukulie hatua kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa hatua hii ninamwelekeza Katibu Mkuu, yapo mambo ambayo Wabunge wanne wameyazungumzia kuhusiana na kile Kiwanda cha Tanga na ile kemikali, ambayo inazalishwa pale. Ninamwelekeza Mheshimiwa Katibu Mkuu aliangalie jambo hilo, wafanye tathmini ya haraka, ili tuweze kuokoa kiwanda hiki na vilevile tuokoe viwanda vingine ambavyo kwa kweli, vina hali mbaya kutokana na kutokuwepo kwa uwiano wa tozo na kodi kati ya bidhaa zinazoletwa kutoka nje ya nchi na namna ya uzalishaji unavyofanyika katika viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kulinda viwanda, ninaomba nizungumzie namna ambavyo tunalinda biashara. Jukumu la Serikali ni kuwezesha biashara, hususani katika biashara za sekta binafsi. Ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliwahi kusimama hapa Bungeni na mara kadhaa alisimama huko nje akisema baadhi ya taratibu ambazo tunaweza tukafanya tukaboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia dhamana za mali zisizohamishika; jambo ambalo ninawashukuru sana Waziri wa Fedha na *BOT,* wameanza kulifanyia mchakato. Ninawashukuru sana wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa sababu, yapo mambo ambayo tayari wanayaangalia ukiwemo Mfumo wa Dhamana za Mikopo *(Credit Guarantees)* ambazo zinasaidia benki kuchukua sehemu ya hatari za mikopo na hivyo kusaidia ukuaji wa biashara. Vilevile kuna mambo mengine ikiwemo fedha za kijani *(green financing)* pamoja na mifumo ya kidijiti, ambayo yanachagiza biashara ndogondogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya mambo ambayo yanazungumzwa sana katika biashara ni masuala yanayohusiana na mikopo, pamoja na riba kwa wafanyabiashara. Pamoja na kwamba, riba zetu zimekuwa zikishuka taratibu kwa sababu, ukiangalia kwa mwaka uliopita tu, zimetoka 15.50% mpaka 15.11%.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo bado tunafanya vizuri, ikiwemo mikopo kwa sekta binafsi kwa sababu, takwimu zinatuonesha imeongezeka kwa 23.5% na sasa tunazungumzia takriban shilingi trilioni 44.6. Ambacho tunataka kuwaambia, Jumuiya ya Wafanyabiashara, ni Serikali ipo makini kuhakikisha tunawezesha viwanda na uendelevu wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Mheshimiwa Magreth, mdogo wangu, amezungumza suala la biashara za kidijiti; ninakubaliana na yeye kwa 100%. Mfumo wa biashara unavyoenda duniani kwa sasa umebadilika, kuna biashara za bidhaa vilevile kuna biashara za kidijiti. Mojawapo ya maeneo ambayo yanaleta fedha nyingi kwa sasa ni mfumo wa kidijiti wa kuuza bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Magreth kwamba, hapa bado kuna kazi ya kufanya, lakini jambo la kuleta heri ni kwamba, sisi ndani ya sekta tumejipanga kuangalia upya eneo hilo. Biashara ya dunia imebadilika kwa kasi sana, ukiangalia mwelekeo wake kwa sasa, ukiangalia mwaka 2024, mauzo ya huduma za kidijiti duniani yalifikia Dola za Marekani trilioni 4.9. Ukiangalia mauzo yote yale ya huduma za

biashara *(services trade),* ambayo yalikuwa shilingi trilioni 8.695, nusu yake ilikuwa inatokana na huduma za kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Magreth kwamba, sasa ni wakati wa kuratibu miundombinu ya kuuza nje huduma zetu za kidijiti na ni eneo ambalo linafungua fursa za kibiashara kwa vijana wengi zaidi, japokuwa yapo mambo ya kufanya, ambayo ninaamini tutaendelea kuyafanya vizuri kwa uratibu na sekta nyingine ikiwemo Sekta ya Mawasiliano, ya dada yangu, Mheshimiwa Angela Kairuki, Sekta ya Fedha, pamoja na sekta nyinginezo ambazo zipo katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie masuala muhimu ya mwisho, kisha nihitimishe. La kwanza ni kuhusu kulinda biashara za Watanzania; tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ni yeye ambapo Julai mwaka jana amesababisha kuwepo kwa katazo ambalo linataka baadhi ya biashara zifanywe na wazawa. Kutokana na katazo lile sisi ndani ya sekta tumesimamia kwa nguvu kubwa sana. Tumehakikisha leseni 900 ambazo zinafanya biashara ambazo zinatakiwa kufanywa na wazawa tumezizuia kupitia *BRELA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo ipo kwenye eneo hili ni baadhi ya wafanyabiashara kuzunguka mlango wa nyuma. Kariakoo tumepambana, zaidi ya 95% tumedhibiti, changamoto iliyopo ni kwamba, wageni wanaomba leseni kwa majina ya wazawa na wamehamisha biashara kwenda kwenye *godown* kwa hiyo, sasa tumekubaliana tutaanza kuwafuata kwenye *godown* hukohuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huko kwenye kuwafuata kwenye *godown* nitaongea na kaka yangu, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Katambi. Yeye ndiye mwenye Idara ya Uhamiaji, ili sasa tuunganishe nguvu kati yetu sisi na Halmashauri, ambayo iko chini ya Waziri Shemdoe, ambaye kwa muda wote tumeshirikiana vizuri kudhibiti pale kwenye Soko la Kariakoo, pamoja na yeye, ili aina mpya ya biashara iliyojitokeza baada ya kudhibiti hii na yenyewe tuendelee kuidhibiti. Ambalo ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ni, Sekta yetu ya Viwanda

na Biashara itasimama mstari wa mbele kulinda biashara za wazawa kwa sababu, ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Waziri wa Madini, Mheshimiwa Mavunde, na yeye analo tamko lake la biashara zinazotakiwa kufanyika katika Sekta yake ya Madini. Ninamshukuru pia, Mheshimiwa Bashiru na yeye amekuja na mambo yake ya kulinda biashara za wazawa katika sekta ya mifugo kwa hiyo, ndani ya Serikali tumejiratibu vizuri, kwa ajili ya kulinda biashara za wazawa. Waheshimiwa Wabunge, ninawahakikishia tunafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika hoja zangu, Mheshimiwa Rashid amezungumza hapa kuhusiana na sukari ya Mahonda. Leo siyo siku muhimu ya kutoa somo kuhusiana na Katiba, lakini ninaomba uniruhusu niseme kwa dakika moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya Nne imeweka pale mambo ya Muungano na katika Ibara ile ya Nne ina-*establish* nyongeza ya kwanza, ambayo inaeleza mambo 22 ya Muungano kwa hiyo, siyo kweli kusema mambo ambayo tunajadili kupitia Kamati za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hayana msingi wa Kikatiba. Masuala yote ambayo yanajadiliwa na viongozi wakuu yamefuata utaratibu uliowekwa ndani ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya Nne na Nyongeza ya Kwanza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli za Bunge letu.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mahonda. Mheshimiwa Mbunge amesema katika Wizara ambazo zinasababisha kuzorotesha mazingira ya kufanya biashara kwa ndugu zetu ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo siyo kauli ya kiungwana. Katika maeneo ambayo tunashirikiana vizuri sana katika kukuza biashara ni katika Sekta yetu ya Viwanda na Biashara. Ninatoa mifano mitatu kupitia *TBS;* tumekubaliana namna ya kuenenda kupunguza *duplication* na kupunguza taratibu za udhibiti. Mambo yakifanyika *ZBS* sisi huku tunakubali kupitia *TBS* na huo ndiyo undugu ambao tumekuwa tukiuishi kwa miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *BRELA* na Zanzibar *Business and Property Registration Agency* tumefanya vizuri sana. Tuna ushirikiano mkubwa sana kuhakikisha tunawezesha biashara kwenye usajili, lakini vilevile usajili wa kampuni, majina pamoja na hataza na tumekuwa tukifanya hivyo kibiashara na kindugu tukienenda katika undugu ambao tunao baina yetu sisi wawili. Vilevile, kupitia *TRA* na *ZRA* masuala yote ya kikodi yamekuwa yakitatuliwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho chini ya Wizara yetu, tunayo Taasisi ya *TanTrade,* ambayo ni ya Muungano, imekuwa ikifanya kazi vizuri kwa uwiano kuhakikisha mazingira ya biashara yanaenda vizuri. Sisi ndani ya Serikali tumekubali sukari ya Mahonda ije iuzwe katika Soko la Tanzania Bara. Hatuwezi kufanya utaratibu kadri tunavyofanya na nchi nyingine. Hatuwezi kufanya *JTC* na ndugu zetu wa Zanzibar. Hatuwezi kufanya *JPC* na ndugu zetu wa Zanzibar. Hatuwezi kuwa na *bilateral* na ndugu zetu wa Zanzibar kwa sababu, nchi hii ni moja, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; siku nyingine Mheshimiwa Mbunge akisimama kuongea basi aepuke kutumia kauli ya sisi fulani kwa sababu, sisi wote ni wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kuhitimisha. Ninaomba nimshukuru tena Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninaomba niwashukuru wenzangu ndani ya sekta yetu. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi. Ninawaambia wananchi wa Mikumi, wanaye Mbunge bora na imara sana, waendelee kumuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Katibu Mkuu wetu, Balozi Waziri Rajab, kwa namna ambavyo tunashirikiana katika Wizara. Ninamshukuru Naibu Katibu Mkuu, lakini chini ya sekta yetu tuna taasisi 13 na nina wakuu wa taasisi 13, ambao wanafanya kazi ya kukuza sekta ya viwanda na biashara kwa uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru sana, pamoja na Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa bodi zetu zote, washirika na wadau wetu wote, zikiwemo jumuiya mbalimbali za wafanyabiashara. Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, ikiongozwa na Mwenyekiti wetu Kazembe na Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, ikiongozwa na Ndugu yetu Severin. Tunawaomba waendelee kutupa ushirikiano kwa kadri ambavyo tunashirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninaomba niwashukuru wafanyabiashara na wawekezaji wote wa viwanda ambao wanaratibiwa kupitia *TPSF* na *CTI*. Mara zote wamekuwa wakitupa ushirikiano wa kutosha na ninawaomba tuendelee kushirikiana hivyo hivyo kwa maslahi ya Sekta yetu ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara

Kifungu 1001 – *Admininstration and Human Resource Management*.....Sh. 25,582,486,063

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……Sh. 930,282,600

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 3,475,284,000
Kifungu 1004 – *Government and Communication Unit*……...Sh. 751,560,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*…….……Sh. 624,361,000
Kifungu 1006 – *Legal Services Unit*……..….Sh. 685,717,000
Kifungu 1007 – *Management Information System*…..Sh. 636,569,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*.…….Sh. 672,383,860
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*…..…..Sh. 668,169,144

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2001 – *Industry*.....Sh. 14,194,641,589
Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises Division*.....Sh. 8,613,975,433
Kifungu 3001 – *Trade Integration Unit*.....Sh. 2,993,310,000
Kifungu 4002 – *Commodity Market Development*.....Sh. 44,293,790,311

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*……..Sh. 2,500,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……..Sh. 3,800,000,000
Kifungu 1007 – *Management Information System*…..Sh. 150,000,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*…….Sh. 100,000,000
Kifungu 2001 – *Industry*……..Sh. 17,634,398,000
Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises Division*……....Sh. 5,055,705,000
Kifungu 4002 – *Commodity Market Development*……..….Sh. 4,450,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Mtoa hoja.

T A A R I F A

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 122 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Ahsanteni. Ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Judith Kapinga; Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha unaokuja 2026/2027.

Waheshimiwa Wabunge, ninaipongeza Kamati yetu ya Bunge inayosimamia Wizara hii, Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati kwa kazi kubwa mliyoifanya

ya kuisimamia sekta hii. Pia, tunawapongeza Wabunge mliopata nafasi ya kutoa mawazo na michango yenu kwa Wizara hii wakatekeleze, kama ambavyo tumependekeza.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya pongezi hizo, basi ninawatakia kila la heri katika utekelezaji wa bajeti yenu. Ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi Siku ya Jumatatu, tarehe 25, mwezi huu, saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 7.46 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 25 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA